

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Arobaini na Moja – Tarehe 31 Mei, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaanza kikao chetu cha Arobaini na Moja, Katibu.

NDG. LINA KITOSI – KATIBU MEZANI:-

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO):

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2018/19.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa Bajeti na Majukumu ya Wizara

ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

MWENYEKITI: Ahsante. Katibu.

NDG. LINA KITOSI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Swali letu la kwanza linaelekezwa Ofisi ya Waziri Mkuu na linaulizwa na Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, kwa niaba yake Mheshimiwa Amina Mollel.

Na. 341

Utekelezaji wa Mpango wa Ukimwi 90-90-90

MHE. AMINA S. MOLLEL (K.n.y MHE. HAWA M. CHAKOMA) aliuliza:-

Je, Serikali inatekelezaje Mpango wa UKIMWI wa 90-90-90?

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mollel. Majibu, Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza mpango wa 90-90-90 kwa kufanya mambo yafuatayo:-

(i) Serikali imeridhia Mkakati wa Shirika la Afya Duniani (*WHO*) wa kupima VVU na kutibu bila ya kuzingatia kiwango cha kinga mwilini (*CD4*);

(ii) Serikali imetoa Waraka unaoagiza utekelezaji wa mkakati huu tangu Oktoba, 2016;

(iii) Utaratibu umewekwa wa kuhakikisha watu wote wanaogundulika kuwa na VVU wanaanzishiwa dawa za kufubaza VVU (*ARV*) mara moja; na

(iv) Serikali baada ya kubaini mapungufu ya wananchi kujitokeza kupima maambukizi ya VVU kuitia utafiti, imeandaa kampeni mbalimbali kwa ajili ya kuhamasisha wananchi kujitokeza kupima VVU ili kujua hali zao na hasa mkazo mkubwa utaelekezwa kwa wanaume ambaao utafiti umeonesha kuwa hawajitokezi sana kupima na kujua hali zao. Kampeni hii inategemewa kuzinduliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu tarehe 19 Juni, 2018 hapa Mjini Dodoma. Aidha, kampeni hii itahusisha kusambaza ujumbe wa uhamasishaji kuitia vyombo vya habari, mabango, vipeperushi na makongamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito kwa wananchi wote kuendelea kupima afya zao ili watambue hali zao na kuchukua hatua stahiki. Pia natoa wito kwa wananchi kushiriki kikamilifu katika kampeni hiyo mara itakapoanza kwa nchi nzima.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mollel.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri kutoka kwa Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, hivi majuzi tu ulizinduliwa upimaji wa VVU unaofadhiliwa na *USAID*, Shirika la Kimarekani, nataka kufahamu nini mkakati wa Serikali kumaliza tatizo hili hasa kitakwimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kutokana na tatizo hili la VVU hasa kwa waathirika wengi ambaao kwa namna moja au nyingine dawa zimekuwa pia ni tatizo. Wapo wanaotumia kikamilifu lakini kwa wengine upatikanaji wake

ni changamoto lakini pia upatikanaji wa dawa unapaswa uendane na lishe. Nini sasa mkakati katika kusaidia wananchi wale ambao kipato chao ni cha chini lakini wana maradhi haya na kutokana na ukosefu huo wa lishe wanasababisha vifo. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Afya, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Amina Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalı lake la kwanza ameelekeza katika suala la changamoto za takwimu. Niendelee kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba takwimu zetu za masuala ya UKIMWI ziko vizuri. Serikali kuititia Taasisi ya TACA/DS pamoja na Wizara ya Afya, Kitengo cha UKIMWI ndio wanaoratibu takwimu zote za masuala ya UKIMWI na nimthibitishie katika malengo haya ya 90-90-90 takwimu zetu kama nchi ziko vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalı la pili amezungumzia suala la upatikanaji wa dawa. Naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba upatikanaji wa dawa za UKIMWI ni asilimia 100 na tunazisambaza nchini kote. (akofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia amegusia kidogo suala la lishe, ni kweli tunatambua kwamba kumekuwa na changamoto ya lishe katika baadhi ya makundi lakini sisi mkakati wetu tunajaribu sana kutoa elimu katika jamii na kwa wale ambao kabisa wanaonekana wana changamoto ya lishe basi kwa wale wachache kuna utaratibu maalum wa kuweza kuwasaidia. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kupata nafasi ya kuuliza swalı moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hali ya maambukizi katika Jiji la Dodoma inaongezeka kwa kasi sana; na kwa kuwa katika baadhi ya nchi nyingine duniani wanatumia njia mbadala mbali na damu, wanatumia mate kuweza kutambua wale waathirika wa VVU. Naomba Serikali ituambie ina mkakati gani wa ziada wa kuwatambua wale waliopata athari hii ya VVU kwa njia ya kutumia mate na hasa tukianzia na Mkoa huu wa Dodoma?

MWENYEKITI: Ahsante. Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Masoud, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mkoa wa Dodoma maambukizi yamepanda kutoka asilimia 2.4 hadi asilimia 5, sawa na Mikoa ya Tanga na Mwanza. Kwa hiyo, tunafanya utafiti maalum wa kuangalia kwa nini katika baadhi ya mikoa maambukizi ya UKIMWI yamepanda mwaka 2012 mpaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la njia mbalimbali za kupima, ni kweli tumekuwa na changamoto ya kuwapata watu kupima hasa wanaume na tumeona njia ambayo itaweza kusaidia wanaume kupima UKIMWI ni njia ya mtu kujipima mwenyewe. Jana tulikuwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na moja ya kifaa ambacho tutakitumia; lakini sheria kidogo zinatukwaza, inasema kipimo cha kujipima mwenyewe haiwezekani. Kwa hiyo, tumemuandikia Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili aweze sasa kuleta mabadiliko madogo ya sheria iweze sasa kuruhusiwa kwa mtu kujipima ikiwemo kwa kutumia kipimo cha mate ambapo ndani ya dakika 15 utaweza kujua kama una maambukizi ya UKIMWI au hapana. Tunaamini mtu akishajipima mwenyewe na kujiona kwamba ana maambukizi itakuwa ni kichocheo cha kwenda katika kituo cha afya ili aweze kuthibitika na hivyo tumuingize katika mpango wa dawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai, kama alivyo sema Naibu Waziri, dawa za *H/V* zipo kwa asilimia 100, changamoto yetu watu wapime. UKIMWI si tena sentensi ya kifo, ukiwa na UKIMWI ukipima tunakuungiza mara moja kwenye mpango wa dawa unaishi maisha safi na salama bila changamoto zozote. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Salma Kikwete.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nini mpango kabambe wa Serikali kwa maeneo yale ambayo UKIMWI uko chini ya asilimia moja, kuhakikisha kwamba tatizo hili linaondolewa kabisa kwa maeneo hayo?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Jenista Mhagama.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salma Kikwete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzindua Taarifa ya Takwimu za UKIMWI tarehe 1 Desemba, 2017 nchi kwa ujumla tumeweza kujua hali ya UKIMWI katika mikoa yote. Tumeiagiza Tume ya Kudhibiti Ukimwi Nchini (*TACAIDS*) kuhakikisha kila mkoa unatengeneza mkakati wao kulingana na hali ya UKIMWI ilivyo katika mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale ambao maambukizi yao ni machache, viongozi wa mkoa na taasisi zinazohusika wahakikishe wana-*retain* ile hali ama kuhakikisha maambukizi hayapandi ama yanaondoka kabisa na ile mikoa ambayo maambukizi yako juu mikakati ya mkoa huo ni kuhakikisha maambukizi yanashuka chini. Kwa hiyo, kila mkoa unatengeneza mkakati kutokana na hali halisi katika mkoa husika. Kwa hiyo, Serikali inalismamia sana suala hili na lengo letu ni kufika hiyo 90-90-90, ama huko mbele tuendane na

matakwa ya kiulimwengu ya kufika 00-00-00. Kwa hiyo Serikali inazingatia sana suala hilo.

MWENYEKITI: Tunashukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri. Swali hili nimelipa muda mrefu kwa sababu ya umuhimu wake na kwa faida za afya ya Watanzania.

Tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Hassanali Mohamedali Ibrahim, Mbunge wa Kiembe Samaki linalekezwa kwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, kwa niaba yake Mheshimiwa Hamida Abdallah.

Na. 342

Tatizo la *Parking* katika Jiji la Dar es Salaam

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH (K.n.y MHE. IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI) aliuliza:-

Wananchi au taasisi zilizopewa vibali vya kupaki magari hadi saa 12 jioni katika Jiji la Dar es Salaam sasa wanatumia vibali hivyo kupaki kwa saa 24. Hali hiyo imeibua usumbufo kwa wananchi wanaotaka kupaki magari yao kuanzia saa 12 jioni:-

Je, ni lini Serikali itakomesha suala hilo ili kuwaondolea wananchi usumbufo wanaoupata?

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Hamida. Majibu, Mheshimiwa Kandege, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassanali Mohamedali Ibrahim, Mbunge wa Kiembe Samaki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria Ndogo ya Maegesho ya Magari katika Tangazo la Serikali (*GN*) Na. 60 la mwaka 1998 na marekebisho yake (*GN*) Na. 41 ya mwaka 2017, maegesho ya kulipia pamoja na maegesho yaliyohifadhiwa (*Reserved Parking*) yanapaswa kutumika kuanzia saa 2.00 asubuhi mpaka saa 12.00 jioni, baada ya muda huo maegesho yote yanatakiwa kuwa wazi kwa ajili ya matumizi ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaagiza Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini ikiwemo Jiji la Dar es Salaam kusimamia vyema utekelezaji wa sheria hii na kuhakikisha chanzo hiki cha mapato kinasimamiwa ipasavyo ili halmashauri zinufaike na chanzo hiki.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Hamida.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali lakini napenda kuuliza swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kimekuwa ni chanzo kizuri cha mapato katika maeneo ya majiji, manispaa na maeneo mbalimbali nchini. Hata hivyo, kumekuwa na kero kubwa sana kwa sababu ya kutosimamiwa vizuri kwa sheria hii. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri amewatangazia Wakurugenzi wa Halmashauri pia wangepelekewa maagizo haya kwa maandishi ili sheria hii iweze kusimamiwa na kupunguza kero ambayo ipo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, umepewa ushauri mzuri tu, unauchukua?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba nijibu na nipokee ushauri wa kutoka kwa Mheshimiwa Hamida na nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo yake anasema kwamba chanzo hiki pamoja na kwamba ni cha uhakika lakini kimekuwa kero na mimi naomba niungane naye. Katika maeneo mengi unakuta kwamba mtumiaji anapo-park inakuwa kama ni suala la kuviziana, kwamba je, huyu atakosea ili adhabu iweze kutolewa. Naomba niwaagize Wakurugenzi wote kusimamia sheria hii lakini pia alama za *parking* ziwe ni zile ambazo zinaonekana kwa kila mtu ambaye anatumia gari ili anapo-park isije ikaonekana kwamba ni *wrong parking*.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum bado linaelekezwa kwa Ofisi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, kwa niaba yake Mheshimiwa Salma Kikwete.

Na. 343

Mkakati wa Kupunguza Vifo vya Akina Mama na Watoto

MHE. SALMA R. KIKWETE (K.n.y MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA) aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ina mkakati madhubuti wa kupunguza vifo vya akina mama na watoto:-

(a) Je, ni lini Zahanati ya Kiboga katika Kata ya Msongola itafunguliwa ili wananchi wapate huduma ya afya?

(b) Kwa kuwa wananchi wa Mtaa wa Mbondole katika Kata ya Msongola walitoa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa zahanati, je, ni lini zahanati hiyo itakamilika?

MWENYEKITI: Ahsante sana. Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiboga na Luhanga ni mitaa miwili inayopakana ambayo hapo awali ilikuwa mionganoni mwa vitongoji katika Kijiji cha Mvuti, Kata ya Msongola. Wananchi wa Mtaa wa Luhanga kwa nguvu zao wenyewe walianza ujenzi wa zahanati na Serikali ikawaunga mkono na sasa jengo la zahanati ya Luhanga lipo katika hatua za upakaji rangi, kuweka madirisha na milango. Mtaa wa Kiboga bado hauna zahanati hivyo halmashauri inatakiwa kutenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa zahanati. Hata hivyo, wakazi wa Kiboga wanapata huduma za afya katika Zahanati ya Mvuti ambayo ipo ndani ya kilometra tano ambayo ni matakwa ya utekelezaji wa Mpango Maalum wa Uimarishaji Afya ya Msingi 2009 - 2017.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Zahanati ya Mbondole imebaki kupigwa rangi na kuwekewa milango ili ikamilike na kuanza kutoa huduma. Halmashauri ya Wilaya ya Ilala imetenga shilingi milioni 70 katika mwaka wa fedha 2017/2018 ambayo inaweza kukamilisha ujenzi huo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Salma Kikwete.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na majibu mazuri ya Serikali, naomba nimuulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, tatizo la zahanati katika nchi yetu limekuwa likipungua siku hadi siku lakini kwa baadhi ya maeneo, maeneo mengi wananchi wameweza kuweka nguvu kazi zao kuhakikisha kwamba zahanati zinapatikana ili kupunguza vifo vya akina mama

na watoto. Je, lini Serikali itamaliza yale maboma yote kuhakikisha kwamba tatizo hili linaisha? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, swalii hili linarandana sana na kituo cha afya kilichopo kule Lindi katika Kata ya Mnazi Mmoja. Je, ni lini watawahakikishia wananchi wa Lindi wanamaliza lile jengo pamoja na kwamba wameshawapa kiasi fulani cha fedha? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege, kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la kumalizia maboma ambayo wananchi wameingiza nguvu zao, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Salma, naye ni shuhuda, jinsi ambavyo Serikali inaelekeza nguvu zake kuhakikisha kwamba maboma yote tunayamalizia hatua kwa hatua. Ndiyo maana tumeanza na ujenzi na ukamilishajii wa vituo vya afya 208 na juzi vimeongezeka viwili, tumekuwa na 210. Naomba nimhakikishie kwamba jitihada ambazo zimefanywa na wananchi Serikali itahakikisha kwamba tunamalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili linalohusiana na Kituo cha Afya cha Mnazi Mmoja, naomba nimpongeze Mheshimiwa Salma kwa jitihada zake za kuwapigania wananchi wa Mkoa wa Lindi. Nilipata fursa ya kwenda kutizama kazi ya ujenzi wa Kituo cha Afya Lindi, kazi niliyoilacha ilikuwa inaenda vizuri. Naamini katika muda ambao tumekubaliana kwamba vituo vya afya hivi vijengwe kwa kuzingatia miezi mitatu na wananchi wa Lindi kwa maana ya Kituo cha Afya Mnazi Mmoja kwa jitihada nilizoziona na nguvu kazi na ari yao ya kujitoa, naamini ndani ya muda huo kituo cha afya kitaweza kukamilika. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Musa Ntimizi na Mheshimiwa Chikambo.

MHE. MUSA R. NTIMIZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mkakati wa kupunguza vifo nya mama na mtoto Jimboni Igalula tumeanzisha ujenzi wa vituo nya afya vitano kwa nguvu za wanachi na Mbunge ambapo tumefikia katika hatua ya boma. Je, Serikali ina mpango gani kusaidia nguvu hizi za wananchi ukizingatia hatuna kituo hata kimoja cha afya katika Jimbo la Igalula? Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana, yale ya wali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swalii hili la Mheshimiwa Ntimizi, kwanza naomba nimpongeze Mbunge huyu, katika kazi ambayo ameifanya ni kuhamasisha wananchi wake kujenga vituo nya afya vipya lakini bado havijajengwa. Nikiri wazi kwamba amefika ofisini kwangu na kuweza kuweka kipaumbele katika suala zima la Jimbo lake. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama tulivyoongea ofisini kwetu jinsi gani tutafanya ofisi yetu isaidie katika suala zima maeneo yale tupate vituo nya afya hasa tukianza na vituo nya afya viwili, jambo hili ni *commitment* ya Serikali, tutajitahidi kwa kadri iwezekanavyo ili wananchi wa eneo lile la Jimbo la Igalula waweze kupata huduma ya afya.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Chikambo.

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupunguza vifo vya akina mama wajawazito ni pamoja na uwepo wa vifaa vya kujifungulia katika hospitali zetu lakini mpaka hivi tunavyozungumza, ziko hospitali, zahanati na vituo vya afya akina mama wanatakiwa waende na mabeseni na mipira kwa ajili ya kujifungua. Ni lini tatizo hili litarekebishwa na Serikali yetu? Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la dada yangu Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Ruvuma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuna changamoto ya vifaa mbalimbali lakini lazima tumshukuru Mheshimiwa Rais, tukumbuke hapa katikati aliweza kutoa vifaa kwa karibu Halmashauri zote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na uboreshaji wa vituo hivi vya afya 208 tunavyovijenga ambavyo jumla yake pamoja na vifaa itagharimu karibu shilingi billioni 156, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote siyo muda mrefu sana vituo hivi vinavyokamilika, vifaa hivi tutavisambaza maeneo mbalimbali. Ni imani yangu kubwa kwamba tutapunguza kero kubwa sana katika suala zima la vifaa vya kujifungulia katika vituo vyetu vya afya na zahanati zetu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, Mbunge wa Rungwe na linalekezwa kwa Waziri wa Madini.

Na. 344

Uwepo wa Madini na Gesi Asilia – Wilayani Busokelo

MHE. FREDY A. MWAKIBETE aliuliza:-

Halmashauri ya Busokelo ina utajiri mkubwa wa madini na gesi asilia aina ya *carbon dioxide*:-

Je, ni lini Serikali itaenda kufanya utafiti wa kutosha kwenye Kata ya Lufilyo ambapo kuna madini aina ya *marble* (marumaru)?

MWENYEKITI: Ahsante. Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Biteko, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTO M. BITEKO) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, Mbunge wa Rungwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uwepo wa madini ya *marble* katika Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo ambapo Kampuni ya Marmo Granito inamiliiki leseni moja ya uchimbaji wa kati yenye Namba *ML 250* ya mwaka 2006 na leseni 10 za uchimbaji mdogo wa madini hayo zenye namba *PML 0007657 – 0007666* za mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utambuzi huo ni kutokana na utafiti wa awali uliofanywa kati ya mwaka 2005 hadi 2007 na Kampuni ya *BGR* ya Ujeruman kwa ushirikiano wa taasisi za Serikali (*STAMICO* na *GST*). Utafiti huo ulipelekea kugunduliwa kwa madini hayo yenye rangi ya kijani na nyeupe katika Kijiji cha Kipangamansi kilichopo katika Kata ya Lufilyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali kuitia Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini

Tanzania (*GST*) itaendelea kufanya utafiti wa awali wa kijiolojia ili kubaini maeneo mengine yenye madini hayo katika Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo. Vilevile utafiti wa kina utafanyika ili kubaini ubora na wingi wa upatikanaji wa madini hayo na kuishauri Serikali. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwakibete.

MHE. FREDY A. MWAKIBETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, napenda kuweka kumbukumbu sahihi kwamba mimi ni Mbunge wa Jimbo la Busokelo na si Rungwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Halmashauri ya Busokelo ina utajiri mkubwa sana wa madini aina ya *marble* pamoja na *carbon dioxide gas*. Serikali imekiri hapa kwamba madini ya *marble* yanapatikana katika Kijiji cha Kipangamansi, Kata ya Lufilyo. Je, ni lini Serikali itakuja kufanya tafiti katika milima ya safu za Livingstone kwani inasadikika pia kuwa kuna madini aina ya dhahabu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Waziri tumekuwa tukiongea mara nyingi kwamba atutembelee Halmashauri ya Jimbo la Busokelo ili apate kushuhudia wananchi wangu wanaojishughulisha na hizo shughuli za *marble*. Ni lini Waziri atakuja kuwatembelea wananchi wa Jimbo langu na kuona shughuli hizo za madini? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Doto Biteko.

NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTO M. BITEKO): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwakibete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu namuomba radhi kidogo Mheshimiwa Mbunge kwa kukosea kutaja jina lake. Nieleze tu kwamba Mheshimiwa Mwakibete ni miongoni mwa Wabunge ambao kwa kweli katika kufuatilia masuala ya madini kwenye Jimbo lake amekuwa mstari wa mbele. Kama alivyoeleza hapa, mara nyingi amekuwa akitualika Wizara twende kwenye Jimbo lake na mara ya mwisho tulizungumza tukakubaliana tutakwenda. Nataka nimuhakikishie kwamba tutakwenda mara baada ya kukamilisha Bunge la Bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni lini tutafanya utafiti kwenye Milima ya Livingstone, naomba nimjulishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Taasisi yetu ya *GST*inaendelea kufanya tafiti mbalimbali kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini ili kubaini maeneo yenye madini ikiwemo eneo la Busokelo na Luflyo kama alivyoomba.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Alfredina Kahigi.

MHE. ALFREDINA A. KAFIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika nchi yetu kuna madini ya aina mbalimbali kama vile *ruby*, *sapphire blue*, ulanga na *tin* katika Mkao wa Kagera, Wilaya ya Karagwe. Je, Serikali ina mkakati gani wa kutangaza madini haya katika soko la dunia kama inavyotangaza tanzanite, dhahabu na almasi? Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu, Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Biteko.

NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTO M. BITEKO): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Kahigi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, madini yote ambayo tunayachimba hapa nchini ni wajibu wetu kama Serikali kuyatangaza kwamba yapo ndani ya nchi na kuwavutia

wawekezaji waje kuwekeza katika madini hayo. Madini ya *tin* na madini mengine aliyoyataja tunaendelea na mkakati huo wa kuyatangaza duniani kote na ndiyo maana ataona hata leo akienda hapo nje atakuta tuna maonyesho mbalimbali. Baada ya bajeti hii tutakuwa na vipindi mbalimbali vya redio, televisheni, magazeti na machapisho mbalimbali kwa ajili ya kutangaza utajiri tulionao ndani ya nchi yetu yakiwemo madini ya *tin* na haya mengine ya vito aliyoyataja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kiruswa na Mheshimiwa Neema Mgaya.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza kwa niaba ya wananchi wa Longido ambao pia ninu furaha kwamba Madiwani wao karibu wote leo wapo hapa kama wageni wa Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido sawa na Busokelo, kwamba tuna utajiri mkubwa wa madini ya rubi. Kwa kuwa madini ya rubi ukiyakata ili kuyaongezea thamani kulingana na utaratibu uliotolewa na Serikali yanagika. Kwa kuwa Mawaziri walishatembelea na wakajua changamoto hiyo, wanatuambia ni lini utaratibu huo utakamilika ili wananchi waweze kuyauza mawe haya waendelee kunufaika?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu, Naibu Waziri wa Wizara ya Madini, Mheshimiwa Biteko.

NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTO M. BITEKO): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba mimi pamoja na Naibu Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Nyongo tulikwenda Longido na hasa kwenye eneo la Mundarara anbako kuna machimbo ya rubi. Wananchi wa kule

wanajihusisha na shughuli hiyo na changamoto aliyoizungumza Mheshimiwa Mbunge walitueleza kwenye mazungumzo yetu na wao. Jambo ambalo linapaswa lieleweke hapa ni kwamba Sheria yetu mpya ya Madini imezuia kabisa usafirishaji wa madini ghafi kwenda nje ya nchi. Lengo ni kwamba tunataka teknolojia na ajira zibaki ndani ya nchi kuliko kuzisafirisha kwenda nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo madini ambayo yana upekee wa aina yake katika ukataji. Serikali kupitia Wizara ya Madini na Tume ya Madini tunaandaa mwongozo wa namna bora zaidi ya kuwasaidia wananchi ili waweze kupata fursa ya kuuza madini haya.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Neema Mgaya.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Njombe kuna wananchi wengi sana wameomba leseni kwa ajili ya utafiti na uchimbaji wa makaa ya mawe. Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini wananchi hawa mtawapa leseni hizo ili tuweze kuinua uchumi wa Mkoa wetu wa Njombe?

MWENYEKITI: Majibu tafadhali, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Madini.

NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTO M. BITEKO): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Neema William Mgaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Neema Mgaya yuko mstari wa mbele kuwapigania wananchi wa Mkao wa Njombe na hususan wanawake. Naomba nichukue nafasi hii nimpongeze kwamba juhudhi zake si bure, wananchi na wanawake wa Mkao wa Njombe wanaziona na sisi kama Serikali tutamuunga mkono kwa hatua alizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo la lini tutaanza kuwapa leseni, naomba nimpe taarifa njema Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Serikali kuititia Tume yetu ya Madini ambayo imeteuliwa hivi karibuni, tumeanza kutoa leseni kwa wachimbaji wadogo zote ambazo zilikuwa zimeombwa na tunapitia maombi mengi ambayo yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa kwamba mpaka sasa kuna jumla ya zaidi ya leseni 5,000 tunazitoa nchini kote. Wananchi wa Mkoa wa Njombe ambao wapo kwenye maombi hayo na wao watahudumiwa kama wengine. Nashukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kakoso.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliahidi kusaidia wachimbaji wadogo wadogo. Jimboni kwangu wapo wachimbaji wadogo wadogo wa Kata ya Katuma ambao wanajishughulisha na uchimbaji wa dhahabu. Je, Serikali inachukua hatua ipi ya kusaidia wachimbaji wadogo waweze kufanya shughuli zao?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Madini, kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTO M. BITEKO): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Moshi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ni kuwasaidia wachimbaji wadogo na kuwainua ili watoke kwenye uchimbaji mdogo waje kwenye uchimbaji wa kati, na walio kwenye uchimbaji wa kati waende kwenye uchimbaji mkubwa. Kazi ya Serikali, hatua ya kwanza ya kuwasaidia wachimbaji wadogo ni kuwarasimisha. Kila mahali ambapo tunakuta kuna wachimbaji wadogo ambao hawapo rasmi tunawarasimisha kwa kuwaweka kwenye

vikundi na baadaye kuwapatia leseni wawe na uhalali wa kuweza kuchimba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya pili ni kuwapatia mafunzo ya namna bora ya uchimbaji kwa kuzingatia sheria lakini vile vile utunzaji wa mazingira. Kazi hizi zote Mheshimiwa Mbunge ataziona baada ya bajeti hii kwa sababu hii ni Wizara mpya, tutakuwa na progamu maalum ya kuwasaidia wachimbaji wadogo wakiwemo wachimbaji wake wa Kata ya Katama.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, linaulizwa kwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Na. 345

Kupunguza Viwango vya Riba katika Benki Nchini

MHE. KHATIB SAID HAJI aliuliza:-

Viwango vya riba katika benki hapa nchini ni vikubwa na vimeduwa ni kikwazo kwa Watanzania wengi kuweza kukopaa na kufanya biashara:-

Je, Serikali inachukua hatua gani ili Benki ziweze kupunguza viwango hivyo vya riba?

MWENYEKITI: Ahsante. Naibu Waziri, Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Kijaji.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara huria ya sekta ya benki ilianza tangu mwaka 1991 mara baada ya kuitishwa wa Sheria ya Usimamizi wa Benki na Vyombo vya Fedha ya

mwaka 1991. Kupitia sheria hiyo, wawekezaji walifungua benki binafsi hapa nchini na gharama za huduma za bidhaa kuamuliwa na nguvu ya soko. Hivyo basi kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Benki na Vyombo vya Fedha ya mwaka 1991, Serikali haina mamlaka ya moja kwa moja ya kupunguza viwango vya riba katika soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ukweli kwamba bei ya huduma na bidhaa katika sekta ya fedha inaaniliwa na nguvu ya soko, Serikali kwa upande wake imekuwa ikichukua hatua za kisera ili kuhakikisha kuwa riba katika soko zinapungua. Baadhi ya hatua zilizochukuliwa na Serikali kupitia Benki Kuu ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuzitaka benki za biashara kutumia mfumo wa kuhifadhi na kutoa taarifa za wakopaji (*credit reference bureau system*).

(ii) Kwa sasa Benki Kuu inatoa mikopo ya muda mfupi kwa benki za biashara kwa kiwango cha asilimia 6.89.

(iii) Benki Kuu imeshusha riba (*discount rate*) kutoka asilimia 16.0 hadi asilimia 9.0.

(iv) Benki Kuu imepunguza kiwango cha chini cha amana kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu na benki za biashara (*Statutory Minimum Reserve Requirement*) kutoka asilimia 10.0 hadi asilimia 8.

(v) Serikali imeendelea kulipa malimbikizo ya madai yaliyohakikiwa kwa lengo la kupunguza kiwango cha mikopo chechefu na kuchochea ukuaji wa shughuli za uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hatua hizi za kisera kuchukuliwa na Serikali, baadhi ya benki za biashara hapa nchini zimeanza kupunguza riba ya mikopo. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itaendelea kuchukua hatua za kisera ili kuhakikisha kuwa riba za mikopo katika soko zinaendelea kupungua. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Khatib.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza katika hili napenda kwa dhati kabisa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudzi zake katika kuhakikisha benki zinaendelea kupunguza riba za mikopo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la kwanza, ni kweli benki zimeanza kuitikia wito huu na kipekee niipongeze Benki ya *CRDB* kwa kuwa wa kwanza kuitikia wito huu. Hata hivyo, inaonekana mikopo ambayo inapewa unafuu wa riba na kwa haraka ni ya wafanyakazi na watumishi wa umma lakini mikopo ya kibiashara bado mabenki yanaonekana kususua katika kufikia lengo hilo. Je, Serikali inatoa kauli gani ya kuzitaka benki kushusha riba kwa mikopo ya kibiashara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, mara nydingi tu katika Bunge hili nimekuwa nikisema kwamba kiwango kikubwa cha riba katika benki kinatokana na kiwango cha *T-Bills* ambacho kinapangwa na Serikali *BOT*. Je, Serikali inatoa kauli gani kuwa riba zinazotozwa na *microfinances* ambazo ndiyo kimbilio kubwa la wananchi wa kawaida? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Fedha na Mipango.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Khatib Said Haji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, Serikali kwa nia thabiti kabisa imechukua hatua za kisera na benki zetu za kibiashara kwa kuanza wameanza na mikopo hii ya watumishi. Ni imani yetu kama Serikali benki zitashusha riba kwa wakopaji wote wakiwemo wakopaji wanaokopa kwa ajili ya biashara zao kwa kuzingatia watu hawa wanapatikana wapi na nini wanadhamiria kukifanya. Cha msingi nachotaka kuwaomba wafanyakia kubiashara wetu

ni kuwa na mipango thabiti wakati wanachukua mikopo hii ili kuhakikisha pesa wanazokopa zinaweza kurejeshwa na hivyo kuleta imani kwa benki zetu kwa wafanyabiashara wetu kwamba ni wakopaji wa uhakika na ni imani ya Serikali yetu kwamba riba zitaendelea kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swalı lake la pili, napenda kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba kwa kutambua umuhimu wa wajasiriamali wadogo, kwa kutambua umuhimu wa Watanzania wanaokwenda kukopa katika *microfinances*, Serikali yetu ya Awamu ya Tano ilizindua Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo ya Fedha Desemba, 2017. Dhamira kubwa ya sera hii ni kuhakikisha kwanza tunawatambua wakopeshaji kwenye huduma ndogo za kifedha lakini pia kuhakikisha tunawalinda wakopaji kwenye sekta hii ya huduma ddogo za fedha ili wawe na uhakika wanakopa nini na sheria, taratibu na kanuni za utawala bora ziweze kufuatwa hata kwenye sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali yetu inatambua mchango wa bei ya *T-Bills*. Sasa hivi tumeweza kupunguza bei ya *T-Bills* kwa kiwango kikubwa ili kuhakikisha pia bei ya fedha zinazokopeshwa inakuwa ndogo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Mheshimiwa Munde na Mheshimiwa Lubeleje.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii na nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kujibu vizuri na Serikali kuwa na mkakati mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza *deposit rate*, maana watu wengi hawaweki fedha benki kwa sababu riba ni ndogo sana na riba ya kukopesha ni kubwa sana. Kama mkakati huu ukitekelezwa benki itakuwa na fedha nyingi ya kukopesha kwa riba ndogo. Naomba jibu, je, Serikali ina mkakati gani kuhusu suala hili?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Fedha na Mipango majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyeekiti, napenda kujibu swali moja la nyongeza la mtani wangu, Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyeekiti, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, Serikali inashughulika na Sera ya Sekta ya Fedha na nimeainisha hatua mbalimbali tulizozichukua. Moja katika taratibu zilizopunguzwa ni *statutory minimum reserve rates* za mabenki yetu. Tumeona sasa, kama nilivyosema tangu awali, riba zinapungua na hivyo hata *deposit rate* nayo itaweza kuongezeka ili kuona kwamba Watanzania wanaweza kuweka fedha zao katika benki zetu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Munde.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyeekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, niungane na Mheshimiwa Mbunge aliyeuliza swali la msingi kumpongeza Rais kwa kupigania kupunguza riba kwenye benki, lakini kwenye taasisi ndogo ndogo, kwa mfano *PRIDE*, *FINCA*, Tunakopesha mpaka navyoongea sasa hivi riba inafika asilimia 33. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwadhibiti hawa watu wanaofikisha riba mpaka asilimia 33 na kusababisha akina mama kunyang'anywa vitu vyao kila siku? Maana yake pesa ile sasa inakuwa haizai kazi yake ni kurudisha riba inapofikia miezi sita mama yule anaanza kunyang'anywa vitu vya ndani. Mheshimiwa Waziri ana mkakati gani wa kukomesha tabia ya kufikisha riba asilimia 33?

MWENYEKITI: Sijakuelewa, umesema *FINCA*?

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema *FINCA*, *PRIDE* na taasisi kama hizo.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali moja la nyongeza la dada yangu, Mheshimiwa Munde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, tumepitisha Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo ya Fedha na moja ya malengo yake ni kuhakikisha kunakuwa na uzingatiaji wa kanuni za utawala bora kwenye taasisi zinazotoa huduma kwenye sekta ndogo ya fedha. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Sheria ya Huduma Ndogo ya Fedha iko katika hatua za mwisho na ni imani yangu ndani ya mwaka huu sheria hii itapitishwa ili kuwalinda wakopaji wadogo katika sekta ndogo ya fedha. Naamilini itakuwa ndiyo mkakati wetu na suluhisho la kuwalinda watu wetu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lubeleje.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami naomba niulize swali moja tu. Kwa kuwa benki zote ziko chini ya Wizara ya Fedha na kwa kuwa *CRDB* wameanza kupunguza riba, je, kwa nini benki nyingine zisipunguze riba ili wananchi na wafanyabiashara waweze kupata mikopo kuliko hali ilivyo sasa?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali moja la nyongeza la kaka yangu Mheshimiwa George Lubeleje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwenye jibu langu la msingi na nizipongeze Benki ya *CRDB*, *NMB* na *ABC*, benki zote hizi zimeshusha riba yao kutoka zaidi ya asilimia 20 mpaka asilimia 17. Ni imani ya Serikali kwamba benki zote

zitafuata mwanzo huu mzuri ulioanzwa na benki hizi tatu nilizozitaja kama njia mojawapo ya kuakisi jitihada njema za Serikali ya Awamu ya Awamu ya Tano na Mheshimiwa Rais wetu dhamira yake ya kuhakikisha Watanzania wanapata fedha za mitaji kwa bei iliyo chini kabisa.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea, sasa mtanielewa kidogo, muda wangu si rafiki, msinilaumu. Tunaendelea, Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni anamuuliza swali Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa niaba yake Mheshimiwa Machano.

Na. 346

JKT Kutumika Kuajiri Vijana Nchini

MHE. MACHANO OTHMAN SAID (K.n.y. MHE. USSI SALUM PONDEZA AMJADI) aliuliza:-

Vijana wa Kitanzania wanakabiliwa na tatizo sugu la ukosefu wa ajira na hivyo nguvu kazi kupotea badala ya kutumika kwa uzalishaji:-

(a) Je, Jeshi la Kujenga Taifa lina mpango gani wa kutumia nguvu kazi ya vijana kwa kuanzisha miradi ya kilimo cha kisasa ili kuondoa tatizo la ajira?

(b) Je, ni vijana wangapi wamenufaika na ajira kwa kila mwaka kuitia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)?

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Machano. Majibu, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafunzo ya kijeshi ambayo vijana huyapata kwa muda wa miezi sita, vijana hao pia hujifunza shughuli mbalimbali za uzalishaji mali katika kambi wanazopangiwa baada ya mafunzo ya kijeshi. Shughuli hizo hufanyika ndani ya mwaka mmoja na nusu kati ya miaka miwili ambayo wanajitolea wanapokuwa JKT. Baada ya kumaliza muda huo, tunaamini kwamba vijana wanakuwa wamepata ujuzi ambapo wanaweza kujajiri au hata kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Kujenga Taifa lina mashamba makubwa ya kilimo yanayotumia pembejeo na zana za kisasa za kilimo kama vile mbegu bora, matreksa, mashine za kupandia na mashine za kuvunia (*harvesters*) hutumika. Mashamba hayo hulimwa kama mashamba darasa kwa ajili ya kuwafundishia vijana walioko JKT. JKT hulima mashamba hayo, si kwa lengo la kuajiri vijana, bali kuwapatia ujuzi ambao watautumia baada ya kumaliza muda wa mafunzo ya JKT. Baada ya kumaliza mafunzo wanaweza kuanzisha miradi ya kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafunzo hayo, vijana hupewa mafunzo ya ujasiriamali ikiwa ni pamoja na mafunzo ya ufugaji wa nyama, samaki na nyuki, kupanda na kuvuna miti ya mbao, kuongeza thamani ya mazao ya nafaka na mbegu za mafuta ambayo Wizara ina imani kwamba yatawawezesha vijana hawa kujitegemea kwa kutumia stadi za ufundi, kilimo, mifugo na uvuvi walivyojifunza wakiwa JKT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya vijana walioajiriwa na vyombo vya ulinzi na usalama kuanzia mwaka 2003 hadi 2017 jumla yao ni 42,593. Aidha, idadi ya vijana 3,576 wameajiriwa na SUMAJKT *Guard Ltd*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machano.

MHE. MACHANO OTHMAN SAID: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uzinduzi wa Ukuta wa Mererani ambao Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua, Mheshimiwa Rais aliridhika sana na kazi ambayo imefanywa na Jeshi na kuahidi kwamba vijana 2,500 wa JKT ambao walishiriki katika ujenzi huo waajiriwe na vyombo vya ulinzi vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Je, ni hatua gani ambazo zimefikiwa kuhusu ajira za vijana wale hadi hivi sasa?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu ya swali hilo, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Mwinyi.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Machano Othman Said, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya kuwaajiri vijana walioshughulika katika ujenzi wa Ukuta pale Mererani. Zoezi hilo kwa kweli limeshaanza, polisi wamepokea vibali vya ajira, usaili umeanza na ni mategemeo yetu kwamba vyombo vingine vya ulinzi na usalama watakapokuwa wamepata vibali wataendelea kuwachukua vijana hawa.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini, linaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Masoud.

Na. 347

Fidia kwa Wananchi Waliochukuliwa Ardhi na JWTZ

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM (K.n.y. MHE. ESTHER N. MATIKO) aliuliza:-

Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) limejitwalia maeneo ya wananchi wa Kenyambi na Bugosi kinyume kabisa na sheria baada ya kukaribishwa kwa hifadhi ya muda

kufuatia kukatika kwa mawasiliano kati ya kambi yao iliyopo Kata ya Nyandoto na Tarime Mjini:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali imeshindwa kuwalipa fidia wananchi hao waliochukuliwa ardhi yao na JWTZ tangu mwaka 2007?

(b) Je, ni kwa nini JWTZ wasirudi kwenye kambi yao iliyopo Kata ya Nyandoto yenye eneo kubwa kuliko kuchukua maeneo yaliyo katikati ya makazi?

MWENYEKITI: Ahsante. Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu tafadhali.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuititia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inatambua umuhimu wa kulipa fidia ya ardhi iliyotwaliwa. Uthamini kwa ajili ya fidia kwa wananchi umefanyika tangu mwaka 2013. Ufinyu wa bajeti ya Serikali ndiyo umechelewesha kufanyika kwa malipo ya fidia hiyo. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali kuititia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilitenga shilingi bilioni 20.03 kwa ajili ya ulipaji wa fidia na masuala mengine yanayoendana na upimaji wa maeneo. Naamini fedha hizo zikipatikana, ulipaji wa fidia ya ardhi utafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Nyandoto lipo chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Tarime. Mwaka 1992 Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania lilikabidhi eneo hilo kwa Halmashauri ya Wilaya ambayo imelipangia matumizi mengine.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la kwanza, wananchi wa Kenyambi na Bugosi huko Tarime wameanza kukata tamaa baada ya huo uthamini uliofanyika tangu mwaka 2013, ni miaka mitano sasa. Bajeti iliyotengwa ya mwaka 2017/2018 ni shilingi bilioni 20, je, katika mwaka huu unaoisha fedha hizi kama zikipatikana wananchi wa Kenyambi na Bugosi huko Tarime watalipwa fidia? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, kwa muda mrefu Serikali imekuwa na kawaida wanapochukua maeneo ya wananchi kwa matumizi ya jeshi hawalipi fidia, wanafanya hivyo kwa sababu wananchi hawana cha kufanya. Serikali ituambie, ni kwa nini tangu mwaka 2006 imekuwa ikitoa taarifa ya utekelezaji wa kupima maeneo, kuthamini na kutoa fidia lakini haifanyi hivyo? Ni kwa nini Serikali isifanye utaratibu wa kufanya matembezi ya hisani ili wananchi wapate fidia zao kwa sababu Serikali inaonekana imeshindwa? Nashukuru sana.

MWENYEKITI: Majibu, Waziri wa ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Mwinyi.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba fedha zikipatikana ndiyo kipaumbele kitatolewa kwa wananchi wa eneo hilo tunalolizungumzia kwa sababu tumewapa ahadi muda mrefu, tangu mwaka 2013 uthamini umefanyika. Mheshimiwa Mbunge anayehusika, mwenye jimbo lake, mara nydingi amekuwa akiniuliza na mimi huwa nampa majibu kwamba fedha tukizipata basi kipaumbele kitatolewa kwa eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pilli, kwamba Serikali huwa hailipi fidia, kwa kweli lengo la kulipa fidia lipo, lakini kama mnavyotambua kuna changamoto za kibajeti. Ni mategemeo yetu kwamba fedha hizi zikipatikana kwa kweli tutapunguza maeneo mengisana ambayo yanatudai, kwa sababu hizi shilingi bilioni 20 zikipatikana siyo kwamba tutaweza kufikia maeneo mengi. Ni mategemeo yetu kwamba fedha hizi zitapatikana kama ambavyo Wizara ya Fedha ilishatoa ahadi hapa. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba hakuna sababu ya kufanya matembezi ya hisani katika hili, tutakachofanya ni kuendelea kuhimiza wenzetu wa Wizara ya Fedha wakiweza kupata fungu hili basi watupatie ili na sisi tuweze kutimiza ahadi zetu.

MWENYEKITI: Ahsante. Kwa sababu ya muda tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi na linalekezwa kwa Waziri wa Kilimo.

Na. 348

Ushirika wa Mazao wa Kuweka na Kukopa

MHE. MASHIMBA M. NDAKI aliuliza:-

Serikali imedhamiria kufufua tena Ushirika wa Mazao na Kuweka na Kukopa:-

Je, kwa nini Serikali isiwe inawasilisha Bungeni ukaguzi wa Hesabu za Vyama vyta Ushirika unaofanywa na *COASCO* kila mwaka ili Bunge lipate nafasi ya kuzijadili kama inavyofanyika kwa ripoti za *CAG*?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu, Naibu Waziri, Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mashimba

Mashauri Ndaki, Mbunge wa Jimbo la Maswa Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*) ni shirika la umma lilianzishwa kwa Sheria Na.15 ya mwaka 1982 ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2005 kwa lengo kuu la kufanya ukaguzi wa hesabu za Vyama vya Ushirika Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti ya ukaguzi unaofanywa na Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*) inawasilishwa kwa chama cha ushirika husika na kujadiliwa na wanachama katika Mkutano Mkuu kwa mujibu wa kifungu cha 55(5) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 pamoja na kifungu cha 4(1)(b) cha Sheria ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika Na. 15 ya mwaka 1982 iliyorekebisha mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013, vyama vya ushirika nchini husajiliwa na Mrajisi wa Vyama vya Ushirika. Sheria hii inaelekeza pia kuwa vyama vya ushirika vinapaswa kukaguliwa na *COASCO* au taasisi zingine za ukaguzi zilizoidhinishwa na Mrajisi. Aidha, ukaguzi wa vyama vya ushirika hufanywa pia katika vipindi tofauti kulingana na misimu ya mazao na shughuli za vyama ambapo ripoti za ukaguzi huwasilishwa katika mikutano mikuu ya vyama husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa vyama vya ushirika ni taasisi za kijamii, hivyo ripoti za ukaguzi huwasilishwa katika mikutano mikuu ya vyama husika na kujadiliwa na wanachama wake wenywewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mashimba.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru kwa majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la kwanza, kwa kuwa Bunge lako limechaguliwa na wananchi na wananchi hao ndio wanachama wa Vyama vya Ushirika wa Mazao wa Kuweka na Kukopa, kwa nini Serikali inaona mashaka kuleta taarifa za *COASCO* hapa Bungeni ili zichambuliwe na kujadiliwa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, kama kikwazo ni Sheria ya Ushirika aliyoitaja Mheshimiwa Waziri, nataka kuuliza, ni lini sasa Serikali itailleta sheria hiyo hapa Bungeni ili ifanyiwe marekebisho na hivyo kutoa nafasi ya kujadili hesabu hizi za ushirika za wananchi wetu na ukizingatia Serikali sasa hivi inaweka nguvu nydingi kuufufua ushirika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Kilimo, kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naomba nimjibu Mheshimiwa Ndaki Mashimba maswali yake mawili madogo ya nyongeza kwa pamoja na kwa ufupi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia sana masuala yote ya vyama vya ushirika na amekuwa ni mfuatiliaji mzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama nilivyojibu kwenye majibu yangu ya msingi, kama Serikali tuko katika kufanya mapinduzi ya vyama vya ushirika kwenye kuboresha, kufufua na kuimarisha. Kwa maana hiyo, sote tuelewe kabisa kwamba kila zao lina msimu wake katika kulima na kwa maana hiyo hata katika ukaguzi wa mahesabu unatofautiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo sisi kama Serikali hatupati kigugumizi jambo lake tumelipokea. Kama nilivyosema katika ille jibu langu la msingi, kwenye ile Sheria Na. 6 ya mwaka 2013, kifungu cha (4)(1)(b), tatalichukua jambo hili na tatalifanyia kazi ili tuweze kuleta Bungeni kwa ajili ya kurekebisha hiyo sheria ndogo ili mfumo mzima wa vyama vyaya ushirika na ile dhana nzima ya kuimarisha, kufufua na kuboresha vyama vyaya ushirika iweze kutiliwa mkazo. Nakushukuru.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea kwa sababu ya muda. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Viti Maalum na linaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Desterius Mipata.

Na. 349

Kuwasaidia Wanaoshindwa Kuendelea na Masomo

MHE. DESDERIUS J. MIPATA (K.n.y. MHE. AIDA J. KNENAN) aliuliza:-

Kila mwaka kuna wanafunzi wanaoendelea na masomo (waliofaulu) na waliofeli wengi hubaki nyumbani kwa kukosa fedha na sifa za kuendelea na masomo:-

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwasaidia wanaoshindwa kuendelea na masomo?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu ya Serikali, Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenan, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka Serikali huwapima wanafunzi kupitia Mitihani ya Taifa inayosimamiwa na Baraza la Mitihani la Tanzania (*NECTA*) baada ya kumaliza elimu ya msingi na elimu ya sekondari, ambapo wale waliofaulu huendelea na masomo katika ngazi inayofuata. Kwa wanafunzi ambao hawakufaulu mitihani ya kidato cha nne na cha sita, wanaruhusiwa kufanya tena mitihani kama watahiniwa wa kujitegemea (*Private Candidates*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima viro vituo vinavyotoa masomo ya elimu ya sekondari nje ya mfumo rasmi, kwa kusoma masomo ya kidato cha kwanza na pili kwa mwaka mmoja na kufanya mtihani wa maarifa unaofahamika kama (*Qualifying Test*) na endapo mwanafunzi atafaulu ataruhusiwa kufanya mtihani wa kidato cha nne kama mtahiniwa binafsi. Katika programu hii, walengwa 10,420 wamesajiliwa katika mwaka 2017; kati yao 6,074 ni wanawake na 4,346 ni wanaume. Aidha, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima huandaa na kuendesha programu za elimu mbadala kwa vijana na watu wazima kulingana na mahitaji yao. Programu hizo hutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kama vile ujasiriamali, stadi za maisha, ufundi wa awali na programu za kisomo cha kuijendezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia VETA inatoa mafunzo ya ufundi stadi kulingana na mahitaji ya soko la ajira ambapo jumla ya wanachuo 35,000 wanahitimu kila mwaka katika vyuo 732 viliviyosajiliwa na VETA nchi nzima. Mafunzo wanayopata yanawasaidia wahitimu kuwa na stadi za kuwawezesha kuajiriwa au kujajiri katika sekta rasmi na isyo rasmi. Aidha, Serikali inaendelea kuvii marisha Vyuo 55 vya Maendeleo ya Wananchi (*FDCs*) ili viweze kuongeza wigo wa kudahili wanafunzi katika nyanja mbalimbali za mafunzo na hivyo kutoa fursa zaidi kwa wanafunzi wanaoacha masomo kwenye mfumo rasmi wa elimu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mipata.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza Mkao wa Rukwa hauna chuo chochote cha ufundi cha VETA na Serikali hapa imetuahidi mara nyingi kwamba tutapata chuo hicho. Je, ni lini chuo hicho kitajegwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Chala kinaendesha shughuli zake kwenye majengo ya Kanisa Katoliki na kwa kuwa Kanisa Katoliki wanahitaji majengo yao na wananchi wameanza kuchukua hatua ya kujenga majengo mengine ili kuhamishia huko chuo, je, Serikali iko tayari badala ya kufanya ukarabati kwenye majengo yale yaliyokuwa ya *mission* wahamishie juhudil hizo kwenye wazo hilli la wananchi ambapo wanajenga majengo kwa maana kuhamisha Chuo cha Chala?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa kifupi tu, Naibu Waziri, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Olenasha.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mipata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Mkao wa Rukwa kutokuwa na Chuo cha *VETA*, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba lengo la Serikali ni kujenga vyo vyua *VETA* katika mikoa na wilaya zote. Kwa hiyo, tuna mpango wa kujenga chuo katika Mkao wa Rukwa kama tutakavyofanya katika mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la kuangalia uwezekano wa kuwaunga mkono wananchi katika kujenga chuo wilayani kwake badala ya kutumia kile cha Chala, nafikiri walete maombi Wizarani na sisi tutakaa nao. Kimsingi Wizara tuko tayari kuwaunga mkono wananchi

na wilaya ambazo zenyewe zinaanza kujenga na kuwasaidia hata kwenye miundombinu kadri hali ya fedha itakavyoruhusu.

MWENYEKITI: Ahsante. Swali letu la mwisho kwa leo linaulizwa na Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa, Mbunge wa Ludewa.

Na 350

Kujengwa Bandari na Gati Ziwa Nyasa Wilaya ya Ludewa

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA aliuliza:-

Bandari zilizopo Ziwa Nyasa upande wa Wilaya ya Ludewa zipo mbalimbali kutoka moja hadi nyingine hivyo kusababisha wasafiri kutembea umbali mrefu kupata huduma ya usafiri:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza bandari katika maeneo ya Nkanda, Nsele na Makonde katika Tarafa ya Mwambao?

(b) Je, ni lini zitajengwa gati katika bandari zilizopo Ziwa Nyasa hususani eneo la Wilaya ya Ludewa?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu, Naibu Waziri, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Eng. Nditiye.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa Mngwali, Mbunge wa Ludewa, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuititia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (*TPA*) imepanga kuboresha

na kujenga miundombinu ya bandari na gati mbalimbali katika Ziwa Nyasa. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali kupitia TPA imetenga fedha kwa ajili ya kuendeleza Bandari za Mbamba Bay, Itungi, Kiwira, Ndumbi, Manda, Matema, Liuli na Lupingu-Wilayani Ludewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zabuni za kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na kuandaa nyaraka za zabuni na kumpata mkandarasi atakayejenga bandari na gati hizo ilitangazwa Februari, 2018. Kazi ya Mshauri Mwelekezi tunategemea itakamilika kabla ya mwisho ya mwaka huu 2018 na kazi ya ujenzi tunategemea itaanza mapema mwaka 2019. Ni matumaini yangu kwamba baada ya kuboresha na kujenga bandari na gati hizo, wananchi wa vijiji vya Nkanda, Nsele, Makonde, Yigha katika Tarafa ya Mwambao watakuwa wamesogezwa huduma karibu na vijiji vyao.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ngalawa.

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu hivyo vijiji alivyovitaja nilizunguka naye kuanzia kijiji kimoja mpaka cha mwisho. Kwa hiyo, anaelewa vizuri umbali wa bandari kutoka bandari moja kwenda bandari nyingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, pamoja na azma nzuri ya Serikali ya kujenga gati katika eneo la Wilaya ya Ludewa, Mwambao wa Ziwa Nyasa, je, ni lini hasa hivyo vijiji alivyovitaja kwa maana ya Yigha, Makonde, Nsele, Chanjale, na Nkanda vitapata huduma hiyo ya kupakia na kushusha abiria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa sababu tulikuwa naye Mheshimiwa Naibu Waziri katika ziara ile na ameona malalamiko na usumbufu ambao watu wanaupata. Je, Serikali ina mpango gani kuwasaidia na kuhakikisha kwamba wanaondokana na kero hiyo?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu, Naibu Waziri, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Eng. Nditiye.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Deogratias Ngalawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikiri kwamba nilifanya ziara ya Mwambao wa Ziwa Nyasa, Tarafa ya Mwambao tukiwa na Mheshimiwa Deogratias Ngalawa ambapo nilipata nafasi ya kupitia vijiji vyote alivyovitaja. Nichukue nafasi hii vilevile kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri sana na kubwa anayoifanya kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma ya meli katika eneo lile ambalo lina changamaoto kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mbunge kwamba baada ya mchakato wa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ambao utajumuisha pamoja na mambo mengine kulipa fidia, ambayo nichukue tena nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Deo Ngalawa kwa jinsi anavyoishi vizuri na wananchi wake na wanavyotoa ushikiano kwa TPA, tuna hakika baada ya taratibu hizo ujenzi utaanza mara moja. Nimhakikishie tu kwamba kabla ya Juni, 2019 lazima baadhi gati zitaanza kutumika na wananchi wataanza kupata huduma hiyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Njeza.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niulize swali dogo tu, ni lini ujenzi wa Bandari Kavu utaanza ya Mbeya ambayo ni ya kimkakati kwa ajili ya kuhudumia mizigo ya nchi jirani za Zambia, Malawi na DRC? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu, Naibu Waziri, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Eng. Nditiye.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Njeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tunalo eneo ambalo tumelichukua kupitia Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa ajili ya kuweka Bandari Kavu katika Mkoa wa Mbeya. Sasa hivi utaratibu unaoendelea ni kuhakikisha tunalipa fidia kwa wananchi kwa eneo lile ambalo kwa kweli nikiri kwamba ni la kimkakati kwa ajili ya kuhudumia mizigo ya Zambia, Malawi na hata DRC. Tukishamaliza mchakato wa kulipa fidia kwa wananchi, tutaweka mipaka na kutengeneza ramani kwa ajili ya kutengeneza bandari hiyo kavu ili iweze kutoa huduma hizo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lucy Mayenga.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikipata takribani shilingi bilioni 5 kutohana na meli za nje zinazoingia Tanzania kwa ajili ya kufanya uvuvi mkubwa. Je, Serikali sasa na hasa Wizara hii iko tayari kuanzisha bandari maalum ya uvuvi kwenye Bahari ya Hindi ambayo itakuwa inasaidia meli kubwa kutoka nje zinazokuja kwa ajili ya uvuvi ziweze kufanya kazi ili Serikali iweze kupata faida? Kwa sababu sasa hivi meli hizi kubwa zimekuwa zinapata takribani shilingi bilioni 500 na nchi yetu imekuwa ikipata shilingi bilioni 5 tu. Je, Serikali iko tayari kuchukua wazo hili kuanzisha bandari hiyo ili nchi yetu iweze kufaidika? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tuko tayari kuchukua wazo hilo na tutashirikiana kwa karibu sana na Wizara ya Uvuvi na Mifugo kuhakikisha kwamba wanatuunesha maeneo stahiki kwa ajili ya kujenga bandari hizo.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kipindi chetu cha maswali kimemalizika na maswali yamekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni matangazo, nianze na wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Wageni waliopo Jukwaa la Spika, tunao wageni wa Mheshimiwa Spika, Mbunge wa kutoka Bunge la Uingereza, *The House of Commons*, Bwana Stephen Times na ameambatana na mke wake Willen Stephen. *Is the pleasure to have you with us here.* Pamoja naye anao wafuatao; Mheshimiwa Timoth Ingram ambaye anatoka *Tiffany UK Working Staff* pamoja na Bwana Jastine Nyamoga *Tiffany Country Representative of Tanzania.* Karibuni sana. (*Makof*)

Tunao wageni 40 wa Mheshimiwa Spika ambao ni walimu kumi na wanafunzi 30 kutoka Shule ya Sekondari ya Sagara Kongwa wakiongozwa na mwalimu Imani Matonya. Karibuni sana. (*Makof*)

Tunao wageni 13 wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni wanafunzi wa Shule ya Sendari ya Wasichana ya Askofu Anton Mayala kutoka Kwimba Mkoani Mwanza wakiongozwa na Mwalimu Mkuu Padri Daniel Kadogosa. Karibuni sana wageni wetu. (*Makof*)

Tunao wageni wengine wanne wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni viongozi wa Benki ya NBC wakiongozwa na Ndugu Theobald Sabi, Mkurugenzi Mtendaji. Karibuni sana. (*Makof*)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Angella Kairuki, Waziri wa Madini ambao ni Profesa Simon Msanjila - Katibu Mkuu; Profesa Shukran Manya - Kamishina wa Madini; Jenerali Venance Mabeyo - Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Tanzania; Brigedia Jenerali Charo Yateri - Mkurugenzi Mtendaji wa SUMAJKT; Profesa Florens Luoga - Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania; na Nora Vagnes Traahold - Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkaazi wa *UNDP*nchini. (*Makofi*)

Vilevile wapo Watendaji Wakuu wa Tume ya Madini wakiongozwa na Profesa Idris Kikula - Mwenyekiti wa Tume ya Madini. Profesa karibu sana. Ameongozana na Kanali Sylvester Ghuliku - Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa STAMICO; Ndugu Vicent Willium Pazzia - Mkuu wa Chuo cha Madini na Ndugu Eric Mpesa - Mratibu wa Kituo cha Jemolojia Tanzania. (*Makofi*)

Wapo pia Wakuu wa Mikoa na Wilaya ambao ni Ndugu Alexander Mnyeti - Mkuu wa Mkoa wa Manyara; Ndugu Adam Malima - Mkuu wa Mkoa wa Mara; Ndugu Zainabu Tellack - Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga; Mhandisi Robert Gabriel - Mkuu wa Mkoa wa Geita; Dkt. Kebwe Stephen Kebwe - Mkuu wa Mkoa wa Morogoro; Dkt. Rehema Nchimbi - Mkuu wa Mkoa wa Singida; Ndugu Christina Mndeme - Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma; na Ndugu Zefania Chaula - Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro. Karibuni sana wageni wetu, tunaelewa kwa nini mko hapa, mnatoka kwenye maeneo ambayo sekta hii ya madini ina mchango mkubwa sana kwa nchi yetu. (*Makofi*)

Wengine ni Watendaji wa Taasisi ya Uhamasishaji, Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia wakiongozwa na Kaimu Mwenyekiti wa Bodii, Ndugu Augustina Rutaihwa, hawa ni wa TEITI. (*Makofi*)

Wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri wa Madini ni viongozi na Wanachama wa Chama cha Akiba na Kukopa cha Same (SATESA) wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Omari Mchome. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Doto Biteko, Naibu Waziri wa Madini ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo lake la Bukombe wakiongozwa na Ndugu Charles Likinyiko. Karibuni sana. (*Makofî*)

Tunao wageni wa Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Naibu Waziri wa Madini ambaye ni Mwalimu Stalla Stanslaus Budodi, mama yake mzazi na Mheshimiwa Naibu Waziri. Karibu sana mama yetu. (*Makofî*)

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo siku ya leo; tunao wanafunzi 100 kutoka Chuo cha Madini hapa Dodoma. Karibuni sana. (*Makofî*)

Tunao wanafunzi 30 na walimu watano kutoka Shule ya Sekondari ya Denis kutoka Morogoro. (*Makofî*)

Tunao wanafunzi 60 na walimu 10 kutoka Shule ya Sekondari ya Kisasa. Karibuni sana wanafunzi. (*Makofî*)

Tuna wanafunzi 100 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Kigoma Marwa. Karibuni sana. Wanafunzi wote nawaomba msome kwa bidii, maarifa na nidhamu kubwa na ikiwezekana, ndugu zangu wa Kagera wanasesma someni mpaka nyuma ya *blackboard*, unamaliza kabisa mpaka nyuma ya *blackboard*.

Tunaendelea, tuna wanafunzi 17 wa Mheshimiwa Asha Mshua. Hawa ni wanafunzi waliopo katika Chuo cha Mipango – Dodoma wakiongozwa na Spika wa Bunge la wanafunzi ambaye ni Ndugu Haniff Ally Hassan. Popote mlipo karibuni sana. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo ya wageni lakini kuna tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Anna Lupembe, Mwenyekiti wa Ibada ya Chapel ya Bunge letu. Waheshimiwa Wabunge wa imani ya Kikristo mnatangaziwa kuhudhuria ibada katika Chapel ya Bunge, Ukumbi wa Pius Msekwa, ghorofa ya pili, leo siku ya Alhamisi tarehe 31 Mei, 2018 mara baada ya shughuli za Bunge

kusitishwa saa 7.00 mchana. Aidha, leo kutakuwa na Mtumishi wa Mungu, Askofu Israel Wandamba wa Kanisa la Potters House kutoka Dar es Salaam. Waheshimiwa Wabunge wote Wakristo mnaombwa kuhudhuria na mnakaribishwa.

Tuwatambue wageni wa Wizara hii ya Madini kwa siku ya leo muhimu, tunao pia viongozi kutoka *Tanzania Chamber of Mines, FEMATA* na Makampuni mbalimbali ya madini wawakilishi wao wako hapa. Kama nilivyosema, hii ni sekta muhimu yenye mchango mkubwa, karibuni sana. (*Makofi*)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

MWENYEKITI: Kama sitaki je? (*Kicheko*)

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba, mwongozo.

MHE. ZAYNABU M. VULU: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

MWENYEKITI: Acha wachukue majina basi, taja majina.

MHE. ESTER M. MMASI: Esther Mmasi

MHE. ZAYNABU M. VULU: Zaynabu Matitu Vulu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mmasi.

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7) nikiomba mwongozo wa Kiti chako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati unahitimisha hapo mbele umewaasa vijana hawa waweze kusoma na kuzingatia umuhimu wa masomo wawapo katika shule zao. Hata hivyo, napenda Bunge lako Tukufu hili lisadiki na kuamini kwamba vijana hawa wawapo vyuoni sasa hivi tunaamini kabisa wamefika kukosa ulinzi na wamefika kukosa mazingira tulivu ya wao kuweza kujisomea na kuweza kutimiza azma zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Tanzania kama nchi tumesaini sheria mbalimbali za kumlinda na kumhifadhi mtoto wa kike ili kuondokana na ukatili wa Kijinsia. Rejea Sheria ya *SOSPA* akini pia rejea Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoangalia kwenye *social media* tumeona kuna taharuki kubwa sana mitaani. Wiki mbili zilizopita yuko Mwalimu anayeitwa Mwalimu Ayoub Mlugu wa Shule ya *St. Florence* – Dar es Salaam, ambaye alishtakiwa na walimu wake pamoja na wanafunzi, baada ya kuona taharuki imeenea, walikwenda wakamshtaki Mwalimu huyu kwenye uongozi wa shule. Hata hivyo, katika kuhifadhi taswira ya shule ile, Mwalimu Mkuu wa Shule ile aliagiza taarifa hizi zisitoke katika chombo chochote cha Serikali au wazazi wa wanafunzi hao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa navyoongea Mwalimu Ayoub amewajeruhi kisaikolojia lakini pia inawezekana amewajeruhi kiafya watoto wanaosadikika ni wanne. Nasimama kwa Bunge lako Tukufu hili nikiomba mwongozo

wa Serikali sambamba na mchango wangu wa Bunge liliopita ambapo nilisimama katika Bunge hili na kuwataja walimu waliokuwa na viashiria vya kuwataka wanafunzi kimapenzi. Nilimtaja Kelvin Njunwa wa Chuo cha Uhasibu – Dar es Salaam lakini Wizara baada ya mchango wangu iliagiza na Mwalimu yule akasimamishwa. Napoongea hapa Kelvin Njunwa amenitumia salamu akisema kwamba chuo kimemsafisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa heshima na unyenyekevu katika Bunge lako hili Tukufu nikiomba kauli ya Serikali ni lini tutasimama katika kulinda na kuwahifadhi vijana hawa waweze kusoma kwenye mazingira tulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha na naomba kutoa hoja ijadiliwe.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walismama)

MWENYEKITI: Mimesimama kufanya nini? (*Kicheko*)

WABUNGE FULANI: Kuunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Yeye kaomba mwongozo, ametumia Kanuni ya 68(7). Mheshimiwa Vulu, ni hilo hilo?

MHE. ZAYNABU M. VULU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kukushukuru kwa kunipa nafasi hii lakini na mimi nataka nisimame hapo hapo ambapo mwenzangu alikuwa ameelezea. Mimi kwa masikitiko na majonzi makubwa sana...

MWENYEKITI: Unasimama kwa Kanuni ipi?

MHE. ZAYNABU M. VULU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa sana niliyokuwa nayo mimi pamoja na wazazi wengine wote wanawake na wanaume, nimesimama hapa kutaka kujua ni lini Serikali itachukua hatua kutokana na jambo lililotokea. Mimi hoja yangu iko hivi, kwa kuwa wale ni watoto wadogo na ni watoto wa kike, wameharibiwa kisaikolojia, kikubwa zaidi na ambacho ni kibaya, watoto wale wanakua, wazazi wao wanawategemea watakapomaliza masomo na wao waje wawe na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa picha zinazagaa kwenye mitandao na si kwa tukio hili tu, matukio mengi picha za watoto zimekuwa zinatoka kwenye mitandao na ipo sheria ambayo inawalinda watoto. Je, Serikali inataka kutueleza nini katika suala ambalo watoto hawa picha zao zimezagaa wakati kuna sheria ya *cybercrime*? Ni hatua gani zitachukuliwa kwa yule ambaye ameanza kuchukua picha zile na kuzisambaza kwenye mitandao? Pia yule aliyefanya tendo hili, Serikali ina mkakati gani kwake na wengine wote ambao wanafanya matendo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata mwongozo wako Mheshimiwa Rais na kauli ya Serikali. Samahani ni Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Nimeshtuka kidogo. (*Kicheko*)

MHE. ZAYNABU M. VULU: Mheshimiwa Mwenyekiti, limegusa sana hisia.

MWENYEKITI: Nakuelewa. Nimeombwa miongozo miwili, lakini kama mliviyowasikia Waheshimiwa Wabunge walioniomba miongozo, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) hayo waliyoyasema ni matukio ambayo hayakutokea mapema humu Bungeni. Hata hivyo, kwa vile ni tukio la kusikitisha, kufadhaisha na kuudhi na Serikali na sheria za nchi zipo, nadhani Serikali kama wataweza sasa hivi kulisemea

hili mimi nitawapa fursa ya kufanya hivyo. Kama mnataka muda zaidi mtasema ili mje mpewe fursa hiyo. Mheshimiwa *Chief Whip*.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imesikia kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. Kwa kweli hata sisi kama Serikali jambo hili siyo jambo ambalo linaleta radha kwa namna yoyote ile ni jambo lenye ukakasi mkubwa. Pamoja na ukakasi wake lakini linahitaji kufanyiwa kazi ya kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama Serikali tupewe nafasi ili tuweze kulitazama kwa mapana yake na ikikupendeza Kiti chako kwa muda utakaona unafaa basi Serikali ije kusema hapa ndani ya Bunge jambo hili limechukuliwa hatua gani stahiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo haituzui kama Serikali kuanza kulishughulikia jambo hili kwa haraka. Kwa hiyo, Wizara zinazohusika na jambo hili zimeshaanza kulifanya kazi lakini kwa muktadha wa kulieleza Taifa na Waheshimiwa Wabunge basi tutatumia Kanuni zetu na utaratibu utakaotupangia na Serikali itatoa taarifa rasmi kwenye Bunge lako. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa *undertaking* uliyofanya. Katika wakati muafaka Serikali itapewa nafasi ya kuweza kusema yale ambayo inayo na hatua ambazo inakusudia kuchukua.

Baada ya kusema hayo, kuna tangazo, kuna mgeni wa Mheshimiwa Lubeleje ambaye sikuwa nimeletewa jina wakati natangaza wageni, ni Mheshimiwa Ezekiel Chimombo anatoka Mpwapwa. Karibu sana popote ulipo. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

NDG. LINAH KITOSI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Wizara ya Madini

MWENYEKITI: Ahsante. Mtoa hoja, Waziri wa Madini, Mheshimiwa Angellah Kairuki. (Makofi)

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kuitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu, Mpango na Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018. Aidha, nallomba Bunge lako Tukufu likubali kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana tena. Aidha, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Hotuba ya Bajeti ya Wizara yangu kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nakushukuru kwa kunipa fursa hii adhimu ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu kwa mara ya kwanza Bajeti ya Wizara ya Madini. Kama unavyofahamu, Wizara hii iliundwa Oktoba, 2017 baada ya kuvunjwa kwa iliyo kuwa Wizara ya Nishati na Madini na hivyo kufanya bajeti hii kuwa ndiyo ya kwanza ya Wizara mpya ya Madini. Wizara ya Madini inategemea sana mawazo, ushauri na maelekezo ya Bunge lako Tukufu ili kuimarishe na kukuza Wizara hii mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kunithea kuwa Waziri wa Madini;

Wizara ambayo ni muhimu kwa uchumi wa nchi yetu. Namshukuru pia kwa kunipa Manaibu, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo na Mheshimiwa Doto Biteko. Tunamuahidi Mheshimiwa Rais tutatekeleza maelekezo anayoyatoa kwa ufanisi na uadilifu na tutatekeleza majukumu yetu vyema na tutatumia ujuzi na maarifa yote tuliyopewa na Mwenyezi Mungu na tulijoifunza kusimamia sekta hii ipasavyo ili Taifa letu linufaikie na rasilimali za madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake makini katika usimamizi wa rasilimali za nchi. Sote ni mashahidi wa jinsi uongozi wake unavyogusa wananchi wa Tanzania hususan katika matumizi sahihi ya rasilimali za Taifa katika kuwaleta maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawashukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mama yangu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa miongozo wanayonipatia katika kutekeleza majukumu yangu kikamilifu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hili la usimamizi wa rasilimali katika sekta ya madini ninayoismamia, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Spika, kwa kuunda Kamati ambazo zilishughulikia changamoto zillizopo katika sekta ya madini. Mapendekezo ya Kamati zote yamefanyiwa kazi na baadhi ya mapendekezo yanaendelea kutekelezwa na napenda kuwahakikishia kuwa Wizara yangu itatekeleza mapendekezo yote kama yalivyotolewa na Kamati hizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimpongeze Spika, Mheshimiwa Job Ndugai, Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson na Wenyevit wa Bunge kwa kuendesha Bunge kwa weledi mkubwa, hekima, busara na kwa umahiri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kipekee pia kuwashukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Dunstan Kitandula,

Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri na Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa michango yao mahsus i wakati wa uchambuzi wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 na Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu ya Bunge imetoa maoni mbalimbali na ushauri mzuri unaoboresha utekelezaji wa majukumu yetu na kuhakikisha sekta ya madini inalinufaisha Taifa. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ya Madini itafanya kazi kwa karibu sana na Kamati hii kwa manufaa na masilahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kuwashukuru kwa dhati viongozi wenzangu wa Wizara ya Madini, Mheshimiwa Nyongo na Mheshimiwa Biteko Manaibu wangu pamoja na Profesa Msanjila, Katibu Mkuu. Viongozi hawa na watendaji wote wa Wizara kwa hakika wamekuwa wakinipa ushirikiano wa hali ya juu, ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu na kutekeleza majukumu yao kwa kujituma kwa tija na kwa ufanisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naliahidi Bunge lako kuwa kwa ari na kasi tuliyonayo tutahakikisha kwamba rasilimali za madini zinanufaisha Taifa na mchango wa sekta ya madini unaongezeka katika Pato la Taifa katika maendeleo ya jamii na kupunguza umaskini nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kipekee kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu, familia, ndugu, jamaa na wananchi wa Jimbo la Songea Mjini kwa kuondokewa na mpendwa wao Mheshimiwa Gama na Jimbo la Buyungu Kigoma kwa kuondokewa na mpendwa wao Mheshimiwa Kasuku Bilago.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naomba kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwapongeza Mheshimiwa Janeth Masaburi kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge; Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel;

Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro, Mheshimiwa Monko na Mheshimiwa Maulid Mtulia kwa kuchaguliwa na kuteuliwa kuwa wawakilishi wa wananchi kwenye Bunge hili. Kwa hakika uwakilishi wenu ni kielelezo cha kuaminiwa kuwatumikia wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kipekee kabisa kuchukua nafasi hii kumshukuru kwa dhati ya moyo wangu mume wangu mpenzi, Balozi Mbelwa Kairuki pamoja na watoto wetu Precious Kemilembe, Ester Kokubelwa pamoja na Hyubati Mwesigwa Kairuki. Nawashukuru sana kwa kunivumilia, kuniunga mkono na kuniombea kwa Mwenyezi Mungu ili niweze kutekeleza majukumu niliyopewa na Mheshimiwa Rais ya usimamizi wa sekta hii nyeti ya madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na Hati Idhini Na. 142 ya tarehe 22 Aprili, 2016 iliyofanyiwa marekebisho tarehe 15 Oktoba, 2017, majukumu ya Wizara ya Madini ni kubuni, kuandaa na kusimamia sera, mikakati na mipango ya kuendeleza sekta madini; kusimamia migodi na kuhamasisha shughuli za uchimbaji; kuratibu na kusimamia uongezaji thamani madini kwenye biashara ya madini; kukuza ushiriki wa wazawa kwenye shughuli za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini nchini; kusimamia na kuratibu shughuli na maendeleo ya wachimbaji wadogo; kusimamia taasisi na mamlaka zilizo chini ya Wizara; kuratibu na kusimamia maendeleo na utekelezaji wa majukumu kwa watumishi wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba, katika mwaka wa fedha 2017/2018 iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya Sh.998,337,759,500

kati ya fedha hizo shilingi bilioni 938.6 sawa na asilimia 94 ya bajeti yote ilikuwa ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 59.7 sawa na asilimia 6 ya bajeti yote ilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018, ukiondoa fedha zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za sekta ya nishati, sekta ya madini ambayo sasa inasimamiwa na Wizara ya Madini iliinidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi bilioni 52.4. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 21.7 sawa na asilimia ya 41.53 ya bajeti yote zilikuwa ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 30.6 sawa na asilimia 58.47 ya bajeti yote zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa Wizara na taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida shilingi bilioni 13.9 sawa na asilimia 45.37 zilitengwa kwa matumizi mengineyo na shilingi bilioni 16.7 sawa na asilimia 54.63 zilitengwa kwa ajili ya mishahara. Aidha, Wizara ilipangiwa kukusanya maduhuli ya Serikali ya kiasi cha shilingi bilioni 194.6. Hadi kufikia tarehe 31 Machi mwaka huu, Wizara ilipokea shilingi bilioni 19.1 kutoka Hazina ambayo ni sawa na asilimia 36.56 ya bajeti yote ya Wizara ya shilingi bilioni 52.4 kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kati ya fedha zilizopokelewa Sh.834,976,618 ni fedha za maendeleo sawa na asilimia 3.83 ya bajeti yote ya maendeleo ya shilingi bilioni 21.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi ya kawaida shilingi bilioni 18.3 zilipokelewa ambazo ni sawa na asilimia 59.81 ya fedha zote za matumizi ya kawaida zilizotengwa ambazo zilikuwa ni shilingi bilioni 30.6. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa shilingi bilioni 8.2 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 10.1 ni kwa ajili ya mishahara kwa watumishi wa Wizara na taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ulizingatia pamoja

na mambo mengine Hati Idhini ya kuanzishwa kwa Wizara ya Madini; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015-2020; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano; Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030; Sera ya Madini ya Mwaka 2009; Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na marekebisho yake ya 2017 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2018. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile umezingatia maoni na ushauri wa Kamati Maalum ya Mheshimiwa Rais ya kuchunguza aina, wingi na thamani ya madini mbalimbali yaliyopo kwenye mchanga wa madini au makinikia unaosafirishwa nje ya nchi iliyoongozwa na Profesa Abdulkarim Mruma; Kamati Maalum ya Mheshimiwa Rais ya kuchunguza masuala ya kisheria na kiuchumi kuhusiana na mchanga wa madini unaosafirishwa nje ya nchi iliyoongozwa na Profesa Usoro; Kamati Maalum ya Spika ya Kuchunguza Biashara ya Tanzanite iliyoongozwa na Mheshimiwa Biteko ambaye kwa sasa ni Naibu Waziri wa Madini; Kamati Maalum ya Spika ya Kuchunguza Biashara ya Almasi iliyoongozwa na Mheshimiwa Musa Zungu; na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 maeneo yafuatayo yalipewa kipaumbele: Kuimarisha ukusanyaji mapato ya Serikali; kudhibiti utoroshwaji wa madini; kuendeleza wachimbaji wadogo na wakati wa madini; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani wa madini; kuimarisha usimamizi, ufuutiliaji na ukaguzi wa migodi ikiwemo ukaguzi wa afya, usalama, mazingira na uzalishaji wa madini katika migodi midogo, migodi ya kati na migodi mikubwa; kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya madini na kuboresha sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali kuhusu rasilimali madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kipaumbele kiliwekwa katika kuimarisha taasisi zilizo chini ya Wizara. Maeneo mengine ya kipaumbele yalikuwa ni kuwajengea

uwezo watumishi wa Wizara katika fani mbalimbali na kuendelea kuboresha mazingira ya ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2017, sekta ya madini ilikuwa kwa asilimia 17.5 ikilinganishwa na asilimia 11.5 ya mwaka 2016. Kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji wa sekta ya madini kulitokana na kuimarishwa kwa udhibiti wa biashara haramu na utoroshaji wa madini; kuimarishwa kwa ukaguzi na usimamizi katika sehemu za uzalishaji, biashara ya madini na usafirishaji wa madini nje ya nchi; Kuongezeka kwa viwango vya mrabaha na kuanzishwa kwa ada ya ukaguzi wa madini kufuatia marekebisho ya Sheria ya Madini na Kanuni zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mchango wa sekta ya madini katika Pato la Taifa umeendelea kuimarika ambapo katika mwaka 2017 mchango huo uliflikia asilimia 4.8 na kwa upande wa thamani ya madini ya mauzo nje ya nchi, yalifikia dola za Marekani bilioni 1.8 kwa mwaka 2017. Ni matarajio yetu kuwa thamani ya mauzo itaendelea kuongezeka tena baada ya kukamilisha mageuzi makubwa ambayo tulianzisha ikiwa ni pamoja na uongezaji thamani madini ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwezi Julai, 2017 hadi Machi, 2018 takribani kilo 30,953.59 za dhahabu zilizalishwa na migodi mikubwa na ya katni na kusafirishwa nje ya nchi. Vilevile kilo 221.4 za dhahabu zilizalishwa na wachimbaji wadogo wa madini na wachenjuaji wa marudio. Aidha, kiasi cha karati 248,083.94 za almasi kilizalishwa na Mgodi wa Almasi wa Mwadui uliopo Shinyanga. Pia kiasi cha karati 43,283.31 kilizalishwa katika Mgodi wa *El-hilal* na Tanzanite ghafi yenye kilogramu 535.9 kilizalishwa na Mgodi wa *Tanzanite One*. Vilevile kiasi cha kilo 516,408.93 cha madini mengineyo ya vito nayo kilizalishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa makaa ya mawe, jumla ya tani 385,352 zilizalishwa kwenye Mgodi wa Ngaka, Mkoani Ruvuma. Aidha, tani milioni 3.1 za madini ya

ujenzi na viwandani zilizalishwa. Uzalishaji huu kwa ujumla wake uliwezesha Serikali kukusanya mrabaha wa shilingi bilioni 155.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mageuzi mbalimbali ambayo tumeyafanya Wizara iliratibu mnada wa madini wa vito vya Tanzanite uliofanyika tarehe 18 hadi 21 Desemba, 2017. Katika mnada huo, Tanzanite yenye uzito wa kilo 47 iliweza kuuzwa kwa jumla ya dola za Kimarekani 820,744,000 ambayo ni sawa shilingi bilioni 1.8. Mapato yaliyokusanya na Serikali ni mrahaba wa shilingi milioni 110.3, ada ya ukaguzi ni shilingi milioni 18.3 na ushuru wa huduma shilingi milioni 5.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Madini ilipangiwa kukusanya jumla ya shillingi bilioni 594.6 na Bunge lako Tukufu kutoka kwenye vyanzo mbalimbali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2018 jumla ya maduhuli shillingi bilioni 225 yalikuwa yamekusanya. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 115.59 ya lengo lililowekwa katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kufanya ukaguzi wa uzalishaji wa madini kwenye migodi mbalimbali ili kuhakikisha kwamba Serikali inapata takwimu sahihi za madini yanayozalishwa ndani na nje ya nchi; thamani halisi ya madini hayo; na mrabaha stahiki unaopaswa kulipwa. Kufuatia jitihada hizo, hadi kufikia Machi, 2018, Ofisi yetu ya Madini, Chunya imeweza kukusanya kiasi cha shilingi milioni 718.6 na kwa upande wa Ofisi ya Madini Mwanza iliweza kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 9.8 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi milioni 416 na shilingi bilioni 6.1 zilizokusanya na ofisi hizo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika kudhibiti shughuli za uzalishaji na biashara ya madini ya Tanzanite ambayo hupatikana Tanzania pekee, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, iliweza kujenga ukuta wenye mzingo wa km.24.5 katika migodi ya Merarani

ili kudhibiti utoroshwaji wa madini ya Tanzanite kwenda nje ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Madini ilizuia uingizaji wa madini yanayopatikana nchini kama vile makaa mawe na jasi ili kuhakikisha kwamba madini haya yananunuliwa hapa nchini. Kutokana na udhibiti huo, jumla ya tani 431,029.14 za makaa ya mawe yenyewe thamani ya dola ya Kimarekani 18.3 milioni ziliuzwa hadi kufikia Machi, 2018. Aidha, Wizara imeanza maandalizi ya uanzishwaji wa masoko ya madini ya dhahabu na vito ikiwemo tanzanite, almasi na madini mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha udhibiti dhidi ya utoroshwaji wa madini, Serikali imeendelea na mkakati wa kukabiliana na biashara ya haramu ya madini ambapo Wizara kwa kushirikiana na vyombo vya Ulinzi na Usalama, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na Mamlaka ya Bandari zinaendelea kufanya ukaguzi kupitia madawati yaliyopo katika viwanja vya ndege, bandari na mipaka ya nchi. Aidha, Serikali imekuwa ikiwafikisha wahusika wa matukio hayo katika vyombo vya sheria. Wizara bado inaona kuna changamoto ya utoroshwaji wa madini pamoja na kupungua kwa matukio ya ukamataji kwa watoroshaji wa madini. Azma ya Wizara ni kuimarisha udhibiti kwenye mipaka yote ili hatimaye kuondoa kabisa mianya ya utoroshaji wa madini nchini. Natoa rai na kuwaomba wadau wa sekta ya madini na wananchi wote kushiriki katika ulinzi wa rasilimali madini ili ziweze kuwa na manufaa makubwa zaidi kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba Juni, 2017, Mheshimiwa Spika aliunda Kamati ya Maalum ya Bunge, iliyosughulikia namna shughuli za uchimbaji na uuzaaji wa madini ya Tanzanite unavyofanyika nchini. Kamati hiyo ilitoa mapendekezo mbalimbali ikiwemo kuwepo kwa mfumo mpya wa udhibiti wa madini ya tanzanite.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mapendekezo hayo, tarehe 20 Septemba, 2017, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John Pombe Magufuli aliliagiza Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kujenga ukuta kuzunguka eneo la migodi ya Tanzanite Mererani ili kudhibiti utoroshwaji wa madini hayo. Kufuatia agizo la Mheshimiwa Rais, ukuta huo ulanza kujengwa kuanzia tarehe 1 Novemba, 2017 na kukamilika tarehe 15 Februari, 2018 na kuzinduliwa na Mheshimiwa Rais tarehe 6 Aprili, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na udhibiti huo, katika kipindi kifupi tu cha miezi mitatu cha Januari hadi Machi, 2018 Wizara imefanikiwa kukusanya mrabaha wa kiasi cha jumla ya shilingi milioni 714.6 ambapo katika kiasi hicho shilingi milioni 614 zinatokana na makusanyo kutoka kwa wachimbaji wadogo. Kiasi hicho kilichokusanywa kwa miezi mitatu kinazidi jumla ya makusanyo ya mrabaha wa miaka 3 kwa pamoja iliyopita kutoka kwa wachimbaji wadogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Bunge lako Tukufu litapendezwa kufahamu kwamba katika mwaka 2015 tulikusanya mrabaha wa shilingi milioni 166.8, mwaka 2016 shilingi milioni 71.8 na mwaka 2017 kwa mwaka mzima shilingi milioni 147.1 ukililinganisha na sasa miezi mitatu tu tumepata shilingi milioni 714. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majukumu mengine, Wizara ina wajibu wa kuhakikisha usalama wa shughuli za uchimbaji migodini na ni kwa msingi huo Wizara imeendelea kufanya ukaguzi mbalimbali ambapo kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018, jumla ya leseni 2,204 zilikaguliwa. Wizara pia iliendelea kufanya uchunguzi wa ajali na matukio yanayotokea migodini kwa lengo la kubaini changamoto za kiusalama ili kuweza kuzuia matukio ya aina hiyo katika migodi. Napenda kutoa rai kwa wachimbaji na wawekezaji wote katika sekta ya madini nchini kufuata maelekezo ya kanuni za afya, usalama na utunzaji mazingira zilizopo ili waweze kuwa salama katika shughuli zao za uchimbaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kama ilivyorekebishwa mwaka 2017 na Kanuni zake zinasisitiza umuhimu wa utunzaji wa mazingira. Kama nilivyoleza awali, shughuli za utafiti, uchimbaji na uchenjuaji wa madini zinapaswa kuhakikisha usalama wa watu na mazingira katika maeneo wanayofanyia kazi. Kwa mujibu wa Sheria ya Madini moja ya sharti inayotolewa katika leseni kwa wachimbaji wa madini ni pamoja na kutoa tamko la utunzaji wa mazingira ambapo kwa mchimbaji mdogo hutakiwa kuwasilisha Mpango wa Utunzaji Mazingira au *Environmental Protection Plan* kwa Afisa Mkazi wa Madini. Kwa upande wa mchimbaji wa kati na mkubwa wamiliki hutakiwa kuandaa Tathmini ya Athari za Mazingira na Mpango wa Kutunza Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa matumizi ya baruti kwenye shughuli mbalimbali ziliwemo utafutaji wa mafuta na gesi na uchimbaji wa madini ili kuhakikisha shughuli hizo zinafanyika kwa usalama na madhumuni yaliyokusudiwa uliendelea kufanyika. Wizara itaendelea kuwawezesha wachimbaji wadogo kujajiri kupitia sekta ya madini kwa kuwatambua, kuwaendeleza, kuwarasimisha na kuwapatia maeneo ya uchimbaji wa madini; kuwapatia taarifa za kijiolojia; kuwapatia taarifa za kiufundi; na kuwawezesha kupata huduma za kifedha, masoko, mafunzo ya kiteknolojia na maarifa ya kisasa kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uchimbaji ili nao waweze kukua na waweze kuwa wachimbaji wa kati na wakubwa katika siku za baadaye. Sisi kama Serikali tunaamini uchimbaji mdogo si hadhi ya kudumu bali ni hatua ya mpito tu kuelekea katika uchimbaji wa kati na mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu za kufanya hivyo ziko wazi, kwa kuwa wachimbaji wadogo endapo wataweza kufanikiwa kukua mapato yao yanaweza kuwekezwa zaidi kwenye sekta ya madini na sekta nyingine nchini na hivyo kuchangia zaidi kwenye ukuaji wa sekta ya madini. Pia watachangia katika ukuaji wa pato la Taifa, watachangia katika uchumi na hatimaye pia wataweza kuwanufaisha watanzania wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilikamilisha utafiti wa kina wa kijiosayansi uliohusisha uchorongaji na ukadiriaji wa mbale katika maeneo ya wachimbaji wadogo kwenye maeneo sita ya ujenzi wa Vituo vya Umahiri vya Katente Bukombe, Itumbi, Chunya pamoja na Kona Z Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tutajenga vituo Kapanda (Mpanda), Buhemba (Musoma) pamoja na Kyerwa (Bukoba). Vituo hivyo vitatumika kwa ajili ya mafunzo ya uongezaji thamani madini na uchimbaji salama pamoja na kuongeza uzalishaji, tija na hivyo kuongeza mapato kwa wachimbaji wadogo. Ukadiriaji wa mbale umeonesha kuwepo kwa wakia 47,605 za dhahabu katika maeneo ya Mpanda, wakia 10,737 za dhahabu katika eneo la Buhemba na wakia 46,663 za dhahabu katika eneo la Chunya Itumbi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande kwa Kantente, mbale zimeonesha wakia 9,459 za dhahabu. Maandalizi ya ujenzi wa vituo hivyo yanaendelea. Aidha, matokeo ya utafiti huo yatatumika kuainisha njia bora za uchenjuaji kwenye kila eneo na kuwasaidia wachimbaji wadogo kupunguza upotevu wa madini wakati wa uchenjuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa mgodi wa mfano wa Lwamgasa unaendelea kujengwa ambapo umefikia asilimia 70. Mgodi huu utawezesha Chama cha Washirika wa Kijiji cha Lwamgasa na wachimbaji wanaozunguka mgodi huo kuchimba na kuchenjua dhahabu kwa kutumia teknolojia sahihi na yenyewe gharama nafuu. Vilevile mafunzo mbalimbali yamekuwa yakitolewa kwa wachimbaji wadogo ambaao katika mwaka wa fedha uliopita jumla ya wachimbaji 4,468 walipatiwa mafunzo katika mikoa 13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali chini ya uongozi makini wa Mheshimiwa Rais, imefanya mageuzi makubwa na ya msingi kwenye Sekta ya Madini. Tunalishukuru Bunge lako Tukufu kwa kuridhia na kuitisha marekebisho ya Sheria ya Madini iliyotuwezesha kuweza kufanya utekelezaji wa sheria hiyo, lakini pia kuiwezesha Wizara kutunga Kanuni za Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Madini inamtaka mmiliki wa leseni ya utafutaji na uchimbaji wa madini kuandaa Mpango wa Mwaka wa Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii (*CSR*). Mpango huo ni lazima ukubalike kwa pamoja na Mamlaka ya Serikali ya Mtaa husika au Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kushirikiana au kushauriana na Waziri anayehusika na Serikali za Mitaa na Waziri wa Fedha. Aidha, kila Halmashauri ya Serikali ya Mtaa inapaswa kuandaa Mwongozo wa Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii, kusimamia utekelezaji wa mpango kazi wa uwajibikaji wa kampuni kwa jamii na kutoa elimu kwa umma kuhusu miradi ili yopo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya Sheria ya Madini ya mwaka 2017 yamewezesha kufanyika kwa mabadiliko katika usimamizi wa Sekta ya Madini ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Serikali imeendelea na jitihada mbalimbali za kuhakikisha shughuli za uongezaji thamani madini zinafanyika ndani ya nchi ikiwa ni pamoja na kusimamia ipasavyo zuio la kusafirisha madini ghafi nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia ilitoa matangazo ya kukaribisha uwekezaji katika ujenzi wa vinu vya uchenjuaji kwa ajili ya usafishaji na kuongeza thamani madini ya metalii au *smelters na refinery* hapa nchini. Tumeweza kupokea jumla ya maombi 27 ya uwekezaji kwenye *smelter* na ya *refineries* na uchambuzi hivi sasa unaendelea ili kumpata mwekezaji atakayekidhi vigezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa madini ya vito Wizara imeendelea kukijengea uwezo kituo cha Jimolojia (*TGC*) ili waweze kuimarisha miundombinu yake. Vilevile *TGC* imepata usajili wa kudumu kutoka *NACTE* kwa kutoa mafunzo ya Diploma katika *Gem and Jewellery Technology* ambayo yameanza mwezi oktoba mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia iliingia mkataba na kampuni ya *Center for Development of Gem and Jewellery Technology* kutoka India, kuleta wakufunzi ambao watatoa

mafunzo mbalimbali ya vito na usonara katika kituo hiki cha *TGC* wakishirikiana na wakufunzi wazawa. Aidha, *TGC* imeendelea kutoa mafunzo ya usanifu wa madini ya vito katika ngazi ya Stashahada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha uliopita, kazi zilizotekelezwa kupitia mradi wetu wa *SMMRP* ni pamoja na kupatikana kwa washauri waelekezi kwa ajili ya kusanifu na kusimamia ukarabati na upanuzi wa ofisi saba za madini za mikoa ili viweze kuwa vituo vya umahiri ambavyo ni Bariadi, Bukoba, Chunya, Mpanda, Musoma Tanga pamoja na Songea. Pia kuiwezesha *GST* kufanya utafiti wa kijiolojia kwa ajili ya ukadiriaji wa mbale katika maeneo yanayokusudiwa kuanzishwa vituo vya mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Madini inasimamia jumla ya taasisi sita ambapo mojawapo ni pamoja na Tume ya Madini. Tume yetu ya Madini ilianza kutekeleza majukumu yake tarehe 30 Aprili, 2018. Kazi zilizotekelezwa na Tume ya Madini hadi sasa katika mwezi huo mmoja tangu waweze kuanzishwa ni pamoja na kupitia, kuchambua na kuhakiki maombi ya leseni za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini yaliyowasilishwa na waombaji wa leseni baada ya tarehe 4 Julai, 2017. Maombi yote yanaendelea kuandaliwa leseni husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Tume ilichambua na kuhakiki maombi ya leseni za utafutaji na uchimbaji wa madini yaliyowasilishwa baada ya tarehe 4 Julai, 2017. Aidha, katika uchambuzi wa maombi ya leseni Tume ilibaini kuwepo kwa migogoro minne katika maeneo yaliyoombewa leseni, Taarifa za Upembuzi Yakinifu zisizojitosheleza, kutokuwepo kwa Taarifa za Mpango wa Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii, kutokuwepo kwa Mpango Ushirikishwaji wa Wazawa katika Miradi ya Madini na kutokuwepo kwa Tamko la Kiapo cha Uadilifu (*Integrity Pledge*). Waombaji wote wa leseni ambaao wameonekana wana upungufu wamejulishwa ili waweze kuwasilisha taarifa zinazohitajika kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake *GST* imeweza kupima na kuchora ramani za jiolojia na jiomeria katika mfumo wa *Quarter Degree Sheet* kwa *scale* ya 1:100,000 kwenye maeneo mapya yaliyopo Mahenge na Malinyi. Pia wameweza kufanya ugani wa jiolojia na jiomeria ili kuweza kuboresha ramani mbili za Wilaya ya Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi husika *GST* kwa kushirikiana na *Geological Survey of China* ilifanya utafiti wa kina wa jiomeria katika maeneo ya Mbeya na utafiti wa awali katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Dar es Salaam, Morogoro, Pwani, Tanga, Kilimanjaro, Manyara, Arusha na Mara. Lengo kubwa lilikuwa ni kutafuta madini mbalimbali. Pia *GST* ilikusanya taarifa na sampuli katika maeneo ya Kondoa na Chemba ili kuweza kupata vyanzo vya nishati ya joto ardhi kwa ajili ya maeneo ambayo yako mbali na gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *GST* iliendelea na kazi ya kuratibu majanga asilia ya jiolojia ambapo takwimu kutoka vituo nane vya kudumu vya kupimia matetemeko ya ardhi viko Dodoma, Mbeya, Arusha, Mtwara, Geita, Singida, Babati na Manyara zilikusanywa kuchakatwa na kuhifadhiwa kwenye kanzidata. Kwa kutumia takwimu hizo *GST* iliweza kuainisha maeneo yenye vitovu vya matetemeko ya ardhi na kuboresha ramani inayoonesha maeneo yenye vitovu vya matetemeko ya ardhi na kutoa taarifa hizo kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile *GST* ilifanya utafiti maalum wa kuangalia ubora na wingi wa madini ya *JAS* katika maeneo ya Makanya na Bendera kwa Wilaya ya Same, Wilaya ya Mwanga, Itigi (Manyoni), Msagali (Mpwapwa) na Manda (Chamwino), Mpindiro, Mandawa na Mbaru (Lindi) pamoja na Mkomole (Sumbawanga). Pia katika tafiti nydingi zilizofanywa na wataalam wa jiosayansi ya uchenjuaji zimebainisha kwamba madini mengi yamekuwa yakibaki katika visusu (*tailings*) baada ya kuchenjuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatokana na wachimbaji wadogo kutofahamu tabia tofauti za miamba na mbale hivyo kupelekea kutotumia njia bora za uchenjuaji. Ni vyema

wachimbaji wadogo wakafahamu njia bora za uchenjuaji kwa kufanya majaribio ya sampuli za mbale katika maabara mara kwa mara ili waweze kutambua mtiririko mzuri, aina ya miamba, kiwango cha usagaji, njia pamoja na mbinu za uchenjuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai kwa wachimbaji wadogo endapo hawafahamu tabia za mbale ya sehemu wanayochimba madini kabla ya kuanza uchenjuaji wapeleke sampuli za mbale (*bulk samples*) kwenye maabara zetu za *GSI* ili ziweze kuchunguzwa na waweze kutambua njia bora za uchenjuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Chuo chetu cha *MR*/kimeweza kudahili jumla ya wanafunzi 542 katika mafunzo mbalimbali ya muda mrefu katika fani mbalimbali. Aidha, katika kutoa mafunzo maalum, chuo kimeingia Mkataba wa Makubaliano na Kampuni ya *Acacia* kwa ajili ya kuwafundisha wafanyakazi wake 20 kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia mwezi Januari, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha mafunzo yanayotolewa na Chuo cha Madini yanakidhi matakwa ya mtaala na mfumo wa ufundishaji, Serikali imeboresha Maabara za Jiolojia, lakini pia imeweza kutoa vifaa vya maabara kupitia mradi wa *SMMRP* wenye takriban dola za Kimarekani 500,014.9. Maabara hizi zitakiwezesha Chuo cha *MR* kuweza kutoa mafunzo kwa vitendo na kufanya tafiti mbalimbali. Pia kupitia mradi wa *ISTEP*, Chuo cha *MR* kimepata vifaa vya kisasa vya kusaidia kutoa mafunzo ya vitendo katika fani mpya ya upimaji ardhi na migodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kusaidia wachimbaji wadogo, Chuo chetu cha Madini kina mpango wa kufanya tafiti kuhusu kutengeneza njia mbadala ya uchenjuaji madini ya dhahabu kwa wachimbaji wadogo. Lengo la utafiti huo ni kuweza kusaidia kupatikana kwa njia bora yenye ufanisi wa kuchenjua madini ya dhahabu kwa wachimbaji wadogo nchini na lengo kubwa ni kuondoa matumizi ya kemikali ya

zebaki katika uchenjuaji wa dhahabu kama ambavyo inatakiwa na Mkataba wa Kimataifa wa Minamata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya *STAMICO* ni pamoja na kuwekeza katika shughuli za uchimbaji na utafutaji madini, kuwekeza katika uchenjuaji, uongezaji thamani na uuza ji madini na kutoa huduma na ushauri wa kitaalam na kiufundi katika Sekta ya Madini wakiwemo wachimbaji wadogo katika nyanja ya jiolojia, kihandisi, kimazingira na uchorongaji miamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *STAMICO* pia imeendelea kutekeleza miradi yake mbalimbali kupitia mgodi wa Kabulo, Mradi wa ubia wa *Tanzanite One*, vilevile na mradi wake wa *STAMIGOLD* pamoja na Buhemba. *STAMICO* ilianza kuchimba makaa ya mawe katika kilima cha Kabulo ili kukidhi mahitaji ya mawe hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mgodi wa *Tanzanite One*, migodi ya *Tanzanite* iliyopo Mererani ni pamoja na mgodi uliomilikiwa kwa ubia na *STAMICO* na kampuni ya *TML*. Ipo pia migodi mingine inayomilikiwa na wachimbaji wazawa wenye leseni za uchimbaji mdogo na wa kati. Uendeshaji wa mgodi baina ya *STAMICO* na *TML* wote mnafahamu umekuwa na changamoto nyingi zilizosababishwa na kasoro katika Mkataba wa Ubia na Mkataba wa Uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kutohana na kasoro hizo zilizobainishwa na Kamati Maalum ya Spika ya Kuchunguza Uchimbaji na Biashara ya Madini ya *Tanzanite*, Serikali iliagiza Timu ya Majadiliano ya Serikali kukutana na wamiliki wa *TML* na *STAMICO* ili kujadiliana na kubaini kasoro hizo na kupendekeza namna bora ya uchimbaji, biashara na uendeshaji wa mgodi huo ili kulinufaisha Taifa kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia kwa kukamilika kwa majadiliano hayo, Serikali imeagiza leseni ya uchimbaji wa ubia baina ya *STAMICO* na *TML* irudishwe Serikalini ili

utaratibu mpya uandaliwe utakayoiwezesha Serikali, *TML* na mwekezaji wa kimkakati kushirikiana katika uchimbaji, uendeshaji na biashara ya madini ya *tanzanite* katika mgodi huo kwa kuzingatia sheria yetu ya madini.

Aidha, majadiliano ya wachimbaji wadogo yanaendelea baina ya timu ya majadiliano ya Serikali na wamiliki wa migodi hiyo ili kuleta manufaa zaidi kwa Taifa kutokana na madini ya *tanzanite*. Vilevile kwa kutambua umuhimu na upekee wa madini ya *tanzanite* duniani kwamba yanapatikana Tanzania pekee, Serikali inakamilisha utaratibu wa kuyatangaza madini ya *tanzanite* kuwa madini maalumu au *specified minerals*. Utaratibu wa kuyatangaza utakamilika katika mwaka huu wa fedha wa 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mgodi au mradi wa dhahabu wa Buhemba unahuisha uchenjuaji wa mabaki ya mchanga wa dhahabu na uchimbaji wa dhahabu katika miamba migumu. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, shirika limeendelea na utafiti kwa lengo la kuendelea kubaini kiasi kingine cha mashapo ya dhahabu kilichopo katika miamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mradi wa dhahabu wa *BUCKREEF*, hivi sasa tumeelekeza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na *STAMICO* waweze kuititia mkataba upya wa ubia kutokana na mbia kuchelewa kuanza uzalishaji kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *STAMICO* kwa kushirikiana na mbia mwenza ilifanya tathmni ya maeneo yanayofaa kuachiwa kwa wachimbaji wadogo katika maeneo ya leseni za utafiti Lwamgasa *West*, Nyamalimbe 2, pamoja na Lwamgasa *South 2*. Matokeo ya tathmini hiyo yalibainisha kwamba maeneo hayo yanafaa kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Utaratibu unaandalila ili kuweza kuyaachia maeneo hayo kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika letu la *STAMICO* pia linao mradi wa kokoto wa Urema Zomozi na ilifanya utafiti

katika wingi na ubora wa miamba katika leseni zake 10 na utafiti huo umebaini kuwepo kiasi cha mashapo tani milioni 41.5 za kokoto zinazoweza kuchimbwa kwa zaidi ya miaka 50. Shirika linaendelea kutafuta fedha au mbia kwa ajili ya mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *STAMICO* pia kwa kushirikiana na Wizara imeendelea kusimamia ujenzi wa mgodi wa mfano katika eneo la Lwamgasa utakaowanufaisha wachimbaji wadogo katika eneo hilo ili waweze kujifunza teknolojia sahihi ya uchimbaji na uchenjuaji wa madini. Mgodi wa dhahabu wa Geita ulihusika pia kufanya upembuzi yakikifu katika eneo la mgodi huo wa mfano. Aidha, hadi sasa kupitia mradi wetu wa *SMMRP* umeshatumia takriban dola za Kimarekani 263.8 katika ujenzi wa mgodi huo wa mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania pia kama mnavyofahamu ni mwanachama wa mpango wa uhamasishaji uwazi na uwajibikaji katika rasilimali madini, mafuta na gesi asilia tangu mwaka 2009. Katika kutekeleza mpango huo, Serikali ilianzisha kasi ya uhamasishaji, uwazi na uwajibikaji katika rasilimali mafuta, gesi pamoja na madini ya *TEITI*/yenye jukumu la kuhamasisha Serikali kuweka mifumo ya uwazi na uwajibikaji katia usimamizi wa rasilimali za madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2017/2018 wa fedha *TEITI* ilikamilishwa na kutoa kwa umma ripoti ya ulinganisho wa malipo yaliyolipwa na kampuni za madini, mafuta na gesi na mapato yaliyopokelewa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Tumewasilisha ripoti hiyo kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019, umezingatia dira ya Taifa ya maendeleo 2025, Ilani ya Uchaguzi, Mpango wa Taifa wa Maendeleo pamoja na nyaraka nyingine. Kwa upande wa mwaka ujao wa fedha, kazi zilizopangwa kutekelezwa

kwa mwaka ujao ni pamoja na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali, kuwaendeleza wachimbaji wadogo na wa kati wa madini, kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini, kuimarisha ufuatiliaji na ukaguzi wa usalama wa afya na mazingira, kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika miradi ya kimkakati ya Sekta ya Madini, kuendelea kuboresha mazingira ya kuwawezesha wananchi kufaidika na rasilimali madini, kuelimisha umma na kuboresha mawasiliano kati ya Wizara na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itendelea kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na shughuli za madini ambako kwa mwaka wa fedha 2018/2019, lengo ni kukusanya shilingi bilioni 310.5 ikiwa ni ongezeko la asilimia 59.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali yanayotokana na shughuli za madini, Wizara inatarajia kuimarisha ukaguzi wa migodi ili kupata taarifa sahihi za uwekezaji, uzalishaji, mauzo na kodi mbalimbali, kudhibiti utoroshwaji wa madini katika maeneo ya uzalishaji na kutokea nchini (*exit points*), kuimarisha ukaguzi wa madini ya ujenzi na viwandani, kufuatilia taarifa za ununuvi na uuza kwa wafanyabiashara wa madini, kufuatilia wadaiwa wa tozo mbalimbali za madini kwa mujibu wa sheria, kudhibiti uchimbaji na uchenjuaji haramu wa madini na kuboresha na kuimarisha mfumo wa kutoa leseni za madini na kutunza taarifa zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa rai kwa wamiliki wa leseni za madini kuacha kukwepa au kuchelewa kulipa kodi, kulipa mrabaha stahiki na tozo nyingine zilizopo kwa mujibu wa sheria za nchi. Kwa wale watakaobainika kukiuka matakwa ya kisheria, Serikali itawachukuliwa hatua kali ikiwa ni pamoja na kufuta leseni zao na kuwafikisha Mahakamani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza mpango wa kuendeleza wachimbaji wadogo, Wizara itaendelea

kutenga maeneo yanayofaa ambapo jumla ya maeneo manne yanatarajiwa kutengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *GST* itabainisha uwepo wa mashapo ya madini katika maeneo hayo tutakayotenga, lakini pia Wizara kupitia *STAMICO* itafanya kazi ya kuelimisha wachimbaji wadogo namna ya kutumia teknolojia ya kisasa na rahisi, kuongeza uzalishaji na tija wakati wa uchimbaji na uchenjuaji wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara itaendelea kuhamasisha uwekezaji katika shughuli za uongezaji thamani madini na kuendelea kutoa leseni za uchenjuaji na uyeyushaji wa madini ya metali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara itakamilisha kazi ya kuwapata wawekezaji katika vinu vyta uchenjuaji na usafishaji wa madini. Aidha, Wizara itaandaa Muswada wa Sheria ya Uongezaji thamani madini ili kukuza na kusimamia vyema shughuli za uongezaji thamani madini nchini, uwepo wa viwanda vyta uyeyushaji, usafishaji wa madini na shughuli nyiningine za uongezaji thamani tunatarajia utaongeza mapato ya Serikali, ajira na kukuza matumizi ya teknolojia nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa madini ya vito, Wizara itendelea kukiimarisha Kituo cha *TGC* ili waweze kutoa wataalam wengi zaidi kwenye fani ya ukataji na ung'arishaji wa madini ya vito, jimolojia pamoja na usonara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za uchimbaji wa madini zinapaswa kusimamiwa kwa karibu kwani huweza kuambatana na athari za kiafya, usalama na uharibifu mkubwa wa mazingira. Ili kuondokana na athari hizo, Wizara itaendelea kuimarisha kaguzi migodini na maeneo ya uchenjuaji wa madini, kuongeza huduma za ugani hususan kwa wachimbaji wadogo, kuimarisha ushirikiano na taasisi nyiningine za Serikali zinazohusika na usimamizi wa masuala

ya Afya, Usalama na Mazingira. Pia tutaendelea kukagua na kuhakiki kiasi na ubora wa Madini yanayozalishwa katika migodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai kwa wachimbaji wa madini na wale wanaofanya shughuli za uchenjuaji, hususan madini ya dhahabu kuhakikisha wanaimarisha miundombinu ya mabwawa ya kuhifadhi mabaki yenye kemikali. Pia kwa upande wa wachimbaji wakubwa na wa kati wahakikishe wanawasilisha Mpango wa Ufungaji Migodi kwa wakati. Wachimbaji wakubwa na wa kati wanapaswa pia kuweka hati fungani ya uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya leseni za utafutaji wa uchimbaji wa madini yanapaswa kuambatana na mpango wa matumizi ya bidhaa na huduma za ndani katika maombi ya leseni husika. Iwapo bidhaa hizo hazipatikani ndani ya nchi, bidhaa hizo zinapaswa zipatikane kwa kutumia kampuni za ndani ya nchi iliyoingia ubia na Kampuni ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile mmiliki wa leseni anapaswa kuwasilisha katika Tume ya Madini, taarifa inayoonesha matumizi ya bidhaa na huduma za ndani katika kipindi cha siku 60 baada ya kwisha kwa mwaka wa kalenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia itaendelea kuishirikisha jamii katika shughuli za kiuchumi ambazo jamii inaweza kuzimudu. Sheria ya Madini inamtaka kila mmiliki wa leseni ya uchimbaji wa madini, uchenjuaji, uyeyushaji, usafishaji wa madini, kuandaa mpango wa mwaka wa Uwajibikaji wa Kampuni kwa jamii na kuwasilisha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kuzisihi Halmashauri zetu kuandaa Miongozo ya Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii na kuhakikisha kwamba wanasi mamia utekelezaji wake na kuwa elimisha wananchi katika maeneo yao kuhusiana na mipango ya uwajibikaji wa Kampuni kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai kwa mamlaka nydingine za Serikali hususan Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuziandaa jamii zilizopo katika maeneo ya migodi kushirikiana na Kampuni za Madini ili kufanikisha malengo ya mipango yao. Wizara yangu pia itafanya mikutano ya ana kwa ana na wawekezaji na itatoa pia elimu kwa umma kuhusu rasilimali madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka ujao wa fedha pia tutavutia wawekezaji kwa kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji kwa wadau na tutaandaa jukwaa la wawekezaji katika Sekta ya Madini au *Tanzania Mining Forum*, tutawezesha upatikanaji wa taarifa ya kijiolojia zinazohitajika katika shughuli za utafutaji wa madini na tutashikiriki katika mikutano na warsha za ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tutaweza kuboresha mfumo wetu wa kieletroniki kwa utoaji na usimamizi wa leseni za madini ili kuendana na marekebisho ya Sheria za Madini na kanuni zake. Pia Wizara kuititia Tume ya Madini, itaendelea kushughulikia maombi ya leseni za madini kwa wakati na kuhakikisha kwamba maombi yote yanayowasilishwa yanashughulikiwa na kujibiwa mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Madini kwa kufuta leseni zote zinazokiuwa matakwa ya sheria hiyo ili kutoa nafasi kwa wawekezaji wengine wenye uwezo ya kuyaendeleza na maeneo mengine zaidi kuyatenga kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zilizopangwa kutekelezwa na *SMMRP* ni pamoja na kuanza ukarabati na upanuzi wa majengo ya ofisi saba za madini zitakazotumika kama vituo vya umahiri wa masuala ya madini. Pia tutaendelea kukamilisha ujenzi wa mgodi wa mfano wa Lwamgasa Geita kwa ajili ya wachimbaji wadogo na kusimika mitambo ya uchenjuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kwamba Wizara hii ya Madini ni mpya, katika mwaka ujao wa fedha, Wizara yetu na Taasisi zake inatarajia kuajiri watumishi wapya 314 wa kada mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Tume ya Madini itaendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na rasilimali madini, watatathmini na kushughulikia changamoto katika utekelezaji wa sheria na pia wataweza kushughulikia migogoro mbalimbali na majukumu mengine kama ilivyoainishwa katika sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *GST* wataboresha kanzidata ya miamba na madini ya Taifa ili kuongeza uelewa wa jiolojia ya nchi na upatikanaji wa madini mbalimbali nchini ili kuchochaea uwekezaji katika Sekta ya Madini, kuratibu shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini, kuititia taarifa za robo mwaka za shughuli hizo ili kuweza kuhakiki usahihi wa taarifa hizo na kuboresha kanzidata ya Taifa ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Chuo cha Madini tutaendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi 850, lakini pia tutaendelea kuangalia uwezekano wa kuanzisha kozi nyingine mpya, tutaona namna ya kuwasaidia wachimbaji wadogo, tutaendeleza ujenzi wa miundombinu na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *STAMICO* tumepanga kuendeleza mradi wa dhahabu wa Buhemba kwa kuanza kuchenjua visusu, kufanya uchorongaji ili kujiridhisha na kiasi cha mashapo kilichopo. Pia tutanunua na kusimika vifaa vya uchimbaji na uchenjuaji pamoja na shughuli za uendelezaji wa mradi. Vile vile kuititia *STAMICO* tutaendeleza mradi wetu wa Kiwira kuchimba makaa ya mawe katika Kilima cha Kabulo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakusudia pia kutafuta mtambo wa kusafisha makaa ya mawe katika mradi wa Kabulo, ikiwa ni sambamba na kununua mtambo

wa kusaga makaa (*crusher*) ili yaweze kulingana na vipimo vyatya husika. Pia tunatarajia kuanza mradi wa kuchimba kokoto katika eneo la Ubena Zomozi na tutaendelea kuimarisha shughuli za kibiashara za uchorongaji, kutoa ushauri za utaalal kwa Sekta ya Madini, kuratibu na kuendeleza wachimbaji wadogo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *TEITI*/pamoja na majukumu mengine, tutaanzisha *register* ya taarifa na majina ya watu wanaomiliki hisa katika Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kueleza tu kwamba, tunashukuru sana kwa ushirikiano mkubwa ambao tumeupata kwa washirika mbalimbali wa maendeleo. Kipekee napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana washirika wetu wote wa maendeleo, ikiwa ni pamoja na Benki ya Dunia, Umoja wa Nchi za Ulaya, Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Canada, Marekani, Jamhuri ya Watu wa Korea, Misri, Japan pamoja na Australia. Serikali itaendelea kushirikiana na washirika hao na wadau wengine wa maendeleo katika kuendeleza Sekta ya Madini nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutoa shukurani za kipekee kwa Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) - Taifa, UWT Mkoa wa Dar es Salaam, Viongozi na Wanachama wote wa Chama cha Mapinduzi na UWT kwa kushirikiana nami na kuendelea kuniamini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia Shirikisho la Vyama vyatya Wafanyakazi (*TUCTA*) kwa kuniamini kuwa mwakilishi wao katika Bunge hili; na kwa ushirikiano mkubwa ambao wameendelea kunipatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naendelea kuishukuru kwa mara nyingine tena familia yangu kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tena kuwashukuru kipekee Manaibu Waziri wangu Mheshimiwa Nyongo na Mheshimiwa Biteko kwa ushirikiano wao thabiti katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara. Sikuwepo kwa muda, nilikuwa nimepata mtoto, lakini waliweza kufanya kazi kubwa katika kipindi ambacho sipo na kipekee nawashukuru sana na ni Mwenyezi Mungu ndiye atakayewalipa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawashukuru Katibu Mkuu, Profesa Msanjila; Mwenyekiti wa Tume ya Madini, Profesa Kikula,Makamishna wote wa Tume ya Madini, Kamishna wa Madini, Makamishna Wasaidizi, Wakurugenzi Wakuu wote wa Idara na Vitengo, Viongozi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara wakiwemo Wenyeviti, Wajumbe wa Bodii, Watendaji Wakuu na Watumishi wote kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kipee napenda kulishukuru Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. Chini ya uongozi mahiri wa kaka yangu Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo kwa kujitolea katika ujenzi wa Ukuta wa Mererani na kwa ulinzi ambaao anaendelea kuutoa katika ukuta huo. Kaka yangu tunasema ahsante sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhitimisha napenda kusema yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Madini ni Sekta muhimu katika kukuza uchumi na kutoa mchango mkubwa kwa Taifa na Dira yetu ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025. Aidha, ili kuhakikisha sekta hii inainufaisha nchi hii ipasavyo, Wizara yangu itaimarisha usimamizi wake na kudhitibi utoroshwaji wa madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wizara ya Madini itaendelea kuhamasisha uwekezaji katika shughuli za utafutaji, uchimbaji na uongezaji thamani madini ili kuongeza mchango wa Sekta ya Madini katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Madini, kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018 na Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa wa 2018/2019, naliomba sasa kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, Bunge lako Tukufu likubali na kuidhinisha mapendekezo ya bajeti ya Fungu 100 la Wizara ya Madini lenye jumla ya kiasi cha Sh.58,908,481,992/= kwa ajili ya matumizi ya Wizara na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchanganuo wa maombi hayo ya bajeti ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya maendeleo ni Sh.19,620,994,000/=. Kati ya fedha hizo, Sh.16,800,000,000/= ni fedha za ndani na Sh.2,820,964,000/= ni fedha za nje. Kwa upande wa bajeti ya matumizi ya kawaida ni Sh.39,287,517,158/= ambapo Sh.18,334,255,000/= ni kwa ajili ya mishahara na Sh.20,553,292,992/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo au OC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena nitoe shukurani za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba yetu inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Madini kwa anuani ya www.madini.go.tz. Vilevile hotuba hii ina majedwali kadhaa na vielelezo mbalimbali kwa ajili ya kutoa ufanuzi wa masuala na takwimu muhimu kuhusu Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante hoja imetolewa na imeungwa mkono.

HOTUBA YA WAZIRI WA MADINI, MHE. ANGELAH
JASMINE MBELWA KAIRUKI (MB.), AKIWASILISHA
BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA
WA FEDHA WA 2018/19 – KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

1. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa hoja kwamba, kufuatia Taarifa iliyowasilishwa leo Bungeni na MwenyeKITI wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili, na kuitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu, Mpango na Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18. Aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu likubali kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19.

2. *Mheshimiwa Spika*, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana tena. Aidha, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Hotuba ya Bajeti ya Wizara yangu kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19.

3. *Mheshimiwa Spika*, vilevile, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii adhimu ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu kwa mara ya kwanza Bajeti ya Wizara ya Madini. Kama unavyofahamu Wizara hii iliundwa mwezi Oktoba, 2017 baada ya kuvunjwa kwa iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini, na hivyo kufanya bajeti hii kuwa ndiyo ya kwanza ya Wizara mpya ya Madini. Wizara ya Madini inategemea sana mawazo, ushauri na maelekezo ya Bunge lako Tukufu ili kuimarisha na kukuza Wizara hii mpya.

4. *Mheshimiwa Spika*, namshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kunitfea kuwa Waziri wa Madini; Wizara ambayo ni muhimu kwa uchumi wa Nchi yetu pamoja na

Manaibu wangu, Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo (Mb.), na Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko (Mb.). Tunamuahidi tutatekeleza maelekezo anayoyatao kwa ufanisi na uadilifu na tutatekeleza majukumu yetu vyema na tutatumia ujuzi na maarifa yote tuliyopewa na Mwenyezi Mungu na tuliyojifunza kusimamia Sekta hii ipasavyo ili Taifa letu linufaikie na rasilimali za madini.

5. *Mheshimiwa Spika*, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake makini katika usimamizi wa rasilimali za nchi. Sote ni mashahidi wa jinsi uongozi wake unavyogusa wananchi wa Tanzania hususan katika matumizi sahihi ya rasilimali za Taifa katika kuwaletea maendeleo.

6. *Mheshimiwa Spika*, pia ninawashukuru Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) kwa mlongozo wanayonipatia katika kutekeleza majukumu yangu kikamilifu.

7. *Mheshimiwa Spika*, katika suala hili la usimamizi wa rasilimali za nchi na hususan katika Sekta ya Madini ninayoismamia, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais na wewe binafsi kwa kuunda Kamati ambazo zilishughulikia changamoto zilizopo katika Sekta ya Madini. Mapendekezo ya Kamati zote yamefanyiwa kazi na baadhi ya mapendekezo mengine yanaendelea kutekelezwa. Nawahakikishia kuwa, Wizara yangu itatekeleza mapendekezo yote kama yalivyotolewa na Kamati hizo.

8. *Mheshimiwa Spika*, vilevile, nikupongeze wewe binafsi, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb.), na Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha Bunge kwa weledi mkubwa, hekima, busara na kwa umahiri.

9. *Mheshimiwa Spika*, ninachukua fursa hii pia kuwashukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula (Mb.), Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri

(Mb.) na Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa michango yao mahsus i wakati wa uchambuzi wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 na Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19. Kamati imetoa maoni mbalimbali na ushauri mzuri unaoboresha utekelezaji wa majukumu yetu na kuhakikisha Sekta ya Madini inanufaisha Taifa. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ya Madini itafanya kazi kwa karibu na Kamati hii kwa manufaa na maslahi ya Taifa.

10. *Mheshimiwa Spika*, sina budi kuwashukuru kwa dhati Viongozi wenzangu wa Wizara ya Madini Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo (Mb.), Naibu Waziri, Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri na Profesa Simon Samwel Msanjila, Katibu Mkuu Viongozi hawa na Watendaji wote wa Wizara wanani pa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu na kutekeleza majukumu yao kwa kujituma, tija na ufanisi. Naahidi Bunge lako kuwa kwa ari na kasi tuliyonayo tutahakikisha rasilimali za madini zinanufaisha Taifa na mchango wa Sekta ya Madini unaongezeka katika Pato la Taifa, maendeleo ya jamii na kupunguza umaskini nchini.

11. *Mheshimiwa Spika*, napenda kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu, familia, ndugu, jamaa na wananchi wa jimbo la Songea Mjini kwa kuondokewa na mpendwa wao, Mheshimiwa Leonidas Tutubert Gama (Mb.), na Jimbo la Buyungu, Kigoma kwa kuondokewa na mpendwa wao Mhe. Kasuku Samson Bilago (Mb). Aidha, naomba kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwapongeza Mheshimiwa Janet Masaburi kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge, Mheshimiwa Dkt. Godwin Ole Mollel, Mbunge wa Jimbo la Siha, Mheshimiwa Stephen Lemomo Kiruswa, Mbunge wa Jimbo la Longido, Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini, Mheshimiwa Justin Joseph Monko, Mbunge wa Jimbo la Singida Kaskazini na Mheshimiwa Maulid Said Mtulia, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni, kwa kuchaguliwa na kuwa wawakilishi wa wananchi katika Majimbo hayo. Kuchaguliwa

na kuteuliwa kwao ni kielelezo cha kuaminiwa na wananchi ili kuwawakilisha ipasavyo katika Bunge hili.

12. *Mheshimiwa Spika*, napenda kipekee kabisa kuchukua nafasi hii kumshukuru Mume wangu Mpenzi Balozi Mbelwa Kairuki pamoja na watoto wetu wapendwa kwa kunivumilia, kuniunga mkono na kuniombea kwa Mwenyezi Mungu ili niweze kutekeleza majukumu niliyopewa na Mheshimiwa Rais ya usimamizi wa sekta hii nyeti ya madini.

13. *Mheshimiwa Spika*, baada ya utangulizi huo, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18; na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19.

2.0 DIRA, DHIMA NA MAJUKUMU YA WIZARA

Dira na Dhima ya Wizara

14. *Mheshimiwa Spika*, Dira ya Wizara ni kuwa Wizara inayoheshimika Afrika katika kuendeleza rasilimali za madini ili ziweze kuchangia kwa ufanisi katika uchumi wa Taifa na ustawi wa Watanzania. Aidha, Dhima ya Wizara ni kuzibadili rasilimali za madini ziweze kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa Taifa na maendeleo endelevu.

Majukumu ya Wizara

15. *Mheshimiwa Spika*, kulingana na Hati Idhini (Na.144 ya tarehe 22 Aprili, 2016 iliyofanyiwa marekebisho tarehe 15 Oktoba, 2017, majukumu ya Wizara ya Madini ni:-

(i) Kubuni, kuandaa na kusimamia Sera, Mikakati na Mipango ya kuendeleza Sekta ya Madini;

(ii) Kusimamia migodi na kuhamasisha shughuli za uchimbaji pamoja na utafutaji wa madini kwa kutumia tafiti za kijiofizikia na kijiolojia (*Geophysical na Geological surveys*);

(iii) Kuratibu na kusimamia uongezaji thamani madini kwenye biashara ya madini; kukuza ushiriki wa Wazawa (*local content*) kwenye shughuli za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini nchini;

(iv) Kusimamia na kuratibu shughuli na maendeleo ya wachimbaji wadogo; kusimamia Taasisi na

Mamlaka zilizoko chini ya Wizara; na

(v) Kuratibu na kusimamia maendeleo na utekelezaji wa majukumu kwa watumishi wa Wizara.

3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2017/18

(a) Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18

16. *Mheshimiwa Spika*, itakumbukwa kuwa katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini iliidhinishiwa Bajeti ya jumla ya **shilingi 998,337,759,500**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 938,632,006,000** sawa na **asilimia 94** ya Bajeti yote ilikuwa ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo na **shilingi 59,705,753,500**, sawa na **asilimia 6** ya Bajeti yote ilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

(b) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18

17. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 ukiondoa fedha zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za Sekta ya Nishati, Sekta ya Madini ambayo sasa inasimamiwa na Wizara ya Madini, iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **shilingi 52,445,367,000**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 21,783,000,000** sawa na **asilimia 41.53** ya Bajeti yote zilikuwa ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo na **shilingi 30,662,367,000** sawa na **asilimia 58.47** ya Bajeti yote zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara na Taasisi zake. Kwa upande wa fedha za Matumizi ya Kawaida,

shilingi 13,912,800,000 sawa na **asilimia 45.37** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (O.C) na **shilingi 16,749,567,000** sawa na **asilimia 54.63** zilitengwa kwa ajili ya Mishahara (P.E) ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizopo chini yake. Aidha, Wizara ilipangiwa kukusanya maduhuli ya Serikali ya kiasi cha **shilingi 194,663,501,763.18**.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2018 Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 19,173,608,450.31** kutoka Hazina sawa na asilimia **36.56** ya Bajeti yote ya Wizara ya **Shilingi 52,445,367,000** kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18. Kati ya fedha zilizopokelewa, **Shilingi 834,976,618** ni fedha za Maendeleo sawa na **asilimia 3.83** ya bajeti yote ya Maendeleo ya **Shilingi 21,783,000,000**. Kwa upande wa Matumizi ya Kawaida, **Shilingi 18,338,631,832.31** zilipokelewa sawa na **asilimia 59.81** ya fedha zote za Matumizi ya Kawaida zillizotengwa ambazo zillikuwa Shilingi **30,662,367,000**. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida zillizopokelewa **Shilingi 8,227,481,851** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (O.C) na **Shilingi 10,111,149,981.31** ni kwa ajili ya Mishahara (P.E) kwa watumishi wa Wizara na Taasisi zake.

19. *Mheshimiwa Spika*, utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18, ulizingatia pamoja na mambo mengine: Hati Idhini ya kuanzishwa kwa Wizara ya Madini Namba 144 ya tarehe 22 Aprili, 2016 iliyoanyiwa marekebisho tarehe 15 Oktoba, 2017; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025; Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2015 - 2020; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21); Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; Sera ya Madini ya Mwaka 2009; Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Marekebisho yake ya Mwaka 2017 na Kanuni zake. Vilevile, umezingatia maoni na ushauri wa Kamati Maalum ya Mheshimiwa Rais ya kuchunguza aina, wingi na thamani ya madini mbalimbali yaliyopo kwenye mchanga wa madini (Makinikia) unaosafirishwa nje ya nchi iliyoongozwa na Profesa Abdulkarim Hamis Mruma; Kamati Maalum ya Mheshimiwa Rais ya kuchunguza masuala ya kisheria na kiuchumi kuhusiana na mchanga wa madini unaosafirishwa nje ya nchi

iliyoongozwa na Profesa Nehemiah Eliakim Osoro; Kamati Maalum ya Spika ya kuchunguza Biashara ya Tanzanite iliyoongozwa na Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko (Mb.) ambaye kwa sasa ni Naibu Waziri wa Madini; Kamati Maalum ya Spika ya kuchunguza Biashara ya Almasi iliyoongozwa na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.); na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

20. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18, maeneo yafuatayo yalipewa kipaumbele: kuimarisha ukusanyaji wa Mapato ya Serikali yatokanayo na rasilimali madini; kudhibiti utoroshaji wa madini; kuendeleza wachimbaji wadogo na wa kati wa madini; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; kuimarisha usimamizi, ufuatilaji na ukaguzi wa migodi ikiwemo ukaguzi wa afya, usalama, mazingira na uzalishaji wa madini katika migodi midogo, ya kati na mikubwa; kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini na kuboresha Sera, Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali kuhusu rasilimali madini.

Vilevile, kipaumbele kiliwekwa katika kuimarisha Taasisi zilizo chini ya Wizara hususan Tume ya Madini, Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST), Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Chuo cha Madini (MRI), Kituo cha Jimolojia Tanzania (TGC) na Taasisi ya Uhamasishajji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi asilia (TEITI).

Maeneo mengine ya kipaumbele yalikuwa ni kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara katika fani mbalimbali pamoja na kuendelea kuboresha mazingira ya ofisi.

(c) *Ukuaji na Mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa*

21. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka 2017, Sekta ya Madini ilikua kwa asilimia 17.5 ikilinganishwa na asilimia 11.5 ya Mwaka 2016. Kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji wa Sekta ya Madini kulitokana na kuimarishwa kwa udhibiti wa biashara haramu na utoroshwaji wa madini; kuimarishwa kwa

ukaguzi na usimamizi katika sehemu za uzalishaji, biashara ya madini; na usafirishaji wa madini nje ya nchi; kuongezeka kwa viwango vya mrabaha na kuanzishwa kwa ada ya ukaguzi wa madini kufuatia marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 yaliyofanyika Mwaka 2017 na Kanuni zake.

22. *Mheshimiwa Spika*, vilevile, mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa umeendelea kuimarika ambapo katika Mwaka 2017 mchango huo ulifkia **asilimia 4.8**. Kwa upande wa thamani ya mauzo ya madini nje ya nchi, mauzo yalifkia **Dola za Marekani 1,810,697,000** mwaka 2017. Ni matarajio yetu kuwa thamani ya mauzo itaendelea kuongezeka tena baada ya kukamilisha mageuzi makubwa ambayo tuliyanza ikiwa ni pamoja na uongezaji thamani madini ndani ya nchi.

(d) *Uzalishaji na Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18*

23. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwezi Julai, 2017 hadi Machi, 2018 jumla ya **kilo 30,953.59** za dhahabu zilizalishwa na Migodi Mikubwa na ya Kati ya Bulyanhulu, Buzwagi, Geita, New Luika, North Mara na STAMIGOLD na kusafirishwa nje ya nchi. Vilevile, **kilo 2,021.4** za dhahabu zilizalishwa na wachimbaji wadogo wa madini na wachenjuaji wa marudio. Aidha, kiasi cha **karati 248,083.94** za almasi kilizalishwa katika Mgodi wa Almasi wa Mwadui (Williamson Diamond Limited) uliopo Shinyanga, pia kiasi cha karati **43,285.31** kilizalishwa katika Mgodi wa El Hilal na Tanzanite (ghafi) yenye kilogramu **535.99** ilizalishwa na Mgodi wa TanzaniteOne. Vilevile, kiasi cha **kilo 516,408.93** cha madini mengineyo ya vito kilizalishwa. Kwa upande wa makaa ya mawe jumla ya **tani 385,352** zilizalishwa kwenye Mgodi wa Ngaka Mkoani Ruvuma. Aidha, tani **3,125,399** za madini ya ujenzi na viwandani zilizalishwa. Uzalishaji huu kwa ujumla wake uliwezesha Serikali kukusanya mrabaha wa **Shilingi 175,518,751,221.49**.

24. *Mheshimiwa Spika*, kutokana na mageuzi ambayo tumeyafanya, Wizara iliratibu mnada wa madini ya vito ya

tanzanite uliofanyika tarehe 18 hadi 21 Desemba, 2017. Lengo la mnada huo lilikuwa ni kukuza biashara ya ushindani baina ya wachimbaji na wauzaji wa madini haya na wanunuzi wa kimataifa ili kupata bei bora zaidi na ya ushindani kwa njia ya uwazi na kuwapatia wachimbaji wa madini ya tanzanite soko la uhakika. Katika mnada huo, tanzanite yenye uzito wa **Kilo 47** iliuza kwa jumla ya **Dola za Marekani 820,744** sawa na **shilingi 1,839,476,075**. Mapato yaliyokusanywa na Serikali ni mrabaha wa **shilingi 110,368,564.50**, ada ya ukaguzi **shilingi 18,394,760.75** na ushuru wa huduma wa **shilingi 5,518,428.20**.

25. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maduhuli ya Sekta ya Madini, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Wizara ya Madini, ilipangiwa kukusanya jumla ya **shilingi 194,663,501,763** na Bunge lako Tukufu kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vikiwemo mrabaha; ada ya mwaka; ada za kijiolojia; ada ya uchambuzi wa madini; uchapishaji na uuzaaji wa nyaraka za zabuni; stakabadhi nyinginezo; marejesho ya fedha za Serikali; tozo mbalimbali zinazotokana na adhabu na ada za ukaguzi. Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2018 jumla ya maduhuli ya **shilingi 225,006,324,173.21** yalikuwa yamekusanywa. Kiasi hiki ni sawa na **asilimia 115.59** ya lengo liliowekwa katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18.

26. Mheshimiwa Spika, ongezeko la makusanyo ya maduhuli limetokana na kuongezeka kwa viwango vya mrabaha kutoka asilimia nne hadi sita kwa madini ya metali, na kutoka asilimia tano hadi sita kwa madini ya vito; kuanzishwa kwa tozo ya ukaguzi ya asilimia moja ya mauzo ya madini; usimamizi wa biashara ya madini na kuimarissha udhibiti wa utoroshwaji wa madini kwa kushirikiana na wananchi na Vyombo vya Ulinzi na Usalama.

(e) Udhibiti wa Biashara ya Madini

27. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufanya ukaguzi wa uzalishaji wa madini kwenye migodi mbalimbali ili kuhakikisha kuwa Serikali inapata takwimu sahihi za madini yanayozalishwa na kuuzwa ndani na nje ya nchi;

thamani halisi ya madini hayo; na mrabaha stahiki unaopaswa kulipwa. Uguzi huo hususan kwenye migodi na mitambo ya uchenjuaji umekuwa ukifanyika kwa kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama. Kufuatia jitihada hizo, makusanyo ya mrabaha yameongezeka. Kwa mfano, hadi kufikia mwezi Machi, 2018 Ofisi ya Madini (Chunya) imeweza kukusanya kiasi cha **shilingi 718,667,100.41** na Ofisi ya Madini (Mwanza) kiasi cha **shilingi 9,843,380,762.80** ikilinganishwa na **shilingi 416,968,335.28** na **shilingi 6,181,589,371.75** zilizokusanywa na Ofisi hizo kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17, sawia. Wizara pia imeanzisha utaratibu mpya wa uombaji wa vibali vya kusafirisha madini nje ya nchi, ambapo mchimbaji au mfanyakia shara wa madini hulazimika kuwasilisha sampuli GST kufanyiwa uchunguzi wa kimaabara ili kufahamu ubora stahiki wa sampuli au madini yanayoombewa kibali cha kusafirishwa nje ya nchi. Vilevile, katika kudhibiti shughuli za uzalishaji na biashara ya madini ya tanzanite ambayo hupatikana Tanzania pekee, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ilijenga ukuta wenye mzingo wa kilomita 24.5 katika Migodi ya Mirerani kwa lengo la kudhibiti utoroshwaji wa madini ya tanzanite kwenda nje ya nchi.

28. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Madini ilizua uingizaji wa madini yanayopatikana nchini kama vile makaa ya mawe na jasi ili kuhakikisha madini haya yananunuliwa hapa nchini kwa lengo la kukuza soko la ndani la madini hayo. Kutokana na udhibiti huo, jumla ya **tani 431,029.14** za makaa ya mawe zenye thamani ya **Dola za Marekani 18,314,709.53** ziliuzwa hadi kufikia Machi, 2018 ikilinganishwa na **tani 429,682.85** ziliuzwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 zenye thamani ya **Dola za Marekani 16,931,162.29**. Vilevile, **tani 121,186.82** zajasi zenye thamani ya **Dola za Marekani 3,120,024.09** ziliuzwa kufikia Machi, 2018 ikilinganishwa na **tani 181,080.34** ziliuzwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 zenye thamani ya **Dola za Marekani 5,283,526.13**. Wizara imeanza maandalizi ya uanzishwaji wa masoko ya madini ya dhahabu na vito ikiwemo tanzanite, almasi na madini mengine. Maandalizi haya yanashirikisha Timu ya

Wataalamu na wadau mbalimbali wa biashara ya madini na Serikali.

29. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha udhibiti dhidi ya utoroshwaji wa madini, Serikali imeendelea na mkakati wa kukabiliana na biashara haramu ya madini ambapo Wizara kwa kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) inaendelea kufanya ukaguzi kupitia madawati yaliyopo katika viwanja vya ndege, Bandari na mipaka ya nchi.

Kufuatia kaguzi hizo, jumla ya **matukio 9** ya biashara haramu ya madini yenye thamani ya **Dola za Marekani 229,037.85** na **shilingi 1,500,000,000** yaliri potiwa kutokea katika Vituo vya Kutokea (*Exit Points*) nchini katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Aprili, 2018 ikillinganishwa na **matukio 11** ya biashara haramu ya madini yenye thamani ya **shilingi 268,700,000** yaliyotokea Mwaka wa Fedha wa 2016/17. Aidha, Serikali imekuwa ikiwafikisha wahusika wa matukio hayo katika Vyombo vya Sheria.

Wizara bado inaona kuna changamoto ya utoroshwaji wa madini pamoja na kupungua kwa matukio ya ukamataji kwa watoroshaji madini. Hivyo, azma ya Wizara ni kuimarisha udhibiti kwenye mipaka yote ili hatimaye kuondoa kabisa mianya ya utoroshwaji wa madini nchini.

30. Mheshimiwa Spika, pamoja na uimarishaji huo, bado kuna changamoto mbalimbali katika udhibiti wa shughuli za madini nchini. Hivyo, natoa rai na kuwaomba wadau wote wa Sekta ya Madini na wananchi wote kushiriki katika ulinzi wa rasilimali madini ili ziweze kuwa na manufaa makubwa zaidi kwa Taifa.

(f) Ujenzi wa Ukuta kwenye Migodi ya Mirerani

31. Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa mwezi Juni, 2017 ultiunda Kamati Maalum ya Bunge iliyoshughulikia namna shughuli za uchimbaji na uuzaaji wa madini ya

tanzanite zinavyofanyika nchini. Kamati hiyo ilitoa mapendekezo mbalimbali ikiwemo kuwepo kwa mfumo mpya wa udhibiti wa madini ya tanzanite.

32. *Mheshimiwa Spika*, kutokana na mapendekezo hayo, tarehe 20 Septemba, 2017 **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli** aliliagiza Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kujenga ukuta kuzunguka eneo la migodi ya tanzanite Mirerani ili kudhibiti utoroshwaji wa madini hayo. Kufuatia agizo la Mheshimiwa Rais, Ukuta huo ulianza kujengwa kuanzia tarehe 1 Novemba, 2017 na kukamilika tarehe 15 Februari, 2018 na kuzinduliwa na Mheshimiwa Rais tarehe 6 Aprili, 2018.

33. *Mheshimiwa Spika*, kutokana na udhibiti huo, katika kipindi kfupi cha miezi mitatu tu cha Januari hadi Machi 2018, Wizara imefanikiwa kukusanya mrabaha wa kiasi cha jumla ya **shilingi 714,670,000**. Katika kiasi hicho, **shilingi 614,670,000** zinatokana na makusanyo kutoka kwa wachimbaji wadogo. Kiasi hicho kilichokusanywa kinazidi jumla ya makusanyo ya mrabaha wa miaka mitatu iliyopita kutoka kwa wachimbaji wadogo. Pia, Bunge lako Tukufu litapendezwa kufahamu kwamba katika Mwaka 2015 tulikusanya mrabaha wa **shilingi 166,850,000**; Mwaka 2016 **shilingi 71,860,000**; na Mwaka 2017 **shilingi 147,140,000** kutoka kwa wachimbaji wadogo.

(g) Kuimarisha Usalama Migodini

34. *Mheshimiwa Spika*, pamoja na majukumu mengine Wizara hii ina wajibu wa kuhakikisha usalama wa shughuli za uchimbaji migodini. Kwa msingi huo, Wizara imeendelea kufanya kagazi mbalimbali ambapo kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 jumla ya leseni za **migodi 2,204** zilikaguliwa. Kati ya leseni hizo, **6** ni za uchimbaji mkubwa, **134** za uchimbaji wa katika na **2,064** za uchimbaji mdogo. Wizara pia iliendelea kufanya uchunguzi wa ajali na matukio yanayotokea migodini kwa lengo la kubaini changamoto za kiusalama ili kuweza kuzuia matukio ya aina hiyo katika migodi. Katika

Mwaka wa Fedha wa 2017/18, jumla ya ajali **14** ziliripotiwa na kuchunguzwa katika migodi.

Uchunguzi huo uliofanyika ulibaini kuwa wachimbaji **33 walifariki** dunia; **50 walijeruhiwa**, kutibiwa na kuendelea na kazi zao. Matukio hayo ni kama ifuatavyo: Kanda ya Kati (Singida na Dodoma) matukio **5**; Kanda ya Kaskazini (Arusha, Manyara na Kilimanjaro) matukio **3**; Kanda ya Kusini Magharibi (Mbeya, Songwe na Iringa) matukio **2**; Kanda ya Kati Magharibi (Shinyanga na Tabora) tukio **1**; na Kanda ya Ziwa Victoria Mashariki (Mara na Simiyu) tukio **1**. Uchunguzi wa ajali hizo, ulibaini kuwa chanzo kikubwa cha ajali hizo ni kutozingatia kanuni za usalama. Kufuatia uchunguzi huo, ripoti ziliandaliwa na wahusika walipewa nakala ya ripoti husika ili kuboresha usalama katika maeneo yao na wengine **42** leseni zao zilisimamishwa hadi waliporekebisha na kufuata kanuni za usalama mligodini ambapo jumla ya leseni **38** zilikidhi matakwa ya kiusalama na kuruhusiwa kuendelea na kazi. Mathalan, katika eneo la Irasanilo - Solemba, Buhemba shughuli za uchimbaji zilisimamishwa kwa muda wa mwaka mmoja ili kurekebisha kasoro za kiusalama.

35. Mheshimiwa Spika, kanuni ya 71 ya Kanuni za Afya, Usalama na Utunzaji wa Mazingira za Mwaka 2010 inaelekeza wachimbaji kutoa taarifa ya kusudio la kubadilisha teknolojia yoyote katika shughuli za uchimbaji na uchenjuaji na kuwasilisha taarifa hiyo kwenye Ofisi za Madini. Hata hivyo, kumekuwa na hulka ya wachimbaji kutumia teknolojia ya vifaa mbalimbali katika shughuli za uchimbaji bila kuzingatia uwezo na ubora wa vifaa hivyo. Hali hii inasababisha uwepo wa ajali nyingi ambazo zingeweza kuepukika. Mathalan, ajali iliyotokea tarehe 06 Aprili, 2018 Wilayani Bahi, ilisababishwa na winchi inayotumika kubebea mizigo kutumika kubebea watu. Katika uchunguzi ilibainika kuwa wahusika walikuwa hawafanyi ukaguzi wa kamba mara kwa mara. Timu yangu ya ukaguzi ilipowahoji wahusika walionusurika kwenye ajali hiyo, ilibaini kuwa wahusika hao hawakuwa na taarifa kuhusu uwezo wa winchi husika kunyanya mizigo ila yalikuwa ni mazoea ya kutumia chombo hicho. Natoa rai kwa wachimbaji na wawekezaji wote katika Sekta ya Madini

nchini kufuata maelekezo ya Kanuni za Afya, Usalama na Utunzaji wa Mazingira zilizopo ili wawe salama katika shughuli zao za uchimbaji.

(h) Kuimarisha Masuala ya Afya Migodini

36. Mheshimiwa Spika, ili kupunguza athari za kiafya zinazoweza kuwapata wafanyakazi migodini kutokana na uvutaji wa vumbi na hewa chafu kuzidi kiwango stahiki kwa muda mrefu; ukaaji wa muda mrefu kwenye eneo lenye kelele nyingi; na kutumia vifaa vyenye viwango vya chini kulingana na mahitaji ya eneo husika, Wizara yangu imeimarisha ukaguzi wa mazingira ya kazi migodini pamoja na kuhamasisha uwepo na matumizi ya vifaa kinga. Ikumbukwe pia, utumiaji wa vifaa vya kinga ni sehemu ya kuzuia athari za kiafya.

Kutotumia vifaa vya kinga kunaweza kusababisha matatizo ya kiafya kama kuathiri mfumo wa kupumua au kuambukizana magonjwa kama Kifua Kikuu (*TB*) ikizingatiwa kuwa wanafanya kazi kwenye maeneo yenye changamoto ya ujazo wa hewa. Ukaguzi wa mara kwa mara kuhusiana na utumiaji wa vifaa vya kinga umekuwa ukifanyika migodini. Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inaendelea na utafiti ili kubaini ukubwa wa changamoto ya *TB* migodini na kutoa ushauri wa namna bora ya kujikinga na maradhi hayo.

37. Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu; na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto tunaendelea kuimarisha ukaguzi wakati wa kuajiriwa; na upimaji wa afya mara kwa mara kwa wafanyakazi wote wa migodini. Pia, Wizara inaendelea kuweka utaratibu wa kuchunguza afya wakati mfanyakazi anaacha au kuachishwa kazi. Lengo la kufanya hivyo ni kuhakikisha kuwa shughuli za uchimbaji na uchenjuaji madini zinafanywa kwa kujali afya za wafanyakazi.

(i) Kuimarisha Utunzaji wa Mazingira Migodini na Kwenye Miradi ya Uchenjuaji Madini

38. Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 pamoja na Marekebisho yake ya Mwaka 2017 na Kanuni zake zinasisitiza umuhimu wa utunzaji wa mazingira. Kama nilivyoeleza awali, shughuli za utafiti, uchimbaji na uchenjuaji wa madini zinapaswa kuhakikisha usalama wa watu na mazingira katika maeneo wanayofanyia kazi. Kwa mujibu wa Kifungu cha 60 cha Sheria ya Madini, moja ya masharti ya leseni zitolewazo kwa wachimbaji madini ni kutoa tamko la utunzaji wa mazingira ambapo kwa mchimbaji mdogo hutakiwa kuwasilisha Mpango wa Utunzaji wa Mazingira (*Environmental Protection Plan*) kwa Afisa Madini Mkazi. Kwa upande wa uchimbaji wa kati na mkubwa, wamiliki hutakiwa kuandaa Tathmini ya Athari za Mazingira na Mpango wa Kutunza Mazingira (*Environmental Impact Assessment (EIA) and Environmental Management Plan (EMP)*). Lengo kuu la kuwa na maandiko haya ni kuhakikisha mwenye mradi anatambua kuwa shughuli anazofanya zina athari kwa mazingira na kufahamu maandalizi yake kwenye utunzaji na uhuishaji wa mazingira ili kuwa rafiki kwa matumizi ya binadamu akiwa bado anaendelea kuwekeza au anapomaliza uchimbaji katika eneo husika.

39. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Kanuni ya 177 – 184 za Mwaka 2010 za Uchimbaji Salama, Afya na Utunzaji wa Mazingira zinazoelekeza migodi kuwa na miundombinu muhimu ya kutupa mabaki ya miamba, mabwawa ya kutunzia maji na mabaki yenye kemikali yatokanayo na uchenjuaji wa madini (*Waste Rocks Dumps and Tailings Storage Facilities*). Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara yangu ilimuelekeza mmiliki wa Mgodi wa Dhahabu wa Nyarugusu kulipa fidia kwa waathirika kutokana na bwawa la kuhifadhia maji yenye kemikali zilizotumika kuchenjua madini ya dhahabu kumwaga maji hayo katika mashamba na kuathiri mazao ya wakulima kutokana na mvua kubwa kunyesha ndani ya muda mfupi. Licha ya kulipa fidia kwa waathirika, mmiliki alielekezwa kufanya usanifu

mpya wa bwawa hilo ili liweze kuhimili mvua kubwa pamoja na kuandaa mpango wa dharura wa ukusanyaji maji hayo wakati wa mvua. Pia, Wizara imeendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye maeneo hayo ili kuona uhimilivu wa miundombinu husika.

40. *Mheshimiwa Spika*, hali kadhalika, Wizara yangu imeendelea kuhakikisha kuwa migodi ya madini inapofungwa, mazingira ya eneo husika yanaachwa katika hali ya usalama. Kwa mujibu wa Kanuni ya 206 ya Kanuni za Madini (Usalama wa Afya Mgodini na Utunzaji wa Mazingira) za Mwaka 2010, Migodi ya kati na mikubwa inatakiwa kuwasilisha Mpango wa Ufungaji Migodi (*Mine Closure Plan*). Napenda kulitaarifu Bunge Iako Tukufu kuwa, Kampuni ya ACACIA inayomiliki Migodi ya dhahabu ya North Mara, Bulyanhulu na Buzwagi ilishawasilisha Mpango wake wa Ufungaji Mgodi na kuweka Hati Fungani ya Mazingira. Pia, Mgodi wa Dhahabu wa *Geita Gold Mining Limited (GGM)* uko kwenye hatua za kukamilisha utaratibu wa kuweka Hati Fungani. Vilevile, Migodi ya Dangote, TanzaniteOne, New Luika na Williamson Diamonds nayo inakamilisha majadiliano ili kuhakikisha usalama na utunzaji wa mazingira unazingatiwa.

(j) Usimamizi wa Matumizi ya Baruti

41. *Mheshimiwa Spika*, udhibiti wa matumizi ya baruti kwenye shughuli mbalimbali zikiwemo za utafutaji wa mafuta na gesi na uchimbaji wa madini ili kuhakikisha shughuli hizo zinafanyika kwa usalama na kwa madhumuni yaliyokusudiwa uliendelea kufanyika. Katika ukaguzi uliofanywa na Wizara, ilibainika kuwa jumla ya **tani 22,474** za baruti na **vipande 1,749,203** vya fataki vilitumika kwenye shughuli mbalimbali. Aidha, jumla ya **maghala 37** ya kuhifadhia baruti na fataki yalikaguliwa katika Mikoa yote yenye shughuli za uchimbaji wa madini ili kubaini utunzaji salama kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya Baruti ya Mwaka 1963 na Kanuni zake.

(k) *Uendelezaji wa Wachimbaji Wadogo*

42. Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa Sekta ya Madini inatoa ajira kati ya **500,000** na **1,500,000** kutohana na utafiti uliofanywa na UNEP Mwaka 2012, Wizara itaendelea kuwawezesha wachimbaji wadogo kujajiri kupitia Sekta ya Madini kwa kuwatambua, kuwaendeleza, kuwarasimisha na kuwapatia maeneo ya uchimbaji wa madini. Vilevile, Wizara itaendelea kuwapatia taarifa za kijolojia, kiufundi na kuwawezesha kupata huduma za kifedha na masoko.

Aidha, Wizara itaendelea kuwapatia mafunzo ya teknolojia na maarifa ya kisasa kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uchimbaji ili wakue na waweze kuwa wachimbaji wa kati na wakubwa katika siku za usoni. Serikali inaamini kuwa uchimbaji mdogo siyo hadhi ya kudumu bali ni hatua ya mpito kuelekea katika uchimbaji wa kati hadi mkubwa. Sababu za kufanya hivyo zipo wazi kwa kuwa wachimbaji wadogo endapo watafanikiwa kukua, mapato yao yanaweza kuwekezwa zaidi kwenye Sekta ya Madini na sekta nyingine nchini na hivyo kuchangia zaidi kwenye ukuaji wa Sekta ya Madini, ukuaji wa uchumi na Pato la Taifa na hatimaye kuwanufaisha watanzania wengine.

43. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia GST na STAMICO chini ya Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali Madini (SMMRP) ilikamilisha utafiti wa kina wa kijosayansi uliohusisha uchorongaji na ukadiriaji wa mbale katika maeneo ya wachimbaji wadogo kwenye maeneo sita ya ujenzi wa Vituo vya Umahiri vya Katente (Bukombe), Itumbi (Chunya), Kona Z (Tanga), Kapanda (Mpanda), Buhemba (Musoma) na Kyerwa (Bukoba). Vituo hivyo vitatumika kwa ajili ya mafunzo ya uongezaji thamani madini na uchimbaji salama pamoja na kuongeza uzalishaji, tija na hivyo kuongeza mapato kwa wachimbaji wadogo. Ukadiriaji wa mbale umeonesha kuwepo kwa takriban **wakia 47,605** za dhahabu katika maeneo ya Mpanda (D – Reef na Kapanda); **wakia 10,737.33** za dhahabu katika eneo la Buhemba; **wakia 46,663** za dhahabu eneo la Chunya (Itumbi); na **wakia 9,459** za dhahabu katika eneo la Katente. Aidha, ukadiriaji wa mbale

katika maeneo ya Tanga (Kiomoni, Kange na Mkulumuzi) na Kyerwa (Kaborishoke) umeonesha uwepo wa **tani 403,056,469** za miamba chokaa yenye ubora wa zaidi ya **asilimia 48 ya chokaa (calsium)**; na tani **1,409,742.15** za bati sawia. Maandalizi ya ujenzi wa Vituo hivyo yanaendelea. Aidha, matokeo ya utafiti huo yatatumika kuainisha njia bora za uchenjuaji kwenye kila eneo na kuwasaidia wachimbaji wadogo kupunguza upotevu wa madini wakati wa uchenjuaji.

44. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Mgodi wa Mfano wa Lwamgasa unaendelea kujengwa ambapo kwa sasa umefikia asilimia 70. Gharama za mgodi huo ni **Dola za Marekani 584,800**. Mgodi huu utawezesha Chama cha Washirika wa Kijiji cha Lwamgasa na wachimbaji wanaozunguka Mgodi huo kuchimba na kuchenjua dhahabu kwa kutumia teknolojia sahihi na yenye gharama nafuu.

Vilevile, mafunzo mbalimbali yamekuwa yakitolewa kwa wachimbaji wadogo ambapo kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18. Jumla ya wachimbaji wadogo **4,468** walipatiwa mafunzo katika Mikoa 13 ambayo ni Manyara, Morogoro, Tanga, Pwani, Shinyanga, Geita, Mara, Katavi, Singida, Dar es Salaam, Mbeya, Lindi na Mtwara. Vilevile, STAMICO kwa kushirikiana na *Tanzania Gender Network Program (TGNP)* na *Women in Mining Association (WIMA)* ilitoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo katika eneo la Mwalazi mkoani Morogoro ambapo jumla ya wachimbaji **37** walipatiwa mafunzo kuhusu namna ya kuchakata madini ya *dolomite* kwa kuzingatia matumizi na mahitaji ya soko.

45. Mheshimiwa Spika, mafunzo mengine yalito-lewa na Ofisi ya Madini Mirerani kwa kushirikiana na Wakala wa Usalama Mahali pa Kazi (OSHA) katika eneo la Mirerani; Ofisi ya Madini Geita kwa kushirikiana na OSHA katika Mkao wa Geita; Ofisi ya Madini Shinyanga kwa kushirikiana na OSHA na TRA katika Mkao wa Shinyanga; Ofisi ya Madini Chunya kwa kushirikiana na Kampuni ya PAULSAM katika Wilaya ya Chunya; Ofisi ya Madini Singida kwa kushirikiana na Vyama vya Wachimbaji Wadogo na Shirikisho la Vyama vya

Wachimbaji Madini Tanzania (FEMATA) katika Mkoa wa Singida; Ofisi ya Madini Mpanda katika Wilaya ya Mpanda; Ofisi ya Madini Songea; Ofisi ya Madini Musoma katika Wilaya za Butiama, Tarime na Bunda; Ofisi ya Madini Mtwara katika Mikoa ya Lindi na Mtwara; na Ofisi ya Madini Dar es Salaam katika Mikoa ya Morogoro, Tanga na Pwani. Mafunzo hayo yalihusu usalama na afya mahali pa kazi.

(I) Sera, Sheria na Miongozo mbalimbali kuhusu Rasilimali Madini

46. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Serikali chini ya uongozi makini wa Mheshimiwa Rais, imefanya mageuzi makubwa na ya msingi kwenye Sekta ya Madini. Tunalishukuru Bunge lako Tukufu kwa kuridhia na kupitisha Marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kupitia Marekebisho ya Sheria mbalimbali yaliyofanywa na Sheria ya Marekebisho Na.7 ya Mwaka 2017. Katika kuwezesha utekelezaji wa Sheria hiyo, Wizara ya Madini ilitengeneza Kanuni za Madini zipatazo saba ambazo ni:-

- (i) Kanuni za Madini (Haki Madini) za Mwaka 2018;
- (ii) Kanuni za Madini (Biashara ya Madini na Makinikia) za Mwaka 2018;
- (iii) Kanuni za Madini (Huduma na Bidhaa Madini zinazotolewa na Watanzania) za Mwaka 2018;
- (iv) Kanuni za Madini (Madini Mionzi) za Mwaka 2018;
- (v) Kanuni za Madini (Uongezaji Thamani Madini) za Mwaka 2018;
- (vi) Kanuni za Madini (Utafiti wa Kijiolojia) za Mwaka 2018; na
- (vii) Kanuni za Madini (Ukaguzi na Uchunguzi wa Nyaraka) za Mwaka 2018.

47. Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 105 (1) na (2) cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Marekebisho yake ya Mwaka 2017 kinamtaka mmiliki wa leseni ya utafutaji na uchimbaji wa madini kuandaa Mpango wa Mwaka wa Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii (CSR). Mpango huo lazima ukubalike kwa pamoja na Mamlaka ya Serikali ya Mtaa husika au Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushauriana na Waziri anayehusika na Serikali za Mitaa na Waziri anayehusika na masuala ya fedha. Aidha, Kifungu cha 105(4) kinaitaka kila Halmashauri ya Serikali ya Mtaa kuandaa Mwongozo wa Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii, kusimamia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii na kutoa elimu kwa umma kuhusu miradi iliyopo katika maeneo yao. Hivyo, Wizara ya Madini inawahimiza wadau wote wa Sekta ya Madini wazingatie Sheria ya Madini wanapotekeleza majukumu yao.

(m) Uimarishaji wa Usimamizi wa Sekta ya Madini

48. Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2017 yamewezesha kufanyika kwa mabadiliko katika usimamizi wa Sekta ya Madini ambapo majukumu ya iliyokuwa Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA) na baadhi ya majukumu ya Kamishna wa Madini yamehamishiwa Tume ya Madini. Pia, Ofisi zilizokuwa za Kanda na Ofisi za Maafisa Madini Wakazi zipo chini ya Tume ya Madini. Kutokana na mabadiliko hayo, kila Mkoa utakuwa na Ofisi ya Afisa Madini Mkazi na kila mgodi mkubwa na wa kati utakuwa na Afisa Mgodi Mkazi. Mabadiliko hayo yamelenga kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara hususan kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali; kuondoa muingiliano wa majukumu na kuimarisha usimamizi wa rasilimali madini ili kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

(n) Uongezaji Thamani Madini

49. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na jithhada mbalimbali za kuhakikisha shughuli za uongezaji thamani madini zinafanyika ndani ya nchi ikiwa ni pamoja na kusimamia ipasavyo zuio la kusafirisha madini ghafi nje ya

nchi. Wizara ilitoa matangazo ya kukaribisha uwekezaji katika ujenzi wa vinu vya uchenjuaji kwa ajili ya kusafisha na kuongeza thamani madini ya metali - *smelter* na *refineries* hapa nchini. Jumla ya maombi 27 ya uwekezaji kwenye *smelterna refineries* yaliwasilishwa na uchambuzi unaendelea kufanyika ili kupata mwekezaji atakayekidhi vigezo.

50. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa madini ya vito, Wizara imeendelea kukijengea uwezo Kituo cha Jimolojia Tanzania (TGC) kilichopo Arusha kwa kuimarisha miundombinu yake. Vilevile, Kituo kimepata usajili wa kudumu kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) kwa namba ya usajili REG/SAT/033 wa kutoa mafunzo ya *Diploma in Gem & Jewellery Technology* mwezi Oktoba, 2017. Mafunzo hayo yatakuwa ya muda wa miaka 3 na yanatarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2018.

Katika kuwajengea uwezo wakufunzi wazawa, Wizara iliingia Mkataba na Kampuni ya *Centre for Development of Gem & Jewellery Technology* kutoka nchini India kuleta wakufunzi saba (7) ambao watatoa mafunzo mbalimbali ya vito na usonara katika Kituo hiki wakishirikiana na wakufunzi wazawa. Aidha, Kituo kimeendelea kutoa mafunzo ya usanifu wa madini ya vito (*lapidary*) katika ngazi ya Astashahada ambapo jumla ya wanafunzi wanawake 18 walidahiliwa chini ya ufadhili wa Wizara ya Madini pamoja na Kamati ya maonesho ya Madini ya Vito ya Arusha (*Arusha Gem Fair*).

(o) *Kazi zilizotekelizwa kupitia Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali Madini - SMMRP*

51. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 kazi zilizotekelizwa kupitia Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali Madini (SMMRP) ni pamoja na upatikanaji wa Washauri Waelekezi kwa ajili ya kusanifu na kusimamia ukarabati na upanuzi wa Ofisi 7 za Madini za Mikoa kuwa Vituo vya Umahiri ambazo ni Bariadi, Bukoba (**Tazama Picha Na.1**), Chunya, Mpanda, Musoma, Tanga na Songea. Pia, Mradi uligharimia upatikanaji wa Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya upanuzi wa miundombinu ya Chuo cha Madini

Kampasi ya Dodoma. Michoro ya majengo hayo imekamilika na makadirio ya ghamama za ujenzi yanaendelea kufanyika. Kazi nyingine iliyofanyika ni kusimamia ujenzi wa Mgodi wa Umahiri katika eneo la Lwamgasa - Geita ambaao utagharimu **Dola za Marekani 584,800** kwa ajili ya Wachimbaji Wadogo ambapo ujenzi wa shimo la uchimbaji (*mining shaft*) umefikia asilimia 70 (**Tazama Picha Na.2**); kuiwezesha GST kufanya utafiti wa kijolojia kwa ajili ya ukadiriaji wa mbale katika maeneo yanayokusudiwa kuanzishwa Vituo vya Mfano. Maeneo hayo ni Bukombe (Katente); Chunya (Itumbi); Mpanda (D-Reef na Kapanda); Musoma (Buhemba); Kyerwa (Kyerwa); na Tanga (Kiromoni, Kange na Mkulumuzi). Taarifa ya utekelezaji wa utafiti huo imebainishwa kwa kina katika sehemu ya taarifa ya utekelezaji wa kazi zilizofanywa na Taasisi ya Jiolojia na Utafutaji Madini Tanzania.



Picha Na.1: Picha ya Muonekano wa Ofisi ya Madini itakayojengwa Bukoba.



Picha Na.2: Picha ya Muonekano wa hatua iliyofikiwa katikaujenzi wa Mgodi wa Mfano, Lwamgasa – Geita.

52. *Mheshimiwa Spika*, ili kuboresha mazingira ya kazi na kuimarisha utendaji kazi katika Sekta ya Madini, Mradi ulinunua vifaa mbalimbali vya ofisi ambavyo ni vifaa vya ukaguzi, maabara na kemikali kwa ajili ya Wizara, Taasisi za GST, MRI, TGC na Ofisi za Madini za Mikoa. Vifaa hivyo ni vya kupimia viwango vya madini kwenye sampuli mbalimbali na vya ukaguzi wa migodi. Thamani ya vifaa hivyo ni Dola za Marekani 350,000. Vilevile, Mradi uliwezesha kuandaa Mwongozo wa namna bora ya uchimbaji wa madini kwa wachimbaji wadogo nchini (*Training Manual Handbook*). Mwongozo huo utawasaidia wachimbaji wadogo namna ya kufanya utafiti wa awali; uchimbaji na uchenjuaji endelevu; kuzingatia afya na usalama migodini; utunzaji bora wa mazingira; utunzaji wa kumbukumbu za fedha na ulipaji wa kodi na tozo mbalimbali. Mwongozo huo utakamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2018.

(p) Ajira na Maendeleo ya Watumishi

53. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2017/2018, Wizara imepata Kibali cha Ajira Mpya chenye jumla ya nafasi 16 katika kada za Katibu Mahsus 3, Jiokemia 1, Mjiolojia 1, Wahandisi Migodi 2, Watunza Kumbukumbu Wasaidizi 2, Madereva 6 na Mkutubi Msaidizi 1. Vilevile, katika Ikama ya Watumishi kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara imeidhinishiwa nafasi za ajira mpya 53, kuwapandisha vyeo watumishi 196, kubadilisha kada watumishi 7 na nafasi za uteuzi 3. Aidha, katika Ikama ya Watumishi kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18, STAMICO iliidhinishiwa nafasi 36 za kuwapandisha vyeo watumishi. Pia, GST imeidhinishiwa nafasi 36 za kuwapandisha vyeo watumishi, kuwabdalilisha kada watumishi 3 na nafasi 6 za uteuzi.

54. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake 44 katika fani mbalimbali ikiwemo Jiolojia na Utafutaji wa Madini; upimaji

wa ardhi (jomatikia); Sayansi ya Mazingira; Uhasibu; Utawala; Sera za Uchumi; Takwimu na Uhazili. Kati ya hao, watumishi 40 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu katika ngazi za Stashahada, Shahada na Shahada za Uzamili. Watumishi 4 walipata mafunzo ya muda mfupi kuhusu utafiti wa kijolojia na usimamizi wa rasilimali madini yaliyofanyika nchini China.

55. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kutoa huduma ya lishe, chakula na malipo ya dawa zilizo nje ya orodha ya dawa zinazogharamiwa na Bima ya Afya kwa watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI na UKIMWI, ikiwa ni utekelezaji wa Waraka wa Watumishi wa Umma Namba 2 wa Mwaka 2006 na Mwongozo wa Kudhibiti UKIMWI Katika Utumishi wa Umma wa Mwaka 2007.

KAZI ZILIZOTEKELEZWA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

56. *Mheshimiwa Spika*, Wizara ya Madini inasimamia jumla ya Taasisi 6. Taasisi hizo ni Tume ya Madini, Taasisi ya Jiolojia na Utafiti Madini Tanzania, Shirika la Madini la Taifa, Chuo cha Madini, Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia na Kituo cha Jimolojia Tanzania.

(a) *Tume ya Madini*

57. *Mheshimiwa Spika*, Tume ya Madini imeundwa kwa mujibu wa Kifungu cha 21 cha Sheria ya (Marekebisho ya Sheria mbalimbali) ya Mwaka 2017 iliyorekebisha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, na ilianza kutekeleza majukumu yake tarehe 30 Aprili, 2018. Kazi zilizotekelezwa na Tume ni pamoja na kupitia, kuchambua na kuhakiki maombi ya leseni za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini yaliyowasilishwa na waombaji wa leseni baada ya tarehe 4 Julai, 2017. Uhakiki uliofanywa na Tume umebaini kuwepo kwa jumla ya maombi **4,394** ya Leseni za Uchimbaji Mdogo (PML) yaliyokuwa yamependekezwa kupewa leseni. Pia, kulikuwa na maombi **549** ya leseni za biashara ya madini yaliyokidhi vigezo vya kupewa leseni hizo. Maombi hayo yote yanaendelea kuandaliwa leseni husika.

58. Mheshimiwa Spika, vilevile, Tume ilichambua na ilihakiki maombi ya leseni za utafutaji na uchimbaji wa kati wa madini yaliyowasilishwa baada ya tarehe 4 Julai, 2017. Uhakiki huo ulibaini uwepo wa jumla ya **maombi 150** ya leseni za utafutaji wa madini na **15** za uchimbaji wa kati za madini. Aidha, uchambuzi wa maombi ya leseni ulibaini kuwepo kwa migogoro **4** katika maeneo yaliyoombewa leseni; taarifa za upembuzi yakinifu zisizojitosheleza; kutokuwepo kwa taarifa za Mpango wa Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii katika kutoa huduma (*Corporate Social Responsibility – CSR*); kutokuwepo kwa Mpango wa Ushirikishwaji wa Wazawa katika miradi ya madini (*Local Content Plan*); na kutokuwepo kwa tamko la kiapo cha uadilifu – “*Integrity Pledge*”. Waombaji wa leseni wamejulishwa kupitia Vyombo vya Habari kuhusu mapungufu hayo ili wawasilishe taarifa hizo zinazohitajika kwa mujibu wa Sheria.

(b) *Taasisi ya Jiolojia na Utafiti Madini Tanzania – (GST)*

59. Mheshimiwa Spika, majukumu ya msingi ya Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania ni:-

(i) kukusanya, kuchambua, kutafsiri na kutunza takwimu na taarifa mbalimbali za jiosayansi (jiolojia, jiomchemia na jiofizikia) na za upatikanaji madini;

(ii) kutengeneza na kusambaza ramani mbalimbali za jiosayansi; kufanya uchunguzi wa maabara kwa sampuli mbalimbali za miamba, madini, maji, mimea na udongo kwa ajili ya tafiti mbalimbali;

(iii) kutoa idhini ya maandishi kwa sampuli za miamba, udongo na sampuli zilizo katika hali ya vimiminika kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi;

(iv) kusaidia wachimbaji wadogo hasa katika kubaini umbile na aina ya mbale, kutambua aina na ubora wa madini pamoja na namna bora ya uchenjuaji;

- (v) kuratibu majanga asilia ya jiolojia (kama vile matetemeko ya ardhi, milipuko ya volkano, maporomoko ya ardhi) na kutoa ushauri wa namna bora ya kujikinga;
- (vi) kuboresha kanzidata ya Taifa ya jiosayansi na madini;
- (vii) kufanya tafiti maalum za jiosayansi;
- (viii) kufanya tafiti za jioteknolojia na kutoa ushauri unaostahili katika masuala ya ujenzi wa miundombinu na makazi; na
- (ix) kutoa ushauri wa jiosayansi na utafutaji madini kwa wadau.

60. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, GST ilipanga kukusanya maduhuli ya **Shilingi 350,000,000** kutoka kwenye vyanzo vyake mbalimbali. Vyanzo hivyo ni ada ya ushauri elekezi, tozo za ramani au machapisho ya jiosayansi na tozo za huduma za maabara. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2018 GST ilikuwa imekusanya jumla ya **shilingi 294,700,000**. Kiasi hiki ni sawa na **asilimia 84.2** ya lengo ililowekewa kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18.

61. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, GST imepima na kuchora ramani za jiolojia na jioskemia za mfumo wa QDS kwa skeli ya 1:100,000 kwenye maeneo mapya (QDSs 264, 265) yaliyoko Wilaya ya Mahenge na Malinyi; na kufanya ugani (*field checks*) wa jiolojia na jioskemia ili kuboresha ramani 2 za QDS 64 na 65 za Wilaya ya Shinyanga. Vilevile, kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo, GST ilifanya tafiti mbalimbali za jiosayansi. Katika kipindi husika, GST kwa kushirikiana na **Geological Survey of China** ilifanya utafiti wa kina wa jioskemia katika maeneo ya Mbeya (QDS 244 na 245) na utafiti wa awali (*Regional Scale Surveys*) katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Dar- es-Salaam na Morogoro (**Tazama Picha Na.3**), Pwani, Tanga, Kilimanjaro, Manyara, Arusha na Mara kwa lengo la kutafuta madini mbalimbali. Kwa ufadhilli wa Serikali ya Marekani, GST ilikusanya taarifa na sampuli

katika maeneo ya Wilaya za Kondoza na Chemba ili kupata vyanzo vya nishati ya joto ardhi kwa ajili ya maeneo ambayo yako mbali na gridi ya Taifa.

62. *Mheshimiwa Spika*, vilevile, GST na Serikali ya Jamhuri ya Korea Kusini ilisaini Hati ya Makubaliano kwa ajili ya kufanya utafiti kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya kuainisha maeneo yenye uwepo wa madini kwenye maeneo ya Tunduma na Mtwara (QDS 257, 312, 313, 319, 320) yanayopakana na Zambia na Malawi. Aidha, GST ilitengeneza ramani mbalimbali za jiosayansi na kuzisambaza kwa wadau mbalimbali kwa lengo la kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini pamoja na matumizi mengine.



Picha Na. 3: Wataalam wa GST wakiendelea na kazi za Utafiti wa Jiolojia Mahenge.

63. *Mheshimiwa Spika*, GST iliendelea kuboresha huduma za maabara ambapo mfumo wa kompyuta kwa ajili ya kuratibu uchunguzi wa sampuli kwenye maabara uliandaliwa na kusimikwa (*Laboratory Information Management System - LIMS*). Pia, GST imeendelea kutengeneza *Internal Reference Standards* za *limestone*, *phosphate* na dhahabu. Vilevile, GST ilifanya uchunguzi wa kemia, petrolojia, minerolojia, uchenjuaji madini na jioteknolojia kwenye **sampuli 13,633** za miamba choronge, udongo na madini.

Pia, vyungu (*cupels*) **4,558** na *crucibles* **4,626** vilitengenezwa kwa ajili ya kutumika kuyeyushia sampuli za dhahabu ambapo hapo awali vilikuwa vinanunuliwa nje ya nchi kwa gharama kubwa. Vilevile, GST ilifanya uchunguzi

wa kimaabara wa jumla ya **sampuli 361** za udongo, madini na miamba na taarifa zake ziliandaliwa ambapo ziliwasaidia wateja kupata vibali (*export permits*) vya kusafirisha sampuli nje ya nchi kwa uchunguzi zaidi.



Picha Na. 4: Wataalam wa GST wakifanya utafiti wa kina wa madini katika eneo la Itumbi – Chunya.

63. Mheshimiwa Spika, GST iliendelea kuboresha huduma za maabara ambapo mfumo wa kompyuta kwa ajili ya kuratibu uchunguzi wa sampuli kwenye maabara uliandaliwa na kusimikwa (*Laboratory Information Management System - LIMS*). Pia, GST imeendelea kutengeneza *Internal Reference Standards* za *limestone*, *phosphate* na dhahabu. Vilevile, GST ilifanya uchunguzi wa kemia, petrolojia, mineralojia, uchenjuaji madini na jioteknolojia kwenye **sampuli 13,633** za miamba choronge, udongo na madini. Pia, vyungu (*cupels*) **4,558** na *crucibles* **4,626** vilitengenezwa kwa ajili ya kutumika kuyeyushia sampuli za dhahabu ambapo hapo awali vilikuwa vinanunuliwa nje ya nchi kwa gharama kubwa. Vilevile, GST ilifanya uchunguzi wa kimaabara wa jumla ya **sampuli 361** za udongo, madini na miamba na taarifa zake ziliandaliwa ambapo ziliwasaidia wateja kupata vibali (*export permits*) vya kusafirisha sampuli nje ya nchi kwa uchunguzi zaidi.



Picha Na.5: Miamba Choronge–Diamond Drilling (DD) iliyotokana na kazi ya utafiti wa madini katika eneo la Itumbi – Chunya.



Picha Na.6: Uchorongaji kwa njia ya Diamond Drilling (DD) ukiendelea katika eneo la Itumbi - Chunya



Picha Na.7: Uchorongaji kwa njia ya *Reverse Circulation (RC)* ukiendelea katika eneo la Itumbi - Chunya

64. Mheshimiwa Spika, GST iliendelea na kazi ya kuratibu majanga asilia ya jiolojia ambapo takwimu kutoka vituo 8 vya kudumu vya kupimia matetemeko ya ardhi vilivyopo Dodoma, Mbeya, Arusha, Mtwara, Geita, Singida, Babati na Kibaya – Manyara zilikusanywa, kuchakatwa na kuhifadhiwa kwenye kanzidata. Kwa kutumia takwimu hizo, GST iliainisha maeneo yenye vitovu (*epicentres*) vya matetemeko na kuboresha ramani inayoonesha maeneo yenye vitovu vya matetemeko ya ardhi. Aidha, taarifa kuhusu matetemeko ya ardhi yaliyotokea katika maeneo mbalimbali ya nchi katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2017 hadi Machi, 2018 ilitolewa kwa wananchi na kwenye vyombo vya habari. Matukio hayo yameainishwa kwenye **Jedwali Na.1.**

65. Mheshimiwa Spika, vilevile, GST ilifanya utafiti maalum wa kuangalia ubora na wingi wa madini ya jasi katika maeneo ya Makanya na Bendera (Same), Mwanga (Mwanga), Itigi (Manyoni), Msagali (Mpwapwa) na Manda

(Chamwino), Mpindiro, Mandawa, Mbaru, (Kilwa-Lindi) na Mkomole (Sumbawanga); utafiti maalum katika Wilaya ya Mufindi, Kijiji cha Isalavanu kwa maombi ya Serikali ya Wilaya ili kubaini uwepo wa madini yaliyofichwa katika maeneo hayo wakati wa Utawala wa Wajerumani kama ilivyokuwa inadhaniwa na wana kijiji hicho; utafiti wa jiosayansi ulifanyika katika mahandaki yaliyopo katika Kijiji cha Gibeshi Mkoani Simiyu ili kujua kama ni mahandaki ya asili au yamechimbwa na binadamu; utafiti wa jiosayansi katika eneo la Nholi - Dodoma ili kubaini chanzo na uwepo wa madini ya dhahabu katika eneo hilo; uchunguzi wa malikale katika Wilaya ya Same Kata ya Lugulu na Kitongoji cha Vumba pamoja na Mkoani Tanga katika Kata ya Pongwe; kukusanya taarifa za uwepo wa madini na utafiti wa miamba katika Mkoa wa Iringa, Wilaya za Mufindi, Iringa Vijiji na Kilolo; na pia GST ilishiriki katika ukaguzi wa taarifa zilizotumika kupata kiwango cha almasi kilichopo kwa sasa katika Mgodi wa almasi wa Mwadui na kuhakiki uwepo wa kiwango hicho cha almasi na kutoa mapendekezo kwa Serikali.

66. *Mheshimiwa Spika*, Pia, katika tafiti nyingi zilizofanywa na wataalam wa jiosayansi ya uchenjuaji zimebainisha kuwa madini mengi hubakia kwenye visusu (*tailings*) baada ya kuchenjuliwa. Sababu za madini kubakia kwenye mabaki ni kutokana na kutofikiwa kwa kiwango cha ukubwa wa **chembe** (*particle size*) za mbale kinachotakiwa baada ya mwamba kuvunjwa na kusagwa; matumizi yasiyo sahihi ya kemikali zitumikazo kuchenjua na utumiaji wa vifaa visivystahili. Hii inatokana na wachimbaji wadogo kutofahamu tabia tofauti za miamba na mbale hivyo kupelekea kutotumia njia bora za uchenjuaji. Ni vyema wachimbaji wadogo wakafahamu njia bora za uchenjuaji kwa kufanya majoribio ya sampuli za mbale katika maabara mara kwa mara ili kutambua mtiririko mzuri, aina ya miamba, kiwango cha usagaji, njia na mbinu za uchenjuaji.

67. *Mheshimiwa Spika*, natoa rai kwa wachimbaji wadogo, kama hawajui tabia za mbale ya sehemu wanayochimba, kabla ya kuanza uchenjuaji wapeleke sampuli za mbale (*bulk samples*) kwenye maabara za GST

kwa ajili ya uchunguzi ili waweze kutambua njia bora za uchenjuaji. Lengo ni kupunguza madini kubaki kwenye visusu (*tailings*), kuongeza wingi wa uvunaji wa madini, kipato na faida kwa wachimbaji wa madini.

68. Mheshimiwa Spika, GST ilifanya kazi ya kuboresha Kanzidata ya jiosayansi na madini, ambapo jumla ya machapisho 412 yalibadilishwa kutoka katika mfumo wa karatasi na kwenda kwenye mfumo wa digitali; ramani 93 za jiosayansi zilikuwa “*scanned*” na kuhaririwa na kuwekwa kwenye mfumo wa utunzaji wa taarifa na machapisho (*GMIS*); Ramani 17 za jiolojia za mfumo wa QDS zimebadilishwa kutoka mfumo wa karatasi kwenda mfumo wa digitali (*digitization*) kwa lengo la kurahisisha usambazaji na utumiaji. Aidha, GST ilisambaza ramani na machapisho mbalimbali kwa wadau wa Sekta ya Madini kwa matumizi mbalimbali. Vilevile, GST imepokea na kuhakiki taarifa **205** kutoka kwa wamiliki wa leseni za utafutaji na uchimbaji madini kwa ajili ya kujua uhalisia wake na kuzitunza kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Marekebisho yake ya Mwaka 2017.

69. Mheshimiwa Spika, GST ilifanya utafiti wa uchenjuaji mbale za madini ya dhahabu katika maeneo ya Londoni na Sambaru (Singida) kwa ajili ya kusaidia wachimbaji wadogo; na kukamilisha uchakataji wa taarifa za awali za jiosayansi (*Geotechnical and seismological*) ili kuainisha maeneo hatarishi na salama kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika Jiji la Dodoma ikizingatiwa kuwa maeneo hayo yapo katika ukanda wa matetemeko ya ardhi.

Aidha, GST ilitoa ushauri elekezi wa jiosayansi kwa kampuni 10 za utafutaji na uchimbaji madini ya metali na ya viwandani. GST pamoja na hayo ilipokea taarifa zenye jumla ya **leseni 247** za utafutaji madini (*Prospecting licences*), leseni **12** za uchimbaji wa kati wa madini (*Mining licences*) na leseni **6** za uchimbaji mkubwa kwa ajili ya kuhakiki ili kujua uhalisia wake na kutunza kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Marekebisho yake ya Mwaka 2017. Kati ya taarifa za leseni zilizofanyiwa tathmini zimebainisha

kuwa taarifa za kampuni 10 hazikidhi vigezo vilivyotolewa na GST na vilivyoainishwa kwenye Sheria. GST imezielekeza kampuni hizo kuziboresha taarifa hizo.


(c) *Chuo cha Madini – (MRI)*

70. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Madini kimeen- delea na majukumu yake ya kutoa mafunzo ya muda mrefu ya utaalalm wa kada ya kati (Ufundu Sanifu) katika fani za madini, mafuta na gesi asilia; kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wachimbaji wadogo wa madini hasa katika nyanja za jiolojia na utafutaji madini, uhandisi uchimbaji madini, uhandisi uchenjuaji madini, uhandisi na usimamizi wa mazingira migodini; kutoa mafunzo maalum (*tailor-made courses*) kwa wadau kulingana na mahitaji yao; kufanya tafiti katika Sekta za Madini, Mafuta na Gesi; na kutoa ushauri elekezi (*consultancy*) katika Sekta hizo.

71. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi 542 katika mafunzo ya muda mrefu katika fani za Jiolojia na Utafutaji Madini; Uhandisi Uchimbaji Madini; Uhandisi Uchenjuaji Madini; Sayansi za Mafuta na Gesi; Uhandisi na Usimamizi wa Mazingira Migodini; na Upimaji wa Ardhi na Migodi. Katika kutoa mafunzo ya muda mfupi, Chuo kimeweza kufundisha na kutoa vyeti kwa wafanyakazi 33 wa migodini ili kuwajengea uwezo wa kufanya kazi kwa ubora. Aidha, katika kutoa mafunzo maalum, Chuo kimeingia Mkataba wa Makubaliano (MoU) na Kampuni ya Acacia North Mara kwa ajili ya kuwafundisha wafanyakazi wake 20 kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia mwezi Januari, 2018. Pia, Chuo kina Mikataba ya Makubaliano na Taasisi ya Jiolojia na Utafutaji Madini Tanzania (GST), *Earth Sciences Institute of Shinyanga (ESIS)*, *Zimbabwe School of Mines (ZSM)*, *Dedan Kimathi University of Technology (DeKUT)*, *Dares Salaam Marine Institute (DMI)*, *Tanzania Geothermal Development Company (TGDC)*, *Chuo cha Cégep Limoilou – Canada*, Chuo Kikuu cha Montpellier – Ufaransa, Mgodi wa Dhahabu wa Acacia – North Mara na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

72. Mheshimiwa Spika, Vilevile, Chuo cha Madini kimeanzisha mafunzo ya fani mpya ya Upimaji wa Ardhi na Migodi (*Land and Mine Surveying*) kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada. Jumla ya wanafunzi 24 wamedahiliwa na kuanza masomo ya Astashahada mwezi Januari, 2018. Mafunzo haya yatazalisha Mafundi Sanifu wa kupima ardhi na migodi.

73. Mheshimiwa Spika, katika kuhanikisha mafunzo yatolewayo na Chuo cha Madini yanakidhi matakwa ya mtaala na mfumo wa ufundishaji, Serikali imeboresha maabara za Jiolojia, Uhandisi Uchimbaji na Uhandisi Uchenjuaji kwa kutoa vifaa vya maabara (**Tazama Picha Na.8**) kupitia mradi wa SMMRP ulio chini ya Wizara vyenye thamani ya **Dola za Marekani 514,924.81** Maabara hizi zitakiwezesha Chuo kutoa mafunzo kwa vitendo na kufanya tafiti mbalimbali. Aidha, kupitia Mradi wa *Improving Skills Training for Employment Program (ISTEP)* unaotekeliza kwa kushirikiana kati ya Chuo cha Madini na Chuo cha *Cégep Limoilou* kilichopo nchini Canada, Chuo kimepata vifaa vya kisasa (**Tazama Picha Na.9**) vya kusaidia kutoa mafunzo ya vitendo katika fani mpya ya Upimaji Ardhi na Migodi. Vifaa hivi vimegharimu jumla ya **Dola za Kanada 40,000**.





Picha Na. 8: Baadhi ya vifaa vya Maabara ya Chuo vilivyonunuliwa kuititia Mradi wa SMMRP.



Picha Na.9: Baadhi ya vifaa vya Maabara za Chuo vilivyonunuliwa kuititia Mradi wa ISTEP.

74. Mheshimiwa Spika, katika kusaidia wachimbaji wadogo Chuo kina mpango wa kufanya tafiti kuhusu kutengeneza njia mbadala ya uchenjuaji madini ya dhahabu kwa wachimbaji wadogo. Madhumuni ya utafiti huu ni kusaidia upatikanaji wa njia bora yenye ufanisi wa kuchenjua madini ya dhahabu kwa wachimbaji wadogo nchini na kuondoa matumizi ya kemikali ya Zebaki kwenye uchenjuaji wa dhahabu kama inavyotakiwa na Mikataba ya Kimataifa ikiwemo Makubaliano ya Minamata kuhusu utunzaji wa mazingira na afya za watu na viumbe mbalimbali katika mazingira yetu.

(d) *Shirika la Madini la Taifa – (STAMICO)*

75. Mheshimiwa Spika, majukumu ya Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) ni pamoja na kuwekeza kwenye shughuli za uchimbaji na utafutaji madini; kuwekeza katika uchenjuaji, uongezaji thamani na uuzaaji madini; na kutoa huduma na ushauri wa kitaalamu na kiufundi katika Sekta ya Madini wakiwemo wachimbaji wadogo kwenye nyanja za kijiolojia, kihandisi, kimazingira na uchorongaji miamba.

76. Mheshimiwa Spika, STAMICO imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya uchimbaji wa madini nchini ikiwemo ya uwezeshaji wa wachimbaji na miradi ya ubia. Utekelezaji wa shughuli hizo unahusisha uzalishaji wa makaa ya mawe katika Mgodi wa Kabulo; uzalishaji wa madini ya Tanzanite katika Mradi wa Ubia wa TanzaniteOne; uzalishaji wa madini ya dhahabu katika Kampuni Tanzu ya STAMIGOLD; na uendelezaji wa Mradi wa uchimbaji wa dhahabu wa Buhembba.

(i) *Mradi wa Makaa ya Mawe wa Kabulo, Kiwira*

77. Mheshimiwa Spika, Shirika lilianza uchimbaji wa makaa ya mawe katika kilima cha Kabulo kilichopo eneo la Kiwira, Mkoani Songwe mwezi Aprili, 2017. Lengo ni kukidhi mahitaji ya makaa ya mawe nchini.

78. Mheshimiwa Spika, tangu mradi uanze mwezi Aprili, 2017 hadi kufikia mwezi Machi, 2018, Shirika limezalisha jumla ya **tani 8,674** za makaa ya mawe yenye thamani ya **shilingi milioni 555.1** na kiasi cha **tani 2,827.7** za makaa ya mawe zimeuzwa kwa jumla ya shilingi **180,972,800**. Aidha, kiasi cha **tani 5,846.30** za makaa ya mawe zimehifadhiwa katika eneo la mgodi wakati jitihada za kutafuta wateja zikiendelea.

79. Mheshimiwa Spika, vilevile, Shirika lilifanya ukarabati wa maabara ya kupima ubora wa makaa ya mawe katika Mgodi wa Kiwira sanjari na matengenezo ya vifaa vyta maabara ikiwemo kuweka mfumo mpya wa umeme. Ukarabati huo uligharimu kiasi cha **shilingi 7,566,000**. Pia, Shirika lilifanya ukadiriaji wa mashapo ya makaa ya mawe katika leseni yake ya utafiti ya Kabulo PL Na. 9963/2014 iliyopo wilayani lleje, Mkoa wa Songwe ambapo ukadiriaji huo umeonesha uwepo wa tani **milioni 300** za makaa ya mawe.

(ii) *Mgodi wa TanzaniteOne*

80. Mheshimiwa Spika, migodi ya Tanzanite iliyopo Mirerani ni pamoja na mgodi unaomilikiwa kwa ubia baina ya Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na Kampuni ya TanzaniteOne Mining Limited (TML). Ipo pia, migodi mingine inayomilikiwa na wachimbaji wazawa wenye leseni za uchimbaji mdogo na wa kati. Uendeshaji wa mgodi baina ya STAMICO na TML umekuwa na changamoto nyingi zilizosababishwa na kasoro katika Mkataba wa Ubia na Mkataba wa Uendeshaji. Kutokana na kasoro zilizobainishwa na Kamati Maalum ya Spika ya Kuchunguza Uchimbaji na Biashara ya Madini ya Tanzanite, Serikali iliagiza Timu ya Majadiliano ya Serikali kukutana na wamiliki wa TML na STAMICO kujadiliana ili kubaini kasoro hizo na kupendekeza namna bora ya uchimbaji, biashara na uendeshaji wa mgodi huo kwa lengo la kulinufaisha Taifa kuliko ilivyo sasa. Kufuatia kukamilika kwa majadiliano hayo, Serikali imeagiza Leseni ya Uchimbaji wa Ubia baina ya STAMICO na TML irudishwe Serikalini ili utaratibu mpya uandaliwe

utakaowezesha Serikali, TML na mwekezaji wa kimkakati kushirikiana katika uchimbaji, uendeshaji na biashara ya madini ya Tanzanite katika mgodi huo kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Madini, Sura ya 123 kama iliyorekebishwa na Bunge Mwaka 2017. Aidha, majadiliano na wachimbaji wadogo yanaendelea baina ya Timu ya Majadiliano ya Serikali na wamiliki wa migodi hiyo kwa lengo la kuleta manufaa zaidi kwa Taifa kutokana na madini ya Tanzanite. Vilevile, kwa kutambua umuhimu na upekee wa madini ya Tanzanite duniani kwamba yanapatikana Tanzania tu, Serikali inakamilisha utaratibu wa kuyatangaza madini ya Tanzanite kuwa madini maalum (*specified minerals*). Utaratibu wa kuyatangaza utakamilika katika Mwaka huu wa Fedha wa 2017/18.

(iii) ***Mgodi wa Dhahabu wa STAMIGOLD***

81. *Mheshimiwa Spika*, Kampuni ya STAMIGOLD ni Kampuni tanzu ya Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) ilioanzishwa Oktoba, 2013. Kampuni hii inamiliikiwa kwa ubia kati ya STAMICO asilimia 99.98 na Msajili wa Hazina asilimia 0.02. Kampuni hii ilipewa jukumu la kuendeleza Mgodi wa dhahabu wa STAMIGOLD Biharamulo Mine (SBM) ambao ulirithiwa kutoka kampuni ya Pangea Minerals LTD iliyokuwa mmiliki wa awali kupitia Leseni ya Uchimbaji Mkubwa Na. SML 157/2003.

82. *Mheshimiwa Spika*, wakati STAMICO inakabidhiwa mgodi huu, gharama za uendeshaji zilikuwa juu ikilinganishwa na mapato yaliyotokana na mauzo ya dhahabu kwa kuwa katika kipindi hicho bei ya dhahabu ilikuwa chini kutokana na m dororo wa uchumi duniani hususan katika Sekta ya Madini. Pamoja na tatizo hilo, Kampuni ilijiendesha kwa hasara na kusababisha deni la **takriban shilingi bilioni 64** hadi kufikia mwezi Machi, 2018. Hata hivyo, deni hili linahakikiwa na Vyombo vya Serikali ili kujua uhalali wake na namna ya kuondokana nalo.

83. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi Julai, 2017 hadi Machi, 2018 Mgodi umezalisha na kuuza jumla ya **wakia 3,967.92** za dhahabu na **wakia 400.85** za fedha zenye thamani ya **shilingi 11,459,212,821.83**. Kutokana na mauzo hayo, Serikali imepokea mrabaha wa **shilingi 802,144,897.53**.

84. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine Menejimenti ya Mgodi imeweza kuchukua sampuli 10 za visusu (*old tailings*) vilivyoachwa mgodini hapo na kupeleka kwenye Maabara ya *African Minerals and Geoscience Centre (AMGC)* iliyopo Kunduchi, Dar es Salaam ili kuthibitisha kitaalamu kiasi cha dhahabu kilichomo. Kiasi cha visusu kilichopo ni tani 8,600,000. Kwa mujibu wa ripoti ya maabara, visusu hivyo vya dhahabu vina wastani wa gredi ya **gramu 1.15** kwa tani ambapo ni sawa na takriban **wakia 300,000**. Vilevile, thamani ya visusu hivyo itatambuliwa kwenye vitabu rasmi kuwa ni mali ya Kampuni kwa ajili ya kumbukumbu na udhibiti wa mali hiyo.

(iv) ***Mradi wa Dhahabu wa BUHEMBA***

85. Mheshimiwa Spika, Mradi wa Dhahabu wa Buhemba uliopo Wilaya ya Butiama, Mkoa wa Mara unahuishisha uchenjuaji wa mabaki ya mchanga wa dhahabu na uchimbaji wa dhahabu katika miamba migumu. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Shirika limeendelea na utafiti kwa lengo la kuendelea kubaini kiasi kingine cha mashapo ya dhahabu kilichopo katika miamba ambapo kazi zilizofanyika zilihusisha uchorongaji wa miamba.

(v) ***Mradi wa Dhahabu wa BUCKREEF***

86. Mheshimiwa Spika, Mgodi wa Buckreef unamili-kiwa kwa Ubia kati ya STAMICO na Kampuni ya TANZAM 2000 kwa asilimia 45 kwa 55. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, STAMICO kwa kushirikiana na Wizara ya Madini na Ofisi ya

Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaupitia upya mkataba wa ubia. Hii ni kutokana na mbia kuchelewa kuanza uzalishaji kwa mujibu wa makubaliano ya Mkataba. Pia, STAMICO kwa kushirikiana na mbia mwenza ilifanya tathmini ya maeneo yanayofaa kuachiwa kwa wachimbaji wadogo katika maeneo ya leseni za utafiti Namba PL 6430/2010 (Lwamgasa West); PL 6549/2010 (Nyamalimbe 2); na PL 6547/2010 (Lwamgasa South 2). Matokeo ya tathmini hiyo yalibainisha kuwa maeneo hayo yanafaa kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Utaratibu unaandalila wa kuyaachia maeneo hayo kwa wachimbaji wadogo.

(vi) *Mradi wa Kokoto - Ubena Zomozi*

87. Mheshimiwa Spika, Shirika lilifanya utafiti wa wingi na ubora wa miamba katika leseni zake kumi (10) za uchimbaji kokoto zilizopo Ubena Zomozi, mkoani Pwani. Utafiti huo ulibaini uwepo wa miamba yenyewe kiasi cha mashapo yanayokadirisha kufikia **tani milioni 41.5** za kokoto zinazoweza kuchimbwa kwa zaidi ya miaka 50. Shirika linaendelea na taratibu za kutafuta fedha au kumpata mbia kwa ajili ya mradi huo.

(vii) *Huduma kwa Wachimbaji Wadogo*

88. Mheshimiwa Spika, Shirika kwa kushirikiana na Wizara limeendelea kusimamia ujenzi wa Mgodi wa Mfano katika eneo la Lwamgasa kwa ajili ya wachimbaji wadogo, ambapo hadi kufikia Machi, 2018, ujenzi wa shimo la uchimbaji (*mining shaft*) na usimikaji wa mitambo ya kuchenjulia dhahabu umefikia asilimia 70 (**Tazama Picha Na.10 na 11**). Mgodi huu utawanufaisha wachimbaji wadogo katika eneo hilo kwa kuwawezesha kujifunza teknolojia sahihi ya uchimbaji na uchenjuaji wa madini. Mgodi wa Dhahabu wa Geita (GGM) ulihusika kufanya upembuzi yakinifu katika eneo la mgodi wa mfano. Aidha, hadi sasa Mradi wa SMMRP umeshatumia jumla ya **Dola za Marekani 293,881.2** katika ujenzi wa mgodi huo wa mfano.



Picha Na. 10: Mtambo wa kuchenjua mbale uliosimikwa katika Mgodi wa Mfano wa Lwamgasa.



Picha Na.11: Mlango (*Mine shaft*) wa kuingia kwenye Mgodi waMfano wa Lwamgasa.

- (e) *Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia – (TEITI)*

89. Mheshimiwa Spika, Tanzania ni Mwanachama wa Mpango wa Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia (*Extractive Industry Transparency Initiative*) tangu mwaka 2009. Katika kutekeleza mpango huo, Serikali ilianzisha Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI) chini ya Sheria ya TEITA ya Mwaka 2015. Taasisi hii ina jukumu la kuhamasisha Serikali kuweka mifumo ya uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali za madini, mafuta na gesi asilia ili kuongeza mapato na manufaa yatokanayo na shughuli za utafutaji na uchimbaji wa rasilimali hizo.

90. Mheshimiwa Spika, Taasisi hii pia ina jukumu la kuwajengea uwezo wananchi katika kutumia takwimu zinazotokana na shughuli za uendeshaji wa kampuni za madini, mafuta na gesi asilia kwa kuhoji na kuhamasisha mijadala kuhusu manufaa ya shughuli za rasilimali madini; utoaji wa leseni na mikataba, uchimbaji wa madini, mafuta na gesi asilia; usimamizi na uendeshaji wa kampuni za madini, mafuta na gesi asilia; ukusanyaji wa mapato yatokanayo na madini, mafuta na gesi asilia; na mgawanyo wa mapato na matumizi yake.

91. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, TEITI ilikamilisha na kutoa kwa umma ripoti ya ulinganisho (*Reconciliation report*) wa malipo yaliyolipwa na Kampuni za madini, mafuta na gesi asilia na mapato yaliyopokelewa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/16. Ripoti hiyo ambayo ni ya 8 imewasilishwa kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa ajili ya uchunguzi. Aidha, TEITI ilikamilisha muhtasari wa takwimu za ripoti hiyo zilizowekwa katika vielelezo (*Infographics*) kwa lugha ya kiswahili na kiingereza. Lengo ni kurahisisha ufikishaji wa matokeo ya ripoti za TEITI kwa wadau na kujenga uwezo wa wananchi katika kutumia takwimu zinazotokana na shughuli za uendeshaji wa kampuni, kuhoji Serikali na

kuhamasisha mijadala kuhusu uongezaji wa manufaa ya uchimbaji madini, mafuta na gesi asilia nchini.

(f) *Kituo cha Jimolojia Tanzania - (TGC)*

92. Mheshimiwa Spika, Kituo cha Jimolojia Tanzania (TGC) kina majukumu ya kutoa mafunzo ya uongezaji thamani madini na miamba na utengenezaji wa bidhaa za urembo na mapambo kwa kutumia miamba (**Tazama Picha Na. 12**). Kituo kinatoa mafunzo katika fani za usanifu wa madini ya vito, usonara na uchongaji vinyago vya miamba. Kazi zilizotekelawa na Kituo hiki ni pamoja na uchongaji wa vinyago 69 vya miamba; kutengeneza marumaru (*tiles*) za ukutani 250, *table mats* 80; *tiles* kubwa 100 kutohana na mawe ya Tanga (*Tanga stones/slates*); kutengeneza bidhaa mbalimbali za mapambo kwa kutumia mawe ambazo ni vikuku (*bracelets*) 50, hereni 65, mikufu 89, vidani 120 na pete 60; kung'arisha sampuli za madini ya tanzanite za ubora wa chini (*reject*) za uzito wa kilo 6 kutoka kwa watu mbalimbali; kukata na kusanifu madini ya vito ya taasisi na watu mbalimbali. Kiasi cha madini kilichokatwa na kusanifiwa ni gramu 20 za madini ya tanzanite; gramu 30 za *amethyst*; na gramu 300 za *quartzred aventurine*. Pia, TGC imeendelea kutoa mafunzo ya ukataji na ung'arishaji wa madini ya vito ambapo wanafunzi 38 walidahiliwa katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2017 hadi Mei, 2018. Vilevile, kabla ya Julai, 2017 wanafunzi 65 walikuwa wamedahiliwa na kupata mafunzo ya aina hiyo.



Picha Na.12(a) Mikufu iliyotengenezwa kwa kutumia miamba ya *quartz*, *magnetite* na *azurite*.



Picha Na.12(b) Kinyago cha tai kilichotengenezwa kwa kutumia jiwe la *travertine* na *quartz*.



Picha Na. 12(c): Mawe ya tanzanite yenye ubora wa chini baada ya kung'arishwa kwa mashine ya *tumbler* na kutobolewa kwa ajili ya kutengenezea vidani.



Picha Na.12(d): Marumaru iliyotengenezwa kutokana na mawe ya Tanga (*Tanga stones/slates*).

**4.0 MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA WA
2018/19**

93. *Mheshimiwa Spika*, Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19 umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 - 2020; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21); Malengo Endelevu ya Maendeleo 2030; Ahadi za Serikali Bungeni za Mwaka wa 2017/18; Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti wa Mwaka wa Fedha wa 2018/19; Maagizo ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyatoa kwa nyakati tofauti; Ushauri na Maoni ya Kamati Maalum zilizoundwa na Mheshimiwa Rais kama zillivyoainishwa katika aya ya 12 na ushauri ultiotolewa na Bunge pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa nyakati tofauti, na Ushauri wa Kamati Maalum za Mheshimiwa Spika.

94. *Mheshimiwa Spika*, kazi zilizopangwa kutekelezwala kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19 na Wizara ya Madini na Taasisi zake ni pamoja na kuimarisha ukusanyaji wa Mapato ya Serikali yatokanayo na rasilimali madini; kuwaendeleza wachimbaji wadogo na wa kati wa madini; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; kuimarisha ufuatiliaji wa ukaguzi wa usalama, afya, mazingira na uzalishaji wa madini katika migodi midogo, ya kati na mikubwa; kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika miradi ya kimkakati ya Sekta ya Madini; kuendelea kuboresha mazingira ya kuwawezesha wananchi kufaidika na rasilimali madini; kuelimisha Umma na kuboresha mawasiliano kati ya Wizara na wadau mbalimbali kuhusu masuala ya madini; kusimamia, kufuatilia na kuboresha Sera, Sheria, Kanuni, Mikakati na Miongozo mbalimbali ili kuleta ufanisi na tija katika Sekta ya Madini; kuendeleza rasilimali watu na kuboresha mazingira ya kufanya kazi; na kuwawezesha Taasisi zilizo chini ya Wizara.

(a) Kuimarisha Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali yatokanayo na Shughuli za Madini

95. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na shughuli za madini ambapo kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19 lengo ni kukusanya **Shilingi 310,598,007,000**, ikiwa ni ongezeko la **asilimia 59.57** ikilinganishwa na **Shilingi 194,663,501,763** zilizopangwa kukusanya kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18. Katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali yanayotokana na shughuli za madini, Wizara inatarajia kuimarisha ukaguzi wa migodi mikubwa, ya kati na ya uchimbaji mdogo ili kupata taarifa sahihi za uwekezaji, uzalishaji, mauzo na kodi mbalimbali; kudhibiti utoroshwaji wa madini katika maeneo ya uzalishaji na kutokea nchini (*Exit Points*); kuimarisha ukaguzi wa madini ya ujenzi na viwandani; kufuatilia taarifa za ununuzi na uuzaji (*returns*) kwa wafanyabiashara wa madini (*Dealers & Brokers*); kufuatilia wadaiwa wa tozo mbalimbali za madini kwa mujibu wa Sheria kwa wakati; kudhibiti uchimbaji na uchenjuaji haramu wa madini; na kuboresha na kuimarisha mfumo wa kutoa leseni za madini na kutunza taarifa zake.

96. Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa wamilliki wa leseni za madini kuacha kukwepa au kuchelewa kulipa kodi, kulipa mrabaha stahiki na tozo nyingine zilizopo kwa mujibu wa Sheria za nchi. Kwa wale watakaobainika kukiuka matakwa ya kisheria, Serikali itawachukulia hatua kali ikiwa ni pamoja na kufuta leseni zao na kuwafikisha mahakamani.

(b) Kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo wa Madini

97. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango wa kuwaendeleza wachimbaji wadogo, Wizara itaendelea kutenga maeneo yanayofaa ambapo jumla ya maeneo 4 yanatarajiwa kutengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Aidha, GST itabainisha uwepo wa mashapo ya madini katika maeneo yatakayotengwa. Vilevile, Wizara kuititia STAMICO, itawaelimisha wachimbaji wadogo namna ya kutumia teknolojia ya kisasa na rahisi katika kuongeza uzalishaji na

tija wakati wa uchimbaji na uchenjuaji wa madini. Pia, Wizara kuptitia mradi wa SMMRP itajenga Vituo vya Mfano 4 ambavyo ni Katente (Bukombe); Itumbi (Chunya); Kona Z (Tanga); na Lindi. Vituo hivyo vitatumika kwa ajili ya mafunzo ya uongezaji thamani madini, uchimbaji salama pamoja na kuongeza uzalishaji na tija na hivyo kuongeza mapato kwa wachimbaji wadogo. Vituo hivi pia vinatarajiwa kutoa huduma za uchenjuaji wa madini kwa wachimbaji wadogo.

(c) Kuhamasisha Shughuli za Uongezaji Thamani Madini

98. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2018/19, Wizara itaendelea kuhamasisha uwekezaji katika shughuli za uongezaji thamani madini na kuendelea kutoa leseni za uchenjuaji na uyeyushaji wa madini ya metali. Pia, Wizara itakamilisha kazi ya kuwapata wawekezaji katika Vinu vya uchenjuaji na usafishaji wa madini. Aidha, Wizara itaandaa Muswada wa Sheria ya Uongezaji Thamani Madini ili kukuza na kusimamia vyema shughuli za uongezaji thamani madini nchini. Viwanda vya uyeyushaji, usafishaji wa madini na shughuli nyingine za uongezaji thamani zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali, kuongeza ajira na kukuza matumizi ya teknolojia nchini.

99. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madini ya vito, Wizara itaendelea kukiimarisha Kituo cha Jimolojia Tanzania ili kiweze kutoa wataalam kwenye fani za ukataji na ung'arishaji wa madini ya vito, jimolojia na usonara watakaosaidia kufanya shughuli za uongezaji thamani madini hayo hapa nchini.

(d) Kuimarisha Uguzi wa Usalama, Afya, Mazingira na Uzalishaji wa Madini Migodini

100. Mheshimiwa Spika, shughuli za uchimbaji wa madini zinapaswa kusimamiwa kwa karibu kwani huweza kuambatana na athari za kiafya, usalama na uharibifu mkubwa wa mazingira. Ili kuondokana na athari hizo, Wizara itaendelea kuimarisha kaguzi migodini na maeneo ya uchenjuaji wa madini, kuongeza huduma za ugani hususan kwa wachimbaji wadogo, kuimarisha ushirikiano na taasisi

nyingine za Serikali zinazohusika na usimamizi wa masuala ya Afya, Usalama na Utunzaji wa Mazingira katika kufanya kaguzi mbalimbali migodini ikiwemo utekelezaji wa Mkataba wa Minamata wa kupunguza na hatimaye kuzuia matumizi ya Zebaki katika uchenjuaji. Pia, Wizara itaendelea kukagua na kuhakiki kiasi na ubora wa madini yanayozalishwa na migodi mikubwa, ya kati na midogo.

101. *Mheshimiwa Spika*, nitoe rai kwa wachimbaji wa madini na wale wanaofanya shughuli za uchenjuaji hususan madini ya dhahabu kuhakikisha wanaimarisha miundombinu ya mabwawa ya kuhifadhi mabaki yenye kemikali (*Tailings Storage Facility – TSF*) kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kama ilivyofanyiwa marekebisho Mwaka 2017. Pia, Wachimbaji Wakubwa na wa Kati wahakikishe wanawasilisha Mpango wa Ufungaji Migodi kwa wakati kama ilivyoainishwa katika Kanuni ya 206 ya Kanuni za Madini kuhusiana na Usalama, Afya na Utunzaji wa Mazingira za Mwaka 2010. Wachimbaji wakubwa na wa kati wanapaswa pia kuweka Hati Fungani ya Uhifadhi wa Mazingira (*Environmental Rehabilitation Bond*) kama ilivyoainishwa katika Kanuni ya 207 ya Kanuni za Madini kuhusiana na Usalama, Afya na Utunzaji wa Mazingira za Mwaka 2010.

102. *Mheshimiwa Spika*, Wizara yangu kupitia STAMICO imekuwa ikishiriki kwenye uwekezaji katika madini mbalimbali. Katika kutekeleza jukumu hilo, STAMICO imetengewa kiasi cha **shilingi 8,600,000,000** kwa ajili ya kuendeleza Mradi wa Dhahabu wa Buhemba wa kuchenjua visusu. Pia, STAMICO itaendelea kutafuta fedha kutoka taasisi mbalimbali za kifedha na wabia kwa ajili ya kuendeleza miradi ya Makaa ya Mawe ya Kiwira na Kabulo; Uchimbaji na Uuzaji wa Kokoto wa Ubena Zomozi (Pwani) na Chigongwe (Dodoma). Vilevile, STAMICO itaendelea kuimarisha usimamizi wa Mradi wa Ubia wa TanzaniteOne na Kampuni Tanzu ya STAMIGOLD; kuimarisha biashara ya shughuli za uchorongaji na utoaji wa ushauri wa kitaalam katika Sekta ya Madini; na kuratibu uboreshaji na uendelezaji wa shughuli za wachimbaji wadogo nchini.

(e) *Kuendelea Kuboresha Mazingira ya Kuwawezesha Wananchi Kunufaika na Shughuli za Madini*

103. *Mheshimiwa Spika*, Sera ya Madini ya Mwaka 2009 na Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 pamoja na Marekebisho yake ya Mwaka 2017 zinatoa mwongozo wa namna Kampuni za madini zinavyopaswa kufungamanisha Sekta ya Madini na sekta nydingine za kiuchumi. Wizara itasimamia Sheria katika kukuza ushiriki wa Watanzania (*local content*) kwenye shughuli za utafutaji, uchimbaji, biashara ya madini nchini na Uwajibikaji wa Kampuni za Uchimbaji Madini kwa Jamii (*Corporate Social Responsibility - CSR*).

104. *Mheshimiwa Spika*, katika Kifungu cha 102 cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 pamoja na Marekebisho yake ya Mwaka 2017, maombi ya leseni za utafutaji na uchimbaji wa madini yanapaswa kuambatana na Mpango wa Matumizi ya Bidhaa na Huduma za Ndani katika maombi ya leseni husika. Iwapo bidhaa hizo hazipatikani ndani ya nchi, bidhaa hizo zinapaswa zipatikane kwa kutumia Kampuni ya ndani ya nchi iliyoingia ubia na Kampuni ya nje. Mmiliki wa Leseni anapaswa kuwasilisha katika Tume ya Madini taarifa inayoonesha matumizi ya bidhaa na huduma za ndani ya nchi katika kipindi cha siku 60 baada ya kuisha kwa mwaka wa kalenda. Wizara itaendelea kusimamia Kampuni hizo ili kuhakikisha kuwa Kifungu hicho cha Sheria kinatekelezwa.

105. *Mheshimiwa Spika*, vilevile, Wizara itaendelea kushirikisha jamii katika shughuli za kiuchumi ambazo jamii inaweza kuzimudu. Katika Kifungu cha 105 cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 pamoja na Marekebisho yake ya Mwaka 2017, **kinamtaka kila mmiliki wa leseni ya uchimbaji wa madini, uchenjuaji, uyeyushaji na usafishaji wa madini kuandaa Mpango wa Mwaka wa Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii**. Mpango huo unapaswa kuwasilishwa kwa **Mamlaka za Serikali za Mtaa** husika kwa rejea na idhini. Nawasihi Viongozi katika kila Halmashauri kuandaa Miongozo ya Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii na kusimamia utekelezaji wake. Vilevile, Halmashauri

zinapaswa kuwaelimisha wananchi katika maeneo yao kuhusiana na Mipango ya Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii.

106. *Mheshimiwa Spika*, natoa rai kwa Mamlaka nyingine za Serikali hususan Mamlaka ya Serikali za Mitaa kushiriki kuziandaa jamii zilizopo katika maeneo ya migodi kushirikiana na Kampuni za madini ili kufanikisha malengo ya mipango hiyo.

(f) *Kuelimisha Umma na Kuboresha Mawasiliano baina ya Wizara na Wadau wa Sekta ya Madini*

107. *Mheshimiwa Spika*, Wizara yangu itafanya mikutano ya ana kwa ana na wawekezaji na itatoa elimu kwa umma kuhusu rasilimali madini. Kwa kutambua hilo, kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19 Wizara yangu itatoa elimu kwa umma kuhusu rasilimali madini, uchimbaji, uchenjuaji na biashara ya madini kupitia vipindi mbalimbali vya redio na televisheni; majorida na machapisho mbalimbali; tovuti; mitandao ya kijamii ya Wizara; na kushiriki katika maonesho mbalimbali ya kitaifa na kimataifa na kupitia njia nyingine za upashanaji habari kwa umma. Lengo ni kuhakikisha kuwa wananchi wanapata elimu ya kina kuhusu masuala ya rasilimali madini.

(g) *Kusimamia na Kuboresha Sera, Sheria, Kanuni, Mikakati na Miongozo*

108. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itafanya mapitio ya Sera ya Madini ya Mwaka 2009 na kuandaa Sera ya Uongezaji Thamani Madini na Dira ya Taifa ya Kuendeleza Sekta ya Madini (*Tanzania Mining Vision 2019 - 2035*). Vilevile, Wizara itaandaa Muswada wa kutunga Sheria ya Uongezaji Thamani Madini na Kanuni zake. Aidha, Wizara itaandaa Miswada ya Marekebisho ya Sheria zifuatazo:

(i) Sheria ya Baruti ya Mwaka 1963 na Kanuni zake za Mwaka 1964;

(ii) Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia ya Mwaka 2015; na

(iii) Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Marekebisho yake ya Mwaka 2017.

(h) Kuendelea Kuvutia Wawekezaji Wakubwa kwenye Sekta ya Madini

109. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha wa 2018/19, Serikali itaendelea kuvutia wawekezaji kwa kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji kwa wadau kuhusu fursa za uwekezaji zilizopo katika Sekta ya Madini ikiwemo kuandaa Jukwaa la Wawekezaji katika Sekta ya Madini (*Tanzania Mining Forum*); kuwezesha upatikanaji wa taarifa za kijolojia zinazohitajika katika shughuli za utafutaji wa madini na kushiriki kwenye mikutano na warsha za ndani na nje ya nchi zinazohusu shughuli za madini.

(i) Kuboresha Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini

110. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2018/19, Wizara yangu itaendelea kuboresha Mfumo wa Kielektroniki wa Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini ili kuendana na Marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 yaliyofanyika Mwaka 2017 na Kanuni zake. Pia, Wizara kupitia Tume ya Madini itaendelea kushughulikia maombi ya leseni za madini kwa wakati na kuhakikisha kuwa maombi yote yanayowasilishwa yanashughulikiwa na kujibiwa mapema iwezekanavyo. **Aidha, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Marekebisho yake ya Mwaka 2017 kwa kufuta leseni zote zinazokiuka matakwa ya Sheria hiyo ili kutoa nafasi kwa wawekezaji wengine wenye uwezo wa kuyaendeleza na maeneo mengine zaidi kutengwa kwa wachimbaji wadogo.**

(j) Mipango itakayotekelawa kupitia Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali Madini – SMMRP

111. Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kutekelezwa na Mradi wa SMMRP kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2018/19 ni pamoja na: kuanza ukarabati na upanuzi wa

majengo ya Ofisi 7 za Madini ili zitumike kama vituo vya umahiri vya masuala ya madini. Ofisi hizo ni Mpanda, Songea, Chunya, Tanga, Bariadi, Bukoba na Musoma. Vilevile, Mradi utagharimia upanuzi wa miundombinu ya Chuo cha Madini (Dodoma) kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa shughuli za madini zinazotekelvezwa na WIMA; kuendelea kukamilisha ujenzi wa Mgodi wa Mfano Lwamgasa - Geita kwa ajili ya wachimbaji wadogo na kusimika mitambo ya uchenjuaji; na kuiwezesha TEITI kutengeneza mfumo wa kuunganisha na kuzijumuisha pamoja taarifa za malipo na za uchimbaji mdogo, wa kati na mkubwa.

(k) Kuendeleza Rasilimali Watu, Kuboresha Mazingira ya Kufanya Kazi na Kuziwezesha Taasisi zilizo Chini ya Wizara

112. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza majukumu yaliyopangwa, Wizara itahakikisha inajenga ujuzi wa watumishi kwenye nyanja mbalimbali na itaboresha mazingira ya kazi, na kuwapatia vitendea kazi bora na kwa wakati. Aidha, watumishi watapatiwa elimu kuhusu afya bora, uadilifu, rushwa na madhara yake katika utumishi wa umma na Taifa kwa ujumla.

113. *Mheshimiwa Spika*, kwa kuzingatia kuwa Wizara ya Madini ni mpya katika Mwaka wa Fedha wa 2018/19 Wizara na Taasisi zake inatarajia kuajiri jumla ya watumishi 314 wa kada mbalimbali ikiwemo Wahandisi Migodi; Wajiolojia; Maafisa Rasilimali Watu; Wakufunzi wa fani za Madini; Mafundi Sanifu; Madereva na Makatibu Mahsus. Kati ya hao, watumishi 208 ni kwa ajili ya Wizara, 28 kwa ajili ya GST na 78 ni kwa ajili ya Chuo cha Madini.

114. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itaendelea kutoa elimu kuhusu masuala ya UKIMWI; na kuendelea ku wahudumia watumishi wenyewe ulemavu na wanaoishi na virusi vya UKIMWI na UKIMWI. Aidha, Wizara itaendelea ku wahamasisha watumishi kupima afya zao ili kutambua hali za afya zao ikiwa ni pamoja na kufanya mazoezi mara kwa mara.

KAZI ZITAKAZOTEKELEZWA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2018/19

(i) *Tume ya Madini*

115. Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kutekelezwa na Tume ya Madini kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19 ni pamoja na kuimarisha ukusanyaji wa Mapato yatokanayo na rasimali madini; kutathmini na kushughulikia changamoto katika utekelezaji wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Marekebisho yake ya Mwaka 2017; kutoa Mwongozo wa namna ya kutoa vibali vya kusafirisha madini nje ya nchi; kuimarisha ufuatiliaji wa ukaguzi wa usalama, afya, mazingira, utafutaji na uzalishaji wa madini katika migodi midogo, ya kati na mikubwa; kuimarisha mfumo wa kielektroniki wa kutoa na kusimamia taarifa za leseni za madini ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa leseni na kuondoa migogoro inayotokana na leseni za madini; kuimarisha udhibiti wa utoroshwaji wa madini nje ya nchi; kuimarisha shughuli za uongezaji thamani madini; kuimarisha usimamizi wa biashara ya madini na kushughulikia migogoro yote inayotokana na shughuli za madini.

(ii) *Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania - (GST)*

116. Mheshimiwa Spika, GST inatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19: kuboresha Kanzidata ya miamba na madini ya Taifa ili kuongeza uelewa wa jiolojia ya nchi na ya upatikanaji wa madini mbalimbali nchini ili kuchochaea uwekezaji katika Sekta ya Madini nchini; kuratibu shughuli za utafutaji na uchimbaji madini nchini kwa kupitia taarifa za robo mwaka za shughuli hizo ili kuhakiki usahihi wa taarifa hizo na kuboresha Kanzidata ya Taifa ya madini; kufanya uchunguzi wa sampuli za madini na miamba ili kujua viwango vya madini kwenye sampuli zinazokusanywa na watafiti na watafutaji madini kwa ajili ya kutoa idhini ya maandishi ya kusafirisha sampuli hizo nje ya nchi; kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kufanya tafiti za kijiosayansi katika utafutaji, uchimbaji salama, uhifadhi wa mazingira na uchenjuaji ili kuongeza tija katika

uzalishaji; kuboresha huduma za maabara kwa wadau wa Sekta ya Madini, Kilimo na Ujenzi; kuboresha Kanzidata ya majanga asilia ya jiolojia na kuelimisha wananchi kuhusu namna bora ya kujikinga na majanga hayo; kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya GST kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali; kuendeleza rasilimali watu na kuboresha mazingira ya kufanya kazi.

(iii) Chuo cha Madini – (MRI)

117. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2018/19, MRI inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: kuendelea na Mpango wa kukiimarisha Chuo cha Madini; kuendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi ambapo udahili wa wanafunzi wapya unatarajiwu kuongezeka kutoka wanafunzi 542 hadi 850; kuangalia uwezekano wa kuanzisha kozi mpya kwenye maeneo yanayohusiana na uchimbaji mdogo, madini ya vito na madini ya viwandani; kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya Chuo kwa kujenga jingo la wakufunzi ambalo litakuwa na ofisi za wakufunzi pamoja na Ofisi za WIMA; na kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam.

(iv) Shirika la Madini la Taifa – (STAMICO)

118. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2018/19, STAMICO imepanga kuendeleza Mradi wa Dhahabu wa Buhemba kwa kuanza kuchenjua visusu; kufanya uchorongaji ili kujiridhisha na kiasi cha mashapo kilichopo; kufanya *topographic survey* ya eneo zima la mradi; na ununuzi na usimikwaji wa vifaa vya uchimbaji na uchenjuaji pamoja na shughuli za uendelezaji wa mradi. STAMICO pia itaendeleza Mradi wa Kiwira wa kuchimba makaa ya mawe katika kilima cha Kabulo. Aidha, ili kufanikisha lengo la kuzalisha makaa ya mawe yatakayokidhi mahitaji ya soko, Shirika linatarajia kutafuta mtambo wa kusafisha makaa ya mawe (*washing plant*) katika Mradi wa Kabulo ikiwa ni sambamba na kununua mtambo wa kusaga makaa (*crusher*) hayo, kulingana na vipimo vya mteja husika. Vilevile, STAMICO inatarajia kuanza Mradi wa kuchimba kokoto katika

eneo la Ubena Zomozi mkoani Pwani. Shirika pia litaendelea kuimarisha shughuli za kibiashara za uchorongaji na utoaji wa ushauri wa kitaalam katika Sekta ya Madini na kuratibu uendelezaji wa wachimbaji wadogo nchini.

(v) *Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia – (TEITI)*

119. *Mheshimiwa Spika*, kazi zitakazoteklezwa na TEITI kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19 ni pamoja na kutoa kwa umma ripoti ya malipo ya kodi yaliyofanywa na kampuni za madini, mafuta na gesi asilia kwa Serikali kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2016/17; kuendelea kuelimisha umma kuhusu matumizi ya takwimu zinazotolewa katika ripoti za TEITI kwa njia ya matangazo, vipindi vya Redio na Televisheni, makala pamoja na warsha; kufanya marekebisho ya dosari zillizobainishwa katika tathmini ya utekelezaji wa masharti ya uanachama wa EITI ili kutimiza vigezo vya uwazi vya kimataifa vya EITI vya Mwaka 2016; na kuanzisha Rejista ya taarifa na majina ya watu wanaomiliki hisa katika kampuni za madini, mafuta na gesi asilia.

(vi) *Kituo cha Jimolojia Tanzania – (TGC)*

120. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha wa 2018/19, Kituo cha Jimolojia Tanzania kinatarajia kutekeleza yafuatayo: kuanza kutoa mafunzo ya Stashahada ya teknolojia ya Vito na Usonara (*Diploma in Gem and Jewellery Technology*); kutoa mafunzo ya muda mfupi katika fani za Jimolojia; *Gem and Jewellery Appraisal*; *Gem and Jewellery Marketing*; *Gemstone Faceting*; *Cabochon Cutting*; Utengenezaji wa bidhaa za usonara; na uchongaji wa vinyago vya miamba. Kituo pia kitaendelea na shughuli za ukataji na ung'arishaji wa madini ya vito ya wateja mbalimbali yanayowasilishwa kituoni; utengenezaji wa marumaru za mawe ya Tanga (*Tanga stones/slates*); pamoja na utengenezaji wa bidhaa mbalimbali za usonara na mapambo kama vile mikufu, hereni, bangili, vidani, vikuku na pete kwa kutumia madini mbalimbali.

5.0 SHUKRANI

121. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara ya Madini ilinufaika kwa misaada na ushirikiano kutoka kwa Washirika mbalimbali wa Maendeleo. Naomba nitumie fursa hii kuwashukuru washirika wetu wote wa maendeleo ikiwa ni pamoja na Benki ya Dunia, Umoja wa Nchi za Ulaya, Serikali za Jamhuri ya Watu wa China, Kanada, Marekani, Jamhuri ya Watu wa Korea Kusini, Misri, Japan na Australia. Serikali itaendelea kushirikiana na washirika hao na wadau wengine wa maendeleo katika kuendeleza Sekta ya Madini nchini.

122. *Mheshimiwa Spika*, pia, naomba kutoa Shukrani kwa Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT)-Taifa, UWT Mkoa wa Dar es Salaam, Viongozi na Wanachama wote wa CCM na UWT kwa kushirikiana nami na kuendelea kuniamini. Nawashukuru pia, Shirikisho la Vyama vyta Wafanyakazi kwa kuniamini kuwa mwakilishi wao katika Bunge na kwa ushirikiano wanaonipatia. Vilevile, naishukuru familia yangu kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu.

123. *Mheshimiwa Spika*, niwashukuru Manaibu wangu Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo (Mb.) na Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko (Mb.) kwa ushirikiano wao thabiti katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara. Aidha, nawashukuru Katibu Mkuu, Profesa Simon Samwel Msanjila, Mwenyekiti wa Tume ya Madini, Profesa Idris Suleiman Kikula, Makamishna wote wa Tume ya Madini, Kamishna wa Madini na Makamishna Wasaidizi, Wakurugenzi, Wakuu wote wa Idara na Vitengo, Viongozi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara wakiwemo Wenyevitii, Wajumbe wa Bodi na Watendaji Wakuu na Watumishi wote kwa ushirikiano wao na kuhakikisha kuwa rasilimali madini zinanufaisha wananchi na Taifa kwa ujumla.

Vilevile, ninalishukuru Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania chini ya uongozi mahiri wa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Jeneral Venance S. Mabeyo kwa kujitolea katika ujenzi wa

ukuta wa Mirerani na kwa ulinzi wanaoutoa katika ulinzi wa ukuta huo.

6.0 HITIMISHO

124. *Mheshimiwa Spika*, Sekta ya Madini ni muhimu katika kukuza uchumi na kutoa mchango mkubwa kwa Taifa na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025.

Aidha, ili kuhakikisha Sekta hii inainufaisha Nchi ipasavyo, Wizara itaimarisha usimamizi wake na kudhibiti utoroshwaji wa madini. Vilevile, Wizara itaendelea kuhamasisha uwekezaji katika shughuli za utafutaji, uchimbaji na uongezaji thamani madini nchini ili kuongeza mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa.

Maombi ya fedha kwa kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19

125. *Mheshimiwa Spika*, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 na Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali na kuidhinisha mapendeleko ya Bajeti ya Fungu 100 la Wizara ya Madini ya jumla ya kiasi cha **Shilingi 58,908,481,992** kwa ajili ya matumizi ya Wizara na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19. Mchanganuo wa Bajeti hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Bajeti ya Maendeleo ni **Shilingi 19,620,964,000**: Kati ya fedha hizo, **Shilingi 16,800,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 2,820,964,000** ni fedha za nje; na

(ii) Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 39,287,517,158**, ambapo **Shilingi 18,334,255,000** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 20,953,262,992** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

126. *Mheshimiwa Spika*, naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana katika Tovuti ya Wizara

kwa anuani ya www.madini.go.tz. Vilevile, Hotuba hii ina majedwali na vielelezo mbalimbali kwa ajili ya kutoa ufanuzi wa masuala na takwimu muhimu kuhusu Sekta ya Madini.

127. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana kwa hotuba yako nzuri. (*Makofii*)

Kabla sijamwita Mwenyekiti ngoja nikamilishe orodha ya pili ya wageni wa Waheshimiwa Wabunge walioko Bungeni asubuhi hii.

Mgeni wa Mheshimiwa Leah Komanya, ambaye ni Afisa Kilimo wa Wilaya Meatu Mkoani Simiyu, Ndugu Thomas Shillabu. (*Makofii*),

Wageni wawili wa Mheshimiwa Seif Gulamali ambao ni viongozi wa Wilaya ya Igunga kutoka Mkoani Tabora, karibuni kama mpo. (*Makofii*)

Wageni 25 wa Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, ambao ni Waheshimiwa Madiwani, Makada wa CCM na Watumishi wa Halmashauri ya Longido kutoka Mkoani Arusha wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido, Ndugu Kennedy Ole Moloimet. (*Makofii*)

Wageni 15 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni Viongozi wa Kanisa na Kwaya yao *Potter's House* kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mchungaji Israel Wandamba. Karibuni sana. (*Makofii*)

Wageni 21 wa Mheshimiwa Hassan Masala, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Mikoa ya Lindi na Mtwara. (*Makofii*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu, ambao ni viongozi wa CCM kutoka Mkoaa wa Tabora. (*Makofii*)

Wageni 20 wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, ambao ni wanamaombi wanaotoka hapa hapa Dodoma. (*Makofii*)

Wageni 17 wa Mheshimiwa Asha Juma, ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Mipango kutoka Jijini Dodoma. (*Makofii*)

Wageni 87 wa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, ambao ni Wanachama wa Shirika la Umoja wa Machinga Tanzania. Machinga Tanzania, karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni wa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Aweso Juma ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Mipango wakiongozwa na Spika wao wa Bunge lao la Chuo cha Mipango, Ndugu Hanif Ally Hassan, nakumbuka hawa niliwataja mapema. Karibuni sana hata hivyo. (*Makofii*)

Nimekamilisha orodha ya matangazo, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini, namwona Mwenyekiti mwenyewe, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, karibu sana. (*Makofii*)

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA - MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingu wa rehema, ambaye ametupatia uhai na kwamba tunaweza kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia matakwa ya kanuni ya 99(9) na kanuni ya 117(11) cha Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2017/2018, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa yote ya Kamati iingie katika taarifa rasmi za Bunge. Katika utekelezaji wa majukumu ya kikanuni, Kamati ilifanya vikao kadhaa kwa

lengo la kupokea na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na kufanya uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Pia Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa mwaka wa 2017/2018 pamoja na miradi mingine inayosimamiwa na Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la ziara hizi ilikuwa ni kujiridhisha na ufanisi wa utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na kuhakiki thamani ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha; kwa kuzingatia masharti ya kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2016, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi katika Mikoa ya Mara na Tabora mahususi Nzega na lengo ilikuwa ni kujiona utekelezaji wa bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa kwa mwaka 2017/2018. Miradi iliyokaguliwa ni kama ifuatavyo:-

Mradi wa kwanza ilikuwa mgodi wa dhahabu wa Buhemba; mradi wa pili ilikuwa Chuo cha Madini, Campus ya Nzega; na mradi wa tatu ilikuwa ni mgodi wa wachimbaji wa kati (*CATA Mining*). Maelezo yote ya matokeo ya ukaguzi wa miradi hiyo yapo ndani ya taarifa kubwa kama yanavyosomeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kufuatia hali halisi ambayo Kamati iliona wakati wa ukaguzi wa miradi, Kamati inatoa ushauri ufuataao:-

(a) Wizara ifanye upya tathmini ya uwekezaji katika migodi yote inayorithiwa na *STAMICO* ili kuona kama kuna faida na sababu ya kuendelea na uwekezaji huo. Endapo itaonekana hakuna faida, basi Kamati inaona ni vyema maeneo hayo yakagawiwa kwa wachimbaji wa kati ili waweze kuyaendeleza kuepusha migogoro isiyo ya lazima kwa wananchi.

(b) Kutokana na athari za mazingira iliyoachwa na mwekezaji wa mgodi wa *Resolute* wakati anafunga shughuli zake katika eneo hilo, ni vema Wizara ikakamilisha taratibu zote muhimu zinazotakiwa ili chuo hicho kiweze kukabidhiwa katika Kitivo cha Uhandisi Migodi cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili kutimiza malengo mahususi ya kuanzishwa kwa Chuo hicho.

(c) Ofisi wa Waziri Mkuu iingilie kati suala la Mgodi wa *CATA Mining* kwa kuzikutanisha Wizara za Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Wizara ya Madini ili kupata ufumbuzi wa haraka ya kadhia ili yopo ambayo inatishia mwekezaji aliye po sasa kufilisiwa na mabenki kutokana na kushindwa kuendana na ratiba ya urejeshaji mikopo aliyo chukua kuendeshea mgodi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba mwekezaji huyu ameonesha kwa vitendo nia ya dhati ya kuwekeza na kuendeleza Sekta ya Madini kwa kulipa kodi na tozo mbalimbali kwa Serikali pamoja na kutoa ajira kwa Watanzania takriban 400 wanaozunguka eneo hilo.

(d) Upatikanaji wa fedha za kutosha kwenye miradi ya maendeleo utaongeza kwa kiasi kikubwa makusanyo ya maduhuli kama inavyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa Mwaka 2017/2018. Kazi zilizotekelawa na Idara ya Madini katika kipindi cha kuanzia 2017 hadi mwezi Februari, 2018 zili kuwa ni uthaminishaji wa madini ya vito, usimamizi wa mnada wa *Tanzanite* pamoja na biashara ya madini mbalimbali kama ifuatavyo:-

(a) Madini ya *Tanzanite*; Kamati inapongeza jitihada za Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwenye Sekta ya Madini ya Vito hususan madini ya *tanzanite* kwa maamuzi ya kizalendo ya kujenga ukuta kuzunguka eneo la Mgodi wa *Tanzanite*, Mererani zenye lengo la kuongeza udhibiti katika mfumo mzima wa biashara ya *tanzanite* katika soko la ndani na la nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali za kusimamia biashara hii, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa madini haya yanapata Hati ya Uasilia (*Certificate of Origin*) ili kuweza kudhibiti madini hayo katika soko la nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zilizochukuliwa na Serikali kuendelea udhibiti wa biashara holela ya *tanzanite* katika soko la ndani na la nje, hali ambayo kimsingi uholela huo unasababisha kushuka kwa thamani ya *tanzanite*. Kwa mfano, mnada uliofanyika Desemba, 2017 kilo 47 ndizo zilizouzwa kati ya kilo 535.99 zilizochimbwa. Aidha, kilo 448 zimehifadhiwa katika Benki Kuu Tawi la Arusha pamoja na maghala ya mgodi ili kuruhusu bei nzuri ya soko la *tanzanite* iweze kupanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri kuwa taratibu endelevu zinazoandalisha na Wizara kuhusu mnada wa *Tanzanite* zikamilishwe kwa haraka ili kuboresha Mnada huo ambaao ndiyo tegemeo kubwa kwa wachimbaji na wafanyabiashara ya madini ya *tanzanite*. Mnada huu ukiratibiwa vizuri utaongeza tija ya uwepo wa madini hayo hapa nchini.

(b) Madini ya Almasi; Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutekeleza ushauri na maoni ya Kamati Maalum uliyoiundwa ya kufuatilia mfumo mzima wa biashara ya madini ya almasi hapa nchini, kwani baada ya kuimarisha usimamizi katika mgodi wa Mwadui, katika kipindi cha Julai hadi Februari, 2018, Karati 3.047 zilizalishwa na Karati 137,257.94 zilisafirishwa nje ya nchi. Almasi hiyo ilikuwa na thamani ya dola milioni 32.7 ambayo ni sawa na shilingi bilioni 72.9 na mrabaha wa dola za Marekani milioni 2.25 sawa na shilingi bilioni 5.02 ulilipwa Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Wizara kutoa takwimu na taarifa zote za uzalishaji wa madini ya almasi kutoka kwenye migodi mingine hapa nchini ili kujua mchango wake katika makusanyo ya Taifa letu.

(c) Madini mengine ya vito; nchi yetu ina utajiri mkubwa sana wa madini mengine ya vito kama vile *Ruby*, *Sapphire*, *Garnet*, *Tourmaline*, *Emerald*, *Scapolite*, *Tsavorite* pamoja na *Alexandrite* inayopatikana Wilayani Tunduru pekee. Aina hii ya madini ina thamani kubwa katika soko hivyo ni vema Wizara ikaweka utaratibu mzuri utakaowezesha kuchimbwa kwa madini hayo ili yaweze kuchangia katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Madini hajjaweza kuripoti mchango wa madini mengine ya vito pamoja na uwepo wake katika mikoa yote nchini. Kamati inaishauri Wizara kuwa taarifa zote za madini yanayozalishwa nchini zinapatikana ili kujuu mchango wa madini hayo katika makusanyo ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, madini ya dhahabu. Katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Februari, 2018 jumla ya kilo 31,450 sawa na wakia milioni 1.01 zilizalishwa na kusafirishwa nje ya nchi na migodi yote mikubwa na ya katihapa nchini. Uzalishaji huu umepungua kwa asilimia 28 kutoka wakia milioni 1.42 zilizozalishwa mwaka 2016 pamoja na wakia milioni 1.36 zilizozalishwa mwaka 2015. Kushuka kwa uzalishaji wa madini hayo kumechangia pia kushuka kwa makusanyo ya malipo ya mrabaha wa awali kulinganisha na miaka iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakikishe, mchakato wa uanzishaji wa *smelter* hapa nchini unakamilika kwa haraka ili kuhakikisha kuwa madini yetu yanauzwa yakiwa yameongezewa thamani kama inavyotakiwa na Sheria ya Madini pamoja na Marekebisho yake ya mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasikitishwa na mchango hafifu kutoka kwa wachimbaji wadogo kwenye makusanyo ya mrabaha pamoja na Serikali kutoa ruzuku kwa baadhi ya wachimbaji wadogo ambapo mnufaika wa chini alipata dola za Marekani takriban 50,000 sawa na takriban shilingi milioni 100 na mnufaika wa juu

alipata dola za Marekani 100,000 sawa na takriban shilingi milioni 200 kwa kila mchimbaji katika awamu zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa za makusanyo ya maduhuli kwa kipindi tajwa, hakuna mchango wa wachimbaji wadogo uliopatikana katika makusanyo ya mrabaha. Aidha, kukosekana kwa taarifa za uzalishaji wao, ni ishara tosha kuwa madini haya huuzwa katika soko lisilo rasmi na hivyo kushindwa kuwanufaisha wachimbaji wenye na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Wizara kuimarisha usimamizi wa wachimbaji wadogo ili kuhakikisha kuwa madini yote yanayozalishwa yanaingia katika mfumo rasmi wa ulipaji wa kodi za Serikali ili na wao wachangie katika pato la Taifa kama yalivyo malengo ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madini ya ujenzi na viwandani; Kamati hairidhishwi na makusanyo kidogo tunayopata kama nchi kutoka kwenye madini ya ujenzi na viwandani, jumla ya shilingi bilioni 1.62 tu za mrabaha zililipwa Serikalini pamoja na uwepo wa madini hayo kwa wingi hapa nchini. Aidha, Kamati hairidhishwi na uwekezaji usio na tija unaofanywa na *STAMICO* kushindwa kuhodhi soko la madini hayo ili kuongeza makusanyo kama inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Wizara kuwa kama *STAMICO* inashindwa kuendeleza Migodi ya Madini ya Ujenzi kama ule wa Ubena Zomozi ni vema wakapewa wachimbaji wenye nia ya kuendeleza migodi hiyo na *STAMICO* ikabaki na kazi ya kutoa ushauri wa kitaalam na Serikali ikabaki na kazi yake ya kukusanya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madini ya bati; Kamati inasikitishwa na sababu zinazotolewa na Wizara ya Madini za kushindwa kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Bati kwa ukosefu wa fedha za mtaji wa kununulia mtambo wa kuchakata bati pamoja na ukosefu wa Hati ya Uasili inayosababisha madini hayo kushindwa kuuzwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zinazotolewa na Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*) kimsingi siyo changamoto ambazo wameshindwa kuzipatia ufumbuzi kama Shirika na Wizara yenye dhamana ya Madini nchini. Kamati inaona kuwa kusimama kwa mradi huo siyo kutokana na ukosefu wa mtaji kama inavyoripotiwa bali ni kukosekana kwa utashi wa Serikali kuendelea na utekelezaji wa mradi wa madini hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali inaendelea kusuasua katika uendelezaji wa mradi huo, ripoti ya Benki ya Dunia kuhusu bei ya soko la bidhaa katika *World Bank Community Price Forecast* ya April, 2018 bei ya bidhaa hiyo inatarajiwa kupanda kutoka dola za Marekani 20,225 kwa tani kwa mwaka 2017 hadi kufikia dola 23,000 kwa tani ifikapo mwaka 2030. Hivyo basi, Wizara ya Madini iweke mpango mkakati wa kiuwekezaji kwa ajili ya kuendeleza mradi huo wa madini ya batii kwa kuwa taarifa za Benki ya Dunia zinaonesha wazi kuimarika kwa soko la madini hayo duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makaa ya mawe; Kamati haioni nia ya dharti ya Serikali ya kuendeleza Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira kwa kushindwa kupeleka fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu ambayo ni jumla ya shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kuendeleza shughuli mbalimbali za mgodi huo, pamoja na uhitaji mkubwa wa madini hayo katika viwanda mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Februari, 2018 jumla ya tani 2,477 zenye thamani ya Sh.158,528,000/= zimezalishwa. Takriban ni mwaka mzima sasa makaa hayo hayajaweza kuuzwa kutokana na sababu mbalimbali zilizosemwa na *STAMICO* kuwa ni ukosefu wa miundombinu ya barabara. Kamati inaishauri Wizara ya Madini kushirikiana na Halmashauri husika pamoja na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ili ziweze kutengeneza barabara hiyo ambayo ni muhimu sana kwa ustawi na maendeleo ya mgodi pamoja na Halmashauri hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgodi wa makaa ya mawe wa Ngaka umeendelea kufanya shughuli za uzalishaji ambapo jumla ya tani 340,000 zenye thamani ya dola za Marekani 15,500,000 zilizalishwa na kuuzwa ambapo Serikali ililipwa mrabaha wa jumla ya dola za Marekani 466,345. Kamati inaishauri Wizara kuwa ni vema sasa wakafanya maamuzi thabitibya kabisa ya kuwekeza kwenye miradi ambayo uhitaji wake katika soko la ndani umeongezeka zaidi baada ya zuio la Serikali la uingizaji wa madini hayo kutoka nje. Aidha, ni matumaini ya Kamati kuwa kama uwekezaji huo utafanyika utaongeza makusanyo ya Serikali na hasa mrabaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuonesha uzalendo wake wa dhati katika kulinda rasilimali za madini ambazo ziliikuwa hazilinuafishi Taifa ipasavyo kwa kuunda Tume ya Madini ambayo itakuwa na jukumu la kusimamia ipasavyo maendeleo ya Sekta hii ya Madini nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka 2017/2018. Wizara ya Madini ilipanga kukusanya maduhuli jumla ya shilingi bilioni 194.39 kutoka vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 28 Februari, jumla ya maduhuli ya shilingi bilioni 200.68 zilikusanywa kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya Wizara ya Madini. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 103 ya lengo walilokuwa wamejiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Taarifa ya Hali ya Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina. Hadi kufikia Februari 28, 2018 iliyokuwa Idara ya Madini ambayo ndiyo Wizara ya Madini sasa, ilikuwa imepokea Shilingi bilioni 15.67 ambayo ni sawa na asilimia 13.69 tu ya bajeti ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kiwango hicho cha fedha kilikuwa katika mgawanyo ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za Miradi ya Maendeleo zilizopokelewa zilikuwa shilingi milioni 834 sawa na asilimia 3.83 ya bajeti iliyotengwa na shilingi bilioni 6.7 sawa na asilimia 51 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni nane sawa na asilimia 51 kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasikitishwa na utolewaji wa fedha za miradi usioridhisha kwani hadi kufikia tarehe 28 Februari, Wizara ya Madini ilipokea asilimia tatu tu ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi Fungu 100 kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Makisio ya makusanyo ya maduhuli yanakadiriwa kuwa jumla ya shilingi bilioni 321.6 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ikilinganishwa na shilingi bilioni 194.3 zillizokadiriwa kukusanywa kwa mwaka 2017/2018. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 60.84.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya makusanyo yote kwa mwaka wa fedha 2018/2019 shilingi bilioni 310.5 sawa na asilimia 99.34 zitawasilishwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, shilingi bilioni 2.074 sawa na asilimia 0.66 zitatumika kwa ajili ya kuendeshea shughuli za Taasisi na Wakala zilizoko chini ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019, Wizara ya Madini imeomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 58.908 ikilinganishwa na shilingi bilioni 52.44 zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu katika mwaka wa fedha 2017/2018. Bajeti hii imeongezeka kwa asilimia 11.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hili la bajeti limetokana na uwepo wa Tume ya Madini ambayo inatarajia kuongeza watumishi wengine wapya kwa ajili ya kuendeleza majukumu mapya ya Tume hiyo. Kamati inasitiza Serikali kuhakikisha fedha zinatoka kwa wakati ili Tume hii yenye majukumu makubwa iweze kutekeleza majukumu yake kama inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hairidhishwi na mwenendo wa Serikali kuendelea kutenga fedha kidogo katika miradi ya kimkakati ambayo inahitaji fedha nyingi kama vile miradi wa makaa ya mawe Kiwira na Kabulo. Miradi hii ili iweze kuanza uzalishaji wenye tija ambao tunautarajia kama Taifa zinahitajika fedha za kutosha. Kwa hiyo, Serikali ione umuhimu wa kutoa kipaumbele katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kuwa, kwa kuwa fedha hizo zilizotengwa kwa ajili ya Mradi wa Kabulo hazitatosha kukidhi uzalishaji wenye tija ni bora zikaelekezwa katika mradi mwingine kama vile Mradi wa Kokoto ili uweze kuongeza uzalishaji na kisha kuongeza makusanyo ya Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitoe maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Kamati yako imetekeleza majukumu yake ya msingi yaliyoainishwa katika Kanuni ya 98. Hivyo basi, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao kwa Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kuisisitiza Wizara kuhakikisha inafuatilia fedha za ruzuku zilizotolewa na Serikali kwa wachimbaji wadogo wadogo katika awamu zote mbili. Pia Wizara ihakikishe inafanya upembuzi yakinifu kabla ya kutoa rukuzu awamu nyingine ili kuepuka changamoto zilizojitokeza katika awamu zilizotangulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Kamati hairidhishwi na mwenendo wa utekelezaji wa shughuli za Mgodi wa *STAMIGOLD* kwa sababu lengo la kuanzishwa kwa mgodi huo limeshindwa kutimia na badala yake umekuwa ukizalisha madeni makubwa takribani, bilioni 60 sasa. Wizara iangalie namna bora ya kuendesha mgodi huo au kuufunga kama itaona inafaa kwa maslahi ya Taifa kuliko kuendelea na uzalishaji usio na faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Kamati inaitaka Wizara ya Madini kufanya tathmini na kujiridhisha kama kweli kuna faida tutakayoipata kama nchi kuwekeza fedha shilingi bilioni

8.6 zinazoombwa kwa ajili ya kuendeleza Mgodi wa Buhemba, ilhali hakuna faida tunayopata mpaka sasa katika uwakezaji uliofanyika katika Mgodi wa *STAMIGOLD* zaidi ya kuzalisha madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, Kamati inaona ni vema Mgodi wa Buhemba na ule wa *STAMIGOLD* wapewe wachimbaji wa Kati wenye nia ya kuuendeleza. Hii itakuza Sekta ya Wachimbaji wa kati nchini ambao wameonesha kuwa na mchango mkubwa katika makusanyo ya mapato na Serikali ibaki kwenye ukusanyaji wa mapato pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, Kamati inaendelea kuishauri tena Wizara kupitia upya Mkataba wa Ubia kati ya *STAMICO*na *TANZAM* 2000 ulioingia mwaka 2011 kuendeleza Mgodi wa *BUCKREEF*, kwa kuwa mkataba huo umedhihirika kutokuwa na manufaa ya kiuchumi katika kuendeleza mgodi huo licha ya uwepo wa mashapo yenyе uhakika wa kuzalisha dhahabu na kuliingizia Taifa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, kwa kuwa miradi ya makaa ya mawe imeonekana kuwa na mchango unaoridhisha kwenye makusanyo ya mrabaha takribani dola za Marekani 466.3 zilipatikana kutokana na mauzo ya makaa ya mawe katika Mgodi wa Ngaka. Hivyo basi, Kamati inashauri kuwa miradi yote ya makaa ya mawe ni vyema Serikali ikatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuendeleza miradi hiyo kwa kuwa uhitaji wa malighafi hiyo ni mkubwa sana hapa nchi baada ya zuio la Serikali la kuagiza makaa hayo toka nje ya nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa mwenyekiti, nane, Wizara ya Madini iweke mpango mkakati wa kiuwekezaji kwa ajili ya kuendeleza miradi ya batii kwa kuwa taarifa za Benki ya Dunia zinaonesha wazi kwamba kutakuwa na faida kubwa na bei ya bidhaa itaendelea kupanda hadi kufikia mwaka 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tisa, Wizara kuangalia upya mikataba yote tulioingia na wawekezaji wanaowekeza

katika uchimbaji wa makaa ya mawe ili kujiridhisha kama nchi inafaidika na uwepo wa Kampuni hizo katika uendelezaji wa makaa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi, Serikali iangalie namna bora ya kuwezesha Wakala wa Jiolojia nchini ili iweze kufanya tafiti za madini yote nchini na kuwa na Kanzidata ambayo itatumiwa na wawekezaji toka nje. Hii itapunguza athari kubwa za kimazingira zinazosababishwa na watafiti kutoka nje ya nchi ambao wakimaliza tafiti zao nchi hainufaiki na tafiti zilizofanywa kwenye rasilimali zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi na moja, Wizara ibuni na kuwa na mkakati endelevu wa vyanzo vingine vipyta vyta ukusanyaji wa mapato kuliko kutegemea tozo za madini pekee. Kwani ikitokea uzalishaji wa madini umeshuka Wizara inakosa mapato tullyotarajia kama nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini kwa umahiri wao walioonesha wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii. Wajumbe hawa wamefanya kazi kwa ari kubwa na hatimaye kukamilisha taarifa hii. Naomba kuwatambua Wajumbe hawa kwa majina yao na naomba yaingie kwenye *Hansard* kama yalivyoorodheshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima ya pekee naomba kukushukuru wewe binafsi, kumshukuru Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi mzuri wa Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati kwa Mheshimiwa Angella Kairuki, Waziri wa Madini, pamoja na Manaibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo na Mheshimiwa Doto Biteko pamoja na Watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu, Profesa Simon Msanjila kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati yetu wakati wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naomba nimshukuru Katibu wa Bunge, Ndigu Steven Kagaigai; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athuman Hussein; Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Michael Chikokoto; pamoja na Makatibu wa Kamati, Ndugu Mwanahamisi Munkunda na Ndugu Felister Mgonja; pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Grace Mwenye kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha Taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee naomba niwashukuru wananchi wangu wa Mkinga kwa kuniamini na kuendelea kuniunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 100 - Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019 ambayo ni Sh.58,908,481,992/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA
MADINI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA
MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 PAMOJA NA
MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 –
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 99 (9) na Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, Katika utekelezaji wa majukumu ya kikanuni Kamati ilifanya vikao kadhaa kwa lengo la kupokea na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na kufanya uchambuzi wa makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Pia Kamati ilifanya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; pamoja na miradi mingine inayosimamiwa na Wizara ya Madini. Lengo ni kujiridhisha na ufanisi wa utekelezaji miradi hiyo pamoja na kuhakiki thamani ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inaonesha matokeo ya shughuli zilizotekelawa katika kipindi tajwa pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati.

2.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2017/2018

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayotekelawa chini ya Wizara ya Madini. Ziara hizo ilifanyika katika Mikoa ya Mara na Tabora (Nzega). Lengo la ziara ni kujiona Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, miradi iliyokaguliwa ni kama ifuatayo:-

- i) Mgodi wa Dhahabu wa Buhemba
- ii) Chuo cha Madini Kampasi ya Nzega
- iii) Mgodi ya Wachimbaji wa Kati (CATA Mining)

2.1 Maelezo na Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

2.1.1 Mgodi wa Dhahabu wa Buhemba

Mheshimiwa Spika, Kamati yako ilifanya ukaguzi katika Mgodi unaomilikiwa na Serikali kuititia STAMICO wenyewe leseni ya utafiti (Prospecting Licence) namba PL 7132/2011 uliopo Wilayani Butiama, Mkoa wa Mara.

Mradi huu umegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni uchenjuaji wa mabaki ya dhahabu yaliyoachwa katika kipindi cha Wakoloni na pili ni uchimbaji wa dhahabu katika Miamba migumu iliyothibitika kuwa na mashapo yenyе **wakia 441,772 katika migodi ya 1, Buhemba, 4, Kilamongo South na Kilamongo North** baada ya kufanyika kwa upembusi yakinifu katika Migodi hiyo ya wazi. Aidha, ukadiriaji wa mashapo katika mashimo ya Buhemba Main na Mwizi unaendelea kufanywa na Shirika letu la Madini kadri fedha zinavyoendelea kupatikana.

Mheshimiwa Spika, katika ukaguzi huo Kamati ilielezwa kuwa, ili kuweza kutekeleza mradi huo jumla ya **Shilingi bilioni 8,936,337,023** zinahitajika, ambapo **Shilingi bilioni 6,421,081,912** zitatumika kununua mitambo ya uchimbaji na uchenjuaji na **Shilingi bilioni 2,515,255,111** kwa ajili ya gharama za uendeshaji katika kipindi cha miezi mitatu ya awali ya utekelezaji wa mradi. Aidha, faida ya **Shilingi bilioni 15,655,197,502** inategemewa kutengenezwa kama fedha za uwekezaji zitapatikana.

Mheshimiwa Spika, toka Mwaka 2011 Mgodi ulivyokabidhiwa kwa STAMICO hakuna shughuli yoyote ile ya uchimbaji wala uchenjuaji iliyowahi kufanyika na sababu kubwa ikiwa ni ukosefu wa fedha kwa Shirika hilo pamoja na Mwekezaji atakayekubali kuwekeza katika Mgodi huo.

Aidha, Stamico kushindwa kuendeleza Mgodi huo kwa muda mrefu kumesababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu ya Mgodi, upotevu wa vifaa na uvamizi mkubwa wa Wachimbaji wadogo wadogo katika eneo hilo hali ambayo inahatarisha sana usalama wa maisha yao.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo Migodi mingine inayomilikiwa na STAMICO kurithi madeni makubwa kutoka kwa wawekezaji waliofunga shughuli zao hapa nchini, pia Mgodi wa Buhemba unakabiliwa na deni la **Shilingi milioni 89,021,324** linalotokana na mapunjo ya mafao ya wafanyakazi wa zamani walioachishwa kazi mwaka 2007 wakati Mgodi huo unamilikiwa na Kampuni ya Meremeta.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashindwa kuelewa ni kwa nini Wawekezaji wanapofunga shughuli zao katika Migodi mingi hapa nchini wamekuwa wakiacha Madeni makubwa, ambayo hubebwa na STAMICO wanapokabidhiwa Migodi hiyo na Serikali. Aidha, sintofahamu ya Madeni hayo imeendelea kuwa mzigo kwa Wizara na Serikali kwa ujumla kwa kuwa STAMICO hutakiwa kuyalipa Madeni hayo pale wanapokabidhiwa Migodi hiyo, pamoja na uwepo wa takwa la Kisheria la kuzingatia Wawekezaji wote wanapofunga shughuli zao wanaacha mazingira katika hali nzuri na Madeni yote yamelipwa hususani Kodi na Tozo mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto nyingine nyingi ambazo Kamati ilizibaini katika Mgodi huo ni dhahiri kuwa siyo rahisi kwa Serikali kupata faida kama itaamua kuwekeza. Aidha, uwekezaji huo utakuwa kama ule wa STAMIGOLD ambapo toka kuanzishwa kwake Mgodi huo haujawahi kutengeneza faida zaidi ya kutengeneza hasara (Madeni makubwa) ambayo yamekuwa mzigo mkubwa kwa Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Wizara ya Madini kufanya tathmini upya ya Uwekezaji katika Migodi yote iliyorithiwa na STAMICO ili kuona kama kuna faida na sababu ya kuendelea na Uwekezaji huo. Ni vyema maeneo hayo wakawapatia Wachimbaji wadogo na wa Kati ili waweze kuyaendeleza kuepusha migogoro isiyo ya lazima na wananchi wetu.

2.1.2 Chuo cha Madini Kampasi ya Nzega

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi katika chuo cha madini Kampasi ya Nzega, Mkoani Tabora lilipokuwa eneo la Mgodi wa Resolute. Eneo hili la Mgodi pamoja na rasilimali zake lilikabidhiwa rasmi kwa Chuo cha Madini tarehe 12 Disemba, 2014 kutoka kwa Kampuni ya uchimbaji madini ya Resolute (Tanzania) Ltd baada ya Kampuni hiyo kufunga shughuli za uzalishaji wa Madini.

Mheshimiwa Spika, Kampasi hii ilianzishwa mahsus i kwa ajili ya kutekeleza dhima na malengo ya Chuo cha Madini ambayo ni; kuongeza wataalam wa kada ya kati katika sekta ya Madini katika fani za Jiolojia na Utafutaji wa Madini, Uhandisi Uchimbaji na Uchenjuaji Madini, Usimamizi wa Mazingira Migodini na Upimaji wa Ardhi na Migodi.

Pili ilikuwa ni upanuzi wa Chuo hicho ili kiweze kuendesha shughuli zake kwa ufanisi zaidi kwa sababu ya uwepo wa migodi (*Pits*) ambayo itawezesha wanafunzi kujifunza kwa vitendo. Na tatu ilikuwa ni kuifanya Kampasi ya Nzega kuwa Kitovu cha Mafunzo (*Centre of Excellence*) kwa ajili ya kutoa mafunzo ya rasilimali za madini na mazingira kwa wachimbaji Wadogo Wadogo.

Mheshimiwa Spika, toka eneo hilo limekabidhiwa kwa Chuo hicho mwaka 2014 hakuna shughuli yoyote ile ya Kitaaluma iliyokwisha fanyika katika eneo hilo, pamoja na uwepo wa Miundo mbinu inayofaa kufundishia. Hali hiyo imesababisha eneo hilo kuvamiwa na Wachimbaji wadogo mara kwa mara hivyo kusababisha uharibifu mkubwa wa rasilimali na miundo mbinu ya chuo hicho.

Mheshimikwa Spika, kutokana na athari ya Mazingira ilioachwa na mwekezaji wakati anafunga shughuli zake katika eneo hilo, ni vema Wizara ikakamilisha taratibu zote muhimu zinazotakiwa ili chuo hicho kiweze kukabidhiwa katika kitivo cha Uhandisi Migodi cha Chuo kikuu cha Dar Es Salaam ili kutimiza malengo mahsus i ya Chuo cha Madini.

2.1.3 Mgodi wa Mchimbaji wa Kati (CATA Mining)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ukaguzi katika mgodi wa mchimbaji wa kati katika kijiji cha Kiabakari Mkoani Mara na kujiona uwekezaji katika Mgodi wa dhahabu wa Cata Mining. Mgodi huu unamilikiwa kwa ubia wa asilimia 50 kwa 50 kati ya mtanzania na Mwekezaji kutoka Canada kupitia **leseni namba 483/2015** iliyotolewa mwaka 2014.

Mwaka 2015, CATA Mining iliingia makubaliano na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), kuchenjua mabaki ya mchanga ulioachwa na wachimbaji wa kikoloni na Novemba, 2016, Kampuni hiyo iliingia mkataba mwiningine tena na Jeshi hilo kwa ajili kufanya utafiti wa Madini ya dhahabu katika mgodi wa Kiabakari kupitia leseni namba PL 10645/2015.

Mheshimiwa Spika, Mikataba yote miwili iliyoingiwa na pande hizi mbili ilikuwa na lengo la kugawana faida, ambapo hadi sasa JWTZ imelipwa jumla ya **Dola 690,550**, sawa na **Shilingi billioni 1.3** ikiwa ni sehemu ya makubaliano ya mkataba wa uchenjuaji wa mchanga (**Tailings**).

Mheshimiwa Spika, Mgodi huu unazalisha zaidi ya kilo **303.674** za dhahabu kwa Mwaka, na kulipa mrahaba jumla ya **shilingi 1.085 billion** pamoja na tozo mbalimbali zinazofikia jumla ya **shilingi billioni 1.0**. Kampuni imekwishalipa jumla ya **Dola 529,000.00**, sawa **Shilingi 1,140,788,500/=**, kiasi ambacho kinashinda tenda ya Mgodi wa Kiabakari. Pia Mgodi huo umetoa ajira kwa Watanzania takribani 400 hususani Vijana wanaozunguka eneo hilo la Mgodi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikishwa na sintofahamu inayoendelea kati ya JWTZ na Kampuni ya CATA Mining kupitia leseni namba PL 10645/2015. Kusimamisha uendelezaji wa leseni hiyo kwa katazo kutoka upande wa pili wa Mkataba huo ambaye ni JWTZ. Kitendo hicho ni kumnyima haki Mwekezaji huyo ambaye kimsingi alishafanya uwekezaji mkubwa kwa kutumia fedha za mkopo kutoka katika kwenye mabenki mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa; toka awali JWTZ lilikubali kuingia Mkataba na Mwekezaji huyo kwa vigezo walivyokubaliana katika kuendeleza leseni hiyo, kusimamisha ghafla shughuli za uzalishaji za Mgodi huo imesababisha hasara kubwa kwa Mwekezaji kutokana na gharama alizokwisha ingia katika kuendeleza leseni hiyo.

Na kwa Kuwa; Sheria ya Madini Na. 14 ya Mwaka 2010 katika kifungu cha 95(1) a (v) inamzuia Mmiliki wa leseni ya Madini katika baadhi ya maeneo ambayo yanahitaji Idhini/ Kibali Maalumu kutoka kwa Mamlaka/Waziri mwenye dhamana na eneo hilo kumruhusu mtu huyo kuingia katika eneo hilo na kufanya shughuli zake kwa mujibu wa leseni yake.

Kwa msingi wa kifungu hicho JWTZ ilisharuhusu Mwekezaji huyo kuendeleza leseni hiyo katika eneo hilo kwa makubaliano ya kugawana faida, Kamati inashauri kuwa Kuendelea kumzuia na kumsimamisha Mwekezaji huyo kufanya shughuli zake katika eneo hilo ni kumsababishia hasara ambazo kimsingi zinapunguza mapato ya Serikali na Halmashauri husika.

Hivyo basi, Ni vyema Ofisi ya Waziri Mkuu ikaingilia kati jambo hili kwa kuzikutanisha Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Wizara ya Madini ili kupata ufumbuzi wa haraka wa kadhia hii, ambayo inatishia mwekezaji huyu kufilisiwa na mabenki kutokana na kushindwa kuendana na ratiba ya urejeshaji mikopo aliyochukua kuendeshea mgodi huu.

Ikumbukwe kuwa mwekezaji huyu ameonesha kwa vitendo nia ya dhati kuwekeza na kuendeleza Sekta ya Madini kwa kulipa Kodi na tozo mbalimbali kwa Serikali pamoja na kuajiri Watanzania takribani 400 katika fani mbalimbali.

2.2 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/18

Mheshimiwa Spika, kufuatia hali halisi ambayo Kamati iliona wakati wa Ukaguzi wa Miradi; inatoa ushauri kwamba:-

a) Kufanya tathmini upya ya Uwekezaji katika Migodi yote iliyorithiwa na STAMICO ili kuona kama kuna faida na sababu ya kuendelea na Uwekezaji huo. Kamati inaona ni vema maeneo hayo wakawapatia Wachimbaji wa Kati ili waweze kuyaendeleza kuepusha migogoro isiyo ya lazima kwa wananchi;

b) Kutokana na athari ya Mazingira iliyoachwa na mwekezaji wa Mgodi wa Resolute wakati anafunga shughuli zake katika eneo hilo, ni vema Wizara ikakamilisha taratibu zote muhimu zinazotakiwa ili chuo hicho kiweze kukabidhiwa katika kitivo cha Uhandisi Migodi cha Chuo kikuu cha Dar Es Salaam ili kutimiza malengo mahsus ya Chuo cha Madini, na

c) Ofisi ya Waziri Mkuu iingilie kati jambo hili kwa kuzikutanisha Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Wizara ya Madini ili kupata ufumbuzi wa haraka wa kadhaa hii, ambayo inatishia mwekezaji huyu kufilisiwa na mabenki kutokana na kushindwa kuendana na ratiba ya urejeshaji mikopo aliyochukua kuendeshea mgodi huu.

Ikumbukwe kuwa mwekezaji huyu ameonesha kwa vitendo nia ya dhati kuwekeza na kuendeleza Sekta ya Madini kwa kulipa Kodi na tozo mbalimbali kwa Serikali pamoja na kuajiri Watanzania takribani 400 katika fani mbalimbali;

d) Upatikanaji wa fedha za kutosha kwenye miradi ya Maendeleo itaongeza kwa kiasi kikubwa makusanyo ya Maduhuli kama inavyotakiwa.

2.3 Uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa Mwaka 2017/2018

Mheshimiwa Spika, kazi zilizotekelzwa na Wizara ya Madini katika kipindi cha kuanzia Julai 2017 hadi Februari, 2018 zilikuwa ni kuimarisha usimamizi na udhibiti wa rasilimali zetu kwa lengo la kuongeza makusanyo ya Maduhuli kwa Serikali. Kazi zilizotekelzwa na Idara ya Madini zilikuwa ni

uthaminishaji wa Madini ya vito, usimamizi wa mnada wa Tanzanite pamoja na biashara ya Madini mbalimbali kama ifuatavyo;

2.3.1 Madini ya Vito ya Tanzanite ,Almasi na Madini mengine ya Vito nchini

(a) Madini ya Tanzanite

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza jitihada za Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwenye Sekta ya madini ya Vito hususani madini ya Tanzanite kwa maamuzi ya kizalendo ya kujenga Ukuta kuzunguka eneo la Mgodi wa Tanzanite (Mererani) zenyе lengo la kuongeza udhibiti katika mfumo mzima wa biashara ya Tanzanite katika soko la ndani na la nje. Pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali za kusimamia biashara hii, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa madini haya yanapata **Hati ya Uasilia** (Certificate of Origin) ilikuweza kudhibiti madini haya katika soko la nje.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza hatua zilizochukuliwa na Serikali za kuendelea kudhibiti uholela uliokuwepo wa tanzanite katika soko la ndani na nje hali ambayo kimsingi inashusha thamani ya Tanzanite; Kwa mfano mnada uliyofanyika Disemba, 2017 ni **kilo 47 tu ndiyo zilizouzwa kati ya kilo 535.99 zilizochimbwa. Aidha, kilo 488.99 zimehifadhiwa katika Benki kuu tawi la Arusha pamoja na Maghala ya Mgodi ili kusubiri bei nzuri ya soko la Tanzanite.**

Mheshimiwa Spika, Aidha, Kamati inaishauri kuwa taratibu endelevu zinazoandaliwa na Wizara kuhusu Mnada wa Tanzanite zikamilishwe kwa haraka ili kuboresha Mnada huo ambao ndiyo tegemeo kubwa kwa wachimbaji na wafanyabiashara ya madini ya tanzanite. Mnada huu ukiratibiwa vizuri utaongeza tija ya uwepo wa madini haya hapa nchini.

(b) Madini ya Almasi

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutekeleza ushauri na maoni ya Kamati maalumu uliyoiunda ya kufuatilia mfumo mzima wa biashara ya Madini ya Almasi hapa nchini, kwani baada ya kuimarisha usimamizi katika Mgodi wa Mwadui katika kipindi cha Julai hadi Februari, 2018 **Karati 3,047,784.56** zilizalishwa na **Karati 137,257.94** zilisafirishwa nje ya nchi. Almasi hiyo ilikuwa na thamani ya **Dola milioni 32,653,349.9** ni sawa na **Shilingi biliioni 72,921,000,000** na mrabaha wa **Dola za marekani milioni 2.25** sawa na **Shilingi bilioni 5.02** ulilipwa Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Wizara kutoa takwimu na taarifa zote za uzalishaji wa madini ya Almasi kutoka kwenye migodi mingine hapa nchini ili kujua mchango wake katika makusanyo ya Taifa letu.

(c) Madini mengine ya Vito

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina utajiri mkubwa sana wa madini mengine ya vito kama vile **Rubi**, **Sapphire**, **Garnet**, **Tourmaline**, **Emerald**, **Scapolite**, **Tsavorite** pamoja na **Alexandrite** inayopatikana Wilayani Tunduru tu, aina hii ya madini ina thamani kubwa katika soko hivyo ni vema Wizara ikaweka utaratibu mzuri utakaowezesha kuchimbwa kwa Madini hayo ili yaweze kuchangia katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Madini hajaweza kuripoti mchango wa Madini mengine ya Vito pamoja na uwepo wake katika Mikoa yote nchini. **Kamati inaishauri Wizara kuwa, taarifa zote za Madini yanayozalishwa nchini zinapatikana ili kujua mchango wa Madini hayo katika makusanyo ya Serikali.**


2.3.2 Madini ya Dhahabu

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Februari, 2018 jumla ya kilo 31,450 sawa na **Wakia milioni 1.01** zilizalishwa na kusafirishwa nje ya nchi na migodi yote mikubwa na ya Kati hapa nchini, uzalishaji huu umepungua kwa **asilimia 28** kutoka Wakia **milioni 1.42** zilizozalishwa mwaka 2016 pamoja na Wakia **milioni 1.36** zilizozalishwa mwaka 2015.

Kielelezo Na.1 Kinafafanua zaidi kuhusu uzalishaji wa madini ya Dhahabu nchini.

Mwaka	Wakia(Milioni)
2017	1.01
2016	1.42
2015	1.36

Chanzo: Taarifa za Wizara na usanifu wa Kamati



Chanzo: Taarifa za Wizara na usanifu wa Kamati

Kushuka kwa uzalishaji wa Madini haya kumechangia pia kushuka kwa makusanyo ya malipo ya Mrabaha wa awali kulinganisha na miaka iliyopita.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa na mchango hafifu kutoka kwa Wachimbaji wadogo kwenye makusanyo ya Mrabaha pamoja na Serikali kutoa ruzuku kwa baadhi ya Wachimbaji Wadogo ambapo mnufaika wa chini alipata **Dola za Marekani elfu 50,000** sawa na takribani **Shilingi milioni 100,000,000** na mnufaika wa juu alipata **Dola za Marekani 100,000** sawa na takribani **Shilingi milioni 200,000,000** kwa kila mchimbaji katika awamu zote mbili.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa za makusanyo ya Maduhuli kwa kipindi tajwa hakuna mchango wa Wachimbaji wadogo uliopatikana katika makusanyo ya Mrabaha. Aidha, kukosekana kwa taarifa za uzalishaji wao ni ishara tosha kuwa Madini haya huuzwa katika Soko lisilo rasmi na hivyo kushindwa kuwanufaisha Wachimbaji wenyewe na Serikali kwa ujumla. Kamati inaitaka Wizara kuimarishe usimamizi kwa Wachimbaji wadogo ili kuhakikisha kuwa Madini yote yanayozalishwa yanaangia katika mfumo rasmi wa ulipaji wa kodi za Serikali ili na wao wachangie katika pato la Taifa kama yalivyo malengo ya Wizara hii.

2.3.3 Madini ya Ujenzi na Viwandani

Mheshimiwa Spika, Kamati hairidhishwi na makusanyo kidogo tunayopata kama nchi kutoka kwenye madini ya Ujenzi na Viwandani, jumla ya **Shilingi bilioni 1.62** tu za Mrabaha zililipwa Serikalini pamoja na uwepo wa madini hayo kwa wingi hapa nchini. Aidha, Kamati hairidhishwi na uwekezaji usiyo na tija unaofanywa na STAMICO kwa kushindwa kuhodhi soko la madini hayo ili kuongeza Makusanyo kama inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Wizara kuwa, kama STAMICO inashindwa kuendeleza Migodi ya Madini ya Ujenzi kama ule wa Ubena Zomozi ni vema wakapewa Wananchi wenyе nia ya kuendeleza Migodi hiyo na STAMICO ikabaki na kazi ya kutoa ushauri wa kitaalam na Serikali ikabaki na kazi yake ya kukusanya Mapato.

2.3.4 Madini ya Bati

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa na sababu zinazotolewa na Wizara ya Madini za kushindwa kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Bati kwa ukosefu wa fedha za mtaji wa kununulia mtambo wa kuchakata bati pamoja na ukosefu wa Hati ya uasilia yaani (**ICGLR Certificate of Origin**) inayosababisha Madini hayo kushindwa kuuzwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Changamoto zinazotolewa na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kimsingi siyo changamoto ambazo wameshindwa kuzipatia ufumbuzi kama Shirika na Wizara yenye dhamana ya madini nchini. Kamati inaona kuwa kusimama kwa mradi huo siyo kutokana na ukosefu wa mtaji kama inavyoripotiwa bali ni kukosekana kwa utashi wa Serikali wa kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Madini hayo yenye soko kubwa kwa nchi jirani ya Rwanda.

Aidha, fedha za Mtaji wa kuendesha mradi huo takribani **Shilingi billioni 1.57** zilikuwepo na kutumika kununulia tani **106.267** za Bati kutoka kwa wachimbaji wadogo na kuhifadhia katika ghala. **Hata hivyo; dhamira ya kuanzisha Kampuni tanzu ya Kyerwa Tin Company** imeshindwa kutimia na kuwasababishia hasara Wachimbaji wadogo waliohamasishwa katika uzalishaji na tayari wamewekeza katika uzalishaji wa Madini hayo.

Mheshimiwa Spika, Wakati Serikali ikiendelea kusuasua katika uendelezaji wa Mradi huo, taarifa za Benki ya Dunia kuhusu soko la Madini haya zimeonesha kuwa, bei ya Madini ya Bati inatarajiwa kupanda kutoka **Dola 20,225/MT (Metric Tone)** kwa Mwaka 2017 hadi kufikia **Dola 20,834/MT** ifikapo mwaka 2020. Aidha, bei ya Madini hayo itaendelea kuimarika na kupanda katika kipindi cha miaka mitano ijayo, na ifikapo Mwaka 2030 inatarajiwa kuwa imepanda hadi kufikia **Dola 23,000/MT**.

Kielelezo Na. 2 kinaonesha mwenendo wa Bei ya Madini ya Bati Duniani.



Hivyo basi, Wizara ya Madini iweke mpango Mkakati wa kiuwekezaji kwa ajili ya kuendeleza Mradi huu wa Madini ya Bati kwa kuwa taarifa za Benki ya Dunia zinaonesha wazi fedha ambazo nchi yetu itazipata kutokana kuimari kwa soko la Madini hayo Duniani.

2.3.5 Makaa ya Mawe

Mheshimiwa Spika, Kamati haioni nia ya dhati ya Serikali ya kuendeleza Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira kwa kushindwa kupeleka fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako tukufu jumla ya **Shilingi bilioni 10,000,000,000** kwa ajili ya kuendeleza shughuli mbalimbali za Mgodi huo. Pamoja na uhitaji mkubwa wa Makaa hayo katika Viwanda mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Februari, 2018 jumla ya **tani 2,477** zimezallishwa zenyet thamani ya **Shilingi milioni 158,528,000**. Takribani mwaka mzima sasa Makaa hayo hayajaweza kuuzwa kutokana na sababu mbalimbali zilizoleezwa na STAMICO kuwa ni ukosefu wa Miundo mbinu ya barabara. **Kamati inashauri Wizara ya Madini kushirikiana na Halmashauri husika pamoja na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ili ziweze kutengeneza barabara hiyo ambayo ni ya muhimu sana kwa ustawi na maendeleo ya Mgodi pamoja na Halmashauri hiyo.**

Mheshimiwa Spika, Mgodi wa makaa ya mawe wa Ngaka umeendelea kufanya shughuli za uzalishaji ambapo jumla ya **tani 340,295** zilizalishwa na kuuzwa zenyet thamani ya Dola za marekani milioni 15,500,000 ambapo Serikali ililipwa mrabaha wa jumla ya **Dola za Marekani 466,345.48**.

Kamati inashauri Wizara kuwa ni vema sasa wakafanya maamuzi ya dhati kabisa ya kuwekeza kwenye Miradi ambayo uhitaji wake katika soko la ndani umeongezeka zaidi baada ya zuio la Serikali la uingizaji wa Malighafi hizo kutoka nje. Aidha, ni matumaini ya Kamati kuwa, kama uwekezaji huo utafanyika utaongeza makusanyo ya Serikali hasa mrabaha.

Mheshimiwa Spika, Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuonesha uzalendo wake katika kulinda rasilimali zetu za Madini ambazo zilikuwa hazilinufaishi Taifa ipasavyo kwa kuunda Tume ya Madini ambayo itakuwa na jukumu la kusimamia ipasavyo maendeleo ya Sekta hii ya Madini nchini.

3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI PAMOJA NA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018;

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kushughulikia mambo mengi ya kibajeti ya Wizara ya Madini, Kamati yako ilifanya uchambuzi wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2017/18 katika maeneo yafuatayo:-

- a. Makusanyo ya Maduhuli;
- b. Hali ya upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina; pamoja na
- c. Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati uliotolewa.

3.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa fedha 2017/18

Mheshimiwa Spika; Wizara ya Madini ilipanga kukusanya Maduhuli jumla ya **Shilingi bilioni 194,397,098,763** kutoka vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2018 jumla ya Maduhuli ya **Shilingi bilioni 200,685,683,840** zilikusanya kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya Wizara ya Madini, ongezeko hili ni sawa na **asilimia 103** ya lengo waliojiwekea kwa mwaka wa fedha 2017/18. Zifuatazo ni Sababu zilizoelezwa na Wizara kuchangia kuongeza kwa Makusanyo ya Maduhuli;

- (a) Kuimarika kwa udhibiti wa utoroshaji wa madini kwa kushirikiana na vyombo vyaa Serikali;

- (b) Kuongezwa kwa viwango nya mrabaha kutoka asilimia 4 hadi asilimia 6 kwa madini ya metali, na kutoka asilimia 5 kwenda 6 kwa madini ya vito; na
- (c) Kuanzishwa kwa tozo ya ukaguzi asilimia 1 ya mauzo ya madini.

Mheshimiwa Spika, Ongezeko hili la ukusanyaji wa Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2017/18 ni ishara tosha kwa Kamati na Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Madini imejitahidi kuimarisha usimamizi na uangalizi wa rasilimali zetu kitu ambacho kilikuwa ni kero na aibu kubwa kwa Taifa letu. Kamati inaanmini kuwa Sekta ya Madini sasa itakwenda kutoa mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa kama inavyotarajiwa na Wananchi wetu.


3.2 Uchambuzi wa Taarifa ya hali ya upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, Bunge liliidhinisha jumla ya **shilingi 998,337,759,500** kwa iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini, kati ya fedha hizo **shilingi 52,445,367,000** ilikuwa ni kwa ajili ya Idara ya Madini. Kati ya **shilingi 21,783,000,000** sawa na **asilimia 41.53** ilikuwa kwa ajili ya Miradi ya maendeleo. Aidha, **Shilingi bilioni 30,662,367,000** sawa na **asilimia 58.47** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2018 iliyokuwa Idara ya Madini ambayo ndiyo Wizara ya Madini sasa ilikuwa imepokea **Shilingi bilioni 15,670,239,173** ambayo ni sawa na **asilimia 13.69** ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa fedha 2017/18, kiwango hicho cha fedha kilikuwa katika mgawanyo ufuatao; fedha za Miradi ya Maendeleo zimepokelewa **Shilingi milioni 834,976,618**, sawa na **asilimia 3.83** ya Bateji iliyotengwa na **shilingi bilioni 6,723,898,405** sawa na **asilimia 51** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi bilioni 8,111,364,150** sawa na **asilimia 51** kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa na utolewaji wa fedha za miradi usiyordhisha kwani hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2018 Wizara ya Madini imepokea **asilimia 3.83** tu ya bajeti iliyodhinishwa kwa ajili ya maendeleo, hali hii inakwamisha kwa kiasi kikubwa miradi ya maendeleo ambayo kimsingi ndiyo tunayoitegemea katika kuongeza ukusanyaji wa Mapato ya ndani kwa Wizara hii. Miradi iliyokwamishwa na upatikanaji huu wa fedha usiyordhisha ni; Mradi wa Kiwira, Kabulo, Mradi wa Ununuzi wa Bati, Mradi wa Dhahabu Buhemba, Mrdai wa uchimbaji wa kokoto na Mradi wa STAMIGOLD.

Kielelezo Na. 3 ni uafanuzi wa utolewaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo pamoja na Matumizi ya Kawaida



Chanzo: usanifu wa Kamati na Randama ya Wizara 2018/19

Mwenendo huu wa utolewaji wa fedha kutoka Hazina unapunguza kabisa ufanisi wa Wizara hii mpya ambayo sisi kama Taifa tunatarajia mengi kutoka kwao katika usimamizi wa rasilimali za Madini ambazo kwa muda mrefu tumekuwa hatunufaiki nazo.

3.3 Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati uliotolewa

Mheshimiwa Spika, wakati wa uchambuzi wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/18, Kamati ilioita Maoni, Ushauri na Mapendekezo kuhusu utekelezaji wa Bajeti pamoja na

usimamizi wa Miradi ya maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa mwaka husika. Hata hivyo, baadhi ya Maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa na baadhi bado haujafanyiwa kazi na Serikali kama ifuatavyo:-

a) Serikali kutopeleka fedha zilizoidhinishiwa na Bunge kwenye miradi ya kimkakati kama vile Kiwira kunachelewesha utekelezaji wa miradi hiyo yenyе tija kwa maendeleo ya viwanda hapa nchini.

b) Kamati bado hairidhishwi na ufuatiliaji mdogo unaofanywa na Wizara kwa Wabadhilifu wa Ruzuku zilizotolewa na Serikali katika awamu zote mbili zilizotolewa mwaka 2014/15. Ufuatiliaji huo wa kusuasua umeshindwa kuwachukulia hatua watu wote waliokiuka matumizi ya fedha hizo za umma; na

c) Serikali kupitia Wizara ya Madini bado inashindwa kuwasaidia Wachimbaji wa Kati ambao kimsingi wameonekana kuwa ndiyo wawekezaji wazawa ambao wameweza kuisimamia na kuendeleza sekta ya madini kwa manufaa makubwa, kwa mfano mgodi wa Busolwa Mining bado unakabiliwa na changamoto ya uhaba wa eneo la Mgodi pamoja na kutoa ajira kwa vijana wengi pamoja na mchango wake mkubwa kwa Serikali na jamii inayouzunguka kuliko hata Migodi ya Wawekezaji wakubwa.

4.0 **UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA FUNGU 100 KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19**

4.1 **Mapitio ya Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa fedha 2018/2019**

Mheshimiwa Spika, Katika uchambuzi wa Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/19, Kamati imebaini kuwa malengo yaliyowekwa na Wizara yakiweza kusimamiwa ipasavyo Wizara itaweza kufikia Dira ilijojiwekea yakuwa ; **Wizara inayoheshimika Afrika katika**

kuendeleza rasilimali za madini ili ziweze kuchangia kwa ufanisi katika uchumi wa Taifa na ustawi wa Watanzani.

Mheshimiwa Spika, Wananchi na Taifa kwa ujumla tuna imani kubwa sana na Wizara ya Madini kuwa itaweza kuiweka Tanzania kwenye ramani ya Dunia ya kuwa miongoni mwa wazalishaji wakubwa wa Madini na kwamba Wizara hii itasimamia vyema rasilimali za madini nchini ili ziweze kulinufaisha Taifa kupitia usimamizi mzuri wa Sheria, Kanuni na Malengo Makuu sita(6) Wizara iliyojiwekea. Malengo hayo ni haya yafuatayo:-

- a) Kuboresha huduma kwa waathirika na kupunguza maambukizi ya Virusi vya UKIMWI;
- b) Kuimarisha na kuendeleza Mkakati wa Taifa na Mpango wa kupambana na Rushwa;
- c) Kuboresha utoaji huduma kwa Wadau wa Sekta ya Madini;
- d) Kuongeza Mchango wa sekta ya Madini kijamii na kiuchumi;
- e) Kuwaimarisha Wachimbaji wadogo wadogo wa Madini nchini; na
- f) Kuimarisha mifumo ya ukaguzi na usimamizi wa migodi

Mheshimiwa Spika, Uwepo wa Sheria mpya za *The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, The Natural Wealth and Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms)* na Marekebisho ya Sheria ya Madini zilizopitishwa na Bunge lako tukufu mwaka 2017 pamoja na kuanzishwa kwa Tume ya Madini nchini itasaidia usimamizi mzuri wa rasilimali zetu.

4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

Mheshimiwa Spika, Makisio ya makusanyo ya Maduhuli yanakadiriwa kuwa jumla ya **Shilingi bilioni 321,672,507,000** kwa mwaka wa fedha 2018/19 ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 194,397,098,763** zilizokadiriwa kukusanywa kwa Mwaka 2017/18. Ongezeko hili ni sawa na **asilimia 60.84**.

Kati ya makusanyo yote kwa mwaka wa fedha 2018/19 **Shilingi bilioni 310,598,007,000** sawa na **asilimia 99.34** zitawasilishwa kwenye mfuko mkuu wa Serikali. Aidha, **Shilingi bilioni 2,074,500,000** sawa na **asilimia 0.66** zitatumika kwa ajili ya kuendeshea shughuli za Taasisi na Wakala zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Ongezeko la makusanyo haya limetokana na ongezeko la malipo ya viwango vipyta vya Mrabaha kwenye Madini ya Metali, Vito na kuanzishwa kwa tozo ya ukaguzi wa mauzo ya madini, Kamati yako inaishauri Wizara kubuni vyanzo vingine mbadala vya mapato ambavyo vitakuwa ni endelevu kutokana na rasilimali zilizopo katika Wizara hiyo ikiwa ni pamoja na kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa kutumia Wataalamu walionao katika chuo cha Madini.

4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2018/19 Wizara ya Madini imeomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 58,908,481,992** ikilinganishwa na **shilingi bilioni 52,445,367,000** zilizoidhinishwa na Bunge lako tukufu kwa mwaka wa fedha 2017/18. Bajeti hii imeongezeka kwa **asilimia 11**. Ongezeko hili la bajeti limetokana na uwepo wa Tume ya Madini ambayo inatarajia kuongeza watumishi wengine wapya kwa ajili ya kutekeleza majukumu mapya ya Tume hiyo. **Kamati inasitisiza Serikali kuhakikisha fedha zinatoka kwa wakati ili Tume hii yenye majukumu makubwa iweze kutekeleza majukumu yake kama inavyotarajiwa.**

Mheshimiwa Spika, Wizara imetenga kiasi cha **Shilingi bilioni 19,620,964,000** sawa na **asilimia 32** ya Bajeti yote kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 21,783,000,000** zilizotengwa mwaka 2017/18, Bajeti hii imepungua kwa **asilimia 9.93**. Katika bajeti hiyo ya maendeleo **Shilingi bilioni 16,800,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 2,820,964,000** ni fedha za nje. Aidha, **Shilingi bilioni 17,700,000,000** sawa na **asilimia 90.21** zitaelekezwa kwenye miradi ya Kimkakati. Kamati inaipongeza Wizara kuendelea kupunguza utegemezi wa fedha za nje kwenye Bajeti ya Miradi ya maendeleo.

Pamoja na ongezeko la **asilimia 11** ya Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2018/19 kwa Wizara hii, Bajeti ya Miradi ya Maendeleo imepungua kitu ambacho Kamati inaona kitaathri utekelezaji wa miradi hiyo, ambayo katika Bajeti ya 2017/18 haikupelekewa fedha pamoja na Bunge kuidhinisha fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati yako hairidhishwi na mwenendo wa Serikali kuendelea kutenga fedha kidogo katika miradi ya Kimkakati ambayo inahitaji fedha nyingi kama vile Miradi wa Makaa ya Mawe Kiwira na Kabulo. Miradi hii ili iweze kuanza uzalishaji wenyе tija ambaо tunautarajia kama Taifa zinahitajika fedha za kutosha nyingi zaidi ya zilizotengwa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa, kwa kuwa fedha hizo zilizotengwa kwa ajili ya Mradi wa Kabulo hazitatosha kukidhi uzalishaji wenyе tija ni bora zikaelekezwa katika mradi mwingine kama vile Mradi wa Kokoto ili uweze kuongeza uzalishaji na kisha kuongeza makusanyo ya Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, Wizara imetenga **Shilingi bilioni 39,287,517,992** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida ambayo ni sawa na **asilimia 66.69** ya bajeti yote, ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 21,783,000,000** kwa mwaka wa fedha 2017/18. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida imeongezeka kwa **asilimia 44** ukilinganisha na mwaka 2017/18. Aidha, kati ya fedha hiyo

Shilingi 20,953,262,992 ni kwa ajili ya matumizi Mengineyo(OC) na **Shilingi bilioni 18,334,255,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Spika, Ongezeko hili la bajeti ya Matumizi Mengineyo na bajeti ya Mishahara kwa Wizara hii ni kutokana na kuanzishwa rasmi kwa Wizara ya Madini pamoja na kuanzishwa kwa Tume ya Madini ambayo nayo inatarajiwa kuajiri watumishi wengi pamoja na kufungua Ofisi za Mikoa. **Kamatit inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa fedha zitakazo idhinishwa na Bunge lako tukufu kwa Wizara hii mpya zinatolewa kwa wakati ili Wizara pamoja na Tume ya Madini waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi kama inavyotarajiwa na Wananchi.**

5.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Kamati yako imetekeleza majukumu yake ya msingi yaliyoainishwa katika Kanuni ya 98 (1) na (2) pamoja na kanuni ya 117(11) a Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016. Hivyo basi, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao kwa Wizara ya Madini;

5.1 Kamati inaendelea kuisisitiza Wizara kuharakisha ufuatiliaji wa fedha za Ruzuku zilizotolewa na Serikali kwa Wachimbaji Wadogo wadogo katika awamu zote mbili, Pia Wizara ihakikishe inafanya upembuzi yakinifu kabla ya kutoa rukuzu awamu nyingine ili kuepuka changamoto zilizojitokeza katika awamu zilizotangulia.

5.2 Kamati hairidhishwi na mwenendo wa utekelezaji wa shughuli za Mgodi wa STAMIGOLD kwa sababu lengo la kuanzishwa kwa Mgodi huo limeshindwa kutimia na badala yake umekuwa ukizalisha Madeni makubwa takribani bilioni 60 sasa. Wizara iangalie namna bora ya kuendesha mgodi huo au kuufunga kama itaona inafaa kwa maslahi ya Taifa kuliko kuendelea na uzalishaji usiyo na faida.

5.3 Kamati inaitaka Wizara ya Madini kufanya tathmini na kujiridhisha kama kweli kuna faida tutakayoipata

kama nchi tukiwekeza fedha **Shilingi bilioni 8.6** zinazoombwua kwa ajili ya kuendeleza Mgodi wa Buhemba, ilhali hakuna faida tuliyopata mpaka sasa katika uwekezaji uliofanyika katika Mgodi wa STAMIGOLD zaidi ya kuzalisha madeni makubwa ambayo ni mzigo kwa Serikali.

5.4 Kamati inaona ni vema Mgodi wa Buhemba na ule wa STAMIGOLD wapewe wachimbaji wa Kati wenye nia ya kuuendeleza, hii itakuza sekta ya wachimbaji wa Kati nchini ambao wameonesha kuwa na mchangano mkubwa katika makusanyo ya mapato na Serikali ikabaki kwenye ukusanyaji wa mapato tu.

5.5 Kamati inaendelea kuishauri tena Wizara kupitia upya Mkataba wa Ubia kati ya STAMICO na TANZAM 2000 uliongia mwaka 2011 kuendeleza Mgodi wa Buckreef, kwa kuwa Mkataba huo umedhihirisha kutokuwa na manufaa ya kiuchumi katika uendelezaji wa Mgodi huo licha ya uwepo wa Mashapo yenye uhakika wa kuzalisha dhahabu na kuliingizia Taifa mapato.

5.6 Pamoja na makusanyo ya Mrabaha kuongezeka kwa mwaka wa fedha 2017/18 hususani katika idara ya Madini, Kamati hairidhishwi na uendelezaji wa Wachimbaji wa Kati ambao wana mchangano mkubwa katika makusanyo ya Wizara. **Hivyo basi, Kamati inashauri Wizara kuwa ili kuongeza makusanyo hayo ni vema Wawekezaji hawa wazawa wakasaidiwa kupata ufumbuzi wa haraka kuhusu kero zinazowakabili.** Hii itavutia Wawekezaji Wazawa kuendeleza sekta hii kuliko kusubiri wawekezaji toka nje ambao ndiyo wanaofaidi misamaha ya Kodi mbalimbali.

5.7 Kwa kuwa miradi ya Makaa ya mawe imeonekana kuwa na mchangano unaoridhisha kwenye makusanyo ya Mrabaha takribani **Dola za Marekani 466,345** zilipatikana kutokana na mauzo ya makaa ya mawe katika Mgodi wa Ngaka. **Hivyo basi, Kamati inashauri kuwa; miradi yote ya Makaa ya Mawe ni vyema Serikali ikatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuendeleza Miradi hiyo,** kwa kuwa

uhitaji wa malighafi hiyo ni mkubwa sana hapa nchi baada ya zuio la Serikali la kuagiza Makaa hayo toka nje ya nchi.

5.8 Wizara ya Madini iweke mpango Mkakati wa kiuwekezaji kwa ajili ya kuendeleza Mradi wa Madini ya Bati kwa kuwa taarifa za Benki ya Dunia zinaonesha wazi, fedha ambazo nchi yetu itazipata kutokana na kuimarika kwa Soko la Madini hayo Duniani.

5.9 Wizara kuangalia upya Mikataba yote tulioingia na Wawekezaji wanaowekeza katika uchimbaji wa Makaa ya Mawe ili kujiridhisha kama nchi inafaidika na uwepo wa Kampuni hizo katika uendelezaji wa Makaa hayo.

5.10 Serikali iangalie namna bora ya kuwezesha Wakala wa Jiolojia nchini ili iweze kufanya tafiti za madini yote nchini nakuwa na **Kanzi data** ambayo itatumilwa na Wawekezaji toka nje, hii itapunguza athari kubwa za kimazingira zinazosababishwa na Watafiti kutoka nje ya nchi ambao wakimaliza tafiti zao nchi hainufaiki na tafiti zilizofanywa kwenye rasilimali zake.

5.11 Wizara ibuni na kuwa na mikakati endelevu ya vyanzo vingine vipyta vya ukusanyaji wa Mapato kuliko kutegemea tozo za Madini pekee, kwani ikitokea uzalishaji wa Madini umeshuka Wizara itakosa mapato tunayoyatarajia kama nchi.

6.0 **HITIMISHO**

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini kwa umahiri wao walionunesha wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii. Wajumbe hawa wamefanyakazi kwa ari kubwa na hatimaye kukamilisha Taarifa hii. Naomba kuwatambua Wajumbe hawa kwa majina yao kama ifuatavyo;

- | | | |
|----|----------------------------------|----------------|
| 1. | Mhe. Dustan Luka Kitandula, Mb | - Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb | - M/Mwenyekiti |

- | | | |
|-----|--------------------------------------|----------|
| 3. | Mhe. Mohamed Juma Khatib, Mb | - Mjumbe |
| 4. | Mhe. Ally Mohamed Keissy, Mb | - Mjumbe |
| 5. | Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb | - Mjumbe |
| 6. | Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb | - Mjumbe |
| 7. | Mhe. Bahati Ali Abeid, Mb | - Mjumbe |
| 8. | Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb | - Mjumbe |
| 9. | Mhe. Maryam Salum Msabaha, Mb | - Mjumbe |
| 10. | Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mb | - Mjumbe |
| 11. | Mhe. John Wegesa Heche, Mb | - Mjumbe |
| 12. | Mhe. Hamoud Abuu Jumaa, Mb | - Mjumbe |
| 13. | Mhe. Msukuma Joseph Kasheku, Mb | - Mjumbe |
| 14. | Mhe. Jesca David Kishoa, Mb | - Mjumbe |
| 15. | Mhe. Rashid Ajari Akbar, Mb | - Mjumbe |
| 16. | Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb | - Mjumbe |
| 17. | Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb | - Mjumbe |
| 18. | Mhe. Yosepher Ferdinand Komba, Mb | - Mjumbe |
| 19. | Mhe. James Kinyasi Millya, Mb | - Mjumbe |
| 20. | Mhe. Lameck Okambo Airo, Mb | - Mjumbe |
| 21. | Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb | - Mjumbe |
| 22. | Mhe. Zubeda Hassan Sakuru, Mb | - Mjumbe |
| 23. | Mhe. Hamida Mohamed Abdallah, Mb | - Mjumbe |
| 24. | Mhe. Kiza Hussein Mayeye, Mb | - Mjumbe |
| 25. | Mhe. Frank George Mwakajoka, Mb | - Mjumbe |

Mheshimiwa Spika, nitoe pia shukrani zangu za dhati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati kwa Mhe. Angellah Kairuki, (Mb) – Waziri wa Madini, pamoja na Manaibu Waziri wa Madini Mhe. Stanslaus Nyongo, (Mb) na Mhe. Doto Biteko, (Mb) pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu, Profesa Simon Msanjila kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati yetu wakati wote.

Mheshimiwa Spika, Kwa kipekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndgi. Steven Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndgi. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi, Ndgi. Michael Chikokoto pamoja na Makatibu wa Kamati Ndgi. Mwanahamisi Munkunda na Ndgi. Felister Mgonja pamoja na Msaidizi wa Kamati ndgi. Grace Mwenye kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha Taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 100 Wizara ya Madini kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 ambayo ni **Shilingi Bilioni 58,908,481,992**.

Mheshimiwa Spika, Naunga mkono hoja na Naomba kuwasilisha.

Dunstan Luka Kitandula
MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI
31 Mei, 2018

MWENYEKITI: Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini Mheshimiwa Kitandula. Kamati yako ime-*highlight* maeneo ambayo ambayo nadhani yatasaidia sana Waheshimiwa Wabunge amba mtachangia, ina maeneo mazuri tu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitoe kwenu hoja hii mwanze kuijadili. Pia tuna saa nzima nzuri tu. Ngoja niangalie amsha amsha. Tuone, nianze na Mheshimiwa Abdallah Bulembo atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk na Mheshimiwa Vedasto Ngombale ajiandae. Mheshimiwa Bulembo hayupo. Nataka niuone ule mtitiriko kama nilivyopanga. Mheshimiwa Kanyasu.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunjaalia afya njema na nimepata nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Madini. Nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake na Watendaji wake wote kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza pia Serikali yangu kwa sheria ambayo tulitengeneza mwaka 2017 ambayo imeenda kuboresha kabisa shughuli za madini na

mpaka sasa tayari waombaji zaidi ya 5,000 kwa taarifa ambazo tunazo, waliyokuwa wamekaa zaidi ya mwaka mmoja kusubiri *license* wameshapata, nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake kwenye suala la *CSR*, tulipitisha Sheria ya *CSR* hapa mwaka jana na tukaitengenezea utaratibu ambao utawahusisha Halmashauri ili ziweze kushiriki pamoja na migodi kwenye matumizi ya pesa hasa katika kuchambua miradi na kukubaliana na mgodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali, nadhani kuna maeneo ambayo hatukuyaona vizuri, sisi katika maeneo ya migodi tulikuwa na tatizo la migodi hii kuja na mahesabu makubwa sana yanayoonesha wametumia kwenye miradi, wakati miradi iliyofanyika ni midogo na tatizo hili linaonekana bado linaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja Geita akaomba watu wa Mgodi wampe orodha ya pesa ambazo zimetumika na miradi, hawakumwambia mradi huu wametumia shilingi ngapi. Nadhani angeona suala hilo angeshangaa sana. Mwaka huu baada ya vikao na Halmashauri tumeona tatizo hili litakuja kuwa kubwa zaidi. Kwa mfano, katika hesabu ambayo Halmashauri ya Mji wa Geita wametuletea kwenye miradi ambayo tumependekeza, *cement* wao wanasema ni Sh.48,000/= mfuko, wakati pale mjini mfuko ni Sh.18,000/=. Bati la *gauge* 28 wanasema ni Sh.78,000/=. wakati bati pale mjini ni Sh.22,000/= bati moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nondo ya milimita 16 wamewekwa Sh.52,000/= na kokoto *trip* moja wameweka Sh.80,000/=. Sasa unaona sheria hii imewapa *loophole* ya kuendelea kudanganya kama ilivyo kwenye *transfer pricing*, matokeo yake itakuwa ni Kampuni zao zile zile ambazo wanaziteua, zinawauzia *material* kwa bei kubwa mara nne zaidi. Mradi wa shilingi milioni 10 watajenga kwa shilingi milioni 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri na Waziri wa Sheria tutazame upya sheria hii ili ikiwezekana Halmashauri Kitengo chake cha Manunuzi kishiriki kwenye *Procurement System* nzima kwa bei ambazo ni shindani kwenye maeneo husika na kwa kutumia wazabuni na *local contents*. Bila kufanya hivyo tutarudi kule kule tulikotoka, takwimu zitaonesha mabilioni ya shilingi lakini miradi iliyofanyika ni midogo na pesa zote zinarudi kule zinakotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la pili, ni suala ambalo Mheshimiwa Naibu Waziri pia alikuja Geita kulishughulikia. Pale Geita tunao mgogoro mkubwa wa Mgodi wa *GGM* pamoja na wananchi wa Geita pale, nyumba zaidi 800 zimepasuka kutokana na milipuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wananchi wengi ambao wanaishi kwenye vizingi vyta migodi kwa zaidi ya miaka 18. Mheshimiwa Waziri alikuja akatoa maelekezo mazuri na kabla ya maelekezo yake Mgodi wenyewe ulifanya *study* kuitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Waziri aliyeuwepo, Waziri Kalemani alitoa maelekezo watu wa *GST* wakafanya *studykuonyesha* sababu za mipasuko kuitia *GST*, taarifa zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ametoa maelekezo lishughulikiwe tangu mwezi wa pili, mpaka leo ninavyozungumza, wananchi wa Geita hawajui hatma ya maagizo ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu hawaoni kinachoendelea. Wenye nyumba zile, wengine wanakufa, nyumba zile zilizopasuka zinaanguka, ripoti zote mbili za Serikali zipo mezani, lakini mambo hayashughulikiwi na hayaendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, Mheshimiwa Waziri sehemu ambazo tuna migogoro ya muda mrefu kama Geita, kabla Mheshimiwa Waziri hajaja kwenye ziara ya Jimbo langu iwe ni vyema kuitia zile *documents* zilizopo mezani kwake na kujua wenzake walitoa maagizo gani; kuliko kuja kutoa maagizo yale yale

yaliyotolewa na Waziri mwingine na yasitekelezwe, wananchi wanaona kama vile Mgodi huu unaidharau Serikali. Tunao wananchi katika maeneo ya Magema, tunao wananchi ambao wameteseka kwa muda mrefu sana na hawajapata haki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala lingine la tatu. Katika eneo la Mgusu tunao wananchi watatu ambao wamekuwa na kesi na Mgodi tangu mwaka 1995. Majaji sita ambao wameshiriki kwenye kesi ambalo ilikuwa ni kosa la Serikali, Serikali ilikuwa imewapa */license* wananchi watatu; Felix Isidory Ngowi, Ezekiel Mageese na Philipo Paskali na walikuwa wanaendesha leseni zao za utafiti na uchimbaji mdogo mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya, siyo kwa makusudi Kamishna akatoa leseni nyingine juu ya leseni zile zikiwa bado ziko hai, wananchi hawa wakakamatwa, wakapigwa, wakafungwa lakini wakaenda Mahakamani. Majaji sita wote wametoa hukumu iliyowapa haki wananchi kwa nyakati tofauti tangu mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka leo Mgodi unaendelea kuonesha unakata rufaa. Jaji Matupa, Jaji Bukuku, Jaji Mero, Jaji Nyangarika, wote hawa wamewapa haki wale wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachosikitisha sana ni kwamba hukumu nyingine ya mwisho ilitolewa mwaka 2016 na ikatoa *permanent injunction* ya kuzuia mgodi kuwaondoa wananchi hao kwenye eneo hilo. Kwa namna yoyote wanapokuwa wanaendelea na kesi nyingine, bado Mkurugenzi wa Mgodi na Polisi na wengine waliko pale wameendelea kuwakamata na kuwafukuza na eneo lile lina wachimbaji wadogo zaidi ya 5,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwanza ni aibu kwa Serikali. Majaji hawa wote wameonesha kwamba wachimbaji hawa wadogo

wana haki na kosa ni la Kamishna, lakini bado wanaendelea kuonesha kwamba huyu mwenye Mgodi mtu mmoja ana haki ya kuwafukuza watu na kuwanyanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri wananchi hawa wapewe haki yao, wamekamatwa zaidi ya mara 20, wanawekwa ndani miezi sita, Mgodi hauji kuendelea na kesi, wanatoka, wanapigwa, mali zao zinachukuliwa, wanafukiwa mashimo bila sababu yoyote ile ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawa kwa kweli hawana sababu yoyote ile ya kuendelea kuteseka, kwa sababu vyombo vya Sheria; tuna mazoea wananchi wakifukuzwa huwa wanasalimu amri, wanaondoka. Hawa walikwenda Mahakamani wakafuata utaratibu kwa miaka 20 wameipigania haki yao na wameshinda na hukumu wanayo, lakini Mgodi unaendelea kuwafukuza. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, suala hili lishughuliikiwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la nne, naomba kuishauri Serikali, tunao Mgodi wetu wa *GGM* pale awali ulikadiriwa kuchukua miaka 30 au 25, lakini baada ya sheria hizi mpya tulizotengeneza, ule Mgodi unaanzisha *pit* nyangi na wanafanya kama *lashing*, matokeo yake ninayoyaona, baada ya miaka mitano watafunga Mgodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachoendelea sasa, wakiona tu gharama za kupata madini zimeongezeka, wanahama wanaanzisha *pit* mpya. Matokeo yake wanakwenda wana-*lash* badala ya kuchukua miaka 30, tutaachiwa mashimo na mashimo yale ni makubwa, wataondoka kabla sisi wenyewe tuliotarajia kwamba tutachimba madini haya kwa miaka 30 hatujafaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iangalie namna ya ku-control. Kuna maeneo migodi inachukua zaidi ya miaka 50 kwa sababu wanalazimishwa kufanya utafiti na kumaliza madini yaliyoko chini. Shimo lilitokwenda milimita 200 ukiondoka leo anayekuja hawezi kuchimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni suala la *GST*. *GST* nawapongeza kwa kazi wanazozifanya, lakini nina tatizo moja na *GST*. Mwaka 2016 walikuwa kule Bukombe, nami nikaomba leseni kuititia wachimbaji wadogo wadogo wa Jimbo langu kama tulivyoshauriwa na Mheshimiwa Waziri, wakapewa leseni. Utafiti wa *GST* unaonyesha kuna dhahabu. Wamechimba wamekwenda mpaka mita 100 watu hawapati dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana *GST*, kabla ya kuishauri Serikali iwave wananchi maeneo haya yenye dhahabu, kwa sababu wananchi wanakopa, wanajichanga na pesa zao ndogo, nawaomba *GST* wahakikishe wanatoa elimu ya kutosha kwamba dhahabu hii ipo umbali gani kwa miamba iliyolala vipi? Tunafika mahali sasa tunaacha kuwaamini, ni bora ukatafute *private* watu wengine huko waje wakufanyie utafiti kullko *GST* kwa sababu wanafanya utafiti wa kijanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, Mheshimiwa Waziri naomba sana wananchi wangu wa Geita Mjini na wananchi wa Mgusu waweze kupatiwa haki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk na Mheshimiwa Vedasto Ngombale na Mheshimiwa Catherine Magige, ajiandae.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami niungane na wenzangu kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na afya njema na kuweza kuchangia katika Wizara hii muhimu. Vilevile pia nami nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri ambao wapo sasa hivi katika Wizara hii, lakini tutashauri na kueleza upungufu uliopo, wauchukue na kuweza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo nawatakia ndugu zangu Waislamu wote Tanzania na duniani kwa ujumla mfungo mwema wa mwezi wa Ramadhani. Pia

natoa pole kwa Bunge letu kwa kuondokewa na Mbunge mwenzetu Mwalimu Bilago, Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nitoe tu nami shukurani zangu vilevile kwa Wizara, lakini naona kuna upungufu kidogo, kwa sababu najua vipo vyama vyatia wachimbaji wadogo hususan wachimbaji wanawake, lakini sikuona au hawapo kama ilivyozoleka kwa Wizara nyiningine ambapo wahusika wanakuja kama tulivyoona katika uvuvi na kilimo. Kwa hiyo, nieleze kwanza upungufu au changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa la mashine za kukata madini katika nchi yetu au hizi wanazoziita *mineral cutters*, zipo chache. Sasa nazungumzia hilli kwa sababu hilli tatizo la utoroshwaji wa madini kwa uchunguzi ambao kwa maoni yangu nimeufanya unasababishwa na foleni kubwa ambapo unapokata madini, madini labda ya *gram* moja yanaweza yakatumia kukata kareti kwa muda wa saa nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa madini yanayochimbwa Tanzania ni mengi, matokeo yake sasa kunakuwa na foleni kubwa katika utakataji madini kama vile ilivyo kwa Mkemia Mkuu wa Serikali kwenye Wizara ya Afya ambapo *specimen* moja inaweza ikachukua miaka miwili. Sasa inawezekana hii nayo ikawa ni sababu mojawapo ya kutoroshwa kwa madini yetu kwa sababu teknolojia tulyonayo Tanzania ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naishauri Wizara na Serikali kwamba tuondoe au tupunguze kodi kwenye mashine za kukata madini ili ziwepo kwa wingi ili Watanzania sasa waweze kukata madini kwa muda mfupi baada ya kuwapeleka nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nalionna, ni ushauri wangu kwa Serikali kwamba Chuo cha Madini kinafanya kazi vizuri, lakini ama kipo kimoja au vipo vichache.

Sasa tulipofanya ziara na Kamati yetu ya *PIC*, tulipofika Shinyanga *VETA* tulikuta nao wana kozi ya ukataji wa madini. Naishauri Serikali, kwa kuwa Shinyanga *VETA* imewezezana, basi naamini katika *VETA* nyngine napo kozi zile zinaweza kuendeshwa. Kwa hiyo, naishauri Serikali iweke kozi za kukata madini katika Vyuo vya *VETA*. Kwanza, tuzalishe wataalam wengi wa madini ambao watakwenda kuwasaidia wachimbaji wadogo ili wawe wachimbaji bora, waepuke uchimbaji wa kubahatisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, itakuwa ni ajira kwa watu wetu ambao baada ya mafunzo yale naamini Wizara itaweza kuwaajiri na kuwapa shughuli ya kwenda kuwatemebelea au kwenda katika maeneo ambayo yanachimbwa madini na kuweza kuwafanya wachimbaji wetu wawe wa kisasa kuepuka kufukiwa na vifusi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo naishauri Serikali, Wizara haina *rescue team*. Tumeshuhudia mafuriko yaliyoporomoka ndani ya machimbo ya Mererani, mwaka 2016 kama sikosei, walikuwa watu wengi tu. Ni kwa sababu kama pangekuwa pana zana za kisasa za uokoaji na kungekuwa na *rescue team* ambayo ina vifaa vya kisasa, tungeweza kuokoa maisha ya watu wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hata katika upasuaji wa mawe, kwa mfano, katika kware zilizopo Tanga ilitokea ajali pale, kuna mtu mmoja alilaliwa na jiwe. Kama kungekuwa na *Helicopter Ambulance* naamini angeweza kuchukuliwa akafikishwa Muhimbili Dar es Salaam angeweza kuokolewa maisha yake. Kwa hiyo, Wizara pia ijitahidi basi iwe na japo *Ambulance Helicopter* ambayo itaweza kuokoa maisha ya watu wetu pale itakapotokea ajali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni mabenki kutokuwaamini au kutokuwathamini wachimbaji wadogo. Imezungumzwa hapa kwamba Serikali imanzisha uwezeshaji wa wachimbaji wadogo na kama sikosei katika kitabu cha Kamati imeeleza kwamba kuna wachimbaji ambao walikuwa

wanawezeshwa *U\$ Dollar* 50,000 ambayo ni sawasawa na milioni 100 hadi *U\$ Dollar* 100,000 ambayo ni sawasawa na milioni 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika Mkoa wangu wa Tanga napo kuna madini kule ya aina nyingi tu ya vito ambayo nitayataja baadaye. Ningetaka kujua, vigezo vinavyotumika kuwawezesha wachimbaji wadogo hawa kupata *Dollar* 50,000 na *Dollar* 100,000 ili na wale wachimbaji walioko Tanga waweze kupatiwa msaada huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuliua pia ni idadi ya wale wachimbaji wadogo ambao wamewezeshwa hasa ile *Dollar* 50,000 na 100,000 ni wangapi; na ni maeneo gani ya machimbo katika Tanzania yetu? Ili tuweze kujua na tunapoulizwa na baadhi ya wachimbaji tuweze kuwapa elimu, wafuate vigezo waweze kupatiwa msaada huo wa *Dollar* 50,000 na *Dollar* 100,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile yametajwa madini mengi sana hapa, kwa mfano madini ya jasi, yametajwa almasi, dhahabu, *tanzanite* lakini kuna madini mengine ya thamani ya vito. Kwa mfano, kama vile *uranium* pia hapa sikusikia ikitajwa taarifa yake, lakini kuna *rubbykuna rhodolite*, kuna *green-garnet* kuna *green tourmaline* na kadhalika. Yangechambuliwa katika takwimu ya mapato tujue kwamba *green garnet* kwa mwaka huu imeingizia Serikali kiasi gani? *Green tourmaline* imeingiza kiasi gani? *Rhodolite* imeingiza kiasi gani? *Rose* imeingiza kiasi gani? *Sapphire* imeingiza kiasi gani? Ingekuwa ni takwimu bora zaidi kwa faida ya vizazi vijavyo na pia kwa faida ya Taifa kujua kwamba, kumbe madini tuna faida nayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nasikitishwa kidogo na hii taarifa ya madini ya bati. Tanzania tulikuwa hatuna sababu ya kuwa na nyumba zilizoezekwa kwa majani, matembe, lakini pia kununua mabati kwa bei ghali. Sasa pana taarifa hapa imeeleza kwenye ukurasa wa 18 kwamba kuna masikitiko yaliyolelezwa na Kamati nami nayaunga mkono kwamba imekosekana fedha za kununua mtambo

wa kuchakata bati na vilevile kukosa hati ya uasilia (*ICGLR*) yaani *Certificate of Origin*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nauliza, Wizara inakuwaje ishindwe kupata fedha za kununua mtambo wa kuchakata bati wakati bati ni bidhaa ambayo kwanza ina soko wakati wote? Mabati yanatumika katika ujenzi wa nyumba, lakini pia kwa sasa hivi kwa sheria za ujenzi, kabla ya kujenga lazima uzungushe mabati; na yana soko kubwa ambapo Serikali kama ingekuwa na mtambo huo ingeweza kukusanya fedha nyingi tu ambazo zingesaidia katika matumizi ya masuala mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua, je, ni lini Wizara sasa itanunua mtambo wa kuchakata bati? Vilevile, huu mpango mpaka tukashindwa kununua huu mtambo wa kuchakata bati, siyo hujuma za wenye viwanda vyta mabati kwamba wanatufanyia hujuma kusudi waendelee kuuza mabati kwa bei ghali? Hilo nalo nitataka jibu lake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, niliona katika taarifa hapa, kuna wanafunzi wa Chuo cha Madini Dodoma. Nafikiri vikwazo vingi na changamoto nyingi katika vyuo ni bajeti kuwa ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iongeze bajeti ya fedha katika Chuo cha Madini Dodoma ili wanafunzi wale waweze kujifunza kwa nafasi, lakini pia wasiwe na upungufu na usumbufu katika mafunzo yao. Watakapoingiziwa fedha kwa wakati, naamini wataweza kusoma vizuri na tutazalisha wartaalam bora zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwa Wizara...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako. Mheshimiwa Vedasto Ngombale kama hayupo, Mheshimiwa Maftaha Nachuma. Dakika saba.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami nichangie Wizara hii ya Madini. Nasikitika sana, baada ya kusikia taarifa ya Wizara hapa kwamba bado inazungumza suala la *STAMICO* kuendelea kuwepo kama Shirika la Serikali la kusimamia madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *STAMICO* tumezungumzia kwa muda mrefu sana ndani ya Bunge hili. Kamati mbalimbali zimezungumza juu ya udhaifu wa *STAMICO* kwamba imeshindwa kusimamia rasilimali za madini Tanzania. Leo tunasikitika kuona kwamba mpaka leo Serikali bado imeamua kulea *STAMICO* kama Shirika la Madini wakati inatuingizia hasara katika nchi hii, imeshindwa kusimamia madini yetu ya vito na madini mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate taarifa kwamba kwa nini Serikali pamoja na *STAMICO* kuliingizia hasara Taifa hili bado mnaendelea kuibeba *STAMICO*? Hilo la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nazungumza suala la kuongeza thamani ya madini. Wenzangu wamezungumza hapa kwamba Tanzania tuna tatizo kubwa, madini yetu hayachakatwi hapa Tanzania eti kwa sababu zile mashine zinauzwa bei mbaya; na sababu nyiningine inatolewa kwamba zile mashine kidogo zinahitaji utaalami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana na juzi ndani ya viwanja vya Bunge tunayo mashirika mbalimbali, kampuni mbalimbali za watu binafsi wametuonesha mashine hapa. Zile mashine ni bei rahisi sana. Serikali ingeamua kama kweli ingekuwa na nia ya dharti ya kuchakata madini yetu Tanzania ili yaweze kutoa ajira kwa Watanzania, ingeweza kununua zile mashine. Ni bei rahisi sana tumeambiwa hapa nyuma. Kwa hiyo, naomba Serikali kwamba, iwekeze kwenye kuchakata madini, madini yachakatwe Tanzania; *tanzanite* ichakatwe Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati fulani wakati tunapitia taarifa ya *tanzanite*, *tanzanite* imetoa ajira kwa kiasi kikubwa sana Mji wa Jaipur kule India. Zaidi ya watu laki sita wameajiriwa katika Mji wa Jaipur kule India kupitia madini ya *Tanzanite* ambayo yanatoka Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la ajabu sana, zile ajira zingeweza kutengenezwa hapa Tanzania, Watanzania wetu wakawa wamepata ajira kupitia madini haya ya *tanzanite*, madini ambayo yanapatikana Tanzania pekee duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, wakati umefika sasa wa kuhakikisha kwamba tunanunua zile mashine za kuchenjua yale madini ya *tanzanite*, viwanda viwekwe pale Arusha na maeneo mengine ili Watanzania wetu waweze kupata ajira na siyo tunaenda kuwatajirisha watu wa nje zaidi ya ajira 600,000 kule India, Jaipur. Naomba Mheshimiwa Waziri akija hapa atuambie wana mkakati gani wa kuleta zile mashine kwa wingi za kuchenjua madini ya *tanzanite* ili kudhibiti utoroshaji? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo Kamati ya Madini ya *Tanzanite* ilipendekeza ilikuwa ni ujenzi wa *One Stop Centre*. Kuwe na eneo moja maalum ambalo madini yetu ya *tanzanite* yaweze kuuzwa pale, yaweze kuuzwa kupitia mnada, yaweze kuuzwa kwa njia nyingine. Sasa Serikali imejipangaje kutekeleza agizo hili la pendekezo hili la Kamati ya *Tanzanite* ambayo ililitoa? Mheshimiwa Doto Biteko alikuwa ni Mwenyekiti wa Kamati ile. *One Stop Centre Tanzanite* wamejipangaje mwaka huu kujenga hapa Tanzania ili madini yetu haya yasitoroshwe? Kwa sababu, tunaambiwa kwamba, madini ya *tanzanite* huko nje yamezagaa sana kwa sababu, utoroshwaji ni mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kule Kilimanjaro kuna njia za panya nyingi zaidi ya 300. Sasa hivi tunashukuru kwamba Serikali imeweza kujenga ule ukuta, lakini bado yapo maagizio mengine ya Kamati ambayo yalipendekezwa.

Tunaiomba Serikali, kama kweli tuna nia ya dhati ya kuifanya *tanzanite* iweze kuwanufaisha Watanzania kwa sababu, ni madini yanayopatikana Tanzania tu duniani, tungeweza kudhibiti zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado utoroshwaji tunaamini upo, kwa sababu wachimbaji wadogo wadogo kule wako wengi, kuna leseni zaidi ya 800 pale zimetolewa na agizo hili pia nalo wamelitekelezaje kama Serikali? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Doto Biteko, Mheshimiwa Waziri, kulikuwa na pendekezo la Kamati ya *Tanzanite* kwamba zile leseni zile ziunganishwe kwa sababu, leseni ziko nyingi, zimetolewa zaidi ya leseni 800, eneo dogo la Mererani pale Arusha. Serikali inatekelezaje agizo hili? Kwamba, zile leseni ziunganishwe na wale watu waweke kwenye vikundi, hasa wale wachimbaji wadogo wadogo, ili kudhibiti utoroshwaji wa *tanzanite*. Tunaomba Mheshimiwa Waziri akija atueleze kwamba zile leseni 800 wamezi-*combine* au imekuwaje mpaka leo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la kudhibiti haya madini. Ni jambo muhimu sana kwa sababu haya madini yanapatikana Tanzania tu na eneo dogo tu la Mererani, lakini ukienda huko njie bei zake zimekuwa ni ndogo ukilinganisha na thamani ya madini ya *Tanzanite*. Ukienda maeneo mengi ya India, *South Africa*, yamezagaa kweli kweli na bei zimekuwa ni ndogo mpaka kule Tuckson, Marekani bei zimekuwa ni ndogo kwa sababu yamezagaa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaiomba Serikali ili kudhibiti haya madini, iweze ku-*declare* kwamba atakayepatikana anatorosha madini, basi aweze kuuawa, iwe nyara ya Taifa. Lilikuwa ni mionganoni mwa mapendekezo ya Kamati ya *Tanzanite*, sijui Serikali imejipangaje kutekeleza? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba iwe nyara ya Taifa kwa sababu ni madini ya kipekee, yako Tanzania tu duniani.

Mtu akikamatwa anatorosha ovyo ovyo huko, ili nasi yaweze kutunufaisha, basi ikiwezekana auawe. Naomba Mheshimiwa Waziri atekeleze hili agizo kwamba *Tanzanite* iwe ni nyara ya Taifa kama nyara nyingine. Kwamba, *smugglers* wachukuliwe hatua kali ili watu wasiweze kutorosha nchi yetu iweze kuwa na manufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naomba kuchangia hapa ni suala hili la kampuni hizi ambazo ni kampuni hewa, kuna kampuni nyingi sana za *Tanzanite* zimeanzishwa. Ukipitia zile taarifa, ile Kampuni ya *TML*, nayo inamiliikiwa na Kampuni ya *TML South Africa*. *Tanzanite South Africa* nayo inamiliikiwa na kampuni ya Uingereza. Kwa hiyo, yaani *Tanzanite* ina makampuni mengi sana, kampuni mama, kampuni dada hizi kama tatu, lakini wote hawa wanashughulikia suala moja la *Tanzanite*. Sasa Serikali inakosa mapato sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Wizara hii Mheshimiwa Waziri na Manaibu ni watu makini sana. Wachunguze haya makampuni hewa ambayo yapo, yameanzia pale *TML*, *TML Tanzania*, kuna *TML South Africa*, kuna *TML England* nayo pia ina kampuni mama nyingine huko. Kwa hiyo, hizi kampuni kwa taarifa tulizokwanazo ni kampuni hewa na zinakwepa kodi kupitia mauzo ya *Tanzanite*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba wazipitie hizi kampuni zote ikiwezekana waweze kuzuia wasiziruhusu hizi kampuni kufanya biashara ya madini ya *Tanzanite* hapa Tanzania. Madini haya ni madini yenye thamani sana. Kwa hiyo, naishauri Serikali ihakikishe ya kwamba, inatekeleza hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala hili la madini ya *blue sapphire*. Tanzania hii madini ya *blue sapphire* pale ukienda Tunduru yamejaa sana. Kule...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Yamejaa sana, yanunue. Tunaendelea na Mheshimiwa Catherine Magige, atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Akbar Ajali.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nianze kwa kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kulinda rasilimali zetu yakiwemo madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nielekeze mchango wangu moja kwa moja katika Mkoa wa Manyara, Mererani. Naipongeza sana Serikali na Wizara na Jeshi la Ulinzi kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kujenga ukuta wa Mererani. Kwa kweli, vijana wale walikuwa wazalendo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nampongeza Mkuu wa Majeshi kwa kazi kubwa aliyofanya ya kumaliza ule ukuta wa Mererani kwa wakati. Ingawa Mheshimiwa Rais aliposema kuwa ule ukuta ujengwe, watu walibea sana kuwa hautaisha, lakini Jenerali Mabeyo alijitahidi wakamaliza kwa wakati. Naomba niwapongeza sana. Kweli nchi yetu ina watu wazalendo sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu tu alipoamua kujenga ukuta wa Mererani alitaka madini yetu tuyauze wenyewe na yatufaidishe Watanzania wenyewe ili tulipe kodi na hizi kodi zinufaishe nchi yetu katija sekta mbalimbali. Kwangu mimi ukuta ni ishara tu ya ngome ya ukuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili ukuta huu uwe kumbukumbu, mali zetu ni lazima zitufaidishe sisi wenyewe na sasa mali zetu imetosha kuwanufaisha wageni na Watanzania wachache. Madini yetu yanatakiwa yatunufaishe Watanzania na vizazi vijavyo. Mheshimiwa Rais wetu ana nia hiyo na Watanzania tunamuunga mkono Rais Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa uzalendo huu mkubwa aliouonesha kwa nchi yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuta huu wa Mererani unatakiwa uwe kielelezo cha dhuluma iliyodumu tangu

mwaka 1967 ambapo madini haya ya *tanzanite* yaligundulika. Mheshimiwa Rais wetu tumeona alivyoonesha uzalendo kuzungushia ukuta na kuwa mkali na rasilimali hii ya madini hasa haya ya *tanzanite*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada kubwa ya Mheshimiwa Rais wetu pamoja na Wizara, lakini nataka kusema hivi, madini bado yanatoroshwa. Madini ya *tanzanite* bado yanatoroshwa, yanaenda nchi za nje, wanapitia njia mbalimbali. Naamini sana vyombo vya ulinzi na usalama vifanye kazi. Kama tu mimi Mbunge najua kuwa madini ya *tanzanite* bado yanatoroshwa, nina uhakika kwamba wenywewe wakifuatilia hili watagundua na wawe makini sana na mipaka yetu. Madini ya *Tanzanite* bado yanapita mipakani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwa hii kazi kubwa, Wizara inavyohangaika na Mheshimiwa Rais wetu, watakaokamatwa wanatorosha madini yetu, naomba wachukuliwe hatua kali sana. Hawawezi wakachezea rasilimali zetu ambazo tumekuwa tunahangaika nazo kwa muda mrefu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado niko Mererani. Tumeona wale Wanaapolo wakiwa wanachimba madini na tunaona wale wamiliki wa migodi wakiwa wanahudumia madini. Hii migodi ya Mererani ni kama bahati nasibu. Mtu anaweza akachimba hata miaka 10 au 20 asipate. Kuna kitu kimoja tulikisikia hata kwenye Kamati yangu nilibisha sana kuwa hawa wamiliki wa migodi wawe wanawalipa mshahara hawa wachimbaji kila mwezi. Kwa kweli, tusijidanganye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara wanatakiwa wafanye uhakika wa hiki kitu, wakiangalie kwa umakini, ni ngumu sana. Kwa sababu hawa wachimbaji unakuta wakati mwingine mpaka wanakopa tu ili kulisha migodi yao ili iweze kutoa mawe na unakuta inakaa hata miaka 20 haijatoa. Nasi tangu tunakua tunaonana na Wanaapolo tunaishi nao mitaani, haijawahi kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tu Wizara iangalie mkakati mzuri wa kuweka ili hata watakapopata waangalie hawa wachimbaji ambao tumezoea kuwaita Wanaapolo wapate malipo yao, kwa sababu, kwa kusema hili la kulipwa kila mwezi tusijidanganye, haiwezekani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze moja kwa moja katika Mkoa wangu wa Arusha, Wilaya ya Longido, Kijiji cha Mundarara. Kijiji kile kina wachimbaji wa madini ya aina ya rubi. Wachimbaji hawa wamekuwa wakihangaika muda mrefu sana kujitafutia kipato chao kihalali kabisa, lakini wachimbaji hawa wamekuwa wakipitia changamoto mbalimbali ambapo wana imani kubwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwamba itatatu kero zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa waliyonayo ni madini haya mara wanapopata wanataka yakatwe na madini haya yakishakatwa thamani yake inapungua. Sasa tunakuwa tunafanya nini? Tunataka tuwasaidie wananchi wetu au tunawaumiza? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikatai kunaweza kukawa kuna sheria, lakini Wizara lazima ikae tuangalie hii sheria, kama inawaumiza wananchi wetu, ibadilishwe, tutunge sheria ambayo inawafaidisha. Kwa sababu tunasema madini yanatakiwa yanufaishe Watanzania na wananchi wetu wote kwa ujumla. Sasa kama haya madini yakikatwa yanaumiza wananchi wetu, yanawaumiza hawa wachimbaji, kwa nini tuisangalie sheria ambayo itawasaidia wachimbaji hawa wa Mundarara ili na wenyewe waweze kuchimba kwa amani na waweze kupata thamani na madini yao ili malengo yao waliyokusudia yatimie? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri, dada yangu Mheshimiwa Angellah Kairuki, kaka yangu Mheshimiwa Doto na Mheshimiwa Nyongo nawaamini, najua kwenye hili mtawatendea haki watu wa Mundarara. Nawaombeni sana mnapokuja, mje na jibu la uhakika ili watu wa Mundarara wajue hatima yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba sana watakapotoa vitalu katika maeneo haya waangalie wazawa ambao ni wananchi wa Longido. Wasije wakawapa wageni tukawasahau wananchi wazawa ambao ndio wapo katika maeneo hayo kila siku. Naomba sana Mheshimiwa Waziri hili suala aliangalie kwa makini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nakushukuru sana, siku ambayo niliuliza swalii kuhusu Longido, Mundarara hapa, nashukuru Mawaziri wangu ni wasikivu. Mheshimiwa Nyongo alienda mpaka Mundarara baada tu ya kuuliza lile swalii na akutana na wananchi wa Mundarara. Nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Manaibu wako kwa kuwa wasikivu kwa wananchi na Wabunge kwa ushauri wetu. Ahsanteni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba niendelee kuipongeza Wizara ya Nishati na Madini kwa kazi kubwa inayofanya tangu kuanzishwa kwake. Tumeona maduhuli yanazidi kuongezeka. Kwa mfano, mwaka 2017/2018, Wizara ilipangiwa kukusanya shilingi bilioni 194.66 lakini hadi tarehe 31/03/2018 ilikusanya shilingi bilioni 225 sawa na 115.59%. Mafanikio haya yamechangiwa na juhudhi mbalimbali ikiwemo kurekebisha Sheria ya Madini ya Mwaka 2017. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipongeze sana Serikali, naomba nimpongeze dada yangu ambaye ni Waziri wa Madini wa kwanza, Mheshimiwa Dada Angella Kairuki, unafanya kazi sana mwanamke mwenzetu. Naomba tukutie moyo na wanawake wenzako tunaendelea kukutia moyo, piga kazi tuko na wewe na tunakukubali sana. Huna majivuno, unatusikiliza na uko tayari kushaurika na kukosolewa. Piga kazi dada yangu, tuko na wewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba niwapongeze Manaibu wako Mheshimiwa Nyongo na Mheshimiwa Doto. Vilevile jamani Wizara hii ina viongozi wenye busara sana, wamekuwa pamoja nasi,

tunawasumbua muda mwingu na wamekuwa wakutusikiliza na kutatua kero mbalimbali. Kwa kweli, Mheshimiwa Rais hakufanya makosa kuwapa hiyo Wizara, hongereni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wangu, aendeleee kufanya kazi. Alivyoongea kuhusu ukuta, alivyokuwa anaongea kuhusu madini kuna watu walimdhihaki humu humu ndani, lakini wameshindwa, Watanzania wanamkubali Rais wetu na llani ya Chama cha Mapinduzi inaendelea kutekelezwa, tupo na wewe Rais wetu. Piga kazi, sasa hivi matokeo wanayaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako. Umetusaidia amsha amsha Bungeni. Tunaendelea na Mheshimiwa Akbar, atafuatiwa na Mheshimiwa Seif Gulamali.

MHE. AJALI R. AKBAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii mpya ambayo Waheshimiwa Wabunge wake au Mawaziri wake ni vijana na wapo watatu. Hawa Mawaziri wapo watatu, kwa nini waliteuliwa kuwa watatu na hii Wizara ni nyeti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sidhani kama Mheshimiwa Rais amewapenda sana kwa kuwapendelea ili kuwapungunguzia kazi. Mheshimiwa Rais ameonesha wasiwasi wake kuhusu Wizara hii ambayo ni nyeti. Kwa sababu matarajio ya Mheshimiwa Rais ni mapato makubwa sana katika Wizara hii ya madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja tuliwahi kusikia kwamba mambo ya madini yanatokana na mashetani, sasa haya mashetani ndiyo yanafanya nchi hii isipate madini. Kama kweli sisi hatupati madini, basi namwomba Mheshimiwa Angella aende *South Africa* akamlele Sangoma aje atuchinjie ili tuwezeshwe kupata madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli madini yataendelea kuwa na unyeti na usiri mkubwa sana. Huyo aliyesababisha usiri mkubwa sana sio mtu mwingine isipokuwa ni *STAMICO*. *STAMICO* ni kubwa kuliko Wizara yako Mheshimiwa Waziri. Mawaziri lazima mfanye maamuzi magumu. Bila kuivunja *STAMICO* hamwezi kuleta mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *STAMICO* ni mzigo mkubwa sana kwa sababu ni Shirika la Serikali. *STAMICO* leo imeingia mkataba na *Tanzanite One*, lakini ule mkataba wenyewe una utata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanasheria wa *STAMIGOLD* na *STAMICO* wameshindwa kuelewana. Wanaiomba Serikali ninyi mkae mwapanatishe, wakati tunategemea wataalam wetu wa madini wapo *STAMICO*. Hivi ninyi Serikali mtawapata wapi wataalam? Hebu angalia utata huo. Kwa hiyo, maana yake *STAMICO* ni mzigo kwenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, *STAMICO* wamekuwa ni tatizo. Leo *STAMICO* walikuwa wanamiliki mradi wa makaa ya mawe. Katika mradi wa makaa ya mawe wamechimba yale makaa wamepata tani 8,000.

MWENYEKITI: Mradi wa wapi huo?

MHE. AJALI R. AKBAR: Mradi wa Kiwira Kabulo. Wameuza wamepata shilingi milioni 500. Hebu angalia huo uwekezaji. Ukubwa wa *STAMICO* wanapata shilingi milioni 550 na kilo 2,200 wameweka stoo wanasema wanasubiri kuuza. Inavyosemekana ni kwamba yale makaa ya mawe siyo chochote ila ni uchafu. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba hii ni kampuni ambayo ipo kwa ajili ya kuleta hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Mawaziri, ningekuwa ninyi leo leo jioni hii *STAMICO* ninge-*declare* kuivunja. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *STAMICO* ina madeni makubwa kuliko uzalishaji wake ambao wale watu wa Kiwira wanadai pale. Madeni yaliyoko pale ni makubwa sana, lakini wao wanaonesha kwamba *production* ni milioni 550. Kuna sababu gani ya kuendelea kuwa na Kiwira tena? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo kama haitoshi, hawa watu tena wameingia na *STAMICOLD*. Kule wameumiliki ule mgodi, wamezalisha madeni ya shilingi bilioni 60. Kwa kweli haiwezekani hawa watu kuendelea kuwa ndani ya Wizara hii ambayo ni mpya, tena ina Mawaziri vijana. Wakiendelea kuwa nao, wataondoka nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, *STAMICO* ina majukumu makubwa ikiwa ni pamoja na kuwasaldia vijana. Hivi kweli itaweza kuwasaidia vijana kama wao wenyewe hawajiwezi? Wameandika hapa kwamba ni kutoa ushauri na kutoa huduma kwa vijana. Naomba vijana nchi mzima, kama wanaenda kushauriwa na *STAMICO* watafilisika kama *STAMICO* ilivyofilisika. Wao wasiifuate *STAMICO*, kuna utafiti hapa umefanya na Kampuni kutoka *STAMICO*, wameenda kule, watu wamechimba mita 100 kwenda chini madini hawakuyapata. Maana yake ni utata uliopo ndani ya *STAMICO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiria mwanzoni kwamba kama wameshindwa kwenye madini, basi hawa watu waende kwenye kokoto kule Ubena Zomozi. Hata zile kokoto pale Ubena Zomozi zimewashinda. Kama wameshindwa kuchimba kokoto, mnategemea hii *STAMICO* kweli itatusaidia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile wameomba, wamesema kwamba sasa hivi tunatafuta mwekezaji. Hivi kwenye kokoto unatafuta mwekezaji? Kokoto, yaani mtu ukiwa na shilingi milioni hamsini tu, inatosha kwenda kuchimba zile kokoto. Naomba Mawaziri, kwa kweli hatuna sababu ya kutafuta. Wamesema wanaenda

kutafuta fedha, hizo hela wanaenda kutafuta wapi badala ya kuleta hapa Bungeni ili tuwape fedha wakachimbe zile kokoto?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaotoa fedha ni sisi Waheshimiwa Wabunge, wao wanasema wanafanya mpango wa kutafuta fedha, hizo fedha wanaenda kuomba wapi? Nadhani wangeleta hapa bajeti yao, wakasema maadamu tumeshindwa madini sasa tunataka fedha, shilingi milioni 200 ili tukachimbe zile kokoto. Nadhani ndiyo kazi rahisi ambayo wanayoiweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni hizi zimekuwa ni mzigo kwetu sisi; na madini, karibu asilima 90 ya Watanzania hawayajui. Ajabu asilimia hata asilimia 75 ya hawa Wabunge hatuyajui. Hata mimi ukija kunishauri leo, ukaniambia niingine kwenye biashara ya madini sitayajua. Kwa hiyo, naomba Wizara hii mpya ifanye semina kwa Watanzania, wapate kuyajua haya madini ni nini? Madini, watu wengi hatuyajui na yataendelea kuwa na utata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nimeona ni huo, kwa kuwa Wizara hii ni mpya, lakini napongeza sana jithada ambazo anachukua Mheshimiwa Rais na kuujenga ule ukuta. Anaonesha wasiwasi na bado ameteua Mawaziri wengi kwenye Wizara moja ambayo ni ndogo, lakini ni mpya, tena vijana; anaonesha kwamba bado ana wasiwasi lakini bado anaamini kwamba Wizara hii ikisimamiwa kwa dhati itatoa *production* zenyetija. Nawaomba hawa vijana wasimamie. Huo ndiyo ulikuwa mchango wangu leo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa kuwa hii *STAMICO* itaendelea kuwa msiri na itakuwa mzigo kwetu sisi. Leo waivunje. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Akbar nilidhani nimekuomba uchangie, kumbe unataka kuiua *STAMICO* tu. Haya bwana! Mheshimiwa Seif Gulamali, tutaendelea lakini tutaangalia na muda wetu.

MHE. SEIF K. GULAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami kuchangia Wizara hii ya Madini. Kwanza kabisa napenda tu kupongeza sana Wizara hii ya Madini ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Angellah Kairuki. Pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia pongezi nyingi sana kwa Naibu Waziri ambaye ni Mheshimiwa Doto Biteko pamoja na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo. Kwa kweli Waheshimiwa hawa wanafanya kazi nzuri kwa sababu tunawaona; siyo kama tukiwaona kwenye vyombo vya habari, lakini pia tunawaona wakiwa *field* wanakuja katika Majimbo yetu, wanatembea usiku na mchana kuhakikisha kwamba Wizara hii inakwenda mbele. Hongereni sana Mawaziri na timu zenu zote kwa pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nataka kuzungumza machache tu, lakini katika mchango wangu nataka nijielekeze kama mchangiaji hapa aliyekuwa akizungumzia kuhusu *STAMICO* katika usimamizi mzima wa miradi yote ambayo inasimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *STAMICO* kwa kweli kama ilivyokuwa na wachangiaji wengine, inafeli katika usimamizi wa miradi na rasillmali hizi za Taifa la nchi hii. Hiyo inadhihirisha wazi, kwa mfano, katika migodi kama *STAMIGOLD* na hii tunaita Buhemba. Sisi kama Kamati tulienda pale Buhemba tukajionea ule mgodi ulioko pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Buhemba ilikabidhiwa na Mwekezaji mwaka 2008 na ikarudishwa Serikalini kwenye hiki chombo chetu ambacho ni *STAMICO*. Wakati huo walikabidhi vikiwepo na vifaa; magreda, magari na kila kitu kilichoko mle ndani yakiwemo majumba. Yaani kiasi ambacho unaweza kuanza kesho kuendeleza ule mradi ukasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea, tumekwenda juzi, kabla ya pale kulikuwa kuna kampuni inaitwa *G4ST Limited*, ni Kampuni ya Ulinzi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba

rasilimali zilizokabidhiwa na mwekezaji zinabaki kuwa salama. Hii kampuni ya Ulinzi binafsi iliyokuwa inalinda baadaye ikabidi *i-handle* kwenye Serikali kwa maana ya Jeshi la Polisi. Ule mgodi sasa ukabaki kama hauna mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichokuja kutokea, pale kuna watu walienda mpaka kung'oa madirisha ya nyumba za watumishi, watu wameng'oa madirisha ya milango ya magari na vifaa vyote vilivyomo mle ndani kwenye mgodi. Yaani sasa imetoka kwenye kampuni binafsi, tumeikabidhi Serikali, Serikalini huko sasa ambako tumekabidhi Jeshi la Polisi wamengo'oa kila kitu, yaani vitu vimeibiwa vyote. Hapo hapo maana yake tayari mgodi umerudishwa *STAMICO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu huu ambao migodi yetu inakuwa ipo chini ya usimamizi wa *STAMICO* na *STAMICO*imeendelea kuomba fedha kwa ajili ya kuendesha migodi iliyopo ndani ya nchi yetu. *STAMICO* imefeli. Binafsi kabisa nasema *STAMICO* imefeli na tumeipa fedha kwa ajili ya kujaribu. lendelee kujaribu hivyo hivyo huku ikiendelea kutupa hasara juu ya hasara. Hapa tumeona tuna deni zaidi ya shilingi bilioni 60. Tumezalishiwa na hawa ambao walikuwa wanatusimamia na hatupati faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani sekta binafsi ikisimamia kwenye madini inaleta faida na kampuni inanawiri, mpaka wakati mwagine tunasema kampuni inaiibia nchi yetu. Sasa kama tunaweza tukakabidhi shirika letu wenyewe lisimamie rasilimali lifanye uzalishaji, badala ya kuleta faida linaleta hasara, kwa hiyo hii *STAMICO* kwa kweli, kwa namna moja ama nyingine, sijui kwa sababu wamesema wamekuja watu wapya wanaanza tena mchakato upya kwenye kusimamia, lakini tunapata wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kwamba hata hao wataalam ambao wako chini watabadilishwa mpaka huko chini! Maana yake Taifa hili limekosa watu waaminifu. Watu Wazalendo wamepungua, tunawakabidhi rasilimali kuhakikisha kwamba tunapata, nchi yetu tunafaidika kutokana na madini, lakini hao hao tunaowakabidhi na

wenyewe imepelekea sasa tunapata hasara badala kupata faida. Mchango wangu kwenye *STAMICO* ni huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ya Madini napenda binafsi kuishukuru na kuipongeza kwa sababu katika kuzunguka kwao wamekuwa wanatatua migogoro mbalimbali. Hata walienda kwa Mheshimiwa Kiula pale Jimbo la Mkalama, Kijiji fulani cha Tumuli, wametatua tatizo pale. Mheshimiwa Nyongo nadhani ndio alifika pale, ametatua na sasa hivi tunaenda kupata suluhisho la mgogoro ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge yule alikuwa anakushukuru sana, lakini kwa sababu ni majirani, nami natambua tunahusiana kwa sababu migodi hii inatembea ikitoka pale Tumuli inakuja Shelui na Shelui iko Igunga pale Igurubi. Ametatua mgogoro mkubwa sana katika eneo hili, tunampongeza sana watu wa maeneo ya kule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho nataka kuzungumzia kuna suala hili limeibuka. Tumeona tangazo limetolewa na Mkuu, nafikiri Serikali ya Mkoa wa Geita kwamba inazuia *carbon zisisafirishwe* kutoka Geita kwenda Mwanza. Sasa hii sijaelewa ni sheria inakuja ama inakuwaje? Ndani ya nchi yetu tunazuia usafiriishaji wa *carbon* kupeleka kwenye viwanda sehemu nyingine ambayo mtu anataka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anaamua kupeleka kwenye kiwanda ambacho anaona kinafaa. Haiwezekani ulazimishe kwamba *carbon* niliyonayo ifanyiwe *processing* ndani ya mkoa wangu. Tunatafuta ubora wa kazi zinavyotakiwa kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unaniambia nibaki labda nifanyie hizi *processzote* katika Mkoa wangu wa Geita, lakini ni katika viwanda vilivyoko Geita labda havina ubora wa kuchenjua dhahabu ninavyotaka. Inawezekana nilikuwa na-*expect* kupata kilo moja au kilo tatu. Nikifanyia Geita ama

nikifanyia ndani ya mkoa wangu wa Tabora sipati hizo kilo mbili au tatu, lakini nikipeleka labda mkoa jirani wa Shinyanga, Mwanza au Arusha nikapata kilo tatu, usinizuie mimi ambaye nawekeza, ninayefanya hii kazi kutoka mkoa mmoja kwenda mkoa mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo tangazo tumeliona, watu wenye sekta hii ya madini wanalamika. Namwomba Mheshimiwa Waziri alichukue na atoe maelekezo kwamba hii amri ya kuzuia watu wasisafirishe *carbon* kupeleka mkoa wowote ule katika nchi yetu, iondolewe na isiwepo katika utaratibu ambao ni rasmi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba *carbon* mtu apeleke sehemu yoyote ili mradi afuate sheria na taratibu zilizowekwa na Wizara ya Madini, kwa maana ya vibali na vitu vinginevyo, lakini wasizue watu wasiende katika mkoa mwingine kufanya kazi ambayo ye ye anahitaji. Kazi hizi ni bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine nataka kuchangia suala zima la wawekezaji katika migodi. Wanatumia umeme mkubwa sana na pia gharama za uendeshaji wa migodi hii ni kubwa sana. Naomba Wizara ya Nishati isaidie, gharama za umeme ni kubwa sana katika viwanda hivi. Tuna-*discourage* uzalishaji kwa sababu gharama ya kulipia umeme ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri akae na Waziri wa Nishati ili waone namna gani watakavyoweza kusaidia wawekezaji katika Sekta ya Umeme kwa sababu hizi *units* ambazo wanalipa zinakuwa ni kubwa sana. Tunaomba Mheshimiwa Waziri alichukue hilo na walifanyie kazi ili wapunguze gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanya hizi wata-*encourage* wawekezaji wengi zaidi wawezeka katika Sekta ya Madini. Nafiri hilo Mheshimiwa Waziri atakuwa amelichukua na wataenda kulifanya kazi na watavutia zaidi

wawekezaji kwa sababu mwekezaji anaweza kutumia *generator* akapata faida kuliko kutumia umeme wa Serikali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama mtu akiamua kutumia *generator*, hebu angalia na *generator* ni gharama kubwa sana. Pamoja na gharama kuwa kubwa mtu anaona ni bora kuliko kutumia *TANESCO*, namwomba Mheshimiwa Waziri wakae chini waone ni jinsi gani ambavyo wanaweza kuwasaidia hawa watu ili kuhakikisha kwamba nchi yetu haipotezi mapato ambayo inahitaji katika sekta hii kutokana na kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho nataka kuchangia ni kuhusu suala zima la ruzuku. Hapo siku za nyuma tulikuwa tunatoa ruzuku kwa wachimbaji wadogo wadogo katika kuwawezesha kufanya kazi zao na kuweza kuflikia katika malengo. Mheshimiwa Waziri nasi kule kwetu kwa maana ya Jimbo la Manonga katika Kata zile za Mwashiku, Nguru na Ntobo tuna madini na wachimbaji wadogo wadogo wapo, waliwahi wakati fulani kupata ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Mheshimiwa Waziri, hebu tutilie mkazo katika hili zoezi la kutoa *support* kwa wachimbaji wadogo wadogo, watu wa Jimboni kwangu waweze kupata lakini pia wa maeneo mengine katika nchi yetu wapate hizi ruzuku kutoka katika Wizara. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia kuhakikisha kwamba tunawanyanya wachimbaji wadogo kwenda kuwa wachimbaji wa kat, lakini pia kesho na kesho kutwa watafikia katika *level* ambayo watakuwa walipaji wa kodi wakubwa sana katika nchi yetu. Lengo ni kuhakikisha kwamba tunajikwamua na umaskini tulionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa hatufurahii kuona kila siku tukiendelea kuwa walalamikaji ama tukiendelea kuwa katika hali ya ambayo kila siku ni maskini. Hili neno maskini inatakiwa lifike wakati tuliondoe katika nchi

yetu ya Tanzania. Kuliondoa ni katika kuwawezesha hawa wachimbaji wadogo wadogo na wao wafikie katika *level* ambayo kila sehemu akienda anatambulika, huyu mtu anastahili kuwepo katika nchi yetu hii ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mchango wangu huu mdogo, napenda sasa kuishukuru Serikali, Wizara, lakini Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kweli siwezi kuacha kumshukuru kwa sababu anafanya kazi kubwa sana katika kuhakikisha kwamba rasilimali hii ya madini inalindwa na nchi inanufaika kutokana na rasilimali Mwenyezi Mungu amelijalia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Gulamali kwa mchango wako. Sitamtendea haki Mbunge aliyekuwa anaafuatia kwa sababu ya muda wetu. Kuna tangazo nalirudia tena hili.

Kuna wageni 87 wa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu amba ni Wanachama wa Shirika la Wamachinga Tanzania. Wamachinga mpo? Karibuni sana. Ni Umoja wa Wamachinga nchi nzima na pia sijui kwenye Sekta ya Madini wanaangukia kwenye sehemu ipi, lakini tunao hapa ndio hao. Karibuni sana. (*Makofi*)

Nitangaze ambao tutaanza nao mchana, Mheshimiwa Abdallah Bulembo, Mheshimiwa Vedastus Mathayo, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba na Mheshimiwa Joel Makanya, Mbunge wa Chilonwa. Hawa ndio tutaanza nao jioni, tutaendelea na wengine. Tuna orodha ndefu, sawa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi jioni.

(Saa 6.57 Mchana Bunge lilitishwa hadi Saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimewataja Waheshimiwa Wabunge ambao tutaanza nao sasa hivi, nina Mheshimiwa Abdallah Bulembo, atafuatiwa na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba na Mheshimiwa Joel Makanyaga.

MHE. ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote, nianze kuwapongeza shemeji yangu, Waziri wangu Mheshimiwa Angella Kairuki kwa kazi anazozifanya, Naibu Waziri Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Naibu Waziri Mheshimiwa Doto Biteko, Katibu Mkuu, Mheshimiwa Msanjila na Watendaji wote waliopo ndani ya Wizara hii mpya, nawapongeza sana kwa kazi mnazozifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuona na kuweza kutenganisha Wizara ya Nishati na Madini. Wizara ya Madini ni Wizara nyeti sana katika nchi nyingi, hapa kwetu sasa imeonesha kwamba tunayataka madini yetu yaweze kuleta faida katika nchi yetu. Pia nizipongeze Tume zote zilizoundwa, Profesa Abdulkarim Mruma, siwezi kumsahau kwa kazi kubwa aliyoifanya, Profesa Nehemia Osoro simjui sana lakini Profesa Mruma tunatakiwa tukupongeze na tukupe hati ya shukrani kwa jinsi ulivyojitolea Utanzania wako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, madini katika nchi yetu tulivyoambiwa mara ya kwanza kwamba pato linalopatikana na madini ilikuwa haifiki hata shilingi bilioni moja lakini ukienda kwenye sekta ya madini watu hawa ndiyo wanaosamehewa kodi sana, watu hawa yaani wao ndiyo wao, wale wanaochenjua kidogo ni matajiri, lakini Serikali haipati pesa. Nalipongeza na Bunge kwa kupitisha sheria nzuri sana ambazo zitaongeza mapato kwenye Serikali angalau sekta hii iweze kuchangia uchumi wa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu rasilimali za nchi yetu zimepotea sana lakini leo mwarobaini umepatikana. Nichukue fursa hii zaidi kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi chini ya Rais Mheshimiwa Magufuli kwa jinsi alivyoweza kuwajali wachimbaji wadogo wadogo. Wachimbaji wadogo wamekuwa wakinyanyasika sana katika nchi yao, wakifukuzwa huku na huku, wakipata taabu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu katika nchi hii kwa sababu natoka Kanda ya Ziwa kule, hawajui kazi zaidi ya madini. Wakimwambia yako Singida anaenda, Chunya anaenda, wapi anaenda lakini anaafukuzwa kila siku. Ombi langu kwa Serikali yangu, hebu hawa wachimbaji wadogo, wapate haki ya kuwa na leseni kwamba kuna mahali wanachimba, wako 500 wako 1,000 wapewe uhalali wa kumilliki eneo lile, liwe la kwao. Hawa wachimbaji wadogo, wanachimba kwenye sehemu unaweza kukuta leseni ya Bulembo mchimbaji mdogo yupo, inaleta tabu kidogo. Kwa sababu ni wenzetu, ni vijana wetu, ni watoto wetu, hebu basi tuwawekee utaratibu mzuri angalau wawe na amani, wakijua tunachimba hapa, magaragaja yako hapa, kila kitu kipo hapa, maisha yao yanajulikana yanavyopatikana lakini sasa wamekuwa ni watu wa kubahatisha. Mmewaruhusu wachimbe lakini kila wanapochimba mishale iko pemberi, bunduki ziko pemberi, hebu wapeni nafasi nzuri ili tuonekane thamani tunayowapa na kuna maeneo wanaenda kufanya hiyo kazi yao ili maisha yao waweze kubadilika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni mpya lakini kuna changamoto naomba niwape. Siku za nyuma kuna watu watendaji walikuwa wanakata leseni kama kule kwa Mama Mheshimiwa Wambura au Mheshimiwa Lukuvi, mtu anaweza kutoa hati kwa Bulembo, kesho akatoa kwa Musa kiwanja hicho hicho, ndani ya madini pia neno hilo lipo. Unakuta mtu ana ‘pele’ namba fulani na amemwekeea ‘pele’ pale pale mgongoni na hawa watumishi mmewarithi, tunawaomba sana, hatuna mengi ya kusema kwenu zaidi ya kuwashauri, hebu watafuteni hawa watendaji waliofanya makosa yale wawajibike kwa sababu walikuwa na dhamana

ya Serikali. Unawezaje ukagawa kitalu mara tatu kwa watu watatu tofauti kitalu kimoja? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha atuambie na watendaji wale atawafanya jaze kwa sababu wataipa Tume hii shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine naipongeza Tume iliyoundwa chini ya Profesa na wanakamati wake. Nampongeza Rais na Waziri, Tume ile ni muhimu sana kwa sababu sasa mwarobaini umepatikana lakini Tume ile nina uhakika itapata changamoto nydingi sana kwa sababu ni kitu kipyä kimekuja kuna eneo lenye matajiri wengi, wachimbaji wa dhahabu ni matajiri. Tungekuwa kule Congo, kuanzia Waziri wa Madini na wenzake wote wangekuwa wamevaa cheni za dhahabu tu, mikono imejaa dhahabu si ndiyo? Eneo hili lina mambo makubwa sana. Sasa mnapoenda *ku-deal* na wale watu ambaao ni matajiri, lazima Tume hii tuiombee wawe *serious* sana kwa sababu hawa watu kwenye sekta hii ni matajiri sana ingawa Serikali siyo tajiri. Kwa hiyo, walio teuliwa tunawaamini sana, wanaweze kufanya kazi vizuri sana lakini wawape ushirikiano kuwaonesha kwamba suala hili kwa kazi waliyopewa waitendee haki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kwenye Tume, nawapongeza juzi kuna hati kama 9/10 mmefuta, kwa sababu watu walihodhi ardhı, wakaenda kwenye masoko ya ulimwengu, wakatajirika lakini sisi hatupati kitu. Hata hivyo, kuwanyang'anya isitoshe, waambieni kesho wachimbaji wadogo wadogo waanze kuchimba mpate chochote kama hamjapata watu wa kuwaweka katika maeneo yale. Kwa sababu kunyang'anya ni kitu kingine na kutekeleza ni kitu Kingine. Bajeti ijayo kama mtakuwa hamjafanya chochote pale, nikiwa hai siwezi kuongea hivi nitakuwa naongea kwa sura tofauti, lakini leo sina uwezo wa kusema sana kwa sababu ni kitu kipyä, mmekifanya kwa nia njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yale kwa sababu yanayo rasilimali, kama hamjajipanga wachimbaji wadogo waingie. Unajua hawa wachimbaji wadogo wako wengi katika nchi hii katika sekta hii, ukiwaambia leo kesho watakuwepo 10,000 hata 100,000 wanachimba mnapata

pato kidogo, mmeshaweka sheria, kuliko tunawanyang'anya watu halafu tunakaa nayo tunaanza kutengeneza akili ya kufikirika, unajua bado, aah, tumeondoa kwa sababu hapatumiki, ni vizuri mkaandaa mazingira ya kuweza kupatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina dakika tano ama 10?

MWENYEKITI: Endelea tu Mheshimiwa.

MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipongeze Jeshi la JKT kwa kutengeneza ule ukuta, watu walisema haiwezekani imewezezana. Wizara ya Madini nawapongeza sana kwa ushirikiano wenu, watu kitu walichokuwa wanafikiri kiko mbinguni sasa kiko tayari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Jenerali Venance Mabeyo na Meja Jenerali wa JKT, vijana wamefanya kazi nzuri sana na ya kupongezwa kwa sababu wametia moyo wanalinda nchi yao. Ombi langu kwenu Wizara na Jeshi, pale Mererani hamjafunga *security*. Mmemaliza kujenga ukuta, watu wako kwenye ukuta, haionyeshi faida ya ukuta ule, kama hatujazichunga rasilimali tulizotakiwa kujengea ukuta ule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwenu, zile *security* mnatakiwa kujenga, inawezekana mmechelewa mnajipanga vizuri, jipangeni vizuri sana, wachimbaji wa madini mimi sijui tanzanite, lakini sehemu zingine nina uzoefu, wanaweza kutembea kilometra saba chini, wakatokea mle ndani ya tanzanite wakafanya kazi. Ni vizuri ile *security* mnayotaka kuiweka i-sense kwenda chini kama ni kilometra 10, 12 ili chochote kinachotokea kiweze kujulikana mapema lakini tukiutengeneza ule ukuta, halafu mkauacha muda mrefu, aah, si vizuri kusema sana. Nachoshauri, nguvu tuliyotumia, pesa, muda ni vizuri mkauweka ule ukuta *security* ili watu waone faida ya tanzania ya Tanzania sasa inapatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini, sitaki kutoa usuhuda tangu mmejenga ule ukuta bado ule mchezo wa Nairobi unaendelea tu, hamna jinsi ya kuuzuia, kwa sababu hamna *scanner* ya kumwangalia mtu, tukiingia pale *Airport* unaangaliwa mpaka sindano. Pale kwenye tanzanite inatakiwa mtu anatoka nayo kwenye gari, chombo kinalia, anaambiwa simamisha hilo gari, mtu anakuja nayo kwenye viatu, anaambiwa simama pale, ndiyo tutaweza kuona faida ya hilo ambalo Mheshimiwa Rais na Wizara wamedhamiria kulifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, mimi ni mjasiriamali kidogo wa madini ya *copper...*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Pia tuwe tunajiuliza kwa nini zinotoroshwa, lazima tujielekeze kwenye masuala yote hayo, mifumo yetu ya kodi tuiangalie kwa makini kwenye tanzanite.

Wahesimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Joel Makanyaga na Mheshimiwa Richard Ndasa ajiandae.

MHE. LOLESLA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye bajeti hii ya Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais, kipekee kabisa kwa kuona umuhimu wa Wizara hii ya Madini, ndiyo maana akaanzisha Wizara kamili inayohusika na suala la madini. Kwa kweli nizidi kumtia moyo tu kwamba aendelee kuchapa kazi kwa sababu Watanzania tuko nyuma yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri, pamoja na Naibu Mawaziri wake kwa kazi kubwa wanayoifanya kwenye Wizara hii. Ni Wizara mpya lakini kazi wanazozifanya kwa kweli zinatutia moyo wananchi ambao tulikuwa na changamoto nyingi hapo siku za nyuma. Sasa hivi changamoto zinapungua siku hadi siku, hongera sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Mawaziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri baada tu ya kuteuliwa aliweza kufunga safari akafika mpaka Geita, akaangalia changamoto za wachimbaji wa madini, wakubwa, wa kati na wadogo. Kwa kweli nampongeza sana Waziri na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, ahsanteni sana kwa kusikiliza kero, wananchi wana imani na nanyi kwa kiasi kikubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Nyongo, Naibu Waziri alikuja Nyarugusu akasilikiza kero tukiwa pamoja na watu wakauliza maswali mbalimbali. Nina hakika wanaendelea kuangalia hizi changamoto ili kuzifanya kazi, nasema ahsanteni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru Wizara ya Madini, kwa jinsi ambavyo wametupa heshima kwenye Kijiji cha Rwanagasa kwa kutengeneza kituo cha mfano kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Busanda na Geita kwa ujumla tunashukuru kwa ajili ya kituo cha mfano cha Rwanagasa. Kwenye bajeti hii wamesema kwamba kimefikia asilimia 70 ya utekelezaji, naomba mwaka huu kiweze kukamilika ili wananchi waweze kunufaika na kujifunza mambo mazuri hasa wale wachimbaji wadogo ambao wamekuwa na changamoto kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba nchi hii ya Tanzania inao wachimbaji wadogo wengi sana. Katika takwimu baada ya utafiti wa UNEP mwaka 2012 ni kwamba wachimbaji wadogo 500,000 mpaka 1,500,000 wameweza kuwa na ajira kupitia shughuli za uchimbaji. Kwa sasa hivi

hali halisi inaonesha kama watu 2,000,000 ni wachimbaji wadogo ambao wanajishughulisha na shughuli za uchimbaji madini. Niombe Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara waangalie namna ya kuwasaidia hawa wachimbaji wadogo. Ni kweli wana mchango mkubwa sana kwenye Taifa hili, wakiwezesha kwa kupewa mitaji, pengine hata kwa kukopeshwa kwa riba nafuu, wataweza kufanya kazi zao kwa umakini na mwisho wa siku watakuwa na uwezo wa kuchangia kwenye pato la Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, japokuwa kwenye bajeti sikuweza kuona mahali ambapo mmezungumzia habari ya kuwawezesha kwa kuwapa mitaji, naomba Wizara iangalie uwezekano wa kufanikisha suala hili. Siku za nyuma kulikuwa na programu hiyo ya kuwapa ruzuku wachimbaji wadogo, hebu basi tuangalie namna ya kuwawezesha kwa ruzuku au kwa mikopo yenyeye riba nafuu ili waweze kujilua kiuchumi kuititia shughuli hizi za uchimbaji. Uchimbaji ni shughuli ambazo zinahitaji mtaji wa kutosha ili kuweza kuzifanya kwa umahiri. Kwa hiyo, niombe Wizara iangalie namna ya kuwasaidia wachimbaji wadogo kwa sababu wanahitaji kusaidiwa ili waweze kuchangia katika pato la Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna ule Mgodi wa *Buckreef* ambao ullingia ubia kati ya *TANZAM* pamoja na *STAMICO*. Ni miaka mingi sasa tangu mwaka 2011 lakini hatuoni kitu chochote kinachoendelea kwa ajili ya mchango wa wananchi. Wachimbaji wadogo waliondolewa akapewa *TANZAM* kwa ubia na *STAMICO* lakini hatuajaona faida ya mgodi huu. Nimefurahi kuona kwamba kwenye bajeti wamesema kwamba Serikali inaianya utafiti kuona kama *TANZAM* na *STAMICO* waendelee au vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe suala hili lifanyiwe kazi kwa haraka zaidi kwa sababu tangu walivyoanza mwaka 2011 kuna baadhi ya wananchi walifanyiwa tathmini, wanatakiwa kulipwa fidia, mpaka leo hawajalipwa fidia yoyote na wanaauliza ni lini sasa wataweza

kulipwa fidia zao. Mashamba yao hawalimi, hawafanyi kitu chochote na hawayaendelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huu ubia kati ya TANZAM na *STAMICO* kwa kweli ni kero kubwa sana katika maeneo yetu ya Rwanagasa na sehemu mbalimbali. Niombi Mheshimiwa Waziri mlifanyie kazi jambo hili ili hatimaye liweze kuleta tija. Kwa sababu lengo kubwa ya uwekezaji ni kuleta tija kwa wananchi wanaozunguka maeneo husika lakini pia kwa wananchi wetu kwa ujumla. Mpaka sasa hatuoni tija yoyote kupitia huyu mwekezaji *TANZAM* na *STAMICO*, ni ubia kwa asilimia 45 kwa 55 lakini hatuoni faida yoyote ya kuhusiana na uwekezaji huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hiyo, tunaiomba Serikali sasa iangalie na kuchukua hatua mapema ili hatimaye wananchi waweze kunufaika na uwekezaji au madini yaliyopo katikati yetu. Tunamshukuru Mungu kwamba nchi ya Tanzania tunayo madini ya kutosha, tuna mambo mengi makubwa lakini sasa vitu vingi vimekuwa havitunufaishi vizuri kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa ajili ya kubadilisha hizi sheria, mwaka jana tumeweza kubadilisha Sheria ya Madini ya mwaka 2010 tumpata sheria mpya ya mwaka 2017. Kwa hiyo, najua kabisa kwamba kupitia mabadiliko haya, ndiyo tunaona tija na mabadiliko mazuri ambayo ni kwa manufaa ya wananchi wetu na kwa ujumla kama Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazidi kuiomba Serikali iangalie katika migodi mbalimbali midogo na mikubwa, kwa mfano, katika Mkoa wetu wa Geita tuna rasilimali dhahabu lakini bado wananchi wa pale hatunufaiki ipasavyo. Kwa mfano, mitambo ya uchenjuaji wa dhahabu mingi iko Mwanza wananchi wa Geita hawanufaiki. Kwa hiyo, tunaomba Serikali itusaidie, hata hizi *carbon zinazosafirishwa* kila wakati kutoka Geita kwenda kuchenjuliwa Mwanza siyo mzuri, wananchi wa Geita wanakosa mapato ambapo pengine watoto wetu wangepata ajira pale kupitia

uchenjuaji huu. Kwa hiyo, ikiwezekana tunaomba Serikali itusaidie wawekezaji wajenge mitambo yao ya uchenjuaji hapo hapo Geita ili hatimaye *process* zote za uchenjuaji wa dhahabu zifanyike Geita ili wananchi wa Geita waweze kunufaika na madini ambayo Mwenyezi Mungu amewapatia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkitusaidia hilo hakika wananchi wa Geita hawatawasahau, watajua kabisa kwamba Mheshimiwa Waziri amewasaidia na Mungu ataendelea kumuinua Waziri na kumbariki kwa sababu atakuwa amewasaidia sana. Kwa hiyo, niombe tu Serikali kupitia Wizara hebu wafanye utafiti kidogo juu ya jambo hili. Tunachotaka kupitia dhahabu wananchi wetu waweze kupata ajira. Tunajua kabisa Geita na maeneo mengi ambayo yanashughulika na kuchimba madini miji inakua kutokana na madini yaliyopo nasi tunahitaji kupitia dhahabu tuweze kunufaika zaidi. Kwa hiyo, uchenjuaji na viwanda vile vyta kuongeza thamani ya madini, tunaomba pia vijengwe kwenye Mkoa wetu wa Geita ili wananchi waweze kunufaika zaidi. Ni kama korosho kule Mtware, huwezi ukazungumzia korosho ukiwa Geita yaani kila kitu kinafanyika kule. Kwa hiyo, nasi tunaomba Geita sasa kila kitu kuhusiana na dhahabu kifanyike pale na kuwe na kituo kikubwa ili wananchi wetu pia waone umuhimu wa hiyo rasilimali ambayo Mungu ametupatia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naiomba Serikali iangalie wachimbaji wadogo kwa kuwawezesha mitaji ili tuweze kuona umuhimu wa kuweza kuchangia katika Pato la Taifa kupitia kuwawezesha wachimbaji hao. Kikubwa zaidi Wizara itusaidie kuendelea kuboresha zaidi sekta hii ya madini hasa katika suala zima la usafirishaji wa *carbon* na kuhakikisha kwamba tunajenga mitambo pale Mkoani Geita ili tuweze kunufaika zaidi vizazi vyetu pamoja na wananchi kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana, naunga mkono hoja kwa sababu mambo mengi yamekwisha kufanyika. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Joel Mwakanyaga, Richard Ndassa na Mheshimiwa Deogratias Ngalawa.

MHE. JOEL M. MAKANYAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru sana kupata nafasi hii leo kuwa mmoja kati ya wachangiaji katika hotuba ya Waziri wa Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John Joseph Pombe Magufuli pamoja na Serikali yake yote, kwa namna wanavyofanya kazi kwa umakini mkubwa sana unaotuletea Taifa manufaa makubwa sana ambayo sote tunayaona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia nafasi hii kumpongeza sana Waziri wa Wizara hili pamoja na Naibu Mawaziri wake wote wawili kwa kazi kubwa wanayoifanya ambayo sote tunaiona. Kipekee kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa namna alivyoiwasilisha hotuba hii hapa leo asubuhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii sasa niseme kwamba toka Serikali ya Awamu ya Tano imeingia madarakani tumeona hatua kadha wa kadha zinazochukuliwa ambazo zinalenga kuboresha maslahi ya nchi hii. Tumeona hatua madhubuti zilizokwisha kuchukuliwa mpaka sasa zinazoihusu Wizara hii ya Madini, mojawapo ikiwa ni suala la makinikia, kazi kubwa imefanyika, sisi sote tuna masikio tulisikia, tuna macho tuliona, tunaona jinsi gani mambo yanavyokwenda sasa ukilinganisha na hapo awali kuhusiana na suala zima la makinikia na mapato ya Serikali kuititia jambo hili la makinikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona pia hatua ya ujenzi wa ukuta kuzunguka machimbo ya tanzanite kule Mererani. Kwa hakika mambo haya pamoja na mengine mengi yameongeza kwa kiasi kikubwa sana mapato ya Wizara hii katika uchumi na ujenzi wa Taifa hili la Tanzania. Tunawashukuru sana na kuapongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Dodoma kama inavyooneshwa kwenye kitabu hiki tulichogawiwa cha Wakala wa Jiolojia Tanzania kuhusiana na madini yanayopatikana Tanzania, Dodoma pia ipo kwenye orodha na ina madini mengisana. Dodoma hakuna wilaya ambayo haina madini, kila wilaya ina madini yasiyopungua mawili, matatu ambayo yanapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile sasa Wizara zote ziko Dodoma ikiwepo na yake, naomba waangalie ni namna gani madini haya ikiwemo madini nikel, dhahabu na *chrysoprase* ambayo yanachimbwa kwa wingi sana katika Wilaya ya Chamwino na hasa katika Jimbo langu la Chilonwa yataweza kunufaisha wananchi wetu. Halmashauri hatuna tunachopata kwa maana ya *service levy* na *corporate responsibilities* hatuzioni katika maeneo yetu ambako madini haya yanachimbwa. Kwa hiyo, kwa wao kuwa hapa Dodoma hebu wasaidie Halmashauri zetu ziweze kuwa mionganoni mwa Halmashauri zinazofaidi machimbo haya yaliyopo hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuangalia hiki kitabu niseme tu sijaelewa sana ni kwa nini, kuna madini yanaitwa dhahabu nyeusi (*black gold*) na najua anafahamu, haya ni mawe. Mawe haya kulingana na wachimbaji kwa jinsi tulivyokaa na kuongea nao wanachimba kule Kibaha pia lakini wakilinganisha na hapa Dodoma madini hayo wanayachimba kule Itiso, madini ya hapa yana ubora wa hali juu sana, siyaoni kwenye hiki kitabu. Tulivyokwenda kutembelea kule madini haya ya *black gold* yanatumika kwa sehemu kubwa sana kutengeneza marumaru yenye ubora wa hali ya juu sana na zote zinauzwa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Serikali kuhamia Dodoma kwamba sasa ujenzi mwangi unafanyika hapa Dodoma, hebu nilete rai kwa Waziri, waangalie namna gani wanavyoweza kuhakikisha marumaru zinazopatikana Itiso zinakuwa sehemu kubwa ya ujenzi ya majengo yanayojengwa hapa Dodoma kwa kipindi hiki ili angalau kama Serikali tuweze kuwa na sehemu ya kufanya mchakato

wa yale mawe na kupata *final product* tu-generate ajira kwa ajili ya vijana wetu pia na kipato kwa ajili ya wananchi wetu. Naomba sana Mheshimiwa Waziri akiona inafaa pamoja na Naibu Mawaziri, mmojawapo baada ya bajeti hii hebu tukatembee huko mkajionee wenyewe kwa macho ni nini kinachoendelea kule na ni namna gani kwa ukaribu zaidi mnaweza mkasaidia kuhakikisha kwamba Halmashauri zetu zinaweza kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, niseme kwamba naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Nashukuru sana Mheshimiwa Makanyaga kwa mchango wako, nami nitapenda kufika Itiso.

Tunaendelea na Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Ngalawa na Mheshimiwa Hamida Abdallah ajiandae.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Niunge mkono hotuba zote mbili kwa maana ya hotuba ya Waziri pamoja na hotuba ya Kamati ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita sana katika kushauri na moja litakuwa ni ombi na baadaye Mheshimiwa Waziri atakaposimama kesho basi anisaidie kupata majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa jana kuizinduzia rasmi Tume ya Madini chini ya Prof. Kikula pamoja na wenzake akiwepo pia Prof. Mruma. Sina wasiwasi na watendaji hawa kwa sababu nawafahamu ni wazuri. Mheshimiwa Rais amewaamini na kwa sababu ni watu wenye weledi mkubwa Tume hii ya Madini sasa watalbadilisha italeta taswira ambayo itaakisi matokeo mazuri kwa rasilimali zetu ambazo Mungu Mwenyezi ametujalia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niishauri Serikali, nimejaribu kupitia kitabu naangalia zile takwimu, madini

yanayosafirishwa nje au yale yanayouzwa ndani ukiangalia rasilimali zote tulizonazo, takwimu hizi kama vile zimepikwa, lakini hata kama zimetengenezwa kwa uhakika zitakuwa ni za uwongo kwa sababu madini tuliyonayo na takwimu tulizoonyeshwa hapa hazifanani hata kidogo. Mimi naomba sana Tume hii nategemea mwakani utakapokuja Mheshimiwa Waziri atatuletea takwimu za madini yote, siyo almasi peke yake, dhahabu peke yake, atuletee takwimu za madini yote kokote yanakochimbwa. Kwa mfano, hapa ametulea takwimu za madini yanayouzwa ndani, yanayouzwa nje, ametaja Chunya na Mwanza peke yake, sasa nikawa najiuliza hivi madini yako Chunya na Mwanza peke yake, kwa maana ya Kanda, hizo Kanda zingine kwa nini hawakuonesha? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sababu ofisi hii ni mpya kwa maana ya Wizara iwe inatupa taarifa kamili za kila Kanda ni kiasi gani imokusanya na hili liwe jukumu lao. Nimwombe Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, najua atatoa taarifa yake Machi mwakani, napenda tupate taarifa kamili kwa kila Kanda imefanya nini na imokusanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba Tume hii iongeze ukusanyaji wa maduhuli. Kwa sasa wanasema mpaka Machi wamekusanya shilingi bilioni 310 ni ongezeko la asilimia 59 lakini inawezekana walikisia makisio ya chini, haiwezekani mka-*surpass* kwa asilimia 59 hata kidogo. Tunaomba makisio yafanane na hali halisi ya kile ambacho kinavunwa, makisio hayo ni madogo mno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Tume hii wasiwe na urasimu wa kutoa leseni. Nimwombe Mheshimiwa Waziri anisaidie, kuna machimbo ya dhahabu ya kule Muheza, machimbo yapo sehemu moja inaitwa Magambazi kupitia kampuni ya CANACO, Mheshimiwa Doto mdogo wangu alienda pale akapaona, akazungumza na Mkuu wa Mkoa, mwekezaji yule amewekeza pesa zake nyingi, hebu lisuluhisheni hili ili huju mwekezaji aweze kufanya kazi zake lakini pia Serikali kupita machimbo yale tuweze kupata mrabaha wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tuna *GST*, najua Profesa Mruma alikuwa kiongozi pale, anajua matatizo ya *GST*, kazi zao zinajulikana lakini huyu mtoto *GST* hatumtendei haki kwa sababu hatumpi pesa za kutosha za kwenda kufanya utafiti wa maeneo ambayo kuna madini. Tunampa pesa kidogo lakini tunamwambia akafanye utafiti, hawesi kwenda kufanya utafiti kwa sababu hana pesa za kutosha. Kwa hiyo, niombe sana ili *GST* ifanye utafiti na moyo wa kujitolea ni lazima watu hawa wapewe pesa za kutosha. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwa hayo makampuni ya wawekezaji wanapokuja nishauri sana Mheshimiwa Waziri ushirikishwaji wa wananchi kule kunakochimbwa madini ni wa muhimu. Ni lazima kuwe na sheria inayomtaka mwananchi kushiriki, kwamba wewe mwekezaji wetu, tunashukuru umekuja lakini ni lazima kuwe na *clause* inayosema ni lazima uchangie au ufanye moja, mbili, tatu. Ukimwachia huyu mwekezaji peke yake aamue ye ye kwa jinsi anavyotaka na ataamua, anaweza akatoa au asitoe, lakini kama kutakuwa na *clause* inayosema kwamba lazima utatoa hiki na hiki na hiki hii itasaidia, huo ndiyo utakuwa ushirikishwaji mzuri. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri anazungumzia mambo ya sera na sheria. Wizara imetengeneza Kanuni saba za Madini ambazo sitaki nizitaje kwa sababu ya muda, siyo vibaya kwa sababu hizi Kanuni nafikiri Waheshimiwa Wabunge, najua kwenye mfuko mmetupa zile sheria, tunamwomba sasa Mheshimiwa Waziri hizo Kanuni saba hizo, siyo vibaya akazileta Bungeni hapa na siyo tu kwetu hapa ni vizuri akazishusha mpaka chini kwa *DC* na *RC* kule ambako madini yanachimbwa ili kusudi wajue hizo kanuni zinasemaje. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu Mthamini wa Madini hasa Almasi yupo mmoja tu kama siyo wawili. Sasa Mthamini wa Madini ya Almasi akiwa mmoja au wawili unategemea nini? Anaweza akashirikiana na wale watu wa upande mwininge kuidanganya Serikali. Tuwe na

utaratibu mzuri wa kuwasomesha na siyo madini ya almasi peke yake nafikiri na madini mengine, tuwe na utaratibu wa kuwasomesha hawa wataalam wetu waje wafanye kazi ambayo tunaitaka ili mapato ya Serikali yaongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni kuhusu utoaji wa leseni kwenye maeneo mbalimbali yale ambayo hayaendelezwi. Ndugu yangu amesema hapa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Wazazi Mstaafu, yale maeneo ambayo yamechukuliwa na watu ambao hawayaendelezi, zaidi ya miaka 10, 20, 30, hivi tunasubiri nini kuwanyang'anya? Nashauri kwenye zile leseni muangalie namna nzuri zaidi, mbali ya kuandika jina na anuani muweke na picha ya huyo mwekezaji tuione, hii itasaidia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tena kwamba naunga mkono shughuli za Serikali lakini niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ndassa kwa mchango wako. Mheshimiwa Ngalawa, Mheshimiwa Hamida Abdallah na Mheshimiwa Janet Mbene.

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia Wizara hii muhimu ya Madini. Kwanza kabisa, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Dada yangu Angellah na marafiki zangu, Waheshimiwa Stanslaus Nyongo na Doto Biteko. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye dira ya Wizara hii ya Madini. Ukiangalia dira ya Wizara inasema ni kuwa Wizara inayoheshimika Afrika katika kuendeleza rasilimali za madini ili ziweze kuchangia kwa ufanisi katika uchumi wa Taifa, niishie hapo. Mimi natoka Ludewa, kule kuna chuma ambayo naamini ni madini na kuna makaa ya mawe ambayo naamini kuwa ni madini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukijaribu kuangalia kile chuma cha Liganga naona hakuna *link* kati ya Wizara ya Viwanda na Wizara ya Madini. Ndiyo maana unaweza ukaona hata kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri hajagusia kabisa chuma cha Liganga. Pamoja na kuwa kwamba huu ni mradi kielelezo ambapo tuna imani kwamba katika programu yetu ya miaka mitano ipo na katika programu ya mwaka moja moja ipo, naamini hapa kuna shida ya kutokuwa na *link* nzuri ya kuona kwamba hiki chuma kinaweza kuisaidia nchi kwenda. Kwa sababu ya ile dira ambayo sasa tumeshaizungumza naamini kabisa tunge-*link* haya madini na tukapata ule mwelekeo ambao ni sahihi chuma hiki cha Liganga kingeweza kupewa kipaumbele na kuleta tija kubwa sana kwa maslahi ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunazungumzia miundombinu ya reli na majengo mbalimbali, ukijaribu kuangalia soko la ndani tu peke yake hiki chuma cha Liganga kinaweza kuleta tija kubwa. Kwa hiyo, napenda tu kuwepo na *link* kati ya Wizara hizi mbili badala tu ya kusema kwamba hii imeenda moja kwa moja kwenye Wizara ya Biashara. Ni kweli chuma ni biashara, ni kweli chuma ni uwekezaji lakini chuma ni madini. Kwa hiyo, *at least* Mheshimiwa Waziri angeweza kukiongelea tuone ni namna gani kinaweza kushughulikiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho napenda kukizungumzia ni juu ya suala la makaa ya mawe. Tumeona hapa makaa ya mawe yamezungumzwa Kiwira na Ngaka. Tunayo makaa ya mawe Mchuchuma, licha ya ule Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma kwa maana ya kuzalisha umeme, bado kuna eneo kubwa la Ludewa linayo makaa ya mawe. Je, Serikali imefanya utaratibu gani kwa sababu Ketewaka tunayo makaa ya mawe mengi sana. Maeneo yale yote ya Mwambalasi kuna makaa ya mawe mengi sana, lakini sioni kama Wizara imeshajielekeza kuona licha ya ule mkaa wa mawe ambao unaweza ukazalisha umeme pale Mchuchuma kuna sehemu nyingine ambazo vilevile zingeweza kutumika na kama ambavyo Ngaka wanauza bado na maeneo mengi ya Ludewa yangeweza kuchimbwa

huo mkaa na ukauzwa na ukaleta tija. Tija kwa maana ya wananchi ajira na kwa maana ya Serikali kupata kodi. Kwa hiyo, nadhani *GSTiendelee* kufanya kazi yake nzuri na tuweze kuainisha kwa kiasi kikubwa tuna mkaa kiasi gani maeneo yale kwa ajili ya faida ya wananchi wetu na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao hawa wachimbaji wadogo. Serikali imechukua hatua, niipongeze kwa ajili ya kuwapa mikopo lakini wachimbaji wadogo wanaopata mikopo ni wachache. Kwa hiyo, naamini kwamba tungeweka utaratibu mzuri wa kuwapa elimu hawa wachimbaji wadogo ili waweze kukopa hata kwenye mabenki badala ya kusubiria ruzuku kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini tunao wachimbaji wadogo sana, Ludewa yapo machimbo sehemu za Amani kule, Kata ya Mundindi wapo wachimbaji wadogo wengi lakini hawajui nini wafanye. Wale watu hawana elimu ya kutosha, nadhani sasa Serikali ifike wakati ipeleke elimu ya kutosha kwa wale wachimbaji ili ikiwezekana sasa wajue namna gani ya kuendesha biashara, namna gani ya kutunza kumbukumbu, namna gani wanaweza wakakopeshwa na mwisho wa siku waweze kuendeleza biashara *in sustainable way*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo suala la tanzanite. Tanzanite inapatikana Tanzania tu lakini ukienda kwenye soko la nje madini yaliyopo kule ni mengi zaidi na yanapelekwa na nchi ambayo siyo Tanzania. Nakumbuka mwaka jana tuliongelea hapa juu ya *certificate of origin*, kwamba mtu yejote ambaye anaweza akasafirisha yale madini awe na *certificate* ambayo inatoka kwenye nchi husika. Sijajua Wizara mpaka sasa imeshafikia wapi katika kuhakikisha kwamba haya madini yanapokuwa yanauzwa kule ili isionekane kwamba hawa watu wametorosha au wamefanya biashara haramu, kuwepo na *certificate* maalum ya kuonesha kwamba madini haya yametoka Tanzania. Kwa kufanya hivyo, maana yake tutapunguza sasa ile watu kutorosha madini kuititia kwenye mipaka na maeneo mbalimbali tuweze kupata ile faida. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kujenga ule ukuta. Pia nimshukuru Mheshimiwa Rais, Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Mkuu wa Mkoa wa Arusha na pia *DC* wa Simanjiro Bwana Chaula kwa kufanya usimamizi mzuri na kuhakikisha kwamba ule ukuta umekamilika na pia niishukuru Wizara kwa ujumla wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tuna suala hili la *GST*. *GSTimepewa* majukumu makubwa sana ya kufanya tafiti za madini kwa nchi lakini ukijaribu kuangalia bajeti ambayo wanawekewa ni ndogo sana. Kwa hiyo, kila mmoja hapa na katika Wilaya na Jimbo lake wanahitaji kuona kwamba ni madini kiasi gani yapo na namna gani tunaweza tukayatumia wananchi waweze kunufaika na madini hayo, lakini bajeti wanayopewa *GST* hailingani na haitoshelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine naamini kabisa tunao wataalam pale *GST* lakini ni wachache. Serikali ichukue sasa hatua kuelimisha wataalam wetu wawe wengi ili mwisho wa siku tuweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni juu ya gharama za tafiti. Watu wengi sana wameshika haya maeneo na wana leseni lakini gharama zile zinakuwa ni kubwa kwa maana *GST* iko centred sehemu moja. Kwa hiyo, kila mmoja anayetaka kuja kuitumia *GST* kwa ajili ya kumfanyia tafiti maana yake ni asafiri kutoka aliko aje Dodoma. Sasa wananchi wetu hawana uwezo mkubwa kiasi hicho. Naamini kwamba wangeweka utaratibu ambapo *accessibility* yake iwe ni jirani ili hiki chombo kiweze kutumika kwa unafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tu-*create awareness* kwa wananchi wajue hizi shughuli, kwa sababu *GST* iko Dodoma na naamini wengi wenye machimbo haya hawaijui *GST*, wala hawaijui *GST* maana yake nini. Kwa hiyo, yawepo matangazo ya kutosha, tu-*create awareness* ya kutosha ili wananchi wetu waweze kujua kazi ambazo zinafanywa na *GST* na wakati mwingine kuepukana na matapeli ambao wanawazunguka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la uwekezaji, tumekuwa na wawekezaji wengi sana wageni na inafikia mahali sasa kile kitu ambacho kinafanyiwa tafiti kule Serikali iko *unaware*. Kwa hiyo, ifike mahali sasa hawa wageni wanapokuja kufanya tafiti kuwepo na *element* ya Serikali ili kuweza kujua ni madini kiasi gani, kwa sababu unaweza ukapelekewa ripoti ambayo si sahihi, ripoti ambayo hailingani pengine na hali halisi iliyopo na hii naamini kwamba imeligharimu sana Taifa huko tulikotoka. Kwa hiyo, tukifanya utaratibu huo tutaona tija ya madini yetu na hawa wanaofanya tafiti hasa mashirika ya kigeni lazima yaweze kusimamiwa na tujue ni nini ambacho kinafanyiwa tafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni juu ya utoaji wa leseni. Mara nyingi unakuta kwamba mtu ambaye madini yapo kwenye eneo lake hajui kama pana madini lakini unaambiwa kwamba eneo hilli tayari lina mtu na tayari ana leseni, Serikali ya Kijiji na Wilaya hazijui, nadhani tuweke utaratibu sasa ili...

*(Hapa kengele illilia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Hamida, Mheshimiwa Balozi Kamala ajiandae.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wake kwa kuwasilisha taarifa yao ya mapato na matumizi kwa kipindi hiki cha 2018/2019. Pia nichukue nafasi hii kuwapongeza Mawaziri hao kwa sababu wanafanya kazi

kama timu na nimeshuhudia katika kipindi kifupi tu kazi ambazo zinafanyika za usimamizi wa rasilimali hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa nimpongeze Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa anayoifanya ya kusimamia rasilimali hii ya madini, kwa kweli anastahili pongezi zote. Kwa kila namna tuendelee kumuombea dua njema Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya nzuri, afya njema ili aweze kusimamia majukumu yake ambayo yanaleta faida katika Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze pia Wizara ya Madini kwa usimamizi, kwa muda mfupi wameweza kuongeza mapato kwa zaidi ya asilimia 120. Hii ni kazi nzuri na wameweza kusimamia vizuri na kwa mabadiliko haya ya sheria ambazo tumezipitisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie Mkao wa Lindi. Katika Mkao wa Lindi tumbahatika kuwa na madini mbalimbali. Tunayo *ruby*, *sapphire*, *graphite*, *gypsum*, chokaa, chumvi na dhababu lakini niseme Serikali bado haijafanya maamuzi ya kuweka mazingira wezeshi ya kusimamia rasilimali hizi za madini ambazo zipo katika Mkao wa Lindi ili ziweze kunufaisha Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali wameweza kutoa leseni kwa wawekezaji hawa wa *graphite* ambao wako Ruangwa. Tunategemea sasa waanze mara moja uchimbaji huu wa madini ili wananchi wa Ruangwa waweze kupata ajira lakini uchumi wetu pia uweze kukua katika Mkao wetu wa Lindi na hatimaye Serikali yetu iweze kupata mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunayo *gypsum* ambayo ipo Kilwa katika eneo la Kiranjeranje, Hoteli Tatu na maeneo mengine. Hii *gypsum* ina ubora wa kidunia, ni suala la kujivunia kwamba tuna rasilimali ambayo ipo katika soko la dunia lakini bado Serikali haijatilia mkazo katika usimamizi wake na kuweka mazingira wezeshi kuifanya Serikali yetu

iweze kupata mapato. Sasa hivi kuna uchimbaji tu ambao upo kiholela, kwa hiyo, tunapoteza mapato mengi sana kupertia madini haya ya *gypsum*. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali kusimamia uwekezaji huu wa *gypsum* ili Serikali iweze kupata mapato lakini pia wananchi wa Mkoa wa Lindi tuweze na sisi kukuza uchumi wetu kupertia hii *gypsum*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna wazalishaji wengi wa chumvi nichini Tanzania lakini na kwetu Lindi tuna wazalishaji hao wa chumvi lakini tuna changamoto mbalimbali katika eneo hili la chumvi. Wadau hao wa chumvi mara nydingi wamekuja kuleta kilio chao kwa Serikali lakini bado hatujapata nafasi ya kuwasaidia. Naiomba sana Serikali kuwatazama kwa macho mawili ili wazalishaji wa chumvi nao waingie katika ushindani wa soko na tuweze kuwa na viwanda vyta chumvi katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa chumvi kuna tozo mbalimbali. Ziko tozo ambazo zinatozwa kupertia halmashauri kati ya asilimia 5 - 10 lakini bado utakuta wanunuzi wa chumvi wanaposafirisha njiani tena wanakumbana na tozo zingine mbalimbali. Pia kuna ushuru wa mikoko ambao unatozwa na Wizara hii ya Maliasili na Utalii lakini cha kusikitisha tozo hii inatozwa eneo lote la mikoko. Kwa hiyo, mimi naishauri Serikali tozo hii wangeelekeza katika eneo lile ambalo linazalisha chumvi kuliko kutoza katika eneo zima la mikoko. Tozo hii inatozwa katika kila ekari mbili na nusu Sh.130,000, kwa hiyo bado tunaona wazalishaji wa chumvi wana mzigo mkubwa ukiangalia mlolongo wote wa tozo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna tozo ya kuandikisha mashamba na inatozwa kila mwaka Sh.320,000 na kuna leseni wanalipia kila mwaka. Kwa hiyo, tunaona mzigo ambao upo kwa wazalishaji wa chumvi na kusababisha chumvi yetu ya Tanzania kuuzwa bei ya juu kuliko chumvi ile ambayo inaingizwa kutoka nje ya nchi. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali kuangalia baadhi ya tozo hizi ambazo zinaleta kero kwa wazalishaji wa chumvi na kufanya chumvi iwe bei ya juu basi tuweze kufanya mabadiliko ya sheria ili

tuweze kuwasaidia wenzetu wazalishaji wa chumvi na tuweze kuwa na viwanda vyta chumvi katika nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao wachimbaji wa madini wanawake. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, siyo kwa kuwa yeye ni mwanamke tu lakini kuwatazama hawa wachimbaji wa madini wanawake ili Serikali sasa iwave mafunzo na iwawezeshe kwa kuwapa vitendea kazi na wao waweze kuingia katika fursa hii ambayo ipo ya madini na kupata leseni za kuwaruhusu kuingia katika uchimbaji huu wa madini. Kwa hiyo, hili ni suala muhimu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine tunalo hili Shirika letu la *STAMICO*, hili shirika bado halina miguu. Naiomba Serikali kulisaidia shirika hilli kama ambavyo tumeweza kuwasaidia *ATC*, Kampuni ya Simu, *TANESCO*, basi na hawa *STAMICO* tuone umuhimu wa kuwasaidia ili na wao waweze kupata miguu wasonge mbele. Wanayo mipango na mikakati mizuri lakini wanashindwa kutekeleza kwa sababu tu ya kukosa fedha. Kwa hiyo, hilo ni suala muhimu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Spika wetu kwa kuteua Kamati Maalum iliyoenda kusimamia masuala mazima ya madini. Kwa kweli wamefanya kazi nzuri na tumeona mazao ya kazi ile. Bahati njema tumpata faida katika Kamati ile tumpata Mawaziri. Kwa hiyo, tuna imani kabisa na wao, nasi tunawaunga mkono katika shughuli zao mbalimbali katika kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, naiomba Wizara izingatie maoni na ushauri wa Kamati ya Madini. Tumeshauri mambo mengi sana na kwa bahati njema baadhi ya mambo wameyafanyia kazi, tumeyaona katika kitabu chao. Niwatakie kila la kheri katika bajeti hii, Serikali iweze kutoa fedha kwa sababu Wizara ni

mpya inataka kujipanga vizuri katika kuhakikisha inasimamia rasilimali za nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Jitu Soni na Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi ajiandae.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa kufanya kazi kubwa na kuleta mabadiliko makubwa katika sekta hii ya madini. Pia kwa kuona Wizara hii inastahili kuwa peke yake na Wizara ya Nishati kuwa peke yake ambapo kwa Wizara zote mbili tutapata manufaa makubwa na ufanisi mkubwa wa kazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru Waziri, Naibu Mawaziri wote wawili pamoja na timu yao nzima kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya kuhakikisha kwamba sekta hii sasa inasimama vizuri na nchi yetu iweze kunufaika na rasilimali hii ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia. Naweza kusema kwamba kila aina ya madini yaliyopo duniani na Tanzania yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu la kwanza na siku zote huwa nasema hapa, kwenye bajeti hii nimeona pale mmeandika kwamba Oktoba mtaanza mafunzo katika Kituo cha *TGC* pale Arusha, kituo ambacho kitakuwa kinafundisha Watanzania jinsi ya kuchonga vito lakini pia na kupata mafunzo mbalimbali ya madini yaani vito pamoja na usonara lakini vifaa vinavyotakiwa pale bado havijatosheleza. Badala ya mashine 45 ambazo wanazo mngeongeza mashine zifike 100 na gharama yake siyo kubwa sana. Hii programu ya *Diploma* ni ya miaka mitatu (3) lakini bado mnawenza kuwa na *certificate* ambapo inafanyika *International College Gemstones* - Marekani, Bangkok na maeneo mengine ni miezi sita. Mtanzania ambaye hajui kusoma na kuandika kwa

sababu kuchonga vito ni *art* yaani ile ni sanaa, kwa hiyo, mngeweze kufundisha watu 100 kwa kila miezi sita kwa muda wa miaka miwili (2) mtakuwa na watu 400 na hata mkipata asilimia 20 tu ambao watakuwa wazuri pale tayari madini mengi ya Tanzania tutaweza kusanifu hapa nchini na tutaweza kuongeza thamani na pia ajira itaongezeka kwa wingi sana. Kwa sababu tuna madini kwenye vito aina ya *precious* na *semi-precious*, zote hizo zitapata thamani na biashara hiyo itakuwa nzuri. Kwa hiyo, tunaomba kwenye bajeti hii mhakikishe kwamba mmeweka fedha ya kutosha ya kuwezesha kituo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, siku za nyuma tulishafanya mabadiliko kwenye hizi leseni kubwa za *Prospecting License (PL)* ilikuwa unaruhusiwa kuwa na leseni nyingine za madini ya ujenzi lakini imefika mahali ukienda unanyimwa kuchukua leseni hizo za madini, kwa mfano, ya mawe kwa ajili ya *moram* au kwa ajili ya mchanga. Mtu akishachukua *square kilometer* 100, 200, 300 huko ndani nyie wengine wote sasa mnafanya kazi kienyeji, hamruhusiwi kupata hizo leseni. Nina uhakika kwamba hapa Bungeni tulipitisha sheria, tunashindwa kuamini kwa nini hiyo sheria haitekelezwi na huko chini kwa mfano kwenye Ofisi za Kanda wanashindwa kutupa leseni hizo za madini ya ujenzi ili watu katika Halmashauri zetu na maeneo mbalimbali waweweze kuwa na fursa na haki ya kutumia hayo madini bila kubughudhiwa na huyo mwenye leseni kubwa ya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kama alivyozungumza mwenzangu ni vizuri pia tukayaangalia haya madini aina ya chumvi, kwa sababu huyu mwenye leseni ya madini ya chumvi anatozwa sawa kabisa na yule wa dhahabu au wa madini mengine ambayo yana thamani kubwa. Kilo ya chumvi na kilo ya dhahabu ni vitu viwili tofauti, sasa kwa nini leseni zao zifanane? Kwa hiyo, mngeangalia hii leseni ya chumvi mngeawaondolea kabisa au mngeweka ada ndogo tu ili chumvi yetu ambayo tunazalisha Tanzania iweze kuzalishwa kwa wingi na tushindane kwenye soko la Afrika Mashariki na Kati. Kwa hiyo, hilo naamini kabisa Wizara mtalichukulia maanani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, naomba Wizara pamoja na Wizara ya Fedha zifanye kazi kama Serikali kwa kusaidiana . Leo hii Arusha au Tanzania tungekuwa *center of gemstones* kwa Afrika. Jambo hili limeshindikana kwa sababu ya mifumo yetu ya kikodi kwa sababu mtu akitoka na madini katika nchi hizi ambazo zinatuzunguka kuja kuza Tanzania anabanwa sana mipakani au kwenye viwanja vya ndege na anashindwa kuingiza mzigo wake. Vilevile kama akiingiza na hajaweza kuza siku akitaka kuondoka na mzigo bado inakuwa ni kero na tatizo pale mipakani kutokana na mifumo yetu ya kikodi. Sasa ni vizuri tungeangalia mfumo huo ili watu wote wawe na urahisi wa kuingiza madini yao na wakitaka kuondoka na madini ambayo hawajauza waweze kuondoka nayo kiurahisi ili *centerile* ya Afrika ambapo ilikuwa ni Arusha wanafanya *show* kila mwaka iweze kukua na Tanzania iwe kama Bangkok na Brussels ili nasi kwa Afrika ndiyo tuwe kituo kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuangalie kwenye mfumo wa kodi. Leo hii tunalalamika kwa nini tanzanite au madini yetu ni mengi lakini yanauzwa kwa bei nafuu nje ya nchi. Leo hii ukitaka kuza tanzanite nje ya nchi, *uki-export officially*, kihalali kabisa unalipa asilimia 5 tu ya *royalty*. Ukipeleka tu Kenya hapo asilimia 5 halafu ukitaka kuza hiyo tanzanite iliyochongwa hapa nchini unatozwa asilimia 18 ya *VAT*, ina maana tanzanite itakuwa rahisi Kenya badala ya hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo kwenye dhahabu, bei ya dhahabu sisi hatupangi inapangwa kwenye *World Market Stock Exchange, metalszote*. Unakuta dhahabu yetu ukitaka kuza hapa ni *plus 18 percent locally, 18 percent* kwenye *VAT* una-calculate pamoja na faida na gharama zote, ukipiga hesabu ni zaidi ya asilimia 25 mpaka 30. Sasa unakuta bei ya dhahabu hapa nchini *locally* itakuwa bei ya soko la dunia *plus 25 percent*. Ukienda Dubai ni asilimia 5 tu juu ya ile bei ya soko la dunia, ina maana watu wengi kwa sababu dhahabu hainunuliwi na watu wa kawaida, ni *middle* na *upper class*. Kwa hiyo, mtu anayenunua vitu vya Sh.10,000,000 ukiongeza asilimia 25 ni Sh.12,500,000, hiyo

Sh.2,500,000 inatosha kununua tiketi ya ndege kwenda Dubai, kulala *five star*, kufanya *shopping* na kurudi na unakuwa hujaingia gharama, ndio maana hapa biashara hiyo haikui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya dhahabu Tanzania inayochimbwa na wachimbaji wadogo ni kubwa kuliko ile ya migodi mikubwa. Sasa mgeweka tu *royalty* kama Dubai ilivyoweka asilimia 5, siyo lazima iwe asilimia 5, mnaweza kuweka asilimia 7/8 ili biashara ifanane. Ungekuta biashara halali ingefanyika hapa nchini na watu wengi sana wangkuwa wanunu na Serikali ingepata mapato ya kutosha na huu usonara na nini ungeweza kukua kwa sehemu kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi pia tumebadilisha ile sheria kwamba haturuhusiwi kuuza madini ambayo hayajawa *processed*. Naomba Wizara itoe *definition* ya uhakika kabisa ya maana ya *raw mineral* kwa sababu *raw mineral* haijulikani, ina maana itafika mahali tutashindwa kutuma nje ya nchi madini ya aina yoyote au *metal* yoyote ambayo haijawa *processed*. Sasa ile *definition* mngeiweka vizuri kwa sababu hata kwenye dhahabu ya kawaida kama ni *carat* 24 ni ngumu, unakuta inakuwa na madini mengine ambayo yapo kidogo humo ndani. Sasa utakuta hiyo ni *raw* tutaanza kuingia kwenye mgogoro mwingine. Ni vizuri *definition* zote zikakaa vizuri ili suala hili sasa liweze kusaidia nchi yetu. Muhimu ni kwamba Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Fedha na Wizara ya Madini zikae kwa pamoja waangalie Tanzania inawezaje kuwa *centerya* Afrika kwenye suala hili la vito na pia kwenye *jewellery* na madini yote tunayo hapa *gold*, *silver* pamoja na fedha yote yanapatikana hapa nchini ili Watanzania waweze kunufaika na nchi iweze kupata kodi na mapato mengine kutokana na madini hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa hawa wachimbaji na wafanyabiashara wadogo zile gharama za leseni na ada wanazotozwa mngeangalia iwe ni *fixed rate* ili hata kwa mfano sonara anapoambiwa kwamba biashara hiyo wakitaka kufanya ni lazima wakate leseni ya dola 2,000,

lazima awe na *gemstone dealers license au gold dealers license* ndiyo maana watu wanaingia kufanya biashara ya magendo. Mngeweka vitu kwa bei nafuu na isiyo na urasimu kila mtu angekuwa anafanya biashara halali na Serikali ingekuwa inapata mapato kama nchi nyine zinavyofanya. Nchi ambayo haina hata madini ya aina moja inanufaika kuliko Tanzania ambayo tuna madini ya kila aina lakini niwapongeze Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambapo watu wanaendelea kugundua tatizo kubwa ambalo lipo na wenzangu wamelisemea ni mfano wewe unamiliki eneo lako, kwa mfano, Halmashauri yetu tuna watu ambao wana *primary license* hatujawahi kuwaona, hatujui wanalipa nini na wanalipia wapi, sisi hatupati hayo mapato na siku wakitaka kuanza kufanya kazi tayari wanaingia mgogoro na wanakijiji. Kwa mfano, Halmashauri ya Babati tulipotaka *crusher* ya mawe tulinyimwa kutokana na sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Yahaya Massare atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Bilakwate.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami nichangie Wizara hii ambayo kama itasimamiwa vizuri inaweza kuwa mhimili mmojawapo ambao utachangia katika uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi za dhati sana kwa Mheshimiwa Rais kwa kuona kwamba Wizara hii sasa iwe Wizara Kamili na kama ilivyoundwa na Naibu Mawaziri wawili kaipa thamani kubwa. Niwaombe viongozi walioteuliwa katika nafasi hii, Waziri na Naibu Mawaziri waione thamani ya Wizara hii na waitendee haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na jambo moja ambalo hatulioni sana. Wabunge wenzangu wamezungumza mambo mengi lakini na Wizara wenyeve katika kitabu chao wamejielekeza katika mambo mengi na Kamati pia. Wizara hii inaweza ikafanya kitu kimoja ambacho mimi nakiona ni bora sana. Tumekuwa tunakwenda nchi kama Dubai tunaona uhuria uliopo wa biashara lakini Singapore na maeneo mengine ambayo wamekuwa katika uhuria wa biashara kwa maana ya kwamba unaweza kwenda na mzigo wako pale lakini usiulizwe ili mradi tu unalipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nishauri Wizara hii waanzishe soko huria la dhahabu kwa maana wananchi wa ukanda huu wa nchi 10, 13 za nchi hizi za Afrika Mashariki na Kati zina dhahabu nyingi sana na wananchi wanatafuta mahali pa kuuza dhahabu lakini hawana. Matokeo yake sasa watu wamekuwa wanapitisha dhahabu kinyemela na kwenda kuuza Kenya kwa sababu ya ile fursa iliyopo ya kuuza dhahabu Kenya kuliko ukionekana na dhahabu Tanzania. Nashauri Wizara ije na mkakati ambao utakuwa na soko ambapo Tanzania itakuwa sehemu ambayo itapelekea watu wa nchi jirani kuleta dhahabu yao hapa na kufanya wananchi wa nchi mbalimbali za huko waje wanunue lakini pia itaongeza kwa upande mwingine suala la utalii. Kwa hiyo, itachochea biashara na utalii pia katika eneo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo taarifa mbalimbali katika Wizara ya Madini zikiwepo zile *quarter degree sheet* ambazo zipo zenye taarifa za madini, zile zina taarifa za muda mrefu sana. Naomba Wizara hii kwa kuwa sasa imekuwa Wizara kamili wajikite kuboresha taarifa ili tuwe na *latest* kiasi kwamba mtu ukichukua ile taarifa ya pale uweze kuiuza kwenye maeneo mengine na kufanya wawekezaji waje. Sisi tunakosa wawekezaji mpaka mtu awe na shimo, anatoa dhahabu au aina nyingine ya madini, hatuna taarifa kama zilizofanywa na *geo-survey* wakati ule na zilizofanywa na taasisi zingine. Tumefika mahali tumesahau kabisa kazi

ya kuhuisha taarifa za maeneo ambayo madini yapo katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na masuala ambayo yalikuwepo hapo nyuma, nashukuru sana sasa hivi Serikali imeliona kwamba *gemstone* ni madini ambayo yanatakiwa yachimbwe na wazalendo tu kwa maana wananchi wa Tanzania. Suala hili lilikuwa linaleta kero kubwa hasa tanzanite pale walipoingia ubia na hawa watu wa Afrika Kusini. Hii ilituletea shida kwa sababu ni mionganini mwa rasilimali chache sana ambazo tunazo nchi ya Tanzania na zinapatikana Tanzania lakini nchi za India, Afrika Kusini na Kenya ndiyo walikuwa wanaongoza kuuza tanzanite katika masoko ya dunia. Kwa mpango huu ambao umefanywa na Serikali na hili pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake mkubwa na wa makusudi kabisa kujenga ukuta pale, kwa maana hiyo sasa kama nchi tutanufaika na rasilimali hii ambayo ipo hapa Tanzania pekee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo nataka niombe Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake walione, suala la masoko ya madini haya. Ni vizuri basi kama Serikali ikatangaza madini ambayo yapo katika maeneo yetu, hata hizo tanzanite na rubi na madini ambayo yalisemwa na viongozi mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge masoko yake ni mpaka mtu tu *a-penetrated* mwenyewe kwenda kutafutia soko. Hatuna *latest* taarifa kama nilivyosema kwenye maeneo haya lakini pia ni kwa kiwango gani wazalishaji wetu wa migodi midogo wanatambuliwa na kujengewa uwezo wa kuuza katika soko la dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo, naunga mkono hoja na nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri. Tunaendelea Mheshimiwa Innocent Sebba na Mheshimiwa Bobali ajiandae.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia Wizara hii muhimu. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupa uhai ili kuendelea kuwatumikia wananchi wetu. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo ameendelea kuifanya kuhakikisha haya madini yanawanufaisha Watanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri. Hatua ambazo Mheshimiwa Rais anazichukua kwa huyu Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa uadilifu wenu tunaamini mtasimamia sekta hii muhimu ili iweze kuwanufaisha Watanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niongelee Wilaya yangu ya Kyerwa. Wilaya ya Kyerwa tuna madini ya *tin*, madini haya ni muhimu. Naamini Serikali ikiona na ikayasimamia yanaweza kuliingizia Taifa hili kipato kikubwa pia tunaweza tukatengeneza mabati. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo napenda kulizungumzia mwaka 2016, Mheshimiwa Waziri Profesa Muhongo alifika pale na akajionea mazingira yalivyo. Maeneo yale bado utafiti haujafanyika kuweza kubainisha yale maeneo ambayo yana madini ya batii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Wizara hii imechukua muda mrefu, tangu 2016 walikuja wataalam mara moja na hawajarudi tena. Nimwombe Mheshimiwa Waziri atueleze hatua hizi zitachukuliwa lini ili tuweze kujua ni kiasi gani cha madini tuliyonayo kwa sababu mpaka sasa hivi uchimbaji unaoendelea, wachimbaji wadogo wadogo wanachimba lakini sehemu kubwa ya madini yetu Mheshimiwa Waziri naamini anajua hatuyafaidi bali yanawafaisha majirani zetu. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri pawepo na mkakati na hatua za haraka ili kuweza kunusuru haya madini ambayo ni ya muhimu yasiende kuwanufaisha majirani zetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wachimbaji wadogo wadogo, naishukuru Serikali angalau imeweza kuwatengea maeneo lakini siyo wote, bado wanapata usumbufu sana wanapofanya utafiti wao wakapata sehemu ambayo ina madini wanakuja hawa watu ambao ni wakubwa wanasema haya maeneo ni yetu. Hivyo, wanataabika, bado hawajatengewa maeneo ambayo yataweza kuwasaidia. Niwaombe Serikali, Mheshimiwa Kairuki naamini wewe pamoja na wasaidizi wako ni wasikivu, mtakapokuja kupima yale maeneo ili kujua ambayo yana madini muweze kuwatengea wachimbaji wadogo wadogo ili wawe na uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kuna wawekezaji ambao walifika pale wamekuja kujenga viwanda vyta uchenjuaji. Kuna mmoja ambaye alikuwa hajafuata taratibu Serikali imemsimamisha ili aweze kufuata utaratibu. Niiombe Serikali huyu mwekezaji anapokuja na ninyi muweze kumsaidia haraka ili hawa wachimbaji wetu waweze kupata uhakika wa kuchenjua hayo madini wanayochimba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wale wachimbaji wanapochimba hawana uhakika wa soko, wale ambao wana leseni ya maeneo yale ndiyo wanaochukua yale madini. Wanachukua kwa pesa ni ndogo kwa hiyo wachimbaji wadogo hawapati pesa ambayo inalingana na thamani ya yale madini. Kwa hiyo, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri tuwe na uhakika wa soko na haya madini yatambuliwe. Majirani zetu ndiyo wanayatumia sana lakini sehemu kubwa inatoka kwetu. Tuweke mkakati ambao utaweza kuyatambua haya madini na ikiwezekana tuyatangaze. Bado tunaweza kufungua viwanda ambavyo vinaweza kukusanya madini haya na yakutunufaisha Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nataka kujua hii *STAMICO* ndiyo iliyokuwepo kipindi kile madini haya yanaabiwa na kupotea hovyo. Je, *STAMICO* hii ambayo mnaendelea nayo na naona mnatenga hela kwa ajili ya kuiendeleza, ni

STAMICO mpya au ni ile ya zamani? Inawezekana hawa watendaji bado ni walewale. Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri lazima achukue hatua, kama tunataka kubadilika lazima tubadilishe mfumo wote vinginevyo huku juu mtachukua hatua lakini bado wale wale wanaendelea kufanya uharibifu uliokuwepo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, Mwenyezi Mungu ametujaalia madini mengi sana na ninaamini tukiyasimamia tunaweza kuliingizia Taifa kipato kikubwa sana. Kwa hiyo, niombe sana, hawa wanaosema sijui haya madini yana mapepo, majini na vitu vingine, mimi naamini hilo halipo. Hatuhitaji kwenda kwa waganga, hii rasilimali tumepewa na Mwenyezi Mungu tuisimamie, tuwapate watu ambao ni wazuri kwa msaada wa Mungu aliyetupa rasilimali hizi zitawenza kunufaisha Taifa letu. Ashukuriwe Mungu ametupatia Mheshimiwa John Pombe Magufuli ambaye ameanza kusimama vizuri na ametupa Mawaziri wazuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi niwatakie kila la kheri Waheshimiwa Mawaziri, Watendaji Wakuu wote wa Wizara lakini hii ni vita lazima tupambane kuhakikisha madini haya yanawanufaisha Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Bobali atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza niendelee na kumuombea Kaka na ndugu yangu na Mbunge mwenzetu ambaye leo ameingia kaburini, Mheshimiwa Bilago, Mwenyezi Mungu ampokee na amlaze mahali pema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri na Naibu Mawaziri wote watatu bado ni wapya na huu ni mwaka wao wa

kwanza, kwa hiyo, leo sitakuwa na malalamiko mengi ya kuwashutumu na kuwalaumu, nataka niwashauri. *Personality* zao nawafahamu namna walivyo na namna wanavyoweza kukimbia kwa sababu bado ni vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la leseni za uchimbaji wa madini na utaratibu wa namna zinavyotolewa. Mwaka jana na mwaka juzi nililalamika kwamba kuna watu wamechukua leseni wakisema kwamba wanakwenda kuchimba au kuchukua *gypsum* kwenye eneo la Jimbo la Mchinga hasa katika Kijiji cha Mchinga. Watu hawa leseni wanazo kutoka Wizarani lakini Serikali ya Kijiji, Kata na Halmashauri hazijui. Zipo leseni 15 ambazo zimechukuliwa kwa ajili ya uchimbaji wa madini ya *gypsum* katika eneo la Mchinga lakini Serikali ya Kijiji na Halmashauri hazijui. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua utaratibu ukoje, wakati ule Kamishna wa Kanda wa Madini alikuwa Ndugu yangu Benjamin Mchwampaka na baadaye akaletwa hapa akaja kuwa Kamishna Mkuu na sasa sijui yuko wapi, nilimwambia na suala hili akawa analijua na bahati alinipa ushirikiano wa kunipatia na *addresses* za wale wahusika na ni kweli kabisa alikiri kwamba hao watu wana leseni na wamechukulia leseni pale eneo la Mchinga. Nataka kujua sasa, utaratibu gani unatumika wa mtu akaenda kwenye eneo 'A' akaomba leseni akapewa, wakati wahusika wa pale hawajui? Kwa hiyo, hii ni changamoto kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni suala la *mineral cutter*. Hapa katika viwanja vya Bunge kuna watu ambao wanatuonesha namna tasnia ya madini inavyofanya kazi, tumekwenda kutembelea pale, jana mimi nimetembelea. Wale wanaohusika na suala la ukataji wa madini, nimekwenda kuangalia ile *mineral cutter* yenye we kwa saa moja sijui ni gramu ngapi, ni kitu kidogo kabisa ambacho kinakatwa kwa kutumia saa moja na wakatuambia nchi yetu hazifiki hata mashine 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi nimemsikia mchangiaji mmoja na mimi naunga mkono, hivi kwa nini Wizara isifikirie kununua mashine nyingi za kukata madini ili utaratibu wa ukataji wa madini ukawa unaharakishwa? Nimesikia kwamba kuna watu wanasisimama foleni muda mrefu wakisubiri madini yao yawe yanakatwa kabla ya kusafirishwa nje ya nchi, lakini mjue kwamba madini ni fedha, tena fedha kwelikweli siyo ya masihara, madini ni fedha. Kama mtu anakaa na mzigo wa madini wa nusu kilo au kilo moja akisubiri kukata, hivi mtu huyo anashindwa kwenda kufanya mipango huko mipakani akavuka akaondoka nayo? Badala ya kuwa tunafikiria kwamba Serikali itakuwa inapata fedha kumbe tutakuwa tunapoteza mapato ya Serikali. Kwa hiyo, kama kuna jambo la makusudi mnapaswa kulifanya ni kuhakikisha kwamba hizi mashine za kukatia madini zinakuwa nyingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tuwa-*train* watu wetu. Sekta ya madini ni muhimu kweli, ingeweza hata kuendesha nchi hii peke yake. Kama tutaweza kuweka udhibiti mzuri kwenye madini tunaweza kwenda Tanzania kwa kutegemea sekta ya madini. Chuo cha Madini mkitengene fedha za kutosha tu-*train* watu, tufanye kama ilivyo kwenye kilimo, kuna ma-*Extension Officer* mpaka kwenye Kata, ninyi mngeanzia hata kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Halmashauri kama za kwetu kule Lindi, Ruangwa, ukitaka huduma ya madini unakwenda Kanda. Hivi kwa nini kwenye *level*/ya Halmashauri hakuna watu wenu? Changamoto iliyopo ni kwamba huko kwenye Halmashauri, sifirkii kwamba hakuna Halmashauri ambayo siyo wadau wa madini, mchanga upo huko, kuna *gypsum* na kuna madini mengine ambayo yanapatikana katika maeneo hayo, kwa nini sasa Wizara isi-*train* watu wa kutosha, tutumie chuo chetu wenywewe, mkawa mmeajiri Maafisa Madini kwenye ngazi za Halmashauri, wangekuwa wanatusaidia sana kufanya hizi kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda nyumba zinazojengwa nchi hii Halmashauri zinakusanya mapato

kwenye mchanga lakini Wizara sijui kama mmepata shilingi ngapi kwenye madini ya mchanga. Hapa nimesoma kitabu cha Kamati wanasema mpaka Machi mmepata asilimia 3 za maendeleo, lakini fedha zipo kama mngeweza kuwa na watu kuanzia kwenye ngazi zile za Halmashauri naamini mapato yangetuwa yanakusanya na mngekuwa mnaweza kujidesha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni suala la *STAMICO*, limezungumzwa hapa kwamba *STAMICO* inaitia hasara nchi hii na ni kweli kabisa. Nikifikiria taarifa ambayo ilitolewa na Mwenyekiti wa Kamati Maalum iliyokuwa imeundwa na Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Doto ambaye sasa hivi ni Naibu Waziri wa Wizara hiyo, ilionekana *STAMICO* haina tija kwa Taifa. Nashangaa Waziri, nilitegemea leo angekuja na hatua madhubuti ama kutuambia kwamba analifanya *restructuring* ya Management au mfumo wenyewe anautengeneza upya au anaamua kuiweka pembedi kuja na taasisi nyingine ambayo itakuja kusimamia masuala haya kwa sababu imekuwa ikilaumiwa maeneo mengi. Sasa na lenyewe hili ni jambo la kuliangalia sana kwa sababu kila mtu anayesimama analalamikia *STAMICO*, nadhani kama haina tija ni bora kuachana nayo kuona namna nyingine ya kufanya. Huu ni ushauri wangu mwininge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, mimi binafsi nimetoka maeneo ya Lindi na Mchinga kule, tuna madini ya chumvi. Sasa hivi kumekuwa na utaratibu wa chumvi kuongezewa madini joto na wale wakulima wa chumvi wanalamika sana kwamba upatikanaji wenyewe wa hayo madini joto ni changamoto, lakini siyo upatikanaji tu, wanachokilalamikia kingine pia ni gharama. Sasa nataka kujua, hawa wakulima wa chumvi ni wadogo kama walivyo wachimbaji wadogo wadogo, mna utaratibu gani wa kuwasaidia? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeelezwa kwamba mkulima wa chumvi aliyeko Mchinga anayelima katika lile eneo la Namdima analazimika naye pia aende Mtwara akapate hayo madini joto kwa Kamishna wa Madini wa

Kanda. Kuna utaratibu gani wa kuweza kusaidia? Kama nilivyosema kwamba watu wa Madini kwa nini wasikae kwenye Halmashauri, kwa nini msi-*decentralise* haya mambo ya madini yakawa yanashughulikiwa kwenye ngazi za Halmashauri au walau ngazi ya Mkoa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kumalizia, Wilaya ya Lindi pamoja na Wilaya ya Kilwa tuna *deposit* nyingi sana ya *gypsum*. Naomba sana muandae utaratibu kwa sababu wale watu wanaosomba madini ya *gypsum* wanatumia barabara hizi ambazo zinatengenezwa na *TARURA*, baada ya miezi mitatu au sita *TARURA* wanatumia pesa kuzitengeneza baadaye wao wanatumia magari makubwa wanapita mule wanaharibu zile barabara. Kuna utaratibu gani wa kufanya *compensation*? Kwa sababu kwenye Halmashauri tunaamini kwamba hawa wanaochimba madini ya *gypsum* wanapaswa walipe fidia ya barabara kwa sababu wanaziharibu na magari wanayotumia ni makubwa, kinyume na utaratibu na uwezo wa zile barabara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana mtoe maelezo magari yote makubwa ambayo yanabebea *gypsum*, kwa mfano eneo la kutoka Kilanjelanje pale Kilwa kuingia kule ndani kuna magari mengi makubwa ya tani 18, 30 yanabebea *gypsum* katika barabara hizi za *TARURA* wanatusababishia barabara kuharibika ndani ya muda mfupi sana. Kwa hiyo, tunaomba Waheshimiwa Mawaziri kama kuna chochote ambacho wanapaswa wakitoe kama fidia mtueleze ili nasi tuendelee kuwadai. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, nawatakia kila la kheri Mawaziri watatu wa Wizara hii. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Bobali. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu na Mheshimiwa Janet Mbene ajiandae.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adimu ya kuweza kuchangia sekta hii ambayo inaonekana ina manufaa makubwa kama tutachukua hatua zinazotakiwa. Nianze kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, kama Waheshimiwa Wabunge waliotangulia walivyosema, amesimamia na kama hatua anazozitaka zikichukuliwa madini yataliletea Taifa hili manufaa makubwa kuliko ilivyo sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri ninayemfahamu sana, pengine namfahamu kuliko watu wengi, alikuwa Msaidizi wangu na nafurahi kuona kwamba anapaa juu na Mungu ampe kila analolihitaji ili afanye kazi yake vizuri. Napenda kuwapongeza Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza kumshukuru Rais kwa sababu kama hatutachukua hatua madhubuti, kwa kweli hatutaenda mbali. Nasema hivyo kwa sababu ukiangalia *statistics* zinaonesha kwamba mifugo, kilimo na sekta nyingine zinachangia Pato la Taifa zaidi kuliko madini. Ilivyo sasa hivi, sekta ya madini inachangia kiasi cha asilimia 4 kwenye Pato la Taifa, ni ndogo sana. *Projection* inaonesha mwaka 2025 itachangia asilimia 10, naamini hatua hizi ambazo anazitaka Rais zikichukuliwa tutachangia zaidi hata kuliko asilimia 10 hii ambayo iko *projected*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kuongelea suala la wachimbaji wadogo. Wachimbaji hawa ndiyo kwa kweli wanao-*discover* au ndiyo wanaogundua madini ambayo yapo nchi hii, tunapaswa kuwathamini na kuwatambua. Ilivyo sasa wapo kwenye vikundi lakini *bureaucracy* inawacheleweshea hata kupata leseni. Naomba sana wapate leseni ili waweze kuijendeleza na wawe wenye fedha nyingi kuliko wengine, kuliko hao wanaotoka nje kwa sababu wanaotoka nje watapeleka mali nje bila manufaa kwa nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile Serikali, Mheshimiwa Angellah, angalia sera, kwa nini watu wanakimbiza tanzanite Nairobi, kwa nini wasitake kuuzia Manyara na Arusha, kwa nini? Lazima kwa upande wetu tukiangalia, kama Kenya inataka kuchukua tanzanite yetu hawataweka VAT na sisi tunaweka VAT. Sasa tunafanya nini, tuna mkakati gani wa kuona kwamba madini ya Tanzania hayakimbizwi nje na ni athari kubwa sana yakikimbizwa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimepita kule kwenye maonesho na naomba Waheshimiwa Wabunge wote mkaangalie, inaonyesha kwamba ukipeleka dhahabu bila ya kuchenjua unaweza ukawa unapeleka madini mengine yenye thamani kubwa kuliko dhahabu yenye. Kwa sababu nilipopita kwenye *stall* moja kule nje wanaochimba dhahabu walionesha kwamba katika machimbo yao wamepata dhahabu, wamepata *vanadium*. *Vanadium* ni madini yenye thamani kubwa kuliko dhahabu lakini yanakwenda kuuzwa kama dhahabu. Kwa hiyo, naomba sana tukazanie hili la kuongeza thamani na kuchenjua madini ndani ya nchi ili yale yenye thamani kubwa yatakapoonekana na watu wa madini au wale wataalam waweze kutusaidia kuona kwamba kwenye migodi ile kama ni dhahabu tu au kuna madini mengine ili Tanzania isipoteze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu mwingine wa madini haya kuchenjuliwa hapa ni nini? Ajira ya vijana inakwenda nje. Ukienda India ajira nyingi za Wahindi kama Jaipur inatokana na tanzanite. Ingekuwa imebaki pale Mererani wananchi wa Manyara, Arusha na Watanzania kwa ujumla wengi wangeajiriwa pale badala yake tunawapa ajira Wahindi. Naomba tuangalie sana hizi sera ambazo zinaweza zikawa zinachangia madini yakimbizwe nje badala ya wawekezaji kuja kuchenjua madini haya na kuongeza thamani na kupata vitu mbalimbali kama pete, mikufu na mengine ambayo tunayaafahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hanang au Manyara, sehemu kubwa iko chini ya *Rift Valley* na wanasema kwamba kule kwenye *Rift Valley* hakuna madini lakini tuna maeneo

machache ambayo yako juu na kule kuna madini. Ukienda Hanang eneo linaloitwa Basotu kumekuwa na madini ambayo yana thamani kubwa na wako watafiti wanaoendelea kufanya kazi kule. Naomba watafiti wasisumbuliwe badala yake wapewe *incentive* waweze kufanya utafiti unaotakiwa na baadaye tujue Hanang ina nini nasi tuungane na *Lake Victoria* ambako wanatoa dhahabu kwa sababu inawezekana mwamba ule umetoka kule ukafikia mpaka kwetu au ultoka kwetu kwenda kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kutoa shukrani zangu za dhati, naomba wawekezaji kutoka nje waone kwamba Tanzania siyo shamba la bibi, Tanzania ni nchi ambayo inastahili kupata manufaa ya rasilimali zake na tuna bahati Watanzania tuna rasilimali nydingi za madini, ardhi, mifugo au mambo mengine Mwenyezi Mungu ametupendelea lakini sisi wenyewe hatujipendi. Naomba tujipende ili tulinde rasilimali hizi kama Mheshimiwa Rais wetu anavyotunesha na Mungu ampe maisha marefu na afya njema ili haya ambayo Mwenyezi Mungu ametupa Watanzania wanufaika nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ambayo sijaitegemea, nawe Mungu akupe afya njema. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Janet Mbene.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii. Villevile nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Madini pamoja na Manaibu wake na Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri sana iliyosheheni maelezo ambayo kwa kweli ni mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kwa kuanza na suala zima la kumshukuru Rais kwa maono yake kuhusiana na rasilimali za Taifa letu. Amechukua uthubutu

wa hali ya juu na amepata vipingamizi vingi lakini mwisho wake tunaona kwa nini alikuwa anaelekea huko. Kwa kweli lengo kubwa ni kuhakikisha kuwarasilimali tulizonazo zinatufaidisha kwanza wenyewe Watanzania kabla ya watu wengine. Hatua zilizochukuliwa kwa kweli tunaziona kuwa zitataboreshea mikataba na utendaji mzima wa sekta hii muhimu ya madini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile nzungumzie suala zima la wachimbaji wadogowadogo. Wachimbaji wadogo kama ambavyo wachangiaji wengi wameeleza ni sehemu kubwa na ya muhimu sana katika sekta hii ya madini, lakini wanafanya kazi katika mazingira magumu sana na kwa kuwezeshwa na Serikali wanawenza wakajikwamua kiuchumi na wakachangia vikubwa zaidi katika Pato la Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi ambayo wachimbaji wadogo wanafanya kazi ni kama ya kubahatisha, ama wawe na leseni au wakiwa hawana lakini bado wanahamahama kwa kubahatisha kuwa labda hapa nitapata. Serikali iwaunganishe na wale wanaofanya *geosurvey* ili wanapopata leseni zile ziwe tayari zimeainisha madini yaliyoko ndani ni kiasi gani ili hata wao wenyewe wanapotia nguvu yao pale wawe na uhakika wa kupata mapato vilevile kuchimba kwa njia ambayo haiharibu mazingira yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hilohilo la wachimbaji wadogo, wengi sana wanatumia nyenzo duni. Natambua sana hatua zilizochukuliwa na Serikali za kuwapa mitaji kwa njia ya ruzuku lakini kama ilivyo haitoshelezi. Wachimbaji wadogo wanaoomba leseni ni wengi na mahitaji yao ni makubwa. Kwa kuititia shirika zao zile mbalimbali, basi Serikali itafute njia ya kuhakikisha kuwa wanawaletea vifaa vinavyofaa, wanawapa mafunzo ya kutosha lakini maeneo wanayotengewa yaye ni maeneo yenye rutuba kwa maana ya madini ya kutosheleza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za nyuma kulikuwa kuna utaratibu wa Benki Kuu kununua dhahabu, ule utaratibu

wenyewe haukuwa mbaya isipokuwa uligubikwa tu na tatizo kidogo mwishoni. Nafikiri ni wakati mzuri sasa wa kuangalia jinsi gani tunaweza tukarudisha mfumo ule. Wachimbaji wadogo wengi sana walikuwa wananaufaika na ule mfumo kwa sababu walikuwa na soko la uhakika la dhahabu yao na ilikuwa inawezekana kupimwa wakajua thamani yake na inawasaidia hata wao wenyewe kwenda kupata mikopo kwa sababu tayari wana dhahabu mkononi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda hilo suala liangaliwe kwa sababu nchi nydingi na benki nydingi za dunia wananaunua dhahabu mpaka sasa hivi. Sasa hivi tunaweza tukaingia ubia na wawekezaji ambao wao kazi yao itakuwa kuthamini hiyo dhahabu, kuihakiki na Benki Kuu inakusanya pesa inayotokana na hiyo dhahabu lakini vilevile kuihifadhi. Hii itakuwa ni njia mojawapo ya kuthaminisha dhahabu yetu na kutuweka katika hali ambayo kama Taifa kuwa na pato la kutosha hata kukopesheka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la makaa ya mawe. Tuna makaa ya mawe mengi sana nchini, tukianzia lleje au Songwe, Ludewa, Ruvuma, Njombe, kote huku tuna machimbo mengi ya makaa ya mawe, inasikitisha kuwa mpaka sasa hivi uendelezwaji wake umekuwa wa kusuasua. Hiki ni chanzo muhimu vilevile kwa masuala ya viwanda na uzalishaji wa nishati ya umeme. Kwa hiyo, napenda sasa hivi tufikie mahali ambapo Serikali inajikita kwa nguvu zaidi katika kuwekeza kuchimba makaa ya mawe ambayo ni muhimu sana tunapoelekea uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua vilevile kuhusiana na *STAMICO*. *STAMICO* imepigiwa kelele sana, imelalamikiwa sana lakini *STAMICO* kama mnavyojua Mashirika ya Umma mengi ambayo yalikuwa yamepewa majukumu ya kuendesha shughuli mbalimbali, ni mojawapo ya mashirika ambayo yamekuwa hayapatii fedha ya kutosha kuendesha shughuli zake. Tutawalaumu bure *STAMICO* hapa wakati kumbe hatuwawezeshi. *STAMICO* ina wataalam wazuri sana, ina miradi ilikuwa mizuri sana, kama walishindwa ni kwa sababu hawajawezeshwa vyta kutosha. Sasa hivi

Serikali ihakikishe kuwa *STAMICO* inapewa fedha ya kutosha, inasimamia vizuri migodi na miradi ambayo iko chini yake ili ilete tija. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nataka kuzungumzia Mkoa wangu wa Songwe, hususani Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira. Kumekuwa na sintofahamu ya muda mrefu sana kuhusiana na Kiwira, mara mwekezaji anakuja, mara wanasema hatoshi, mara inakuwa hivi mara vile. Sasa hivi tunaambiwa tangu Aprili mwaka uliopita *STAMICO* wameanza kufanya majaribio ya kuchimba makaa ya mawe na wameanza kuyauza. Napenda kujua sasa kama hiyo itakuwa ni mwendelezo na mikataba gani imeingiwa katii ya *STAMICO* na Wilaya yangu ya lleje na Mkoa wetu wa Songwe kwa ujumla na nini tutegemee katika suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitoe ombi kwa Wizara, tuna daraja dogo sana pale linalouanganisha Mgodi wa Kiwira na Wilaya ya lleje ambalo lingetoa fursa ya mkaa ule kusafirishwa lakini halifanyi kazi kwa sababu limekatika. Je, Serikali kwa kupitia Wizara hii wanaweza wakahakikisha kuwa wanatengeneza hilo daraja la kilometra 7 tu ambalo litawezesha sasa kuitika na makaa ya mawe yaweze kuita pale badala ya kuzungukia Kyela ambako ni mwendo mrefu zaidi na hasa tukiangalia kuwa mkaa huu unapelekwa Mbeya *Cement* ambako ni rahisi zaidi kupitia upande wetu wa lleje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kujua ubora wa makaa haya. Mara tunaambiwa hayafai, mara tunaambiwa yanafaa, mara tunaambiwa yana ubora zaidi kuliko hata yale ya Afrika Kusini mara tunaambiwa sijui yakoje. Naomba tupate takwimu sahihi kujua kama kweli yana ubora gani na hatua zinazotegemewa kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie sasa suala zima la watoto wadogo wanaofanya kazi katika migodi nchi nzima. Kwa kweli hili ni janga na hizi ajira za watoto kwenye migodi zinaathiri sana watoto kiafya vilevile kielimu. Watoto hawa hawaendi shule kwa sababu wanatumika kwenye migodi na sehemu wanazofanya kazi watoto hawa ni

hatarishi sana. Mashimo tu ambayo hayana kinga aina yoyote wanadumbukizwa kule kwa sababu wao kwa udogo wao ni rahisi kupenya matokeo yake wanaathirika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya yote wanaathirika na zebaki wanayotumia kuchenjua ile dhahabu. Wengi sasa wamegundua kama wakienda kuchezacheza na ule udongo wakatia zebaki kidogo wanaweza wakaambulia vijiwe vyta mawe ya dhahabu kwa hiyo wanafanya hivyo, lakini hii ina madhara makubwa sana kwao. Napenda Serikali kwa umoja wao kwa mfano, Wizara ya Madini, Wizara ya Elimu, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, wote washirikiane kuona jinsi gani watahakikisha kuwa watoto wadogo hawafanyi kazi katika migodi ili waendelee na masomo kama kawaida na watakapokuwa wakubwa basi wataingia katika kazi hizi za migodini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusiana na wanawake. Wanawake wengi wamependa na wao kujingiza katika shughuli za migodi lakini mazingira siyo rafiki kwao na vilevile na wao wanapata matatizo kama yale ya wachimbaji wadogo kwa vifaa duni na mitaji ni midogo. Kwa hiyo, wao pia kama kundi maalum la wazalishaji wangesaidiwa kwa sababu wana umoja wao tayari amba unawawezesha na wao kuhusika katika biashara hii ya migodi. Tungependa kuona hilo likifanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi ya yote tunaomba sana *data* tupate kujua mawe ya aina gani, yana thamani gani, tunayo mengi kiasi gani na vito vyta aina gani, vina thamani kiasi gani, tunayo kiasi gani. Hii kwanza moja kwa moja itatusaidia kama Taifa kujua utajiri wetu na kutuwezesha kuwa na ulinganisho mzuri duniani hata katika masuala ya mikopo na masuala mengine ya maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo napenda sana tuwe na takwimu za kutosheleza kuhusiana na rasilimali tulizonazo nchini. Kwa sasa hivi tunazungumzia madini lakini naamini

ni kwa rasilimali zote ambazo Tanzania tunazo na ambazo kwa kweli Mungu ametupendelea na kutupatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu yalikuwa ni hayo, nilikuwa nataka tu kuhimiza suala zima la rasilimali hizi zianze kusaidia Watanzania kwanza na kama ni suala la sera kila mtu alielewe vizuri na ionekane pale ambapo kuna mapungufu basi turekebishe ili mwisho wa yote madini yetu yabakie nchini na yaweze kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kuyeyusha (*smelting*). Tumeambiwa kuwa tunajitahidi kwa kadri iwezekanavyo madini yasipelekwe nje yakiwa ghafi, lakini bado hatuna *smelters* za kutosha kuweza kuhakikisha kuwa hilo linafanyika. Tungependa Serikali ifanye makusudi kabisa kuwekeza katika suala hili kwa sababu hiyo ndiyo itakuwa njia pekee ya kuzuia madini kutoroshwa nje kwa njia ya magendo. (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Allan Kiula.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nishukuru kwa kuweza kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu. Pia nishukuru kwa kupata fursa hii adimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nawashukuru Viongozi wa Wizara tukianzia na Waziri, Naibu Mawaziri wake wawili na timu nzima ya Wizara kwa kazi kubwa wanayofanya ya kufikia maeneo yetu ya madini. Sote tumeona jinsi kazi inavyofanyika, jinsi wanavyowajibika, tutakuwa wanyimi wa fadhila kama hatutawashukuru. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi yupo Mbunge mwezangu wakati anachangia alisemea suala la Tumuli, wachimbaji wa dhahabu walikuwa na mgogoro pale kuhusu mambo ya fidia lakini Naibu Waziri alifika Mheshimiwa

Stanslaus Nyongo akaongea nao na aliongea kwa ujasiri mkubwa sana na alikuwa *focused* na aliweka msimamo wa Serikali na ndivyo nilivyotarajia. Kwa hiyo, alipoondoka pale nilikuwa niko vizuri sana kwa sababu hawa wawekezaji tusipokwenda nao vizuri wakati mwингine wanadharau vyombo nya Serikali, maadam tunasimamia haki kwa hiyo Waziri alifanya kazi kubwa sana na nampongeza kwa hilo pia natambua kwamba alikuwa anafanya kazi kwa niaba ya Waziri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kuna eneo la Dominiki wamegundua madini ya *gypsum* yanachimbwa huko lakini kulikuwa na mgogoro. Nachotaka kusema hapa ni kwamba Maafisa Madini walioko kwenye Kanda na Mkoa wakitoa leseni wao wenyewe waweze kufika katika maeneo husika ili kutoa taarifa hizo kwamba tumetoa leseni kwa mtu huyu na utaratibu ufanyike wa kulipa fidia na yule mwekezaji au mchimbaji aweze kufanya kazi yake bila migogoro yoyote lakini mwekezaji anapoibuka kunakuwa na mgogoro mkubwa usio na lazima na unaosumbua watu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, eneo la Dominiki ni eneo ambalo linazalisha sana vitunguu, mwekezaji alivyofika akaanza kubomoa mashamba ya vitunguu, watu wakawa wanalinganisha *gypsum* na vitunguu maana vitunguu ndiyo maisha yao ya kila siku, kwa hiyo ni jambo ambalo ilitakiwa liangaliwe kwa undani ili tuweze kuona kwamba suala hilo litafanyika vipi kwa uzuri wake. Jambo hilo lilikuwa linaendelea na sasa hivi mambo yanakwenda yanatulia lakini tunachosema ni kwamba hawa Maafisa Madini wasilete migogoro isiyokuwa na sababu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala zima la *reserve* ya madini iliyopo nchini. Tunatambua kwamba kuna madini nchini na tunatambua kwamba kuna *GST* ni muhimu *GST* ikapewa pesa za kufanya utafiti kujua *reserve* iliyopo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema hivi kwa sababu tumeona katika baadhi ya maeneo tunategemea takwimu

za wawekezaji kujua *available resource* iliyoko hapo, sisi hatuvezi kufanya *projection*, mgodi huu utafanya kazi kwa muda gani na tunatarajia kupata kiasi gani. Tunapopata hizo takwimu lazima ziwe *proved* na *GST*, kwa hiyo *GST* akipewa pesa za kufanya utafiti itakuwa ni jambo jema. Pia apewe na vifaa vya kisasa vya kufanya ili waweze kwenda na teknolojia. Kwa kufanya hivyo, nchi itanufaika na ile sera ya Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ya kutaka rasilimali zetu ziweze kulindwa na Sheria mpya ya Madini itakuwa na manufaa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri utafiti wa maeneo gani yenye madini ufanyike Tanzania nzima na hasa katika maeneo ambako Serikali ina ubia kupitia *STAMICO*. Hilo ni jambo muhimu sana ambalo inabidi tuliangalie, yapo maeneo kama Mwadui, *TANGOLD*, Buzwagi, maeneo kama hayo yakifanyiwa utafiti tukajua rasilimali illyopo hapo itakuwa ni jambo jema sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hilo hilo tunao Maafisa Madini ambao wanafanya kazi kwa niaba ya Serikali. Ni wakati muafaka sasa kupitia Wizara lakini Tume ya Madini chini ya Prof. Mruma na mwenzake tuweze kuangalia suala la *integrity*, watu wanaopelekwa kule *integrity* yao iko vipi. Kwa sababu ukipeleka mtu ambaye anaweza ku-*compromise* ina maana rasilimali zetu zitakuwa zinapotea pasipo sababu yoyote. Tunatambua kwamba madini thamani yake ni kubwa, mtu aki-*compromise* pale anaweza kuwa anapata kitu kidogo lakini kwake yeye ni kikubwa kulingana na thamani lakini anakuwa analiumiza Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni ajira za wazalendo. Ni lazima tuangalie mgawanyo wa ajira kama zimekaa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni *Board Members*. Je, *Board Members* walioko huko wana uwezo wa kutafsiri, wanajua wanachokifanya au tunawapeleka tu bila kuangalia uwezo wao? Kwa sababu kuna maeneo

mengine *professionalism* inawapiga kando, unakuta wanakwenda kwenye bodi wakikaa wanakunywa chai wakitoka hapo wanapitisha wanakwenda. Kwa hiyo, suala zima la usimamizi linatakiwa liangaliwe. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kuhusu *STAMICO*, kwa heshima kabisa na taadhima *STAMICO* wamekuwa wanatuangusha sana. Ni wakati muafaka Mheshimiwa Waziri na Wizara waangalie kwamba kuna nini huko *STAMICO* ili waweze kufanya kazi ambayo ilikusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuchangia ni suala zima la wachimbaji wadogowadogo, mikopo ya vifaa imekuwa ikitolewa, lakini bado manung'uniko yapo. Ukiona kuna manung'uniko maana yake utaratibu hauko wazi au hauko vizuri, unaweza ukakuta misaada hiyo inakwenda kwenye baadhi ya maeneo tu. Kwa hiyo, ni vizuri ikafanyika sensa wachimbaji wadogowadogo wakajulikana na mahitaji yao yakajulikana na kinachopatikana kikawekwa kwenye mgawanyo mzuri sasa kwamba tunapeleka huku na huku na huku. Hili ni jambo la *fairness* pia ni la *ku-promote* hao wachimbaji wadogo wadogo kwa sababu baadaye nao wanakuwa wakubwa pia wana mchango mkubwa katika Taifa hili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Madini tunaomba wapatikane kwa urahisi katika maeneo yetu. Ziko Wizara zingine ambao Maafisa wao wanapatikana kwa urahisi lakini bado Maafisa Madini hawapatikani kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa, yuko mchangiaji amezungumza suala la magari makubwa kuja kuchukua madini. Kwa mfano, *gypsum* Dominiki malori yamekuwa yanakuja *semi trailers* yanabeba hayo madini, lakini tunapata ushuru mdogo sana kama Halmashauri madaraja yamevunjika na barabara zimeharibika anayezikarabati ni nani? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo muhimu sana tukaangalie ile *compensation* ambapo wananchi wa

maeneo hayo waliothirika wanaweza wakapata kukawa na *balance*, kwamba madini yakachimbwa lakini barabara na madaraja yakatunzwa. Kwa sababu hatuwezi kushabikia uchimbaji wa madini wakati kuna uharibifu mwingine ambao unatokea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na hayo ya kusema, naunga mkono hoja lakini nampongeza Waziri na Naibu Mawaziri, tunaomba muendelee kuchapa kazi. Watu wanasema mbele kwa mbele hakuna kurudi nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kiula kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Rashid Shangazi.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia katika Wizara hii mpya kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nami niwapongeze Mawaziri wote wanaohudumu katika Wizara hii. Pia nimpongeze sana Katibu Mkuu Profesa Msanjila kwa kazi kubwa ambayo anaifanya na nipongeze dhamira njema kabisa ya Mheshimiwa Rais kutenganisha Wizara hii kutoka Nishati na kuifanya sasa kuwa Wizara kamili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na suala hili la *Corporate Social Responsibilities*. Tumeona miradi mingi sana ya madini bado haijaweza kuleta manufaa kwa wananchi wanaozunguka maeneo ambayo madini yanatoka. Hapa tunaona tatizo liko kwenye sheria. Sera ya Madini iko wazi kabisa inaeleza umuhimu wa makampuni ambayo yanachimba madini katika maeneo husika kuweza kusaidia katika jamii zile zinazozunguka, lakini Sheria yetu ya Madini iko kimya katika jambo hili. Nataka Waziri mwenye dhamana na Wizara kwa ujumla waje na majibu yanayoonesha namna sera na sheria zinavyoweza kuungana na kuweza kuleta *harmonization* kiasi kwamba wananchi

wanaotoka katika maeneo ambayo madini yanachimbwa waweze kufaidika na huduma hizi za kijamii na tusiachwe na mahandaki kama walivyofanya Mgodi wa *Resolute* kule Nzega. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda nilizungumzie ni suala la madini ya ya madini ya *bauxite* ambayo yanapatikana katika Milima ya Usambara, Wilaya ya Lushoto. Tunayo madini mengi sana kule yanapatikana katika Kata za Malindi, Magamba, Soni eneo la Shashui pia na eneo la Makanya kule Lushoto. Madini haya inawezekana kwa kutofahamu tunayatumia kama sehemu ya kifusi barabarani lakini kwa kuwa sasa Wizara hii ina Mawaziri wa kutosha ambao wanaweza wakatembelea maeneo tofauti tofauti niwasih i sana wafike Lushoto waweze kuja kutoa elimu kwa wananchi wa Lushoto ili pamoja na rasilimali nyingine ambazo tunazo basi tuanze kufaidika na rasilimali hii ya madini ya *bauxite* ambayo ni madini muhimu sana na ambayo yana thamani sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, wapo wachimbaji wachache ambao wanachimba madini haya lakini bado katika Halmashauri hatujafaidika kwa kiasi kikubwa na upatikanaji wa rasilimali hii ya madini. Kwa sababu wanayachukua katika malori makubwa na wengi wanapeleka katika nchi jirani ya Kenya, naamini kwamba hata Serikali pia inakosa mapato. Kwa hiyo, pamoja na elimu hiyo watakayokuja nayo lakini watutafutie wawakezaji ambao wanaweza wakaja wakayachenjulia kule Lushoto ili angalau kile ambacho ni stahiki wachukue na yale mabaki yetu basi tubaki nayo tuendelee kutengenezea barabara zetu kwa sababu pia Lushoto tuna uhaba mkubwa wa ardhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la Tume ile ya Makinikia ambayo iliundwa, lakini nimejaribu kupitia katika kitabu suaona mahali popote zile dola milioni 300 zimeandikwa. Sasa namuomba sana Waziri mwenye dhamana atakapokuja kujibu hapa aniangalizie kwamba zile dola milioni 300 ziko katika eneo lipi. Natambua kwamba

Mheshimiwa Prosefa Palamagamba Kabudi ndiyo alikuwa mkubwa wa ile Timu ya Maridhiano, hivyo hili jambo nalo tungeweza kupata majibu lingetusaidia sana kuondoa sintofahamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nizungumzie suala la madini ya urani ambayo yanapatikana katika Hifadhi ya Taifa ya Selous haswa katika eneo la Wilaya ya Namtumbo. Zipo tetesi mitaani zimeenea kwamba yale madini yanachimbwa kwa siri. Ningependa kujua kutoka Serikalini kwamba jambo hili lina ukweli kiasi gani kwa sababu ile ni rasilimali yetu wote na hata kama iko ndani ya hifadhi, bado hifadhi hizi zipo kwa mujibu wa sheria na sheria hizi tunazitunga sisi. Yapo mambo yanaweza yakafanya na tunaweza tukapata muafaka wa eneo hili lakini siyo vizuri kama Wabunge tukaendelea kupata maneno haya kwa siri kwamba urani inachimbwa katika Hifadhi ya Selous haswa katika eneo la Wilaya ya Namtumbo, ingependeza sana kama tungepata majibu kwa uhakika zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo pia ni pongezi kwa Jeshi letu la Ulinzi ni suala la ujenzi wa ukuta katika machimbo ya Mererani, kila Mbunge amesimama hapa amelipongeza ni jambo nzuri. Nataka niseme pamoa na dhamira nzuri ya Rais na jitihada hizo ambazo Jeshi wamefanya, bado kuna jitihada za makusudi zinatakiwa ziangaliwe katika eneo linalogusa kodi, ni kwa nini madini haya yanatoroshwa kuititia nchi jirani ya Kenya, hapa lazima Wizara iende mbali zaidi kulitafutia ufumbuzi. Kujenga ukuta ni jambo moja lakini kutengeneza sera na miongozo mbalimbali inayotoa *incentive* nzuri kwa wasafirishaji hawa wa madini inaweza ikapendeza zaidi ili kuwavutia wasiwe na hamasa ya kuititia nchi jirani katika mipaka ambayo siyo rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo liendane pia na madini katika Kanda ya Ziwa kwamba madini mengi yanatoroshwa kuititia Kenya. Wafanyabiashara wa Kenya wanawaambiwa kabisa hawa wafanyabiashara wadogo wadogo bwana wewe ukishafikisha hapa tayari ni suala

dogo yanakwenda huko duniani. Kwa hiyo, tuziangalie pia sheria zetu haswa katika maeneo ya kodi kwamba kodi zetu ni rafiki kiasi gani kwa wachimbaji hawa wadogo wadogo lakini pia wachimbaji wakubwa ili ziweze kutoa nafasi kwa kuruhusu mambo haya kufanyika ndani ya nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kwa ujumla ambalo limezungumzwa ni *STAMICO*. *STAMICO* kweli ni janga kama ambavyo Wabunge wengi wamesema. Katika vitu ambavyo unawea ukawashangaa *STAMICO* kwamba pia wameshindwa ni katika hata migodi hii ya chumvi. Kutengeneza chumvi ni kazi rahisi sana, ni kuchukua maji ya bahari na kuyaweka katika mabwawa na baada muda tayari chumvi imetengenezwa. Hivi ninavyozungumza Mgodi ule wa *Salt Mining* kule Saadani umekufa, kule Uvinza umekufa, lakini *STAMICO* hawa ndiyo ambao wametufikisha hapa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Mheshimiwa dada yangu Angellah haya maoni ya Wabunge hebu yachukulie kwa kina, sidhani kwamba ni vema sana kufufua hili Shirika la *STAMICO*. Tungekwenda mbali zaidi tukatafuta *solution* nzuri ili angalau tusije tukaingia tena kwenye mtego huu ambao umetufikisha hapa tulipo. Hii migodi midogo midogo ya kokoto na chumvi kama imewashinda sidhani bado tunaweza tukawapa jukumu kubwa hili la haya madini ya *uranium*, *nickel* na madini mbalimbali ambayo yanaendelea kugunduliwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitoe rai kwako Waziri kwamba alichukue jambo hili kama ni angalizo kwa Waheshimiwa Wabunge na kama anadhani kuna namna pekee ya kutushawishi basi siyo vibaya akatungenezea semina na hao watu wa *STAMICO* tukajadili na tukachakata na tukajiridhisha kwamba kweli wanaweza wakabadilika. Kama walivyo sasa naamini kabisa kwamba hili ni janga na tusingependa hela za Serikali ziendelee tena kupotea katika shirika hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Shangazi kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, kwa leo ndiyo tunaishia hapo na hoja hii, tutaendelea kesho. Niwashukuru sana kwa michango yenu na ushauri wenu mlioutoa kwa Wizara hii muhimu. Tumetendea haki Kambi zote zilizomo leo humu za Uwakilishi ndiyo maana tumefika mpaka saa hizi.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo, kuna saa hapa aina ya Seiko, nadhani kuna Mheshimiwa Mbunge amechukua zinafafa, lakini siyo ya kwake. Kwa hiyo, nitaikabidhi kwa Wasaidizi wetu wa humu Bungeni, cheki saa yako tu utaona siyo yenyewe, kama ameshatoka basi kesho watakaa nayo ili mwenyewe hasa apatikane.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la pili ni mwaliko wa futari. Mheshimiwa Spika ameagiza niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa, Meneja wa Benki ya NMB, tawi la Dodoma anawaalika Wabunge wote kwenye futari leo Alhamisi tarehe 31 Mei, 2018, saa 12.00 jioni, Jengo la LAPF, ghorofa ya 5, sote tunaombwa tuhudhurie.

Waheshimiwa Wabunge, sina tangazo lingine na kwa maana hiyo naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho siku ya Ijumaa tarehe 1 Juni, 2018, Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 12.00 Jioni Bunge Lilahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 1 Juni, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*